

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 31 Julai, 2008

(Mkutano Ulianiza Saa Satu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi, siku ambayo tunakuwa na nusu saa ya kumuuliza maswali ya papo kwa papo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina waulizaji maswali wengi, tutakwenda kadri ya muda utakavyofikia. Kwanza kabisa, namwita Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mbunge wa Jimbo la Mchinga atakayeuliza swali la kwanza.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Lindi, bila ya ushauri wa Bodi ya Ushauri ya Mkoa, bila ushauri wa Bodi ya Barabara ya Mkoa na bila idhini ya Wizara ya Ujenzi, aliamua kupindisha barabara ya Mkoa kipande cha kijiji cha Milola kupitia Mputwa hadi Wilaya ya Ruangwa; na kwa kuwa uamuzi huu umekitenga kabisa kijiji hiki cha Mputwa umbali wa kilometra 25 kutoka Makao Makuu ya Tarafa, kijiji ambacho kina shule, zahanati, ghalu na mradi wa maji, uamuzi ambaa unapelekea wanakijiji hao sasa kuzikimbia huduma hizo za msingi na kufuata barabara; je, Serikali kupitia kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, itaona busara leo humu kutoa tamko la kuirejesha barabara ile badala ya kusema barabara ile ina gharama kubwa ya matengenezo kwa kuwa Serikali yetu haikimbii gharama bali inafuata watu? Asante sana!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama utaweza kujibu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeweza kabisa nikatoa tamko la kufanya marekebisho katika matengenezo ya barabara hiyo, lakini nasita kufanya hivyo kwa sababu sina maelezo ya kutosha juu ya sababu zilizofanya uamuzi huo ukabadilika. Lakini niongeze vile vile kwamba kama alifanya uamuzi huo yepe yake bila

kushirikisha Bodi ya Barabara ya Mko, ni dhahiri kabisa Mko mna kila sababu ya kutoa malalamiko kwangu na kwa Serikali kwa ujumla. (*Makofi*)

Naomba nikuahidi Mheshimiwa Mudhihir kwamba, nipe muda nilifanyie kazi na niweze kupata maelezo ya kina kwa nini amefanya hivyo na nitakupa majibu kwa maandishi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante! Tunaendelea na Mheshimiwa...

Leo mtatambua kwamba Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, bahati mbaya ameenda kwenye msiba ndio maana hatujaanza na yeye, maana Kanuni zetu zinasema kama hayupo, mtu mwingine hawezi kuuliza kwa niaba yake. Mheshimiwa Mohamed Missanga, swali linalofuata! Maswali yawe ya Kitaifa!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kuendeleza na kuboresha elimu na hasa elimu ya sekondari hapa nchini; na kwa kuwa Serikali na wananchi wameshirikiana, wamejenga Sekondari katika kila Kata walau moja, sisi Singida kule kila Kata ina sekondari mbili, zingine tatu ili kuwezesha watoto wote wanaofaulu darasa la saba waende *Form One*. Lakini kwa kuwa baadhi ya watoto wanaofaulu kwenda *Form One* wanakosa masomo kwa sababu ya ada ya shilingi 20,000/=; je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuangalia upya sera yake ili kuwawezesha wale watoto wanaokosa nafasi kwa sababu ya ada tufute hii ada ya shilingi 20,000/= na watoto wasome bure au kwa kulipiwa na Serikali kuanzia *Form One* mpaka *Form Four?* (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Missanga kwa swali lake zuri, na mimi nina hakika ni mawazo ya Watanzania wengi kwamba pengine ingekuwa hivyo ingesaidia zaidi. Lakini Serikali imelazimika kufanya hivyo si kwa kupenda. Kwa upande mmoja ni kutohana na ukweli kwamba Serikali peke yake haiwezi kumudu kubeba mzigo mkubwa kama huu wa kujenga shule zote za sekondari na kuwasomesha watoto hawa bure, ndiyo maana tukaomba wananchi kwa kutambua kwamba ni kweli bado sehemu kubwa ni maskini. Lakini shilingi 20,000/= kwa mwaka kwa maana ya shilingi 10,000/= muhula mmoja, 10,000/= muhula wa pili, tuliamini ni kiwango ambacho kingeweza kabisa kubebwa na Mtanzania. Sehemu kubwa kwa kweli ya ada ya mwanafunzi inagharamiwa na Serikali yenyewe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba niendelee kuwasihhi sana Watanzania kwa kutambua umuhimu wa elimu, jambo hili tulipe umuhimu mkubwa, hicho kidogo ambacho Serikali imewaomba wachangie, tuwaombe waendelee kuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, kwa upande mwingine, naomba niseme tu kwamba Serikali imejiwekea vile vile mpango mzuri wa kusaidia wale watoto ambao wazazi wao kwa dhati kabisa ni maskini. Kwa hiyo, tunatenga fedha kila mwaka ndani ya Serikali Kuu, lakini vile vile hata kupitia Serikali za Mitaa na mimi najua hata Wabunge

wengi mnachukua jukumu la kuchangia watoto hawa katika juhudii hizou za kusaidia. Kwa hiyo, naomba wote tuendeleze juhudii hizou kwa nia ya kusaidia Taifa letu. (*Makofii*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, kimsingi elimu ya darasa la saba imepitwa na wakati na jirani zetu wakati mwingine wanatucheka sisi Tanzania elimu ya darasa la saba; na kwa kuwa baadhi ya sababu ambazo zilikuwa zinapelekeea walau watoto waishie darasa la saba ni ukosefu wa shule za sekondari za kutosha zilikuwa hazipo. Maadamu sasa tumejenga sekondari na tunaendelea kujenga sekondari za kutosha, hivi kuna kigugumizi gani cha kuifanya elimu ya chini ya mtoto wa Kitanzania iwe darasa la kumi na mbili? (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, *of course*, swalii lenyewe kidogo la kisekta, mimi si Waziri wa Elimu, mimi ni Waziri Mkuu wa mambo ya jumla sana. Lakini nakumbuka swalii hili limewahi kuulizwa tena na tukatoa maelezo. Lakini nitajaribu kuzungumza na Waziri wa Elimu pengine wapate fursa ya kuja kutoa maelezo ya Kiserikali kuonyesha tu nia yetu ni nini katika hatua hii tuliyonayo na kwa maana hili unalotaka kuuliza Serikali, tuone kama tuna maelezo kwa nini tusifanye kidato cha nne kuwa ndiyo kiwango cha elimu ya msingi inayotakiwa. (*Makofii*)

MHE. ANNA MAULIDAH KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi. Swalii langu ni dogo tu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nchi hii tumejitawala takriban miaka 40 iliyoyopita, tumshukuru Mwenyezi Mungu tuko katika hali ya usalama kabisa na tuendeleze hali hivyo hivyo.

Lakini haki ya msingi ya binadamu ye yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu ni Msahafu na Biblia na haki ya msingi ya mwananchi katika nchi yake ni Katiba. Swalii, naomba unijulishe kuna matatizo gani ambayo yanafanya watu raia wa nchi hii hawawezi kuzipata Katiba, wanahangaika sana kuzitafuta na hiyo inaleta kwamba hawaelewi haki zao za msingi. Msahafu na Biblia tunapata mpaka kule chini, lakini kuna tatizo gani na hizi Katiba? Ahsante! (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Anna Komu, tena mama yangu nakuheshimu sana na nakushuru sana kwa swalii zuri sana hilo. Hakuna tatizo lolote la upatikanaji wa Katiba hizi hata kidogo. Mchapaji Mkuu wa Serikali ndiye mwenye jukumu la kuchapisha Katiba hizi, na Katiba hizi kwa kawaida zinapatikana katika maduka yanayouza vitabu hivi kupitia huyo Mchapaji Mkuu wa Serikali. Sasa kama inawezekana kuna upungufu, tutamwagiza achape nyingi zaidi ziwekwe kwenye maduka ambayo yeye anauza Katiba hizi ili Mtanzania ye yeyote aweze kuzipata bila tatizo lolote. (*Makofii*)

MHE. ANNA MAULIDAH KOMU: Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunapoapishwa hapa Bungeni sisi Wabunge huwa tunapewa nakala za Katiba; Ombi, naomba Serikali kwa kupitia kwako, tutoe Katiba tunapowaapisha Madiwani, hata tunapoapisha Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa hata kama tutaacha vitongoji ili iweze kusaidia na wao kuelewa wanatakiwa wafanye nini kwa wananchi wao. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Komu, kama ifuatavyo, tutajitahidi, tutazingatia ushauri wako, ingawa nina hakika hatuwezi kwenda kwa *speed* ya mara moja kwa sababu idadi ya Wenyeviti ni zaidi ya 10,000. Kwa maana ya Kata kwa Madiwani, unajua mwenyewe tuna Madiwani karibu 4,000. Lakini tutajitahidi tuone linalowezekana angalau kwa kuanzia katika ngazi ya Madiwani. (*Makofii*)

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nina swali dogo tu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Hivi karibuni kumekuwepo na taarifa kutoka vyombo vyahabari vikisaidia kuchangisha fedha kwa ajili ya matibabu ya Watanzania. Kwa mfano, mtoto aliyekatwa mguu kwa ugonjwa wa saratani alikuwa anatakiwa apewe mguu wa bandia. Ningependa kujua, je, Serikali ina msimamo gani kutibu watu kama hawa? (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Utaniwa radhi sikusikia vizuri, sijui kwa nini! Naomba urudie tena kidogo, usogeze *microphone* kidogo!

NAIBU SPIKA: Naomba urudie tena Mheshimiwa Lucy Owenya!

MHE. LUCY F. OWENYA: Nilikuwa nasema hivi, katika vyombo vyahabari hivi karibuni vimekuwa vikisaidia kuchangisha fedha kwa ajili ya Watanzania ambao wanahitaji msaada, kwa mfano, kijana aliyekatwa mguu kwa ugonjwa wa saratani alikuwa anatafuta fedha kwa ajili ya kuwekewa mguu bandia. Nilitaka kujua, je, Serikali ina msimamo gani kusaidia kutibu wagonjwa kama hawa pamoja na kuwasaidia kwa sababu wengi wao, siyo wengi sana wenge kuhitaji msaada kama huu. Serikali ina msimamo gani katika matibabu yao? (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Lucy Owenya, kwa swali lake. Wagonjwa wote kwa ujumla wa Tanzania, inapokuwa ni ugonjwa ambao unahitaji msaada wa Serikali kwa asilimia mia moja huwa tunafanya hivyo. Kubwa tu ni kwamba inabidi ufuate utaratibu kupitia Wizara yetu ya Afya na ikidhibitika kwamba ugonjwa huo ni ugonjwa ambao sisi tunajua tunaweza kuubeba, tunafanya hivyo bila matatizo yoyote. Lakini nadhani suala lako ni pana zaidi kidogo kwa maana tatizo hili kwa upana wake kwamba pengine ingekuwa vizuri Serikali ikawa na mpango mahsus wa watu wa namna hii kuweza hata kuwajua tu wako wapi, tuweze kuona utaratibu badala ya kungoja mtu mmoja mmoja *case* itokee. Kwa hiyo, nadhani ushauri ni mzuri. Tutajihidi tuone kama tunaweza kuainisha aina hii ya wagonjwa kwa lengo la kuwa na mpango madhubuti zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofii*)

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mnamo mwaka 1983, kulitokea zoezi la uhujumu wa nchi (*economy sabotage*) na wakati huo watu wengi walikuwa na hatia na wengine walikuwa hawana hatia ya uhujumu huo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu wengi wamepoteza mali yao hao ambao walikuwa hawana hatia na vielelezo viro, mpaka leo Mheshimiwa Waziri Mkuu hawajalipwa fidia

za mali zao na hasara walizopata. Je, Serikali ya Awamu ya Nne inasemaje kuhusu kuwalipa hao ambao wengine ni wapiga kura wangu wa Jimbo langu na wengine wameathirika kimaisha na kiuchumi. Nakuomba unijibu swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu! (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Aliwahi kujibu kwa siku za karibuni, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Hasnain Dewji, swali lake kama ifuatavyo, ni kweli kabisa mwaka alioutaja mwaka 1983 kulikuwa na zoezi hilo kubwa, nakumbuka lilitikisa kwa kweli nchi nzima. Walikamatwa watu wengi, baadhi yao walionekana hawana hatia, wengine walionekana wana hatia na wakatiwa hatiani na kupewa adhabu zinazostahili.

Lakini baada ya zoezi lile kama utakumbuka Mheshimiwa Dewji, Serikali ilijirudi tena na kuamua kurejea tena zoezi lile kwa maana ya kujiridhisha kwamba wale ambao walionekana kweli walikuwa si wahalifu, isipokuwa tu kwa sababu ya zoezi lenyewe lilivyokuwa kubwa, basi Serikali angalau iwalipe kifuta machozi na zoezi lile limefanyika, kama kumbukumbu yangu itakuwa sijasahau, nadhani mpaka mwaka 1995 hivi au 2000 ndipo Serikali ikasema kama mpaka leo hakuna watu zaidi, basi zoezi hili tunasitisha. Kwa hiyo, tukawa tumeamua kulisitisha kwa nia nzuri, tukiamini kwamba wote waliokuwa na matatizo ya kweli, wameshughulikiwa na mambo yamekwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa siwezi nikamkatalia hilo analolisema, lakini najua nitapata taabu sana kumwomba Rais akubali baada ya uamuvi ule kwa sababu inawezekana tukaanza tena kesi zaidi ya miaka 20 sasa, kuweza kuwa na ushahidi wa ukweli wakati mwengine si rahisi. Lakini kama unaye mtu ambaye unasema *genuinely* ana tatizo, nilettee, tutaweza kuangalia kesi yake tuone kama tunaweza kumsaidia. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nimuulize swali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nalazimika kukuuliza swali hili pamoja na kwamba linaonekana kama ni la kisekta, lakini wewe ndiye msimamizi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni na kwa nchi nzima kwa ujumla na inapoonekana kwamba jambo Wizara pengine inashindwa kulipeleka, inabidi tkuulize wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, shule ya sekondari Iyunga iliyoko Mbeya ilifungwa wiki mbili kabla ya muda wake wa kawaida kwa sababu ya chakula na wanafunzi wa shule ile hawakufanya mtihani. Lakini pia baada ya shule nyingine kufunguliwa, bado hadi leo, shule ile ya sekondari Iyunga haijafunguliwa kwa sababu zile zile kwamba shule haina chakula na wale wanaopeleka chakula pale shulenii wanadai shule shilingi milioni 570 mpaka leo. Hivi Serikali inatamka nini wakati tunalenga kuboresha elimu, bado tunawaweka hawa watoto miezi miwili karibu na nusu nyumbani, tunategemea wapate

elimu ya namna gani na sasa Serikali inatoa tamko gani kwa mambo haya ambayo yanaelekea kudidimiza elimu ya watoto wetu? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Godfrey Zambi, swali lake kama ifuatavyo, kwanza, tunaomba radhi kwa hilo lililotokea kama watoto walifika mahali wakashindwa kufanya mtihani kwa sababu alizozieleza. Mimi nasema tunawaomba radhi sana wazazi wale na hata vijana wenyewe ambao tuliwanyima hiyo fursa. Lakini inawezekana ilikuwa ni kutokana na hali halisi iliyojiteze wakati huo, isingawezekana pengine kutatua jambo hilo kwa haraka, labda busara ikaoenekana tufanye hivyo.

Lakini linalotia simanzi zaidi ni kwamba bado limeendelea na kwamba mpaka leo bado shule ile haijafunguliwa. Najua tuna matatizo haya mengi, lakini tumejitahidi sana kama Serikali kujaribu kuyapatia ufumbuzi na shule nyingi zimeanza tena kufunguliwa na watoto kusoma. Kwa hili la shule ya sekondari ya Iyunga, Mheshimiwa Zambi basi naomba uniachie, maana nikiagiza, haitasaidia. Naomba uniachie mwenyewe, nitalishughulikia na Waziri wa Elimu na mimi nina hakika tutakupa jibu haraka inavyowezekana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante! Naona tuendelee kwa sababu amesema atafanya hivyo. Ndiyo! (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, lipo la msingi. Lipo la msingi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza nakushukuru sana kwa majibu hayo! Lakini pia jana niliongea na Afisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya pamoja na *RAS*, wakasema kwamba wanafikiria wawaombe walimu wafundishe kwa muda wa ziada ili watoto hawa watakapoanza elimu, waweze kufidia muda uliopotea. Lakini kuna jambo la walimu kufundisha muda wa ziada na ye ye ali sema watawaomba, je, Serikali itakuwa tayari sasa walimu watakapofundisha muda wa ziada wawe tayari pia kuwalipa? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ataongea na Waziri wa Elimu kwa maswali uliyouliza!

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa dhana nzima ya kuweka wakala ni kuongeza ufanisi na kupunguza gharama. Hivi sasa marekebisho ya Daftari la Wapiga Kura yanafanywa na Tume ya Uchaguzi ambayo ingetakiwa kupata taarifa zote kutoka kwa Wakala anayeitwa *RITA* ambaye anaweka takwimu za Vizazi na Vifo. Lakini katika suala la vitambulisho vya uraia, Serikali imeunda wakala mwengine anayeitwa *NIDA* ambaye kwa kweli hawezi kufanya kazi yoyote bila kupata taarifa kutoka kwa *RITA*. Kwa kuwa *RITA* ina mtandao nchi nzima, kwa nini Serikali isitumie *RITA*, isiwezeshe *RITA* kufanya kazi hii ya vitambulisho vya uraia badala yake inatumia *NIDA* ambayo haina uwezo wowote? Je, hii ni sera sahihi ya kutumia fedha za walipa kodi wa nchi hii? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, aliposimama nikaanza kutetemeka, lakini bahati nzuri hakunipeleka huko. (*Makofi*)

Lakini naomba nikubaliane na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, *RITA* kwa kweli ndiyo chombo ambacho tunafikiri kinaweza kikafanya kazi hiyo kwa umakini mzuri zaidi na kama bado kuna hiyo hali ya kutoeleweka eleweca juu ya zoezi hili au nani hasa afanye zoezi hili, tutazungumza na Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ndiye tumempa hiyo kazi ya kusimamia eneo hilo na mimi nafikiri tutafaalu tu, usiwe na mashaka. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Atazungumza na Waziri wa Sheria! Ehe, nini zaidi?

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Katika zoezi la marekebisho ya Daftari la Wapiga Kura, Tume ya Uchaguzi inatumia utaratibu gani kuhakikisha kwamba inapofika mwaka 2010 inajua kwamba *Mr. X* atakuwa na haki au hatakuwa na haki ya kupiga kura au *Mr. Y* atakuwa hayupo kabisa kwenye daftari lile. Mnatumia utaratibu gani kufanikisha shughuli hiyo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Jamani, tena Waziri Mkuu aingie kwenye...

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili la kurekebisha Daftari la Wapiga Kura liko katika hatua mbili kubwa. Sasa hivi ni hatua ya kwanza ambapo tunapitia kama unavyoona kwenye matangazo ya luninga na tunajaribu kupata takwimu zote za msingi na zoezi lile sambamba linakwenda linarekebishwa. Lakini kabla ya mwaka 2010 tutalazimika tena kufanya zoezi la uhakiki ili tuwe na uhakika kwamba ifikapo wakati wa uchaguzi, majina yatakayokuwepo kwa kweli yatakuwa ndio yale ambayo tulikuwa mpaka dakika ya mwisho tumeyapata. Sasa inawezekana kwamba dakika zile za mwisho ukakuta pengine mtu mmoja amehama, amehamia sehemu nyingine, amekwenda nje ya nchi, hilo linawezekana. Lakini sidhani kwa utaratibu tulio nao, kama hilo litaleta tatizo kubwa sana, kwanza watakuwa ni wachache na itakuwa ni rahisi vile vile kuwatambua kwa sababu ya utaratibu uliopo hivi sasa. (*Makofi*)

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana!

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa kero za Muungano ni jambo la muda mrefu na kwa kuwa hivi sasa vikao vyake vinafanyika kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; je, vikao vingapi vimeshafanyika na mambo gani yaliyozungumzwa na kutatuliwa na vikao hivyo vitaendelea kwa muda gani kwa mwaka mmoja, yaani vitakaa mara ngapi kwa mwaka? Ahsante!

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge swalii lake kama ifuatavyo, kwanza, nianze na hili la pili kwamba vikao hivi vitaendelea kwa muda gani. Vikao hivi vitaendelea kwa muda wote kwa kadri itakavyoonekana ni lazima kwa upande mmoja kwa sababu masuala haya ya Muungano

yataendelea kuzungumzwa tu mpaka tutakapoona kwamba zile kasoro ambazo ni za msingi zimemalizika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado mimi nadhani kwa *nature* ya Muungano ulivyo, hata ukiondoa yale matatizo ambayo tunasema ni kero za Muungano, umuhimu wa kuendelea kuzungumza kindugu kati ya pande hizi zote mbili, bado ni vizuri ukaendelea kuwepo. Lakini kuhusiana na swali la kwanza, mara tu baada ya uamuzi huu kufanywa na Rais, kikao kimefanyika mpaka sasa kimoja na bahati nzuri na mimi nilishiriki hivi karibuni pale Dar es Salaam na inawezekana baadhi yetu pengine ni wajumbe. Lakini ukiniambia ni mambo gani yalizungumzwa, pengine sitaweza kwa kweli kwa dakika hii kwa sababu sina takwimu zote. Lakini tulichofanya katika kikao kile, kwanza ilikuwa ni kupokea taarifa ya vikao vila ambavyo wenzetu walivifanya, Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu wakati ule kwa maana ya kuona yatokanayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema cha uhakika ni kwamba kwa kweli mikutano ile ina manufaa makubwa kwa sababu niliona katika kikao kile baadhi ya mambo ambayo yalioneckana yana utata, tuliyatolea maelezo na tukakubaliana kwamba yaendeleee. Kwa hiyo, nafikiri kwa vile kuna shauku kubwa pengine juu ya nini hasa kimeishazungumzwa mpaka leo, mimi nafikiri hakuna ubaya, tunaweza tukamwomba Waziri wa Muungano baadaye kadri Bunge litakavyotaka, pengine tujaribu kuonyesha ni mambo gani mpaka sasa yamezungumzwa, yapi bado yanaendelea kwa njia ya kauli ili pengine muweze kupata nafasi ya kujua kinachoendelea katika mazungumzo hayo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante na hajawasilisha hotuba yake, kwa hiyo, kuna nafasi. (*Makofii*)

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alikuwa na utaratibu wa kuhutubia nchi au kuhutubia wananchi katika vyombo vyaa habari kila mwezi; na kwa kuwa sasa hivi imefika kiasi cha miezi miwili/mitatu au hata minne inafika bado hajahutubia Taifa au hajahutubia Watanzania; na kwa vile Watanzania walikuwa wakifutilia sana na wana shauku sana kumsikia Rais wao baadhi ya mambo kwamba anazungumza wazi na hilo halifanyiki; Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kutueleza nini katika hilo na anaweza kutusaidia vipi ili utaratibu ule ukarejea? (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir swali lake zuri kama ifuatavyo, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais alijiwekea utaratibu wa kuzungumza na wananchi kila mwisho wa mwezi kupitia vyombo vyaa habari na alikuwa anatumia luninga zaidi, lakini na redio nazo zilikuwa zinapata fursa hiyo na kwa kweli ni utaratibu mzuri kwa sababu wananchi wanapata fursa ya kumsikiliza na kujua mambo makubwa ambayo wanataka Taifa lijue. Lakini nakubali vile vile kwamba ni kweli kwa miezi nafikiri kama miwili hivi, sina hakika kama ni mitatu/minne, lakini angalau miwili nina uhakika, Rais hakupata nafasi kwa wakati uliotakiwa kuweza kutekeleza hiyo azma yake. Lakini nataka niseme ni kutokana tu na majukumu na hasa baada ya kuwa amekuwa Mwenyekiti wa AU, amelazimika kuwa na

mambo mengi, kwa hiyo, wakati mwingine tarehe zinapofika, yuko nje ya nchi na hajapata nafasi ya kuweza kufanya hiyo kazi. Lakini wala sitaki kusema kwamba nitamshauri kwa sababu najua analijua, nafikiri punde akipata nafasi tu, atarudi tena kwenye utaratibu ule kwa sababu ni mzuri sana kwa Watanzania. (*Makofi*)

MHE. MZEE NGWALI ZUBER: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kumuuliza Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunafaidika nini hasa katika Maonyesho ya Biashara ya Saba Saba wakati ambapo Watanzania hatubadiliki katika mauzo ya nje na ya ndani? (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, rafiki yangu sana huyu Bwana, sasa leo kanipa swali gumu kweli kweli! Lakini maonyesho yale, mimi naamini wengi tunakwenda kwenye maonyesho yale na mimi safari hii nilipata nafasi ya kwenda kushiriki katika maonyesho yale. (*Makofi*)

Mimi nadhani ziko faida nyingi, kwanza ni Watanzania wenyewe kupata nafasi ya kwenda kuona maonyesho yale yana kitu gani na wanapata elimu vile vile kwa sababu baadhi ya vitu tunavyoviona katika maonyesho yale si rahisi kuviona katika mazingira ya kawaida isipokuwa unapokuwa kwenye mkusanyiko wa wazalishaji na wafanyabiashara pale kwenye uwanja wa maonyesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili mimi nilipopita pale nilipata fursa ya kutembelea mabanda ya *Pride*, nikatembelea banda la Mama Mkapa, nikatembelea banda la *SIDO*, kwa hakika mabanda yale mimi yalinipa elimu kubwa sana kuona wajasiriamali wadogo wadogo wanavyoweza kunufaika na taratibu za Serikali zilizopo hivi sasa na kwa mtu mwingine yejote aliyepita pale atatoka na dhamira kwamba kumbe maonyesho yale yana manufaa na ajue ni wapi anaweza akapata elimu inayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu mimi kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa nilipopata nafasi ya kwenda kutembelea na kuona matrekta yale madogo, nikaona matrekta makubwa, nimekwendwa kwenye banda la Nyumbu nikaona matengenezo ya mashine kwa ajili ya kufyatua tofali ambazo zinaweza zikasadia sana kupunguza uhariifu wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli niliporudi niliwaandikia Wakuu wa Mikoa wote kuwataka waende wakatembelee vituo vyote vinavyouza yale matrekta, waende Nyumbu wakaone ile kazi nzuri inayofanyika ili wawe na mipango ya kuweza kuona namna tunavyoweza kutumia matrekta yale madogo, yale makubwa na hata zile mashine za kufyatua tofali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeweza nikasema maneno mengi lakini kwa ujumla nasema maonyesho yale pamoja na haya niliyoyasema yanatuweza vile vile kupata watu kutoka nje kutaka kununua biashara fulani fulani kutoka kwetu, lakini na sisi tunapata

fursa vile vile ya kuona wale walio toka nje tuwe na fursa kuweza kuona ni mambo gani tunaweza tukapata kutoka kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge dakika thelathini kwa Waziri Mkuu zimekwisha, kwa niaba yenu napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba ukae. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwa niaba yenu naomba tena nimshukuru Waziri Mkuu kwa umahiri wake wa kuweza kujibu maswali yetu na kwa sababu huu ni utaratibu mpya inabidi tuendelee kufanya tathmini kila tunapomaliza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumeuliza maswali yale ya binafsi kabisa kisekta, mkimuuiliza hivi si *fair* na matokeo yake huwezi kujibiwa inavyostahili. Tunachokitaka ni maswali ya kisera, ya Taifa na Kimataifa usije ukasema leo kijiji changu fulani, nataka hivi, haiwezekani Waziri Mkuu hawezi kujibu maswali ya namna hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo nimewastahi sana wale waliohusika na naomba wiki ijayo tuwe makini, unapotaka kumuuliza Waziri Mkuu jiandae wiki nzima hata ukishauriana na wenzio swali la namna gani litakuwa sahihi, kwa hiyo tunataka yawe na uzito ule ule. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina vi-note vyta Wajumbe wengi hapa wanasema mnazidi kupunguza umuhimu wa maswali. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 312

Azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma

MHE. OMAR S. KWAANGW' aliuliza:-

Kwa kuwa nia na azma ya Serikali kuhamia Dodoma ni lazima sasa ione kane kwa vitendo:-

Je, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwa Wizara na Idara zote, viongozi na watendaji na gharama za magari na usafiri wakati wa kuhudhuria mikutano yote ya Bunge kwa mwaka 2006/2007?

Je, ni vitendo gani dhahiri vinavyoonyeshwa na Serikali katika juhudzi zake za kuhamia Dodoma ifikapo mwaka 2010?

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA,UTARATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mbunge wa Babati, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kuhudhuria mikutano yote minne iliyofanyika Novemba, 2006, Januari 2007 na Juni/Agosti 2007 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 ilifikia shilingi milioni 872.8. Gharama hizo zilitumika kuwashudumia viongozi, watendaji na pia uendeshaji wa magari na vitendea kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za Serikali kuhamia Dodoma ifikapo mwaka 2010 yamefanyika maamuzi makubwa na vitendo dhahiri vilionekana. Baadhi ya mambo hayo ni:-

(i) Kuongeza Bajeti ya *CDA* mwaka hadi mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na upimaji viwanja. Mwaka 2005/2006 zilitengwa shilingi 400,000,000/= mwaka 2006/2007 zilitengwa shilingi 427,945,000/= mwaka 2007/2008 zilitengwa shilingi 1,412,694,509/= na mwaka huu 2008/2009 zimetengwa shilingi 2,387,825,338/=.

(ii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Bunge na kuzihamisha kazi zote za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Dodoma.

(iii) Ujenzi wa nyumba zaidi ya mia tano za makazi ya viongozi na watendaji wakuu wa Serikali na Taasisi zake.

(iv) Ujenzi wa Vyuo mbalimbali vya Serikali kama vile Chuo cha Mipango (*IRDP*) Chuo cha Madini na Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, sekta binafsi imehamasishwa kujenga vyuo na utoaji wa huduma za afya katika Manispaa ya Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa mwaka huu zitaendeleza kasi za kupima viwanja zaidi ya 10,000 katika maeneo ya Nzuguni, Mkalama na eneo la mnada mpya kando kando ya barabara iendayo Singida. Ujenzi wa uwanja wa maonyesho ya Nane nane, kukamilisha ujenzi wa uwanja wa Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (*Mwalimu Nyerere Square*), kusafisha mifereji mikubwa ya maji ya mvua, kukarabati barabara muhimu za Manispaa ya Dodoma na uthongaji wa barabara katika maeneo ya makazi ya Kisasa katika barabara ya Dar es Salaam. (*Makofi*)

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu yanayoonesha dhahiri vitendo vya Serikali katika kutaka kuhamia Dodoma, kuna ahadi nzito kabisa ambazo zimetajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi kati ya mwaka 2005/20010 na maswali yangu yatakuwa kwenye eneo hilo.

(a) Swali la kwanza katika eneo hilo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 - 2010, moja ni kujengwa kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa - Dodoma na Arusha, ningependa kufahamu katika ahadi hii nzito Serikali inatuambia nini katika kipindi kilichobaki kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kati ya Dodoma - Babati na Iringa- Dodoma?

(b) Swali la pili kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri hakutaja kasi ya Wizara kuhamia Dodoma na katika Ilani imesema; “Kuongeza kasi ya Wizara za Serikali kuhamia Dodoma kwa kuwa sasa Serikali inajenga nyumba nyingi za kuishi watumishi.”

Ningependa kufahamu kwamba mpango wa Serikali kuhamisha Wizara ukoje sasa maana hivyo ndiyo vingeonesha kwamba kweli Serikali inataka kuhamia Dodoma. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA,UTARATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO): Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba kwa sasa mkandarasi anaweza kuanza kazi wakati wowote kujenga barabara ya lami kati ya Mijingu na Babati na sasa hivi upembuzi yakinifu umeshafanyika kwa barabara kati ya Babati - Dodoma na Iringa nayo inaonekana kuna dalili kama siyo wakati wetu huu basi kipindi kingine cha maisha ya Bunge lijalo inawezekana kabisa barabara kati ya Iringa – Dodoma na Babati ikawa ya lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya Wizara kuhamia Dodoma, tukumbuke kwamba waasisi wa suala zima la kuhamia Dodoma miaka ile ya 1970 ya mwanzo na 1980 walikuwa na upeo wa kuangalia kwamba Serikali ndiyo itakuwa inajenga Mji, baadaye hali imebadilika sasa sekta binafsi imeingia hapa katikati na bila sisi kutarajia Dodoma imeanza kuwa kitovu cha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatarajia kwamba katika muda wa miaka kati ya mitano na kumi ijayo wanafunzi laki moja wa vyuo vikuu mbalimbali watakuwa wakisomea hapa Dodoma. Nafahamu Chuo Kikuu cha Dodoma kitapokea siyo chini ya wanafunzi elfu arobaini na Chuo Kikuu katika njia ya kwenda Iringa katika maeneo ya zamani ya shule ya sekondari ya Mazengo kuna Chuo Kikuu cha *St. John's* nacho kinatarajiwa kuwa na wanafunzi elfu kumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi nyingine pia inataka kujenga Chuo Kikuu iitwayo *Jersey East* ambayo inatarajiwa kuwa na wanafunzi elfu arobaini, hivyo ule upeo wa kuanagalia kwamba Dodoma ungekuwa Mji wa Watumishi wa Serikali umebadilika bila matarajio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, zile huduma zilizokua zimeandaliwa kwa ajili ya watumishi wa Serikali kwa vyovypote sasa huduma zile zitakuwa kwa ajili ya wanafunzi na walimu wa vyuo vikuu, hii maana yake ni kwamba sasa hata mpangilio wa Wizara kuhamia Dodoma utabadilika kwa ajili ya huduma ambazo zinahitajika kuwashudumia watu hawa. (*Makofii*)

Matumizi Mabaya ya Fedha za Halmashauri

MGANA I. MSINDAI aliuliza:-

Kwa kuwa chanzo kikubwa cha matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri za Wilaya kupitia kwenye manunuzi ambako mara nyingi taratibu za utunzaji, malipo, upotevu wa nyaraka na kadhalika vimetawala, na kwa kuwa Halmashauri nyingi hazina wataalam wa ugavi (*Store Officers*);

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya hali hiyo?

(b) Je, Serikali inasemaje juu ya Maafisa Ugavi ambao wamekaa muda mrefu sana kwenye Halmashauri moja na ambao mara nyingi wamekuwa vikwazo hata kwa maafisa wasaidizi ambao hupata uhamisho mara kwa mara?

(c) Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuweka nguvu kama ambavyo imefanya kwa wahasibu kusomesha watu wengi wa kada ya manunuzi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SRIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wewe pamoja na Mheshimiwa Philip Marmo, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri kwa ufasaha na kwa umahiri mkubwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa fedha nyingi zimekuwa zikipotea kwa njia ya manunuzi, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilitunga sheria ya manunuzi namba 21 ya mwaka 2004. Sambamba na sheria hiyo Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ametoa kanuni za manunuzi kwa mamlaka za Serikali za Mitaa kwa tangazo la Serikali namba 177 la mwaka 2007, vitengo vya manunuzi na Kamati za Ukaguzi (*Audit Committee*) zimeanzishwa kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ili kubaini, kuimarishe na kudhibiti mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Ni mategemeo ya Serikali kuwa Waheshimiwa Wabunge kama sehemu ya Baraza la Madiwani wataendelea kutoa michango yao katika kuhakikisha Kamati za Ukaguzi zinafanya kazi yenye ufanisi nakuleta tija. (*Makofit*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya zoezi la kubaini watumishi waliookaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika zoezi hilo watumishi mbalimbali walihamishwa kati ya Julai, 2007 hadi Mei, 2008

ikiwa ni pamoja Maafisa Ugavi 18 walikaa zaidi ya miaka mitano katika kituo kimoja cha kazi.

Aidha, kuanzia Agosti, 2007 Makatibu Tawala wa Mikoa wamekasimiwa jukumu la kuwahamisha watumishi ndani ya Mikoa yao ili kuongeza ufanisi, uamuvi huu wa Serikali unamwezesha Katibu Tawala wa Mkoa kurekebisha kasoro mbalimbali zinazotokana na watumishi kukaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu au kuhakikisha kuwa kuna uwiano wa watumishi kati ya Halmashauri moja hadi nyingine ndani ya Mkoa. (*Makofii*)

(c) Mheshimiwa Spika, ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha kwamba wanatenga fedha ya kutosha katika Bajeti ya mwaka ili kuwaendeleza watumishi wake kwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kulingana na mahitaji ya kazi zao wakiwemo Maafisa Ugavi. Aidha, katika kuwaongezea stadi za kazi, Maafisa Ugavi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (*Public Procurement Regulatory Authority*) imeendesha mafunzo kwa Maafisa Ugavi na Wakaguzi wa Ndani ili kuwajengea uwezo ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yangu inaendelea kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha na Uchumi ili utaratibu uliotumika kusomesha na kuajiri Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani katika Halmashauri utumike pia kwa kuwapata Maafisa Ugavi. (*Makofii*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa sababu fedha inayopelekwa Halmashauri kwa ajili ya mafunzo haitoshi, na kwa vile Maafisa Ugavi wengi hawana sifa zinazotakiwa, je, Wizara ya Fedha itachukua hatua ya kutenga fedha kama ilivyotenga kuwasomesha Wahasibu iwasomeshe maafisa ugavi wote?

(b) Kwa kuwa kuna baadhi ya Maafisa Ugavi wanashirikiana na baadhi ya Wakuu wa Idara kufanya manunuzi bila kuwashirikisha Maafisa Masuhuli, Serikali itafanya uchunguzi na Maafisa Ugavi na wale Wakuu wa Idara wanaohusika wachukuliwe hatua za haraka?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Kwanza kabisa ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Msindai kwamba hela ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuwasomesha hawa Maafisa Ugavi hazitoshi, lakini kwa sasa hivi utaratibu tuliojiwekea na kama alivyosema katika swali lake la pili ni kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba fedha zaidi zinatengwa kwa ajili ya kuwasomesha hawa Maafisa Ugavi amba ni muhimu sana katika kuendeleza Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili anazungumzia kuhusu hawa Maofisa kwamba wanashirikiana na kwa hiyo kufikia mahali wakati mwingine kutokuwashirikisha *Accounting Officers* na wizi kuwa unafanyika kule ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mgana Msindai, najua alikuwa Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounting Committee* na kwa misingi hiyo amejenga uzoefu mkubwa sana na kubaini maeneo ambayo yamepoteza hela za Serikali. (*Makofi*)

Sisi tunachofanya ni kwamba mpaka sasa hivi tunaendelea kuchunguza na mahali popote itakapobainika kwamba kuna viongozi wowote au wakuu wa idara wameshirikiana kwa njia hiyo anayozungumza hapa, Serikali haitaacha kuchukua hatua madhubuti kwa hao waliohusika. (*Makofi*)

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, ningependa kujua Serikali kwa nini inatoa uhamisho kwa baadhi ya maofisa katika Halmashauri zetu ikiwemo Liwale kwa wale ambao wanakaribia kustaafuli na utendaji wao unakuwa siyo mzuri kwa kuwa wanahitaji kuwa wazuri karibu ya kustaafuli?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi sana kama analenga wapi lakini anachozungumzia hapa ni watumishi ambao muda wao umekwisha na kwamba wanatengemea sasa kustaafuli wanahamishwa na kwamba kwa nini wanahawmishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu nyingi sana zinazosababisha mtumishi mmoja ahamishwe kutoka eneo moja kwenda nyingine, lakini hakuna wakati wowote ule ambapo zoezi hilo limefanyika bila kuihusisha Halmashauri inayohusika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, kama kuna eneo lolote lile anafikiri kwamba imetokea hivyo ni vizuri tukawasiliana ili tuweze kuona jinsi ya kuweza kutatua tatizo hilo. (*Makofi*)

Na. 314

Ubovu wa Barabara Jimbo la Kawe

MHE. RITA L. MLAKI aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo mengi ya Jimbo la Kawe yamepimwa na watu wamejenga nyumba nzuri kubwa na za gharama; na kwa kuwa maeneo hayo ambayo ni *Mbezi Beach*, Makongo, Changanyikeni, Tegeta na Mikocheni hayapitiki kutokana na ubovu wa barabara.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara na mifereji kwenye maeneo hayo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mrefu wa kuboresha maeneo husika hata ikibidi kutoza kodi kubwa za majengo hayo ili kujenga barabara na mifereji hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Kawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mpango wake wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami ambao ni endelevu kwa kila mwaka tayari imekwishaanza kwa kujenga barabara ya *Kawe Club Oasis* kwa kiwango cha lami na ujenzi unaendelea kwa kasi nzuri. Pia katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni imetengewa fedha kutoka bodi ya mfuko wa barabara kiasi cha shilingi milioni 741.5 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya *Viongozi road* itakayopita maeneo ya *TPDC-Mikocheni* na kuelekea maeneo zilizopo nyumba za Serikali yenyе urefu wa kilometra 3.2 na kiasi cha shilingi milioni 420 kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Ali Hassan Mwinyi yenyе urefu wa kilometra 0.64. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia katika mpango wa matengenezo ya barabara, Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 86 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum kwa barabara ya Kawe - Jeshini yenyе urefu wa kilometra 2.3, kiasi cha shilingi milioni 87 kwa ajili ya Makongo yenyе urefu wa kilometra tano. Matengenezo haya yanafanyika sanjari na matengenezo ya mifereji. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kufanya matengenezo barabara kila mwaka ni endelevu ili kuboresha maeneo mbalimbali yenyе matatizo ya miundombinu kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haina uwezo wa kujenga barabara nyingi kwa wakati mmoja, ujenzi na ukarabati utafanyika kutokana na vipaumbele vya Halmashauri yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kutoza kodi kubwa kwenye majengo, itakumbukwa kwamba kwenye Mkutano wa Kumi na Moja, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada ambao unaiwezesha Mamlaka ya Mapato (*TRA*) kukusanya kodi ya majengo kama wakala. Utaratibu huu utaanza katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam. Kuhusu kiwango cha kodi kinachoamuliwa kutozwa Halmashauri yenyewe ndiyo yenyе kauli kwa kuzingatia hali halisi ya majengo husika. (*Makofi*)

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika Jimbo la Kawe kuna wananchi ambao wamejitolea na mashirika mbalimbali kuchanga fedha na sasa hivi zimefikia shilingi milioni mia mbili na wako tayari kuchanga mpaka shilingi milioni 700:-

(a) Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa ku-centralise ama kuziunganisha juhudzi za Manispaa, *TANROAD*, *World Fund* pamoja wananchi hao ili tuweze kuwa na chombo maalum kitakachoshughulikia barabara za Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu kwa kufanya hivyo watabuni mbinu zaidi za kutafuta fedha?

(b) Nashukuru kwamba *TRA* itakuwa kama wakala wa kukusanya kodi ya majengo kwa ajili ya kutengeneza barabara lakini ninalewa kabisa *TRA* inapokusanya fedha zinakwenda Hazina ambalo ni jungu kuu na linaitwa ni mapato yanatumika kwa Bajeti, je, wananchi walionituma kwamba watakuwa tayari kutoa fedha za majengo nyingi watengenezewa barabara watahakikishwaje kwamba fedha hizo watakazotoa zitatengenezewa barabara Jimbo la Kawe, *Mbezi Beach*, Tegeta, Mikocheni, Sakurveda, Makongo na Changanyikeni? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kwa niaba ya Serikali nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi hawa ambao wamejitokeza kwa sababu huo moyo ambao tunataka kuujenga katika nchi yetu ya Tanzania kwamba wananchi wenyewe wahusike katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama hapa na akaeleza kwamba tunataka kujiwekea utaratibu maalumu ambao utaendesha Jiji la Dar es Salaam katika ujumla wake na kwamba kuna Kamati maalum ambayo imeundwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, matumaini yangu ni kwamba Mheshimiwa Rita Mlaki, atashirikiana na Kamati hii kwa maana ya kutoa mawazo zaidi ili tuweze kuunganisha nguvu zile kwa ajili ya kuweza kufanya lile ambalo analizungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TRA* na sheria ambayo tumeipitisha hapa, mimi mwenyewe nakumbuka niko katika *ALAT* sheria ile wakati inapitishwa hapa mimi nilichangia, moja ya masharti ambayo tumeweka katika sheria ile ni kwamba kutakuwa na kapu maalumu ambalo litawekwa kwa kila Halmashauri itakayohusika, kwa hiyo, tatizo ya kwamba hela hizi zinaokotwa na *TRA* kwa maana ya hii sheria mpya tuliyopitisha hapa na kwamba zitakwenda Hazina hazipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano ambayo tumekubaliana ni kwamba zile *municipalities* za Mkoa wa Dar es Salaam yaani Temeke, Ilala pamoja na Kinondoni watakuwa katika akaunti yao maalum. Jambo hili litafanyika kwa muda wa miaka mitano ili tuweze kuona kama linafanikiwa. (*Makofi*)

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, kwa ruhusa yako Mheshimiwa Naibu Spika naomba nitumie nafasi hii kwanza kabla ya kuuliza swali langu, kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Hai kwa kuunguliwa na bweni la wasichana katika shule ya *Machame Girls* jana usiku.

NAIBU SPIKA: Kanuni 151.

Hatua Zilizochukuliwa kwa Wawekezaji Walioshindwa Kuzalisha

MHE. FUYA G. KIMBITA aliuliza:-

Je, ni hatua gani za dhati zimechukuliwa kwa wale wote waliobinafsishiwa viwanda nchini kwa muda mrefu na hakuna walichofanya kwa maana ya kuvifufua au kuzalisha badala yake wamevifanya kuwa maghala na kutumia hati ya viwanda hivyo kuchukua mikopo katika benki?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inatekeleza sera ya mageuzi ya kiuchumi ambayo ilikwenda sambamba na kujitoa katika uzalishaji na uendeshaji wa mashirika ya umma kwa lengo la kuelekeza nguvu katika kutoa huduma za msingi na kujenga mazingira wezeshi ya kufanya biashara wakati sekta binafsi imebakia na jukumu la uzalishaji na kuendesha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wawekezaji ambao hawakufufua viwanda, makampuni yao kutokana na sababu zisizo za msingi, Serikali ilichukua hatua ya kurudisha viwanda na makampuni hayo Serikalini na kuyauza kwa wawekezaji wengine. Mfano kilichokuwa kiwanda cha *Tanganyika Tegry Plastics Ltd.* ambacho liliuziwa wawekezaji Watanzania, kilirudishwa Serikalini na kufilisiwa waliposhindwa kukifufua. Baadaye kiliuzwa kwa mwekezaji mwengine ambaye amekifufua. (*Makofi*)

Aidha, mashamba ya mpira ya Kihuhwi na Kalungwa nayo yalikuwa yamekodishwa kwa Kampuni ya *Mechantile Freighters Ltd.* ya Kenya ambayo iliposhindwa kufufua mashamba hayo yalichukuliwa na kukodishwa kwa kampuni ya *Jumaan El-Ardhi Ltd.* Kampuni ya *Jumaan El-Ardhi* iliposhindwa kuyaendeleza mashamba hayo yalichukuliwa tena na Serikali. Kwa sasa mashamba hayo yako katika mchakato wa kuuzwa kwa wawekezaji wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni mifano michache inayoonyesha hatua ambazo Serikali imekuwa inachukua kwa wawekezaji wasio na sababu za msingi kutofufua viwanda na makampuni yaliyobinafsishwa. (*Makofi*)

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na utendaji wanaoendelea nao pale Wizarani, naomba niulize maswali ya nyongeza madogo kama yafuatayo:-

Kwa kuwa katika Mji wa Moshi kuna viwanda vingi vilibinafsishwa na hadi leo havijafanya kazi katika Mji wa Morogoro, Mwanza.

(a) Je, ni taratibu zipi zinazotumika katika kuwanyang'anya hawa waliobinafsishiwa na bado hawajaweza kuviendeleza hivi viwanda?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuweka viwanda vyetu vyote hapa nchini chini ya Wizara moja inayohusika ambayo tunaita Viwanda na Biashara?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukubaliana naye kwamba viro viwanda katika Miji mbalimbali kama alivyotaja Miji ya Moshi, Morogoro, Mwanza ambavyo havijafufufuliwa pamoja na kubinafsishwa muda mrefu, lakini vile vile naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba viro vingine ambavyo vimebinafsishwa na vimefufufuliwa na vimekuwa waajiri wakubwa na vile vile vimechangia sana katika kodi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotekea kuna sababu za uwazi na za msingi kama hizo ambazo nimezitaja katika jibu la swali la msingi basi ina kuwa kwa Serikali kuchukua vile viwanda au makampuni, lakini inapotokea kwamba kunakuwa na ubishi wengine wanasema tupeni muda kidogo tuweze kuzalisha au kufufua viwanda hivi baada ya muda huo na wengine wanasema tumeshawekeza kiasi fulani cha fedha. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeona kwamba ni vizuri tukatumia utaratibu wa kufanya tathmini ya viwanda vyote katika nchi yetu wanasesma (kupelemba) kuangalia ni viwanda vipi ambavyo tangu tumebinafsisha vimeanza kufanyakazi vipi ambavyo labda tuvisaidie kidogo vitafanyakazi nzuri na vipi ambavyo kwa kweli kabisa hakuna uwezekano wa kufufuka, zoezi hilo limeanza na katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imefanya zoezi katika Ukanda wa Mashariki yaani Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro na kama unavyofahamu Ukanda huo una viwanda zaidi ya asilimia 50 ya viwanda vyote hapa Tanzania, katika mwaka huu wa fedha ambao umeanza kama Bunge lako Tukufu litaridhia na tunaomba iwe hivyo kwamba Wizara yetu ipitishiwe matumizi yake basi tutaendelea na zoezi hilo katika miji mingine aliyoitaja ikiwa ni pamoja na Moshi na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapohitimisha zoezi hilo vile viwanda vyote ambavyo vitathibitika kwamba havijawekeza chochote na hakuna matumaini kabisa ya kuwekeza napenda kumhakikishia kwamba Serikali itachukua hatua kama zile ambazo zimechukuliwa kwa viwanda au makampuni ambayo nimeyataja katika jibu la swali la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mheshimiwa Mbunge, anapendekeza kwamba viwanda vyote vingekuwa chini ya Wizara moja, Wizara mama. Napenda nimtaarifa Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba mamlaka ya kuunda Wizara iko chini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mamlaka ambayo anapewa Kikatiba. Anapounda Wizara yeye ndiyo anafanya maamuzi kwamba maeneo yapi au sekta zipi ziongozwe na Wizara ipi.

Kwa mfano katika sekta ya viwanda utaona kwamba viwanda ambavyo vinashughulika na uzalishaji wa mazao ya mbao viko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni kutokana na kwamba Wizara ile ndiyo ambayo inasimamia kwa karibu kabisa malighafi ambayo inahitajika katika viwanda vile vya mbao. Kwa hiyo, mamlaka ile inafanya vile kwa kuangalia tija na ufanisi wa kazi. (*Makofi*)

Na. 316

Soko la Kimataifa Katoro

MHE. KABUZI F. RWILOMBA aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Isima, Nyaruyeye, Saragulwa, Buzanaki, Magenge vinazalisha mpunga mwingi wa kutosha hata kuuzwa nchi jirani:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuanzishwa soko la Kimataifa kwenye Mji wa Katoro kwa ajili ya uuzaji wa mpunga?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwiomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa masoko ya Kimataifa ni muhimu sana katika kuendeleza zao la mpunga na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali namba 240 uhitaji wa soko la mazao ya kilimo Namtumbo, liloulizwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, ambalo lilijibiwa tarehe 18 Julai, 2008 na vile vile, kama nilivyojibu swali la nyongeza liloulizwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila nilipokuwa najibu swali la msingi namba 251 la Mheshimiwa Jenista Mhagama lililohusu hitaji la soko la Kimataifa mpakani mwa Tanzania na Msumbiji tarehe 21 Julai, 2008, Serikali ingependa kuona kwamba kuna masoko likiwemo soko la Kimataifa Katoro ambalo lingehudumia vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Kabuzi Rwiomba, ambavyo vinazalisha mpunga kwa wingi kiasi hata kuuzwa nchi jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kuwa kama siyo kuwa na uchumi hafifu masoko yote hayo yangeshajengwa kwa sababu tunajua kwamba yangeinua

biashara za mazao (ukiwemo mpunga) ya wananchi wa vijiji hivyo na wananchi kuweza kupata mapato mengi na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Kabuzi Rwiomba na naomba Halmashauri ya Wilaya inayohusika ili kwa pamoja waweze kuibua mradi wa soko hilo na Serikali kwa kupitia Wizara yangu itashirikiana na taasisi mbalimbali za fedha itajihusisha katika kutafuta vyanzo vya rasilimali zinazohitajika yaani utalaam na fedha kutoka nje na ndani ili kuweza kutekeleza mradi huo. (*Makofi*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema tatizo kubwa ni uchumi hafifu. Lakini naamini kutojenga soko hilo au masoko hayo ni kuzidi kuendeleza uchumi uwe hafifu kwa sababu hivi sasa katika eneo la Katoro kuna watu wengi kutoka Uganda, Rwanda, Burundi na DRC ambao wamekwenda hadi mashambani na wanakuja wanatumia fedha zetu wanununa wanachukua badala ya kutumia dola kama kungekuwa na soko. Kwa hiyo, kuiachia Halmashauri na ina shughuli nyingi maana yake ni kwamba ni hizo fedha zizidi kwenda nje badala ya kuwafaidisha wananchi na Serikali. (*Makofi*)

Swali la pili, hapo Katoro kuna biashara kubwa sana na watu wana fedha, tatizo kubwa walilonalo pamoja na fedha zao ni ujambazi na uvamizi ambao unafanyika na kutokana kwamba hawana benki.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaahidi kutusaidia kushawishi vyombo vya fedha vipeleke benki pale ili wananchi waweze kutunza fedha zao? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri nakupa dakika moja tu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba kutokujenga masoko kunaendelea kudidimiza uchumi wetu. Lakini narudia kusema kwamba Serikali ina nia thabiti ya kujenga masoko yote pale ambapo uwezo wa fedha utawezekana. (*Makofi*)

Ninachotaka kumuomba Mheshimiwa Kabuzi Rwiomba na kumuahidi ni kwamba tukutane tutajaribu kumpa msaada pale Wizarani kwetu katika kubuni mradi huo na vile vile tutajaribu kumuelekeza namna nzuri ya kuweza kupata vyanzo vingine vya fedha ili akichanganya na vile vya Halmashauri yake waweze basi kujenga soko hilo ili kuleta maisha bora kwa wananchi wa eneo lile. (*Makofi*)

Kuhusu matatizo ya ujambazi na benki napenda kusema nitawasiliana na Wizara husika tuangalie la kufanya. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali ulipita, tuliliongeza swalii hilo dakika tano kwa sababu ya maswali marefu na majibu marefu.

Sasa naomba niwatangaze wageni tulionao. Kwanza kabisa, kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa. Hawa ni wageni ambao ni timu ya washauri watalaam wa mradi wa kuanzisha benki ya wananchi huko Rukwa. Sasa hawa nitawataja tu pengine na wengine mnawenza kuwatumia. Yuko bwana

Marcus Nzalia, Mkuu wa msafara naomba asimame, halafu yuko Dr. Samuel Kamanyele, Mwenyekiti wa Mradi, mkishasimama mnakaa. Yuko Bwana Peter Alimandusi, Makamu Mwenyekiti wa Mradi, yupo Gabriel Mnyele, Katibu, yupo Bwana Leizumba Aloyce Meneja wa Mradi, yupo Deus Kisisiwe, Mjumbe, yupo Peter Kiatu Mjumbe, yupo Bwana Levo Kashikila, Mjumbe, yuko Bwana Fortunatus Fuema, Mjumbe, bahati nzuri yuko Bi. Desolata Kapoli, Mjumbe. (*Makofi*)

Maana nilitaka kufikiria ni benki ya wanaume tu, kumbe naye yupo huyu. Ahsante sana tunategemea sana mafanikio makubwa ya benki hiyo na mkifanikiwa na wengine wataweza kuiga. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, huyu ni mke na shemeji zake kutoka London. Naomba wasimame, karibuni sana pole na safari. Halafu yuko mpwa wao Radhia Omar Abdallah anayejinga na Chuo Kikuu cha Dodoma. Kwa hiyo, wamekuja ku-families yuko wapi binti hongera sana. (*Makofi*)

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani ni mume wake tunakufahamu sana karibu sana. Halafu yuko mgeni wa Dr. Festus Limbu na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza, yupo Mchungaji Paul Kuzenza kutoka Mwanza, Mchungaji yuko wapi, ahsante karibu, yuko mgeni wa Mheshimiwa John Malecela ni kijana Joakim Tesha, Joakim yuko wapi tunashukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan ambaa ni Mwenyekiti wa Vijana wa Kanisa la KKKT Magomeni Mviringo ndugu Gosbert Latalala na amefuatana na mke wake Bibi Farida Daudi wako wapi hawa siwaoni, ahsante. (*Makofi*)

Halafu tuna mgeni mwagine yupo Mheshimiwa Mbunge Mstaafu bwana Thomas Ngawaiya, karibu sana. Bwawa Ngawaiya ulipokuwepo tulikuwa hatukai humu sasa ndiyo tunakaa na tumekualika uweze kuona ulipokuwepo hapa tulikuwa tunajenga. Kwa hiyo, sasa ndiyo Bunge hili. (*Makofi*)

Matangazo ya kikazi, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa tano asubuhi katika ukumbi namba 432 utaongozwa na naibu kwa sababu Mheshimiwa Jenista Mhagama atakuja mezani. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, ye ye anaomba niwatangazie Wabunge, Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao leo saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofi*)

Halafu nafikiri kuna tangazo lingine hili nadhani muhimu kwa Wabunge wote kwamba Jumamosi tarehe 2 Agosti, tutakuwa na *VIP Race* yale mashindano yetu ya kukimbia kilometra tano kuanzia Uwanja wa Jamhuri. Zoezi hilo litaanza hapo Uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi na vifaa mtapatiwa baada ya kuwasili vinakotoka huko.

Kwa hiyo, mtatangaziwa ni lini mkachukua vifaa. Kwa hiyo, tarehe 2 Agosti, kuna mashindano ya kukimbia Waheshimiwa Wabunge, kilometra tano kwa hiyo, mjiandae kabisa mazoezi siku mbili ili muweze kufanikisha shughuli hiyo. (*Makofi*)

Nimesahau kutangaza wageni wengine bwana Paul Kyala, Mwenyekiti wa Chama cha Sauti ya Umma sijui yuko wapi. Ahsante karibu sana. (*Makofi*)

Kuna wanafunzi na walimu kutoka Kikuyu „D“ shule ya msingi ni kikundi kingine kinaendelea na ziara hapa Bungeni wako 40 wako wapi na walimu wao, naomba msimame na walimu. Ahsante karibuni sana Bunge liko kwenu kwa hiyo, mnakaribishwa wakati wowote ule. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo naomba kusema Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama anipokee kama mliviyotangaziwa mimi inabidi niende kule Jimboni kuna ziara ya viongozi pale na wanakagua jimbo langu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Jenista Mhagama anipokee.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo na utaratibu na mwongozo uliotolewa na Mheshimiwa Naibu Spika, basi sasa tutaendelea na hatua inayofuata. Ninaomba nimuite Katibu ili aweze kuongoza.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji wa hoja ambayo iliwasilishwa jana mezani na sasa nitamuita Mheshimiwa Ramadhani Maneno, ataanza na Mheshimiwa Juma N'hunga ajiandae. (*Makofi*)

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mtu wa kwanza kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nami kama kawaida nianze kuwashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Makamishna wote wa Vikosi vya Ulinzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu na mimi nianze kwenye matatizo makubwa ya nyumba za wafanyakazi kwa maana ya askari. Kwa kweli kwenye vituo vya polisi na kwenye maeneo mbalimbali ambayo wanaishi, wanaishi katika mazingira magumu sana, lakini hata kwenye nyumba ambazo wanaishi kwenye vituo vya polisi ni

nyumba ambazo zimejengwa kwa miaka mingi, hazijafanyiwa ukarabati, hakuna dalili yoyote ya kuziboresha hizo nyumba tangu zilipokabidhiwa na hivyo vituo huenda ni vya miaka 20 au 25 iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hao askari wengine wanaoishi nje ya vituo vya polisi kwa maana kwenye makazi yale pia wanaishi katika mazingira magumu, wengine ni mbali na mahali pa kazi, na sasa imefikia hatua Serikali ilitazame suala hili la kuweza kuwapatia makazi bora angalau na wao wajisikie kama wanafanya kazi kwa kulitumikia Jeshi kwa uadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kuhusu posho, wenzangu wamelizungumzia sana ni kweli askari wanafanya kazi katika mazingira magumu, askari wakati wote wanaitwa kwenye shughuli mbalimbali, lakini inapofikia kwenye malipo yao wanayostahili inakuwa ni matatizo, na wakati mwingine hawalipwi kabisa kwa maana ya kuwaambiwa askari ni mtu wa kujitolea au askari anapoitwa hatakiwi kuanza kukataa, akubali na kulalamika ni baadaye. Hii dhana ya kulalamika baadaye imepitwa na wakati. Pale wanapofanya kazi wapewe haki zao zinazostahili kama wafanyakazi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la kuwapa motisha, yapo maeneo askari wakifanya kazi kwa bidii tunatangaziwa kwenye vyombo vya habari wanapandishwa vyeo au wengine wanapewa hata misaada ya kumuonyesha kwamba kazi aliyoifanya ni ya ujasiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilichokugundua maeneo yanayotazamwa kwenye jambo hili siyo yote katika nchi hii, wabadilike wawaone wote waliotumikia katika jambo hilo au waliofanya jambo kwa ujasiri basi wapate haki kama ilivyo kwa askari wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano huu ninautoa yupo askari mmoja alipambana na majambazi pale Chalinze, aliumia na alipigwa risasi tumboni, lakini cha kusikitisha matibabu aliyo yapata leo hii jeraha lile alilokuwa kuwa nalo linasikitisha kwa kweli. Lakini mpaka leo anapodai malipo yake ya kuwaambia mimi nilijitibu kwa gharama zangu ukiacha zile za Serikali alikuwa anapelekwa kwenye Vituo vya Afya anazungushwa na hatimaye ameanza kulichukia Jeshi la Polisi kwa kuwa kazi hakuna, anaendelea tu kuwepo kazini huku kwa masikitiko makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini basi angepewa hata ukoplo, ameona isitoshe kazi aliyoifanya basi hata hiyo zawadi ya ukoplo nayo mpeni kwani ule ujasiri aliyoufanya wa kupambana na wale majambazi wa kuweza kuokoa hata lile gari lililokuwa limeibiwa Dar es Salaam lakini umuhimu huo hawajauona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije suala la doria, kila siku nazungumza hapa Bungeni, Jimbo la Chalinze jamani ni kubwa. Jimbo la Chalinze linastahili lipate Wilaya. Nazungumza hivyo kwa sababu gani, Kituo cha Polisi Chalinze ni kikubwa lakini

doria inayofanywa pale Chalinze na wale askari kwa kuelekea Dar es Salaam mpaka Ruvu, kwa kuelekea Morogoro mpakani mwa Morogoro pale Bwawani, lakini hatimaye kuelekea mpakani mwa Tanga sehemu moja inaitwa Manga, lakini pia mpakani mwa Turiani kwa maana ya Morogoro kwa upande wa Kaskazini. Kwa kweli eneo ni kubwa sana wanaloofanya kazi kwa wakati wa doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha kwa kazi hiyo yote wanayofanya kupambana na wahalifu na hasa wa kuweka magogo usiku na kuteka magari, gari waliyokuwa nayo pale ni moja, lakini mafuta wanayopata kufanya kazi hiyo yote ni lita 600 kwa mwezi, inafikia kipindi mafuta yanakwisha mapema kabla ya mwezi haujaisha. Sasa Mkuu wa Kituo cha Polisi pamoja na askari wake wanatumia njia zipi za kuweza kupata mafuta na hatimaye kazi hiyo iweze kufanyika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha katika hali hiyo kila siku wanapopatikana watuhumiwa kwa ajili ya kuapeleka Kigongoni kwa maana ya Bagamoyo wanatumia lita 50 kwa ajili ya kazi hiyo hiyo. Sasa umefika wakati wale mahabusu au watuhumiwa ambao wanapatikana basi Serikali ichukue hatua wapelekwe Ubena ambapo ni karibu zaidi kuna Gereza kuliko kuapeleka Kigongoni ambapo ni mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lita 600 kwa mwezi anazopewa huyo Mkuu wa Kituo cha Polisi kwa kazi hizo zote nilizokwisha kuzieleza. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake mafuta yale ni kidogo mno kufuatana na kazi ile wanayoifanya. Inafikia mahali sasa wanaamua kuingia mitaani kutafuta mafuta au kwa kuzoeana na wafanyabiashara wawape mafuta kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, uadilifu wa Jeshi pale unaondoka na hatimaye kazi haiwezi kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nyongeza ya mafuta ipatikane na hili la mafuta ninalizungumza asiponipa majibu ya kuridhisha Mheshimiwa Waziri juu ya jambo hili hata mimi wakati wa Kamati ya Matumizi naweza nikawa mkorofsi kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri alielewe pamoja na hizo lita 600 nilizozizungumza leo yapata miezi miwili hata lita 10 ya mafuta hajapelekwa pale Chalinze, lakini huduma hizo zinaendelea sasa. Sasa ajiulize Mheshimiwa Waziri yule Mkuu wa Kituo cha Polisi yale mafuta anayapata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nieleze suala la upangaji wa kazi, imefika mahali wakubwa hawawatendei haki wadogo. Upangaji wa kazi hauendani na mazingira jinsi yalivyo ya wale wafanyakazi waliopo. Wapo askari wengine tangu waajiriwe wao ni kusindikiza mahabusu tu na wapo wengine tangu waajiriwe wao ni kukaa benki, lakini wapo askari wengine tangu waajiriwe wao ni kwenda kwenye *road block* kwa maana ya barabarani mle wanapoweka mageti ya usiku. (*Makofi*)

Sasa haya yanaleta utata mkubwa na wengine kulalamika yupi anayestahili kwenda barabarani kwenye mageti na yupi anastahili kulinda Benki au kwenda Mahakamani kusindikiza mahabusu kila siku. Hili naomba litazamwe, linaleta

uchonganishi mkubwa kati ya wafanyakazi wa ngazi ya juu na wale wa ngazi ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine hili la vidhibiti kwa maana ya kwamba mtuhumiwa anapokamatwa na gongo au na bangi, lakini anapokwenda Mahakamani mtuhumiwa ni lazima aambiwe kwamba unashitakiwa kwa kosa labda la kukutwa na bangi au kosa la kukutwa na gongo, atasema tu jibu ni hapana. Lakini cha kusikitisha kile alichokamatwa nacho siyo kile kinachofika pale Mahakamani, kama ikiwa ni lita kumi za gongo alizokamatwa nazo zinaweza kufika Mahakamani lita mbili. (*Makofi*)

Sasa kwa sababu ni utamaduni lazima pale atasema ni hapana kwa shitaka lake hawezi akauliza lita zangu zingine nane zimekwenda wapi? Kwa hiyo, tunaomba kupata ufanuzi vile vidhibiti wenzetu huwa wanavipeleka wapi pamoja na wenzangu wamechangia na fedha wanazozikuta kwenye matukio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko mengi yanapotokea matukio barabarani hasa ajali za barabarani na askari wanapofika kuokoa, lakini vitu vile wanavyovikuta hatimaye havifiki kama inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la magari ya kukokota kwa maana ya *breakdown*, mwenzangu Mheshimiwa Abbas Mtemvu alilisema jana. Kwa kweli yale magari yanaskitisha, yale magari ni mabovu, yale magari yanapokwenda kwenye ajali kwanza yenewe yanafukuzana na yanaweza yakasababisha ajali, lakini habari zilizopo yale magari kwa namna moja au nytingine askari wanahusika kuyamiliki yale magari. Lakini yale magari inafikia mahali kabla hajaenda kwenye tukio, yenewe yanaanza kusukumwa askari akiwemo. Sasa ni jambo la kusikitisha na kuona kwamba gari mbovu linaenda kuchukua gari mbovu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha gari likifika pale hata kama wewe gari lako linastahili kwenda lenyewe mpaka Kituo cha Polisi askari watalazimisha ivutwe ili mradi mkishafika huko biashara ya namna moja au nytingine inafanyika. Tunaomba jambo kama hili kwa kweli lisiendelezwe tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni la dawa za kulevyta. Kwa nini inafikia mahali mshitakiwa anatoka gerezani akafika Mahakamani amelevya. Sasa ulevi huo kaupata saa ngapi wakati pale yupo kwenye ulinzi wa Askari Magereza na anasindikizwa mpaka Mahakamani. Kwa hiyo, hali halisi kabisa Jeshi la Polisi au Magereza linapata dosari kwa maana ya baadhi ya hizo dawa za kulevyta yanapitishwa ndani ya Magereza. Jambo kama hilo ni hatari na haliwezi kuleta mazingira mazuri ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la hati za kusafiria. Sasa hivi tuna utaratibu wa kutengeneza vitambulisho vya uraia, lakini matatizo yaliyopo kwenye hati za kusafiria yanaweza pia yakajitokeza kwenye vitambulisho hivyo vya uraia. Kwa kweli hati za kusafiria kwa asilimia ndogo au kwa asilimia kama 20 au 30 pia baadhi ya

wageni wanazo hati zetu za kusafiria. Ni jambo la hatari sana na hili watu wa Uhamiaji wanalelewa, kwa kweli Kitengo cha Uhamiaji hakina umakini wa kutosha juu ya utoaji wa hati za kusafiria. Wageni wengi waliopo hapa nchini wametengenezewa uraia kwa kupewa hati za kusafiria za Tanzania. Kwa hiyo, hili nalo naomba Mheshimiwa Waziri alitazame kwani linaweza likawa pamoja na hili suala la vitambulisho vyta uraia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho jana wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha hotuba yake ameeleza wafungwa amba walitolewa kwa maana ya kufungwa kifungo cha nje. Mkoaa wa Pwani una magereza mengi sana, lakini pale kwenye orodha yake nimeona Mkoaa wa Pwani ni *zero*. Sasa hivi kweli utaratibu upi walioutumia katika wafungwa wote waliofungwa katika Mkoaa wa Pwani katika magereza yote hawakupatikana hata mfungwa mmoja wa kuweza kupata hali hiyo ya msamaha wa kifungo cha nje? Hili nalo nitaomba kupata ufanuzi ili niweke sawa katika rekodi yangu ya Ubunge katika kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja hii ila nipaye ufanuzi kwa yale ambayo nimekuwa nimyaeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ramadhani Maneno, naomba sasa nimuite Mheshimiwa Juma N'hunga na Mheshimiwa Mariam Mfaki, ajiandae.

MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii asubuhi pia nikuombee Mungu kwamba kazi hiyo unayoifanya ya Uenyekiti na ukikaa hapo kwenye kiti tofauti na wengine wewe hicho kiti unajaa. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani yeze na Naibu Waziri wake, mimi ningesema watu wawili hawa wananiwa ule mfano wa Mwenyezi Mungu alipompa utume Musa maana Waziri ni sawa sawa na Musa na Naibu Waziri ni sawa sawa na Haruna. Maana Waziri anashughulika zaidi katika utekelezaji lakini Naibu Waziri ni msemaji mzuri sana wa Wizara hii. Akisema hapa Bungeni, Bunge linaburudika. Niwaombee kila la kheri katika kazi hii ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeteuliwa kuwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ningekataa kuteuliwa hii Wizara maana nimekaa mimi miaka 22 karibu Mawaziri wengi waliogusa Wizara hii walikuwa na misukosuko hawakutoka salama. Wengine walionitangulia kama Mzee Mwinyi alilazimika kujiuzulu katika Wizara hii hii na Mawaziri wengine si vizuri kuwataja. Ni vema niwaombee dua hawa waliokuweko na mimi pengine nimuone mmoja ni Musa na wa pili Haruna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ningependa kulisema ni tatizo la jimbo langu la Dole. Katika Jimbo langu la Dole kuna Ofisi ya Makao Makuu ya Polisi ya Mkoa wa Kusini. Hii ofisi imejengwa kabla ya Waziri hajazaliwa, hata wewe mwenyewe Mwenyekiti hujazaliwa maana imejengwa kwenye miaka ya 1961 na hajakarabatiwa hii ofisi mpaka hivi leo. Safari hii katika orodha ya kukarabatiwa ofisi hii haimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasikitisha sana, nimekuwa nasimama naliulizia hili jambo, nafanya mawasiliano na Mawaziri mbalimbali, wanajibu maneno mazuri na leo watanijibu mazuri. Lakini mimi Mheshimiwa Waziri nilitaka niwatoe wasiwasi Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mimi simo katika watu ambao watawachachafya. Lakini kiuungwana tu wanijibu kiungwana, basi wachepue kiasi fulani wafanye ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Mwera, Ofisi ya *RPC* wa Mkao wa Kusini Unguja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni utendaji wa jeshi la Polisi. Lazima nikubali na nikiri kwamba jeshi la polisi linafanya kazi vizuri sana. Jeshi la polisi linafanya kazi na zana duni, vifaa vichache, lakini hali ya maslahi yao ni mbaya na mishahara midogo. Posho hazileweki, makazi yao mabaya kupindukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivi sasa kama utaongozana na Mheshimiwa Waziri uende hapo Ofisi ya *OCD* mbele yake utakuta kuna mabanda pale yamejengwa ya mabati, hao ni askari wa muda wanaokuja kwa sababu ya Bunge. Lakini wale askari wa kudumu wanaishi hapo hapo nyuma Dodoma, basi utawahurumia, wanaishi juu bati, chini bati na familia zao zimo humo na hiyo hali siyo hali ya hapa Dodoma tu, ni hali ya Dodoma na sehemu nyingine za Tanzania. Hebu amueni hawa vijana wanaofanya kazi nzuri kuwahakikishia kuwa wanakuwa na makazi mazuri. Kama hilo gumu ni vizuri basi twende katika utaratibu wa pili, maana hawa wengi wao hata wakistaafu, ukipishana nao njiani baada ya muda mchache basi unaweza kuwakimbia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ama sijui hao ma-*RPC*, Makamishna, wengine wanapostaafu wanarudi katika kazi ama ya kilimo ama kwenda kuza gongo. Inasikitisha sana, sasa ni vema basi maandalizi ya askari hawa na viongozi kuhusu suala la ujenzi wa nyumba zao binafsi viandaliwe. Tuwe na utaratibu wa kuwapa mikopo mapema, mikopo ya ujenzi wa nyumba za askari. Kwa mfano hapa Dodoma nimesikia sasa hivi kwamba Waziri alikuwa anasema kwamba kutapimwa viwanja 10,000. Hivi kwa nini katika hivyo viwanja 10,000 polisi wasipewe viwanja 200? Na wao wenyewe wakapatiwa utaratibu wa kukopa Benki wakajenga nyumba zao hapa. Hata kama mtu atahamishwa lakini atabaki na nyumba Dodoma, atakapomaliza shughuli zake atawenza kuishi Dodoma. Lakini mtu anafanya kazi miaka 32 anatoka nyumba hii anaingia nyumba nyingine anatoka nyumba nyingine, mpaka siku ya mwisho amemaliza kazi nyumba hana, hana pa kuishi, amestaafu, marupurupu machache, maslahi machache, basi anakufa kihoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawatunza hawa, tunawasifu vizuri, maana yake nini? Jeshi ndilo linalotegemea katika suala zima la usalama na amani. Jana nilikuwa

nasikia mmoja anasema Karagwe kule wanawategemea sana. Kuna majambazi, hapa Dodoma majambazi, Dar es Salaam majambazi. Lakini wakati mwinge vijana hawa hawa wanaojitoa mhanga katika kupambana na majambazi utashangaa sana, maana yule wa Dar es Salaam aliyepambana na majambazi pale tulisikia kwamba aliongezewa cheo badala ya kuwa *Private* akawa Koplo. Wewe binadamu anataka kupambana na watu basi unamwongezea ka-elfu kadogo tu. Usimpe motisha hasa akaondoka pale akajulikana kwamba huyu kweli kajitolea. Ni vizuri wale wanaojitolea kupambana majambazi wapewe vyeo vinavyoonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hizo ndiyo sifa za jeshi la polisi. Lakini jeshi la polisi kuna dosari, kuna upungufu na huo upungufu kila siku ukienda basi Watanzania au baadhi yao wanakuwa na mashaka na jeshi zima kumbe kuna wachache. Jeshi hili la polisi limebahatika sana lina Mkuu wa Polisi anayetwa Saidi Mwema, yeze kazi yake kufanya wema tu. Niliwahi kumshuhudia Hakimu mmoja kule Zanzibar aliteuliwa na Mzee Karume, akakaa kwa muda wa miaka mitano, alishindwa kumfunga mtu jela. Kila akienda yeze *dismiss case*, anamlipa faini yaani ya moyo wake ulivyo. (*Makofi*)

Sasa na Saidi Mwema ukimwona *IGP* alivyo, Mungu ampe maisha marefu na kazi nzuri. Unamwona kabisa kwamba huyu ni mtu mtaratibu. Ni mtu mwenye heshima, anayeshimu watu wote, si mtu vurugu mech. Anafanyakazi kitaalam. Namtakia afya njema na kazi nzuri. (*Makofi*)

Lakini chombo alichopewa, baadhi yao si watu wazuri, wamehusika ama wanahusika katika mauaji na baadaye wanatangaza kwamba watu waliofariki ni majambazi, ni dosari kubwa sana. Tunapata wasiwasi sana katika mlolongo mzima kwamba eeeh, hivi kweli hawa wote wema ama wengine wana kasoro kubwa, hawa wenye kasoro wanashughulikiwa namna gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usipokisafisha hiki chombo basi bado Watanzania imani zao ni ndogo na ndiyo tegemeo. Jeshi hili lina doa kuhusu suala la rushwa. Kila Mtanzania anamwona *traffic* tu akienda akiwa ana kitambi hata kama cha maumbile anasema huyo anakula huyo. Hata kama huyo hakuhusika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa usipolisafisha jeshi hili bado kuna matatizo. Namshukuru sana Mheshimiwa *IGP* na Waziri wamejithidi kufanya uhamisho wa hapa na pale lakini bado tatizo lipo. Ushauri wangu ni kwamba la leo litengenezwe leo. Nakumbuka mwaka 1982 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikuwa anasema, mtoto ukimpa wembe unamkata pale pale. Kwa hiyo, maumivu wanayapata pale pale. Hawa watu wote waliohusika katika mauaji, kusingizia majambazi na kila kitu hawa lazima washughulikiwe mapema na watangazwe hadharani kwamba wamefanya hivyo. (*Makofi*)

La pili, hili jeshi la polisi kwa kutegemea TAKUKURU kwamba ndiyo itawasadidua kukomesha rushwa hata siku moja haitakomeshwa. Ni lazima jeshi lenyewe liandae chombo chake cha kudhibiti suala la rushwa ndani ya jeshi. Hivi leo unaondoka hapa kwa basi sisi tunabanda mabasi unakwenda kituo cha usoni hapo, dereva

anasimamishwa, anashuka dereva na kondakta wanarudi nyuma kule, wanafanya mazungumzo, wakimaliza wanasema tumekwisha weka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli akiwemo mtu mwininge anayekusudia kushughulikia mambo ya rushwa atamkamata yule? Hivi rushwa inayotumika hapa kwa kuwapa hawa sijui matrafiki, watu gani, aliyejewa haijui nani nchi hii?

Hivi akipokea rushwa, mazingira yake na mshahara wake na uwezo wake, nani anayekuwa hawesi kumjua kwamba huyu kwa kipato chake hana. Maana hakuna askari hata mmoja mfanyabiashara aniambie kwamba leo kuna Kamishna mmoja kazi yake anaendelea kufanya biashara. Lakini leo unamkuta yeze ana mapato zaidi ya mshahara wake kapata wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mambo ya kushughulikiwa. Namshukuru sana Waziri amesema moja katika kasoro ya jeshi hili lina mtindo baadhi ya maeneo kuwabambikizia watu kesi. Wanaobambikiziwa ni wanyonge. Mheshimiwa Waziri kwa bahati nzuri yeze anatoka Mkoa wa Mwanza, huko ndiko kwenye matatizo makubwa sana, anabambikiziwa mtu kesi, anayefuga ng'ombe 500 anatakiwa lazima achague ng'ombe wake apeleke huko kwa wakubwa ili kesi isiende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri hapa Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga ametoa mfano mmoja tu na wewe, kumbe mko wengi, sasa nyie mnatoa mifano midogo midogo na hawa Wamasai hivyo hivyo. Hata kule tulikokwenda kule, kule walikohamishwa wafugaji kule. Kule kumefanyika na mambo makubwa sana kule. Wafugaji wamenyang'anya mifugo yao kwa kubambikiziwa kesi. Sasa mambo haya ni vizuri yakasafishwa ili wananchi wakaondokana na jambo hili, wala si sababu ya kuogopa mtu. Hatuwezi kuendelea na watu ambao wao kazi yao ni kuwabambikizia kesi ni chombo hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki cha polisi kilikuwepo kabla ya Uhuru, kilirithiwa na Waingereza walipokuja hapa walimkuta Mjerumanii. Chombo cha polisi wakati ule kazi yake ni kuangalia utawala wa Kiingereza, kilikuwa hakimthamini Mwfrika au Mtanzania au Mtanganyika wakati ule. Kwa hiyo, rafiki yangu Kombe ukikamatwa kitu cha kwanza kutiwa mkong'oto. Ndiyo na mpaka leo bado wenzetu wanaongoza jeshi hili la polisi mawazo yao mengi yako hapo katika kutia mkong'oto. Ndiyo maana baadhi ya watu wanapoteza maisha, lakini hawana kesi, hawana hatia. Sasa chombo hiki kisipogeuzwa kikaondoka katika utaratibu huo wa kikoloni ikaja katika utaratibu wa kisasa ambao kinamkamata mtu na kumfikisha katika Mahakama na kuhukumiwa huko usoni Mheshimiwa Mwenyekiti kutakuwa na kesi nyingi sana za madai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeliona hili, tumeambiwa Jenerali Kombe, alipigwa akidhaniwa jambazi *White*, Kumbe ni Jenerali alikuwa na kesi imepelekwa Mahakamani. Tumeona juzi juzi wameambiwa majambazi kule Sinza wamepoteza maisha. Hapa nina orodha ya watu wengi wa mwaka 2006 ambao wamepoteza maisha katika mikono ya polisi. Jambo hili ningeshauri sana likaondolewa kwa haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la uhamiaji. Hawa watu wa uhamiaji ni yatima. Mtu wa uhamiaji unaweza ukamwona ana vyeo vimeanzia hapa mpaka mwisho. Lakini mshahara wake huyo ni sawa sawa na koplo wa polisi, inasikitisha sana. Hebu angalieni maslahi ya watu hawa na mishahara yao na wao iendane. Nafahamu watu wa Uhamiaji na watu wa Polisi wakati mwingine wanachukua mafunzo pamoja. Lakini wakiondoka pale tu basi, zile mbwembwe za vyeo za uhamiaji hazifanani hata kidogo na hali halisi. Sasa tunachotaka pale nini, wasichukue rushwa? Watachukua mlungula, watachukua rushwa. Watauza *passsport* kwa sababu mapato yao hayalingani, hayawasakiidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri suala la maslahi ya watu wa Uhamiaji yazingatiwe. Ningeomba sana upandishwaji wao wa vyeo na wenyewe uzingatiwe. Lingine ambalo nitalichangia kwa haraka haraka ni uraia wa nchi mbili. Mimi kwa mawazo yangu wakati muafaka kwa Watanzania kuwa na uraia wa zaidi ya nchi mmoja haujafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma N'hunga, na wewe kwa kweli ni Mbunge wa muda mrefu sana ndani ya Ukumbi wa Bunge. Unanukia kwenye Useneta kwa namna fulani. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mariam Mfaki, halafu Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi ajiandae. (*Makofi*)

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia yale ambayo naona kwamba naweza nikayasemea. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote kuwa hai na kukutana siku ya leo ndani ya Bunge letu hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP* na *RPC* wa Mkoa wa Dodoma. Nitakuwa si mwangi wa fadhila kama nitashindwa kumshukuru ye ye binafsi Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ni kijana mpole, mchapakazi na kwa kweli ameonyesha umahiri kwa muda mfupi tu baada ya kukabidhiwa wadhifa huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile niwahabarische wapiga kura wake wa Jimbo la Mwanza Mjini kwamba wanaye Mbunge ambaye ni msikivu, anasikiliza malalamiko ya watu na anayashughulikia kwa muda mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo ulinisikiliza na ukaifanya kazi kwa muda mfupi. Nakushukuru sana na naomba wapigakura wako wakupe ushirikiano wa kutosha ili uendelee kuchapa kazi za nchi hii. Namwomba vile vile nimshukuru *RPC* wa Dodoma kwa kazi nzuri anayoifanya na kwa kweli kwa kushirikiana na wenzake ndiyo maana mnaona

Waheshimiwa Wabunge mkiwa hapa Dodoma hampati bugudha ya aina yoyote. Kwa hiyo, naomba aendelee na kuchapa kazi hivyo na aendelee si kwa sababu tu ya Wabunge lakini naamini yeche na mchapakazi wa siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mimi niendelee na suala la ujenzi wa vyuo. Wameeleza kuwa Dodoma watajenga Chuo cha Upelelezi. Mimi nasema sisi wa Dodoma tukisikia vitu vipyta vinakuja kwa kweli tunawashukuru sana sana. Tunajua mji wetu utaendelea kuboreka na shughuli zetu na wananchi wetu wataendelea kufaidika kwa biashara zao na mambo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameeleza vile vile wataendelea kupanua vyuo vya Moshi, Kidatu na Dar es Salaam, vyuo vitatu. Mimi ningeomba katika kupanua vyuo hivi basi wajitahidi kuchukua wanajeshi wengi ili waweze kupata mafunzo. Wanajeshi wengi wa kuanzia cheo cha sajenti na kurudi chini mara nyingi hawapati mafunzo ya mara kwa mara hasa wale ambao hawana vyeo na inawezekana ni kwa sababu tu vyuo hivi vinachukua wanafunzi wachache. Sasa mimi niwaombe kabisa ili waweze kufanya kazi zao vizuri hawa ambao ni wa vyeo vya chini waendelee kupatiwa mafunzo na waweze kuwa wataalam wa kutosha na waweze kupambana na shughuli za kulinda wananchi na mali zao kama ilivyo sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo wanayoyapata nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba watawapeleka mafunzo upande wa Uhamiaji vijana 134 watumishi na polisi 140. Nadhani hawa ni wa vyeo vya juu. Mimi kwa kweli najikita kwa wale ambao ni wa vyeo vya chini na ambao ndiyo wachapa kazi ndiyo wanaokimbizana na majambazi, ndiyo wanaofanya kazi kubwa siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe *IGP*, Mheshimiwa Saidi Mwema, jeshi hili linakuwa hai kwa sababu hawa wa chini wanachapa kazi. Ingekuwa hawafanyi kazi mimi nina uhakika pengine mambo yangekuwa siyo mazuri. Kwa hiyo, naomba nimwombe sana awaangalie na awape nafasi za kutosha na hata kuwapandisha vyeo mara kwa mara na kuwapeleka kwenye mafunzo ili waweze kuelimika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine ambalo nilikuwa nimesoma katika kijitabu kidogo na ambalo tayari limeelezwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, kuhusu suala la polisi jamii. (*Makofi*)

Mimi suala hili nimelielewa vizuri na kwa kweli kama tunataka hali ya amani na utulivu iendelee kuwepo nchini ni kushirikiana na mafunzo haya yanayotolewa yanayohusu elimu ya polisi jamii, na niombe Wizara kitengo hiki kiwe ni kitengo maalum ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo kwa wananchi, kuanzia vijijini, mijini na maeneo yote. Mimi nimesoma kijitabu fulani kimeandikwa na Mheshimiwa *IGP* kina maelezo mazuri sana. Yale maelezo yangepaswa yawafikie wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwaombe basi kile kijitabu kichapishwe na kiendelee kutawanywa katika nchi yetu. Kinazungumzia juu elimu ya polisi jamii. Wananchi wakishaelewa nina uhakika watashirikiana na polisi na hapatakuwa na tatizo

lolote. Mimi naamini wananchi wakishirikiana vizuri na polisi hali itakuwa nzuri sana. (*Makofi*)

Naomba nizungumzie suala la mishahara, posho, usafiri na nyumba kwa ujumla. Hivi vitu vikiboreshwu jeshi letu litaboreka sana. Askari anapofanya kazi zake akirudi nyumbani akapata mahali pazuri pa kulala siyo pa kubanana, sio baba anakuja saa sita za usiku inaanza tena heka heka ya kuhamisha watoto, inakuwa sasa ni tatizo. Hebu jamani, tufikirie sisi ni binadamu sote. Dodoma tunazo nyumba kama hizo. Bado kuna nyumba zinaitwa *full suit* hizo za mabati, zipo pale kituo cha Polisi kwenye *Police Quarter*. Halafu kuna nyumba nyingine kule karibu na hospitali, vijumba ni vidogo sana, jamani hawa ni wenzetu, Serikali ijue hilo. Hawa ni wachapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uhakika kama vitu hivi vitashughulikiwa vizuri, mishahara ikawa mizuri, hawatakula rushwa. Kwa habari nilizonazo mtuwie radhi mengine tunayasikia, ni ya kusikia, sisi hatuna uthibitisho kwamba hata hiyo rushwa wanayokula wala siyo kubwa. Kwa mfano hawa wanaozungumzwa polisi wa barabarani, ni shilingi 2,000/= tu akifika pale anapewa shilingi 2,000/= anahesabu magari yake kumi kwa siku anapata shilingi 20,000/= zinatosha kwa kulisha watoto wake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yasingeweza kufanyika kama Serikali itawalipa mshahara mzuri. Kuhusu posho ambazo wanastahili za chakula na vitu vingine, hivi navyo hebu zipelekwe basi kwenye mishahara yao moja kwa moja badala ya kusubiri Mkuu wa Kituo aamue leo kuwapa ama kutokuwapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba haya yaangaliwe, wapatiwe usafiri na wapatiwe nyumba nzuri. Mimi nina uhakika jeshi likitunzwa vizuri, ni vyombo viwili katika nchi hii vikitunzwa vizuri ni Polisi na Mahakama. Kama vitawekwa katika hali nzuri hapatakuwa na majambazi, hapatakuwa na rushwa, hapatakuwa na chochote kibaya. Kwa sababu anapata hela ya kujilisha ye ye mwenyewe, anapata hela ya kujikimu ya kutosha, anapata kila kitu kizuri. Sasa anakula rushwa ya nini? Si kudhalilisha jeshi? (*Makofi*)

Mimi nimwombe Mheshimiwa *IGP* kama kuna wachache wanaoharibu sifa ya jeshi na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, hebu hawa wachache ndiyo wa kushughulikia. Wakati mwengine tunakaa tunalaumu, polisi, polisi, polisi, kumbe wapo wachache. Kwa hiyo, hawa wachache ndiyo wanapaswa kushughulikiwa tena haraka ili waweze kufanya jeshi letu liende vizuri, wafanye kazi vizuri. Lakini vile vile kwa kuboresha haya niliyoyasema, bila ya kuboresha kwa kweli hawataacha kupokea rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia juu ya suala la majambazi. Sisi Dodoma hatuna mapori ya kutisha, tunalo pori moja tu ambalo linatusumbua, pori la Mtungutu barabara ya kwenda Kondoa na polisi wako pale. Sasa mimi huwa naijiliza, mwaka jana au mwaka juzi nilichangia, nikauliza hivi wale polisi wanaopelekwa kule wana bima? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana wamejenga vijumba vya kujijengea, sijui ni wao wenyeewe, sijui ni vipi ndiyo wanalala mle ndiyo wanashinda mle, hivi kweli pale ndiyo pa kushinda askari? Wakinokewa na majambazi, hivi kweli kutakuwa na usalama kwa askari hawa? Hakutakuwa na usalama. Sasa mimi nikuombe Mheshimiwa na niiombe Serikali kwamba vitu kama hivi basi polisi wanaopelekwa pale angalau wawe na bima. (*Makofi*)

Vile vile hili pori si kubwa sana, sidhani kama zinatika kilometra 15. Lakini vile vile ni vizuri ikatafutwa, ufanywe utafiti wa kutosha, hawa majambazi wa kapori kadogo tu hawa wanatoka wapi? Inawezekana labda pengine ni wenzetu humu humu. Watafutwe, waangaliwe na washughulikiwe kikamilifu. Nalisifu jeshi linapowashughulikia majambazi kikamilifu. Siwezi kusema ni nini lakini kwa kweli linatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la magereza ya Msalato. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba wanapata hela kutoka kwa wafadhili ili waweze kuendelea kupanda miti pamoja na magereza mengine nchini. Ni kweli panahitaji kupandwa miti lakini mimi nadhani hela hizo mkipata za kutosha basi pawe na uzio wa ukuta. Sasa lile gereza limebaki tu utafikiri kijiji cha watu fulani fulani hivi, hutaamini kwamba ni gereza. Utafikiri ni kijiji, kakitongoji fulani hivi, mimi niombe tu kwamba hapo napo ni mahali ambapo panahitaji kushughulikiwa, pajengwe ukuta wa kuzunguka na askari waweze kuwa na mahali ambapo wanaweza wakafanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia tena kuhusu suala la uhamiaji. Sina uhakika, hizi Ofisi za Uhamiaji ziko katika kila Mkao au ziko baadhi ya Mikoa na Wilaya au vipi, lakini mimi nasema Uhamiaji wa Mkao wa Dodoma wako pale juu pale tunaita jengo la wanauzwa magazeti ya *Daily News* na magazeti mengine pale, sijui ni chumba kimoja au viwili. Lakini mimi nadhani Dodoma sasa si mahali pa kuweka Ofisi ya Uhamiaji nyepesi kiasi hicho. Ni vizuri muone kwamba mji wa Dodoma sasa hivi ni tofauti na huko tulikotoka, Mheshimiwa Waziri. Ni vizuri ofisi ijengwe tena yenye heshima ya Uhamiaji Mkao wa Dodoma. (*Makofi*)

Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu wakati anajibu swalii alitaja vyuo ambavyo vitaendelea kujengwa na vinavyojengwa Mkao wa Dodoma. Vyote hivi vinatajwa na idadi ya watu watakaishi Mkao wa Dodoma. Mambo haya yote kwa kweli yanahitaji huduma za aina zote ziwepo Dodoma. Kwa hiyo, mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri kama wazo lilikuwa bado halijaja kwamba Dodoma bado ni ile Dodoma ya zamani, hapani. Dodoma ya sasa ni Dodoma ambayo imebadilika na kwa kweli inahitaji kila anayekuja kuwekeza hapa Dodoma au kujenga ofisi akubali kwamba lazima ajenge ofisi inayofanana na Dodoma ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba vile vigeo nizungumzie suala la madereva. Sina uhakika vyuo vya madereva viko vingapi. Mimi nakijua tu kile cha Dar es Salaam wapi pale sijui. Niombe tu kwamba ni kweli ajali nyingi zinasababishwa na madereva ambao pengine si wataalam wa kutosha. Niiombe Wizara na niiombe Serikali

iangalie utaratibu wa kupanua vyuo vya madereva na vile vile inawezekana kabisa kwamba katika eneo la *traffic* wanaweza kufanya utaratibu angalau wa kukutana na madereva baada ya muda fulani ili angalau kuwapiga msasa waweze kuelewa kwamba wanahitajika kufanya kazi yao vizuri. Naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taaluma nzuri na ni taaluma ambayo kwa kweli ni muhimili wa maisha ya binadamu, kwa sababu dereva akiwapakia watu 60, 30, 20, wanategemea yeye ndiye atakayeliendesha hilo gari wafike salama. Sasa watu kama hawa sio wa kuwaacha hivi hivi ni vizuri wafanyiwe utaratibu ni jinsi gani ambavyo watashughulikiwa kupewa wajibu wao, kukumbushwa kazi yao na kuwafanya mambo ambayo kwa kweli ni ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu nisisitize juu ya suala zima la maslahi ya askari wa chini ambaao ndio wachapa kazi, ndio wanaohanganika, ndio wanaolifanya jeshi liwe na sifa nzuri. Kwa hiyo, unajua watu wanasema kwamba polisi ama jeshini, ukitaka ulione jeshi liwe zuri au watendaji wa jeshi ni wazuri, uwe na cheo cha juu. Lakini ukiwa na cheo cha chini ni kwamba kama vile hawathaminiwi, kwa hiyo, mimi niwaombe ma-*OCD*, ma-*RPC*, na viongozi wenye vyeo vya juu jeshini polisi wawathamini hawa wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kana kwamba hawawezi kujibu, ni zile sheria ndizo zinazowafanya washindwe kujibu kwamba ni lazima useme ndio kama una swali utakuja kuuliza baadaye, lakini si kweli kwamba atakuja kuuliza, hawezi kusimama mbele ya Mkuu wake akamuuliza swali, sio rahisi, ngumu sana. Lakini niwaombe tu kwamba mjue na wenyewe ni binadamu wanahitaji upendo wenu, wanahitaji huduma zenu na wanahitaji ushirikiano wenu ili waweze kuafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niliyoyaweka kuzungumzia, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mariam Mfaki, na kwa kweli leo umeanza na sifa lukuki kwa Mheshimiwa Waziri, nadhani sifa zile zimemfikia na zitampa moyo wa kuhitimisha hoja yake leo jioni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Mariam Mfaki, naomba nimuite Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan, ajiandae. (*Makofi*)

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo yale yanayojiri katika Wizara hii. Na mimi sitakuwa mbali na wenzangu waliozungumza hapo awali japokuwa kurudia sio vizuri, lakini na mimi pia nina maelekezo yangu kidogo nitayaeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maslahi ya jeshi la polisi na magereza. Hili limekuwa ni tatizo la kila mwaka tangu mimi niingie hapa tunalizungumzia. Mimi naliona limekuwa kama mamba ambaye anambana binadamu halafu huku jicho moja

anatoa machozi. Kwa sababu mpaka sasa hivi hatujaona hata ule ufumbuzi wa hili jeshi la polisi na magereza kupatiwa kile kinachohitajika. Naishukuru Wizara imejaribu kurekebisha mambo fulani fualni lakini bado haitoshi na nawaomba waendelee na ninawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau wa michezo na kwa kipindi cha nyuma nimewahi kufanya kazi na jeshi la polisi, magereza, kwa sababu katika mikoa hawa watu wako wengi sana na ndio wanamichezo waliopo na nina mazoea nao kiasi kwamba hata kwenye maeneo yao nimekuwa nikipita, kwa kweli nyumba zao zinasikitisha sana. Nimeshaingia mpaka kwenye nyumba zao na hata wilayani kwangu pia nimeshaingia, nyumba zinasikitisha kama walivyozungumza wenzangu. Japokuwa wenyewe kwa sababu ni binadamu wanajaribu kuzipamba kwa chokaa na nini, lakini bado hairidhishi hata kidogo. Suala kubwa ni lile lile kwamba chumba kimoja au vyumba viwili kwa mtu mmoja anaishije, mtu anafamilia.

Kwa hiyo, hii ni mojawapo naomba isisitizwe, lakini natoa ushauri, tayari ushauri ambao nilitaka kuutoa mara ya kwanza nimeukuta hapa wa *NSSF* kuwajengea hizi nyumba, lakini bado kuna mashirika mengine kama *National Housing*, kama vile *PPF*, ambao wangeweza kuwekeza katika kujenga nyumba za askari hawa waweze kuishi na itakuwa rahisi kwao kupata fedha hizo kurudishwa kwa sababu hawa ni wafanyakazi na wana mishahara ambayo itaweza kurudisha zile gharama zao za ujenzi.

Kwa hiyo, mimi nashauri Serikali pia iwatumie na hawa wengine wa *PPF*. Kwa mfano nyumba za Kisasa, zile zimejengwa na Wizara ya Miundombinu, kwa nini maeneo mengine wasipelekwe wakajenga pia kwa ajili ya jeshi hili la polisi na magereza? Mimi naomba pia Wizara iangalie haya maeneo ya *NSSF*, *PPF*, pamoja na hata Miundombinu wenyewe ili wafanye kazi hiyo ya kuwawekea mazingira mazuri polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu maslahi. Rushwa nafikiri ni ule ukosefu wa maslahi ya uhakika, na tuiswape lawama sana hawa wanaopokea rushwa. Naona wakirekebishiwa yale marupurupu yao nafikiri hii biashara ya rushwa itapungua, lakini lingine ambalo ningependa kuzungumzia wenzangu wa mikoa ya Kagera walishazungumza, mimi nilibahatika kumsindikiza Mheshimiwa Savelina Mwijage, Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale walini ambao wako kwenye mipaka kwa kweli wana hali ngumu sana, nimefika, siwezi kukariri majina, lakini nilifika sehemu moja ya Ushirombo ambapo pana mpaka ambao kimsitu ni kidogo sana lakini tunaelezwa kina majambazi na tulizuiliwa hatuwezi kupita lakini ilibidi pale askari watusindikize na wakaenda kulala sehemu nyingine inaitwa Lunzewe. Kwa kweli kwa jinsi walivyochukuliwa ghafla sidhani hata kama pesa ya kwenda kulala kule ya gesti waliweza kupata. Kwa hiyo, hivi vitu vingine vinawafanya hawa askari wajisikie kwamba kama sio mionganoni mwa watumishi walioko hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu niliyoiona kule haifanani na misitu ya kwetu Kusini lakini nashangaa hawa majambazi wanatokea wapi na wanaishi wapi? Kwa

sababu hata njiani sikuona barabara ambazo wanakuja na gari wakavamia na wakaondoka.

Mimi nahisi majambazi wako miongoni mwa vijiji vilivyopo karibu, vifanyiwe kazi na kuangalia kama walivyofanya *operation* ya uvuvi haramu katika mikoa ya kwetu ya kuangalia katika vijiji vilivyopo karibu na bahari na kule pia waangalie hivyo naamini wapo wananchi ambao watawataja wale majambazi ambao wanafanya uhalifu ule katika ile misitu, ni kilometra chache. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hilo naomba ombi waangalie katika maeneo ya vijiji vile, mimi siwezi kuamini Tanzania tuishi kama Nicaragua, watu wanaingia kwenye mapango kwenda kujificha katika nchi yao huru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu elimu. Elimu na mafunzo ni vitu muhimu kwa kila mtumishi. Nasikitika kwamba kuna askari ambao wameajiriwa wakiwa wamemaliza *form six* na *division nzuri* *division I, division II* wanaomba kwenda kusoma wanaambiwa hawawezi kwenda kusoma kwa sababu hawajamaliza mwaka mmoja au hawajamaliza miaka miwili. Naomba wapewe nafasi wakasome na wanataka kujigharamia wenyewe lakini bado hawapewi nafasi, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi wao bado ni vijana ambao wanawenza wakajigharimia kwa vimishahara vyao kidogo wanavyovipata, lakini wakishafika umri wetu sisi wana majukumu ya wake na familia, ni lini wataweza kutenga hela ya kwenda kujigharimia wenyewe kwenda kusoma? Naomba Wizara iwasikilize, kwa sababu sasa ni wakati muafaka kwa wao kujiwekea kitu kidogo kwa kujigharimia wenyewe, wale wanaotaka kujigharimia waruhusiwe, hao wengine kama hawawezi kujigharamia, Serikali haina uwezo, hatuwezi kuzungumza kwa sababu inategemea na mfuko wa Serikali lakini kwa wale ambao wako tayari kujigharamia naomba waruhusiwe. Ni mwaka wa pili huu napata malalamiko ya watumishi wa aina hii kwamba wanataka kujigharamia lakini wanazuiliwa kwa sababu tu hawajamaliza miaka miwili ya kufanya kazi katika jeshi hili, sio haki elimu ni haki ya kila mtumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia, sina mengi kwa kweli hilo la elimu naomba litiliwe msisitizo kwa sababu hawa wanahitaji kupata elimu na kama unavyojua Wizara nyininge ukisomea kitu fulani ni hicho hicho. Kama ukisomea polisi, vyuo vya polisi viko vingi lakini je, taaluma ya vitu vingine ataipata wapi kama hajapata nafasi ya kwenda kusoma Chuo Kikuu? Kwa hiyo, hata kama akishindwa na jeshi la polisi hawezি kwenda kwenye eneo lingine kwa sababu amesomea upolisi tu na hana taaluma nyininge. Kwa hiyo, analazimika kukaa pale kwa sababu tu alichosomea ni upolisi, ataenda kuajiriwa kwenye Wizara ya Miundombinu, ataenda kuajiriwa Wizara nyininge yoyote ile? Haiwezekani. Hili lipewe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu vitambulisho vya uraia. Sasa nauliza swali tu, ni lini hasa vitakuwa tayari? Kwa sababu kwa kweli tunavihitaji na nini hasa kipingamizi kikubwa, kwa sababu imekuwa

ikizungumzwa lakini haifanyiwi kazi. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, wakati ana *wind up* atuelezee ni lini tunaweza kuvipata hivyo vitambulisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalopenda kulizungumza na nilishalizungumza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kuhusu likizo za polisi na hapa pia nimepata malalamiko ya likizo za polisi, wao kama watumishi wengine, wanaomba likizo zao ziwe za mwezi mmoja. Baada ya mwaka mmoja wale watumishi wa ngazi hizo ambao wanaenda baada ya kukaa miaka mitatu halafu baadaye akaenda likizo ya miezi mitatu, wanaomba waende likizo kama watumishi wengine ya kwenda baada ya mwaka mmoja waende likizo ya mwezi mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, likizo nafikiri kila mtu anafahamu maana yake ni nini, likizo maana yake ni kwamba kupumzisha akili baada ya kazi kubwa na tumeshaona hawa wenzetu wanafanyakazi kubwa sana kuanzia mwanzo wa mwaka mpaka mwisho wa mwaka na mimi kama mfanyakazi nikifanya kwa muda wa mwaka mmoja tu tayari ikifika ile tarehe yangu ya likizo nimesha-*adapt* kwamba tarehe ile ikifika ni lazima nipaye likizo kwa hiyo, huwa ninachoka zaidi. Jamani kwa hawa wenzetu itakuwaje? Miaka mitatu ndio apate likizo, anashindwa kufanya kazi zake za maendeleo, kwanza pesa anazopewa wakati wa kwenda likizo hazifanani na muda huo ambaeo anaenda likizo na anaporudi harudishiwi hizo pesa. Zaidi ya hapo anapokuwa kule kwa kuwa likizo ni ya muda mrefu, miezi mitatu, anaishiwa zile pesa ndogo alizoenza nazo mpaka nauki ya kurudia kwao inakuwa ni vigumu. Vile vile miaka mitatu anayokaa kama alikuwa anaendeleza ujenzi sehemu fulani anasubiri mpaka miaka mitatu tena aende akasimamie ujenzi huo, hii haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, wakati wanarekebisha marekebishesh yote yale yanayohusu jeshi hili la polisi, magereza na hili pia waliangalie. Kwa kweli na wao wanahitaji kupumzika, miaka mitatu ni mingi ili wao waweze kupumzisha akili zao. (*Makofi*)

Mimi sina maelezo zaidi, isipokuwa tu niliyotaka kuzungumza ni hayo kuanzia likizo, mafunzo kwa hawa vijana walio katika jeshi la polisi waliokwishapata mafunzo tayari lakini wana taaluma nyingine ambazo wangependa kuzisoma au kwenda Chuo Kikuu, pia lifikiriwe kwa sababu hawa wanajigharimia wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara hii. (*Makofi*)

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpungeza sana ndugu yangu kamanda *IGP* wetu Said Mwema na makamanda wenzake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kupambana na uhaliu nchini mwetu. Nasita sana kumpungeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na ninasita sana kuunga mkono hoja yake, labda tutakapofika kwenye vifungu atakaponieleza naweza kumuunga mkono. (*Makofi*)

Lakini kabla sijaendelea na mchango wangu ningeomba nitoe salaam kwa wapiga kura wangu jimboni kwangu, vijana wangu wa timu ya *Vila Squad*, kwa kupanda daraja na kufanikiwa kucheza *Premier League*, nawapongeza sana na nikirudi tutaonana. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu. Nimempongeza *IGP* kwa kazi nzuri ya kupambana na uhalifu na kwa kweli ule uhalifu mkubwa mkubwa kwa kiasi kikubwa sana umepungua sana kutokana na kazi nzuri anazozifanya. Lakini tunao wahalifu wadogo wadogo hawa vibaka, katika jimbo langu ama katika jiji la Dar es Salaam, kwa kweli ni wengi mno na vitendo wanavyovifanya ni vibaya sana kwa wananchi wetu hasa wale wa hali za chini, wananchi wetu wa maeneo ya Tandale, Hananasif, Kigogo, Magomeni na kadhalika. Wanapoamka asubuhi kwenda kazini basi labda waende kundi, kinyume cha hivyo utakabwa na siku hizi wenye wana loba zao za mbao, unakabwa utanyang'anywa kila kitu. Matukio haya ni mengi sana, yapo ambayo yanaripotiwa lakini yapo ambayo wananchi sasa wameshachoka wanaona kama ni kawaida, wanayaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana jeshi la polisi lijaribu kuweka ulinzi ama kuongeza askari katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, hususan katika jimbo la Kinondoni, kwa sababu uhalifu huo ni mkubwa na kwa kweli unakatisha tamaa. Unapotoka Magomeni ukikatiza kwenda Mkwajuni, lile bonde lile, saa tano asubuhi kweupe utakabwa na utanyang'anywa ulichokuwanacho na bahati mbaya kuna msitu pale pembedi kwa hiyo, akikutia loba wewe anakushushia chini kule wanamaliza shughuli zao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niombe sana jeshi la polisi lijaribu kuongeza ulinzi ili kuweza kuwanusuru wananchi wetu walalahoi ambao wanahangaika kutafuta riziki lakini vibaka ni wengi mno ambao wanawaibia, kuibwa simu ni kitu cha kawaida Dar es Salaam hasa Kinondoni na tunayo mahakama ya simu, ukitoka Tandale kwa Mtogole pale mpaka kwa Tumbo ni balaa, ujue simu na vyote ulivyokuwanavyo utaporwa tu, kwa hiyo, naomba ulinzi uongezwe ili kupambana na hali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisita sana kumpongeza Waziri, kwa sababu ya jambo moja muhimu na nimekuwa nikilisema mara nyingi kwenye Bajeti zao zilizopita, suala la nyumba za askari, na nikuombe Mwenyekiti mwenye we pamoja na Waziri, hebu siku moja tutoke kwa pamoja tukatembee pale Magomeni muone askari wetu tunaowategemea kutulinda wanavyolala kwenye *godown* ambalo limechoka, ni bovu, ndani mle vyumba vyao wamevitenganisha kwa maboksi, kwa viloba na ndani kuna familia nyingi mno zinaishi katika banda lile. Kwa kweli ni aibu kubwa sana kwa jeshi la polisi na kwako Waziri kijana, kuwa na askari ambao wanalala katika maeneo kama yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe hebu siku moja twende ukaone halafu uje uwaambie hali ikoje, Mungu apishe mbali, kama itatokea moto ndani ya banda lile basi tutapoteza watu wengi sana. Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, naomba unieleze ni kwa nini hamjachukua hatua za kuwajengea nyumba pale Magomeni? Eneo ni kubwa, unaweza

ukajenga nyumba za ghorofa unavyotaka. Najua mnajenga Kurasini na kadhalika, lakini hebu angalieni na pale Magomeni, hawa ambao mnategemea watulinde mnawalaza namna ile nasita kusema mnawalaza kama kuku, Mungu anisamehe sana, lakini kwa kweli hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri, kwenye majumuisho yako unieleze ni hatua gani ambazo unazichukua kuhakikisha kwamba lile banda linaondolewa na inajengwa nyumba ya sawa sawa ili askari wetu waweze kuishi. Ni Magomeni, lakini nenda hata Kijitonyama Mabatini, hali ni hiyo hiyo na ukienda *Oysterbay* pia hali ni hiyo hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo vituo vidogo vy'a polisi (*police posts*), tunategemea vitusaidie kule mtaani kupambana na uhalifu. Lakini kituo kidogo cha polisi umeweka askari wawili, Dar es Salaam watu ni wengi sana, uhalifu ni mkubwa sana, askari wawili watafanya nini? Hawawezi kufanya kitu chochote, matokeo yake hata wale wahalifu ambao wanakamatwa na wananchi wakipelekwa pale ukiondoka na mhalifu anaondoka. Wameanza kuvibadilisha na majina sasa badala ya kuviita *police posts* wanaviita *police SACCOS*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujaribu kuhakikisha kwamba hivi vituo kama kweli tumeamua kuweka vituo vidogo kwa ajili ya kuwalinda wananchi wetu basi tuweke na askari wakutosha ili waweze kulinda wananchi wetu kama ambavyo tumekusudia, kuweka askari wawili ni kufanya mzaha, hawa vibaka ninaokueleza wakija wanakuja kundi lisilopungua watu 10 mpaka 15, askari wawili watafanya kazi gani? Kwa hiyo, naomba sana jeshi la polisi lione umuhimu wa kuongeza askari katika vituo vidogo vy'a polisi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimesikia kwenye vyombo vy'a habari kuhusu magari ya abiria kutembea usiku, kama ni kweli kwamba magari ya abiria sasa yaruhusiwe kwenda mpaka saa sita usiku. Hili ni balaa tunalitafuta, tukumbuke wakati amri ile inatolewa hali ilikuwaje? Magari haya ya abiria mchana kweupe yanagongana uso kwa uso, yanauwa watu chungu mzima, leo mnataka kuyatembeza mpaka saa sita usiku, kwa lipi? Mnataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu ni nzuri, gari likitoka asubuhi litawahi tu kufika, kwa nini muwaruhusu waende mpaka saa sita usiku? Au yale tunayoyasema sasa kwamba askari wakikamata dereva wanakwenda nyuma ya basi wanaongea sasa wanataka kwenda mbele ya basi waongee manaa yake ni usiku. Lakini si hilo tu, lipo lingine nimelisikia la *fine* ya shilingi 200,000/= kwa dereva wa magari ya abiria ambaye atakutwa anaongea na simu basi *fine* yake ni shilingi 200,000/=.

Mheshimiwa Waziri, hebu nieleze utafiti ulioufanya kati ya madereva wanaopata ajali kwa kutumia simu na wale madereva wanaopata ajali kwa ulevi na uzembe ni wapi

wanaofanya makosa mengi? Na ni kwa nini tusiwaadhibu wale ambao wanaendesha magari wakiwa ni walevi na wazembe wanasababisha ajali, tunakuja kuangalia hili la simu? Na unipe takwimu kwamba ni ajali ngapi zimetokea kwa sababu ya madereva kuongea na simu. Lakini kama ni kweli kwamba madereva wanasababisha ajali kwa kuongea na simu basi iwe ni magari yote na isiwe kwa magari ya abiria tu, kwa sababu hata huyu wa gari dogo anaweza akaongea na simu akasababisha ajali ya gari kubwa na kusababisha vifo vya watu wengi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba kabisa nipate maelezo ya kutosha ya kina kwamba utafiti umefanyika kwamba madereva wanaendesha wakiwa wanaongea na simu wamesababisha ajali nyingi ndio maana tumeweka adhabu kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la ajira kwa polisi. Mara nyingi nimekuwa nikisoma katika magazeti pale polisi wanapotaka kuajiri, wanaandikwa kwenye magazeti watu wanajitokeza kuomba nafasi hiyo ya kuwa polisi, aah, huu utaratibu unanitia mashaka hivi sasa kwa sababu tumeona baadhi ya matukio mabaya yanayofanywa na baadhi ya askari. Wapo baadhi ya askari ambao sio waaminifu, wanafanya mambo mabaya na hivi karibuni tumeyashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningefikiri jeshi la polisi lijaribu kujipanga upya linapohitaji kuajiri askari. Utumike utaratibu ambao mtawajua kwa kina tabia na mienendo ya hawa ambao mnataka kuwaajiri kuliko kukurupuka na kuwachukua watu tu mkawapeleka mafunzoni sijui miezi sita mkaja mkawapa dhamana kubwa kama hiyo, baadaye huwezi kujua tabia zao, wanafanya mambo mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo Jeshi letu la Kujenga Taifa, kwa nini lisitumike kuwandaaskari ambao watakuja kuwa mapolisi? Kwamba hawa askari waende *JKT*, wafanye kazi *JKT* kule, tabia zao zitajulikana, miendendo yao itajulikana, *then* jeshi la polisi litachukua askari kutoka *JKT* na kuwaajiri. Kupunguza haya matukio mabaya ambayo baadhi ya askari wamekuwa wakiyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uhaba wa askari idadi ya Watanzania imekuwa kubwa idadi ya polisi ni ndogo sana na ndio maana mara nyingine labda wanashindwa kudhibiti mambo mengine, hebu tujaribu kuyaacha kutochana na hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiit, tunazo timu za mpira, kila mkoa ukienda kuna timu za polisi na zinapambana, *RPC* anasimamia timu ile ipande daraja na kucheza *premier league*. Sasa tuna tatizo la pesa kwenye jeshi la polisi lakini maandalizi ya timu hizi yanachukua pesa nyingi sana, lakini uhalifu pia ni mkubwa sasa kwa nini badala ya kuwachukua askari hawa wafanye kazi ya kuwalinda wananchi tunaanza kuwakimbiza kwenye mipira, kila mkoa ukienda kuna timu ya mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikatai michezo ni lazima lakini hebu basi kuwe na timu moja tu ya polisi ijulikane hii ndio timu ya polisi ya nchi nzima, tuisimamie icheze kama ni ligi au ni nini, hizi timu nydingine huku hebu hawa askari wa huku wafanye kazi zile ambazo wanakusudiwa kuzifanya za kuwalinda wananchi wetu kulikokuwa kila *RPC* sasa anasimamia timu yake. Na ni mashindano, matokeo yake anaweza akaacha majukumu yanayomkibili akawa ameegemea sana kwenye kuhakikisha timu inafanya vizuri, lakini anapata wapi pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa anaweza hata akaja akapata fedha za mafisadi ili timu yake ifanye vizuri, kwa hiyo, niombe kabisa hebu tujaribu kulingalia hili twende kwenye kazi yetu ambayo imetuweka ya kulinda mali na kulinda raia wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na kama nilivyosema mwanzo, kama nitaunga mkono hotuba hii ya Waziri, basi ni pale ambapo Waziri atanipa maelezo ya kutosha, kuhusu nyumba za askari pale Magomeni, kinaweza kikaeleweka, kinyume cha hivyo kwa kweli inaniwia vigumu sana kuunga mkono hoja hii kwa sababu askari wanapata taabu, askari hawana mahali pa kulala.

Lakini wapo askari ambao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, askari wa usalama barabarani wanaongoza magari Dar es Salaam, wanafanya kazi katika mazingira magumu, wengine wanagongwa, sijui mnawasaidiaje? Wapo ambao wako kwenye misafara ya viongozi wetu na wenyewe nao ni hatari. Wengine wameshagongwa, sijui tunawasaidiaje inapotokea ajali kama ile, wengine wanapoteza viungo.

Kwa hiyo, niombe tu jeshi la polisi kwa kweli liwe makini sana na lihakikishe kwamba hawa askari ambao tunawatumia kwenye mazingira magumu basi angalau kuwe kuna motisha za kuwapa ili wasivunjike moyo ama wasikate tamaa katika utendaji wao wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba niishie hapo, nimesema siungi mkono mpaka kwenye vifungu Mheshimiwa Waziri, tutakutana huko, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ni nafasi adhimu ambayo muda mrefu nilikuwa nikiitafuta na kwa kuanzia mimi labda ningetofautiana kidogo na baadhi ya wenzangu, mimi nasema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na kama ningemfuata Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, ningesema kweli Mussa kapatikana na Haruna wako pamoja.

Kazi mnayoifanya ni kazi nzuri na ni kazi ya matumaini. Lakini nimpongeze kwa pongezi maalum *IGP* Mheshimiwa Saidi Mwema, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya pamoa na hali ngumu ya Bajeti ilivyo lakini nchi imo katika hali ya utulivu ambaa ndio unatufanya tuweze kukaa hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwamba polisi ninyi ndio Serikali. Kuwepo kwetu hapa ndani, nchi yetu kuwa tulivu na kwamba kila mmoja anakwenda Kusini na Kaskazini, katika kutafuta riziki zake kwa kweli ninyi ndio mnaotusababisha tuwe katika hali hiyo, tunawapongeza na tunasema msivunjike moyo, hii kazi ni nzito, ninyi endeleeni na sisi tuko nyuma yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya bilioni 274 na marupurupu ni ndogo sana kwa Wizara hii. Wizara hii inabeba majukumu kama nilivyoelezea mwanzo kwamba hii ni Wizara ambayo ina kila kitu. Pakizuka moto polisi, pakatokea mapambano polisi, mipakani wizi wa ng'ombe polisi, wanaopigana mitaani polisi, kila kitu polisi na wakati wao wanakwenda katika mapambano na katika kuweka usalama hasa kwa upande wa majambazi unakuta majambazi nao wamejitarisha kupambana nao. Wanakwenda polisi kwa uhakika kwamba sisi tunakwenda kupambana na majambazi, sasa kazi hii ni ngumu, wewe unakwenda kupambana na jambazi anachokifanya yeze hana analolijua isipokuwa kwanza ni kukuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiit, tumeona yale yaliyotokea Arusha, mwaka jana sijui mwaka juzi ule, mwaka jana walikuwa wana kila aina ya zana. Tumeona yaliyokuwa yametokea Ubungo pale, mwaka juzi, sijui mwaka jana, wakati ambaa vijana wanasafrisha pesa, watu wamejipanga huku wamezuia na huku wamezuia. Lakini tumeona juzi yaliyokuwa yametokea Mkoa wa Morogoro, Ifakara kule, wamekwenda jamaa wamejiandaa na polisi wanasema wanakwenda kupambana nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi ni nzito na inataka moyo na ujasiri mkubwa. Kwa hiyo, Ndugu zetu Polisi tukisema hapa kuwalamu hatulaumu kwa maana hatujui kazi zao muhimu wanazozifanya tunawaambia kwa maana ya kwamba wajitayarisho na wakae tayari zaidi na katika lugha ya kwamba wale waliokuwa wabaya wachache waliokuwepo wajirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ndani ya Jeshi lenyewe kunahitaji wapelelezi wa kufutilia wale ambaa wamo ndani ya Jeshi lenyewe la Polisi kwa sababu ziko *incidence* nyingine tunazisikia za kwamba ujambazi mkubwa unaofanyika wakati mwingine zinatumika zana au sare za Polisi na kuna wale waliokuwa wabaya, siyo wema kwa nchi yao au wao wenyewe hawajiamini, wao ndiyo wanaotoa sare zile kuwapa majambazi, halafu wanapewa pesa baada ya kazi ile kukamilika. Tunaomba hilo nalo ikiwezekana liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningerudi kidogo katika suala la ajira, mwenzangu hapa Mheshimiwa Azzan kanifilisi kidogo, lakini ninakuwa nakubaliana na wazo la

kwamba sasa hivi kutokana na hali inavyokwenda, basi bora tungetumia vyombo vyetu au taasisi zetu za JKU au JKT kuchaguliwa vijana kule wakatiwa katika Jeshi la Polisi, yaani wakaajiriwa katika Jeshi la Polisi. Kwanza itakuwa ni muda mrefu wameangaliwa na muda mrefu tabia zao zitakuwa zimeonekana.

Kwa hiyo, ni vizuri baada ya kwenda Mitaani na baada ya kutafuta watu huko na huko na wengine ni wabaya na wengine wanakuwa wameshashindwa hata wazee wao kuweza kuwarekebisha. Kuna kauli zinazungumzwa kwamba kuna baadhi ya Viongozi wa Polisi, yaani Makamishna na kadhalika wanaweka watoto wao au ndugu zao au watu wa karibu zaidi, wanaingia mle, kwamba yechegea gamba la yule aliyemweka na siyo kazi ile iliyompeleka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwa wale Polisi wote wakati wanatoka wanakwenda kwenye *operation* kwa maana kwamba kuna ujambazi mahali umetokea wakatiwe Bima na ikiwezekana baada ya kurejea kwenye *operation*, ile basi angalau kuwe kuna kitu *incentive* fulani wanapewa kwa kazi kubwa waliyokuwa wameifanya. Nadhani haya yamezungumzwa sina haja ya kuzungumza kwa kirefu wenzangu wamejaribu kuyaelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika Jimbo langu la Matema, lakini pia nikija Zanzibar kwa ujumla wake kumekuwa na mambo mengi yametokea ya ujambazi, Mheshimiwa Waziri ningombwa akaliangalia hili. Majambazi wanakwenda Zanzibar kama kwenda kuvamia kitongoji ambacho hakuna watu. Hivi juzi kuna *incident* moja imetokea wakati majambazi wanafukuzana na Polisi, Polisi gari wanadolitumia ni *Land Rover* na majambazi wanatumia gari ambayo ina uwezo zaidi wa kukimbia kuliko *Land Rover*, matokeo yake ni kwamba kapatikana *driver* aliyejikuwa wa majambazi aliyejikuwa akaizungusha gari ile akarudi kule alikotoka, *Land Rover* likabinuka na likaua. Sasa tunachozungumza ni kwamba, hata hawa Askari wanaoshughulikia masuala ya kupambana na majambazi, wapewe vifaa vya kutosha na gari ambazo zina uwezo. *Land Rover* leo unakwenda kukimbia na *Land Cruiser* utaipata wapi?

Sasa ukanda wa Matemwe ni Ukanda wa Utalii, tuna hoteli kubwa kubwa na Zanzibar sasa hivi kwa njia moja ama nyingine ni nchi ambayo inategemea utalii zaidi kuliko vyanzo vingine vya uchumi. Lakini ukitoka hapo kwamba sisi ukanda ule tunai-face Bahari ya Indian Ocean ni kweupe kabisa na ni wazi kabisa kama watakuja majambazi na vyombo ambavyo vina nguvu inawezekana wakaingia katika mahoteli wakafanya wanavyotaka na baadaye wakaondoka. Kwa hiyo, ninashauri ikiwezekana tuweke Police Marine na tuwape vyombo vya kutosha katika kanda hasa zile kanda za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mipakani tunasikia huko sehemu za Mara, Kigoma na sehemu nyingine hapa baadhi ya Waheshimiwa wametaja hebu tusaidieni Waheshimiwa, kule tupeleke doria na tuwe tuna Polisi ambao wamekuwa na tuweze kuondoa matatizo yaliyokuwepo katika maeneo yale. Siyo hivyo, tutakuja kufika mahali ambapo sasa hivi mchangiaji aliyejita sitaki kumwita tena kwa jina lile,

amezungumza kwamba sasa hivi unapita mahali wewe unakabwa na watu wanaokaba na huna la kufanya.

Lakini kingine ni kwamba, tatizo lililokuwepo katika vyombo vyetu vya Polisi, huu wanasema ulinzi shirikishi, watu wako tayari kuisaidia Polisi, lakini matatizo waliyonayo ndugu zetu Polisi wakishapelekewa habari yule aliyetoa habari wanamtaja kwa jambazi. Hakuna watu waliokuwa tayari kuweza kuuawa. Kwa hiyo, siri ziwekwe na kama siri zitawekwa, basi ulinzi shirikishi utakuwa ni ulinzi wa maana kabisa na tutapata ushirikishaji wao katika hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono asilimia mia kwa mia. (*Makofii*)

MWENYEKITI – MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Ahsante sana Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir kwa mchango wako na ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu na Mheshimiwa James D. Lembeli ajiandae.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kulihutubia Bunge lako Tukufu.

Kwanza nianze kwa kupongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara mbalimbali kwa kazi nzuri wanayoifanya, bajeti ni nzuri imeandikwa vizuri, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu ambacho kimeandaliwa cha taarifa ya hali ya uhalifu nchini Tanzania kwa mwaka 2007 Januari mpaka Desemba, kitabu hiki napenda kukiri na kupongeza kwamba ni kitabu ambacho kimeandikwa kitaalamu sana, kimesheheni taarifa zote muhimu na kinatoa fursa ya kuchangia mawazo, kuweka fikra zetu pamoja kwa kusaidiana na Wizara pamoja na Jeshi la Polisi katika kutafuta suluhisho la matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipongeze sana Jeshi la Polisi kwa kuwa na *program* ya maboresho ya Jeshi la Polisi la miaka saba kuanzia mwaka 2007, naamini kwamba *program* hii ikitekelezwa kama ilivyo, italeta ufanisi mkubwa. Naomba kunukuu malengo ya *program* hii kama ilivyoelezwa kwenye kitabu katika ukurasa wa 14 kwamba: “*Program* hii ina malengo makuu yafuatayo: Kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa linalozingatia taaluma na linaloshirikiana na jamii, yaani *Modernisation, professionalism and community Policy*. ”Kwa hiyo, naamini kwamba *program* hii ikitekelezwa vizuri matatizo mengi yaliyopo ndani ya Jeshi la Polisi yatapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu nitaielekeza katika Idara ya Polisi na Idara ya Magereza na nitaanza na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imeonyesha kwamba Polisi mwaka 2007/2008 wamelalamikiwa wakiwa wa kwanza. Wizara nzima malalamiko yalikuwa 1,166 lakini kati ya haya malalamiko 1,164 yaani 99.8%, yalihusu

Polisi. Polisi walilalamikiwa juu ya mambo makuu matatu: Kwanza, ubambikizaji wa kesi, ucheleweshaji wa upelelezi, uporaji wa fedha na mali za watuhumiwa. Nashukuru kwamba Wizara inayatambua hayo. Kwa kweli malalamiko haya yapo na ni ya kweli na ninafikiri yapo sehemu nyingi kama siyo sehemu zote nchini.

Lakini kuna lalamiko lingine ambalo hakulitaja Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, kuna lalamiko kwamba Serikali inaposema tuanzishe au wananchi washirikishwe, yaani ulinzi shirikishi, kuna lalamiko kwamba anapokamatwa mtuhumiwa kwa kosa ambalo liko dhahiri akienda kituo cha Polisi siku mbili au tatu anaachiwa na anarudi tena kuwatambia wananchi waliomkamata kwamba hawamuwezi. Hili lalamiko lipo na ninaomba Mheshimiwa Waziri atambue kwamba hili lalamiko wananchi wengi wanalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba nипитie kwa kifupi, ama tujiulize kwa kifupi, kwa nini malalamiko haya yapo? Kwa nini Polisi walalamikiwe? Polisi wanalamikiwa mojawapo ya sababu kubwa ni maslahi duni na haki za Askari Polisi. Nitazungumzia kwa kifupi masuala ya kiutumishi yanayohusu hasa Askari wa *rank* za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi, kuna utumishi wa Polisi na kuna Utumishi wa Umma. Askari Polisi, hasa hawa wa chini, hawako kwenye Utumishi wa Umma bali wako kwenye Utumishi wa Polisi. Sasa naomba niainishe mapungufu ya Utumishi wa Polisi kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda nimpongeze sana *Inspector General* wa Polisi Said Mwema kwa kuanzisha harakati za haki za Polisi. Nakupongeza sana na aendelee na uzi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuajiriwa hutambuliwa na kustaafuliwa kwa Askari Polisi kuna matatizo makubwa.

Kwanza, Askari akiajiriwa inabidi akae *probation* miaka 12, maana yake ni kwamba anakuwa kibarua kwa miaka 12. Ni mtumishi gani unaweza ukakaa *probation* miaka 12? Serikalini *probation* ni miezi sita, lakini Askari unampa miaka 12 akae *probation*. Hilo ni tatizo la kwanza. Askari wa *rank* ya chini anakuwa kibarua kwa miaka 12 na baada ya hii miaka 12 inabidi achague aidha kukaa kwenye *pension* au kukaa kwenye mkupuo, yaani kwenye *gratuity*. Akiamua kwenda kwenye *pension*, mpaka astaafuli ndiyo alipwe malipo yake na hapo katikati akifa, maana yake atakuwa amefanya kazi ya Kanisa, hatalipwa. Halafu Askari wa namna hii wako wengi! Akiamua kwenda kwenye mkupuo anaweza kuamua kuacha kazi wakati wowote na hulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu unawatia majaribuni Askari wetu, unawaweka katika hali ngumu ya kuamua kwamba aende *pension* ama aende *gratuity*? Iwapo askari akipata bahati apate cheo cha *Assistant Inspector* hapo atakuwa ameukata kwa sababu atakuwa ameingia kwenye masharti ya Utumishi wa Umma. Sasa mpaka afikie cheo cha *Assistant Inspector*, ni lini? Amekaa miaka 12 vyeo vyenyewe kupanda ni

shida mpaka akafike kule. Askari wanasota! Halafu nyongeza ya mishahara ikigota miaka sita hailipwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *pension* watumishi wa Serikali huchangia 5% na Serikali inawaongeza 5% lakini Polisi huchangia 10% zote, kwa nini? Haya mambo yanawakatisha tamaa Askari na ukizingatia kwamba mishahara yenyewe ni kidogo halafu unamwambia achangie 10%! Napendekeza *formula* ya *pension* ya Askari Polisi iangaliwe upya, Askari anafanya kazi miaka 25 analipwa *pension* ya shilingi milioni tatu na nishani. Askari wanasema afadhali muwanyime nishani lakini muwape mabati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Askari wanakaa muda mrefu sana bila kupandishwa vyeo. Utamkuta Askari anasota na kwanja moja ile inayoitwa “Vumilia”, sisi tulikuwa tunaita “Kwanja” tulipokuwa *JKT*, moja miaka 15 bila kupanda cheo. Sasa Askari unamkatisha tamaa kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Askari hawana Bima ya Afya. Hupewa Sh. 200,000/= kwa mwaka na Sh. 200,000/= kwa mwaka ni sawasawa na Sh. 17,000/= kwa mwezi; kwa kigezo gani? Ana familia na watoto anapewa Sh.17,000/. Kwa nini asiingizwe kwenye Bima ya Afya kama watumishi wengine? Hata wanakijiji sasa hivi wana mpango wa Bima ya Afya, yaani wananchi wa kawaida, lakini Askari wanapewa sh. 17,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Askari wanalipwa *house rent allowance* ya Sh. 1,500/= kwa mwezi. Kama hii haitoshi, wana madeni na madai ya miaka mingi ya uhamisho wa safari za kikazi hawajalipwa, unawategemea watafanya kazi kwa morali? Kama hiyo haitoshi Askari akituhumiwa anaadhibiwa mara mbili, kwanza anafukuzwa kazi, halafu Mahakamani, akishinda hata kama na kesi hawezi kurudi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kuunda Idara ya Malalamiko. Lakini malalamiko haya ni jamii dhidi ya Wizara, yaani dhidi ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na kadhalika, lakini hakuna chombo huru kinachomtetea Askari, yaani hana chombo huru kinachoweza kumtetea. Kwa hiyo, unakuta Askari wanakuwa wanyonge, wanaambiwa pokea amri, maswali baadaye na hiyo baadaye hakuna wa kumtetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ma-*OCD* wapewe mafungu ya matumizi katika Wilaya zao, kuna mambo mengine yanahitaji fedha na *OCD* hana fedha mpaka apige simu Mkoani kwa *RPC* ndiyo aletewe fedha, vinginevyo *RPC* sasa inabidi atafute ujanja wake mwenyewe wa namna ya kupata fedha za kushughulikia matatizo ambayo wakati mafungu yamemaliza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nyumba za kuishi Askari limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Mimi naamini karibu 80% huishi uraiani. Askari anapoishi uraiani anaishi na wahalifu inawezekana wengine anawajua kabisa lakini

maadamu anaishi nao kwenda kuwakamata inakuwa shida kwa sababu anaogopa kudhuriwa au watoto wake watadhuriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ijidhatiti kwa kweli huu mpango unaofanyika kwa Maaskari katika maeneo yaliyotajiwa kwenye bajeti uandaliwe mpango mwingine na ninaamini hii iko kwenye maboresho sijasoma maboresho kwa kina lakini naamini kwamba Serikali bado inaweza ikaboresha tatizo la nyumba kwa Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Magu napenda niishukuru Serikali, nyumba za Askari. *Magu Barracks* nyumba zilijengwa mwaka 1976 mpaka mwaka juzi zilikuwa hazina umeme, nashukuru wamewekewa umeme na ninaleta shukurani zao kwako Waziri kwamba wameshukuru sana kwani sasa na wao wanajiona kama ni raia. Ilikuwa ni kero kubwa. Jirani kwa Raia kuna umeme, ye ye ana *television* ndani ya nyumba lakini hawezu kuangalia hata matukio mbalimbali yanayotokea. Kwa hiyo, nashukuru kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna ukarabati umefanyika kwenye nyumba zile za Askari Magu. Lakini ukarabati huo umefanyika nusu, ningeomba katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa *IGP* naomba ukatazame pale Magu ukarabati uliofanywa nusu umaliziwe.

Lakini pia kuna tatizo la vyoo, Askari hawana vyoo. Kunahitajika vyoo viwili kimoja kwenye *line* ya juu na kimoja wenye *line* ya chini. Hili ni suala ambalo kwa kweli siyo la kusubiri, naomba tu Mheshimiwa Waziri afanye marekebisho kidogo kwenye bajeti ili tupate huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia juu ya Polisi ni kwamba Wilaya ya Magu ni kubwa sana, inapakana na Wilaya ya Bunda, Bariadi, Maswa, Kwimba Misungwi na Wilaya ya Illemela. Sasa gari lipo moja tu la Polisi. Kuna matukio yanatokea Kisesa, Shishani Mahaha gari ni moja tu, sasa Mheshimiwa Waziri hebu naomba anisaidie Askari hawa watafanyaje kazi? Matukio haya wataweza kuyadhibiti namna gani? Ukiangalia mpaka tu wa majini, uanzie Kisesa mpaka Ramadi matukio yanayotokea kwenye Mialo ni mengi sana, bado kuna matukio ya wizi wa mifugo, kuna matukio ya Zeruzeru kuuawana kuna matukio mengine mengi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Ndugu *IGP* naomba sasa utusaidie Magu tupate gari la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoke kwenye Polisi niende Magereza. Nilitembelea Gereza la Magu tarehe 24 Mei na ninaomba nimpongeze sana Mkuu wa Gereza lile *SP Faraj* amefanya kazi nzuri, hajasubiri Serikali ilet fedha ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Dr. Festus Limbu kwa mchango wako na kwa kweli umegusa maeneo muhimu kabisa yanayohusu maslahi ya Askari wetu. Nakushukuru sana.

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa James D. Lembeli na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami ajiandae.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza mchango wangu kwa kuwashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kutekeleza kwa haraka sana agizo ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alilitoa ndani ya Bunge hili la kuwatoa nje kwa dhamana na hatimaye kuwafutia mashitaka wananchi 14 wa Kata ya Mwendakulima amba walikuwa ni mionganoni mwa wananchi zaidi ya 400 walioandamana hadi katika lango kuu la Mgodi wa Buzwagi wakidai kusikilizwa na wakidai haki zao. Kwa niaba ya wananchi hao naomba niwashukuru na niwapongeze Viongozi hawa wawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hekima na busara aliyoitumia katika kutoa agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita zaidi katika bajeti nzima ya Wizara hii. Kwa maoni yangu, bajeti hii haistahili ukizingatia uzito wa kazi amba Wizara hii imepewa. Serikali haiitendei haki Wizara ya Mambo ya Ndani na kwa mtazamo wangu ni kwamba hali hii inatokana na historia ya nchi yetu kwamba mara baada ya uhuru mkazo na msisitizo mkubwa wa bajeti ya Serikali ulikuwa katika ulinzi wa mipaka ya nchi yetu.

Mara baada ya Uhuru kila mmoja anafahamu nchi yetu ilikuwa kitovu cha harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika. Kwa hiyo, nchi yetu ilikuwa na maadui wengi na Serikali kwa kweli ilijizatiti kuhakikisha kwamba mipaka ya nchi yetu iko salama. Sasa nafikiri mtazamo huo umeendelea hadi hii leo, wakati mipaka yetu nina hakika iko salama, haina hatari kama iliyokuwepo huko nyuma kwamba leo hii hakuna Mreno, Makaburi hawapo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hali ya dunia imebadilika sasa hivi na mimi siku nyingine huwa najiuliza, hivi kwa nini watu wanazunguka dunia nzima wanasema Tanzania ni kisiwa cha amani wakati kuna Watanzania hapa usiku na mchana hiyo amani ambayo watu wanazunguka wanatangaza haipo, majambazi yametawala kijiji, Dar es Salaam pale kuna siku tunaambiwa majambazi yametawala mtaani kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningiombwa Serikali iitendei haki Wizara hii kwa kuwa na mtazamo mpya ipewe bajeti inayostahili kuweza kuhimili sasa maadui walioko

ndani ya mipaka ya nchi yetu na hao maadui ni majambazi, majambazi yametawala. Lakini Polisi wanalaumiwa, kila mmoja hapa anasema Polisi wanampongeza Waziri, lakini baadaye wanasema majambazi majambazi, hawana pesa.

Bajeti ya *operation*, *operations* siyo *scheduled*, hazipangwi, inatokea ghafla, majambazi yamevamia kijiji fulani, basi Polisi wanaondoka, lakini Polisi hao wote wanaokwenda kwenye *operations* hawalipwi posho zao na wanaidai Serikali mabilioni ya pesa na kwenye bajeti hii hakuna mahali ambapo kuna fungu limewekwa wazi kwa ajili ya kulipa hayo madeni ambayo Polisi wanaidai Wizara. Lakini hao hao tunawategemea waende kwenye *operations* nyinge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama siyo bajeti hii, safari hii mimi naunga mkono hoja hii kwa sababu Wizara mbili nimekataa kuunga mkono hoja, lakini baadaye nimekubali, kwa hii ninaunga mkono hoja, lakini nikiwa na matumaini kwamba Serikali iiangalie Wizara hii kwa jicho tofauti kabisa na miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ukawa na Jeshi la Polisi ambalo ni *effective* wakati katika kila kona ya Jeshi la Polisi kuna mapungufu, idadi ya Polisi hapa nchini haitoshi kuweza kupeleka Polisi kila sehemu ambapo Mbunge anataka, Polisi hawana vitendea kazi magari hawana, Wilaya kama ya Kahama magari mawili. Kutoka Kituo cha Polisi cha Wilaya kwenda Kijiji cha mwisho cha Wilaya ya Kahama katika Jimbo langu ni kilomita 150, ujambazi ulitokea Kata ya Ulowa kilomita 120 kutoka Kahama Mjini lakini kwa *speed* ambayo ni Mwenyezi Mungu tu anajua Polisi waliweza kutoka Kahama Mjini na kuwawahi wale majambazi ambao walikuwa wametangaza uhuru wa masaa matatu wakishambulia nyumba moja baada ya nyinge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Askari wa Kahama kwa kazi nzuri waliyoifanya siku hiyo kuwaokoa wananchi wale wa Ulowa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo niongee kuhusu *Traffic* na ningependa kujua wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hotuba yake aniambie hivi kazi ya *Traffic* barabarani ni kusimamisha mafuso tu, malori makubwa na mabasi na haya magari mengine hayana matatizo?

Nina hakika Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wakienda Dar es Salaam mambo haya wanayakuta, hata ule msururu wa malori pale Chalinze ni utaratibu ambao *Traffic* wajiwakea, mimi sijawahi kusimamishwa pale Chalinze, lakini wakiona lori linakuja huko nyuma tayari wameshakimbia na wakati mwingine wanataka kusababisha *accidents*. Sasa nafikiri uwepo utaratibu mzuri. Hawa watu wapewe majukumu barabarani, kuna vizuizi barabarani, basi Polisi wa kawaida wafanye hiyo kazi. Naamini magari mengi ya wizi yanayotoka Dar es Salaam yanapita humo humo walimo Polisi, lakini gari ndogo Polisi hawasimamishi, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni rushwa, lakini kwa suala la rushwa siwezi kuwalamu sana askari, ni kwa sababu ya vipato walivyonavyo. Serikali ifanye juu chini kuhakikisha kwamba vipato vyao vinaongezwa.

Nina mfano, miaka ya 1990, katika Hifadhi za Taifa kulikuwa na ujangili wa hali ya juu na ujambazi lakini kuanzia mwaka 1995 pale Hifadhi ya Taifa walipoboresha maslahi ya askari, leo hii hakuna jambazi anayeweza kuingia ndani ya Hifadhi ya Taifa akatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni kwa sababu wameboreshewa maslahi, mshahara wa kiongozi wa kikosi cha Hifadhi ya Taifa anapata Sh. 450,000/=, bado *night allowance* zake akikamata silaha na kadhalika. Sasa mtu anapokea mshahara wa Sh. 160,000, ana watoto wanne wengine wanasoma sekondari, anatakiwa alipe karo na unampeleka barabarani, hata ningekuwa mimi ningechukua. Sasa nifanye nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya hali halisi ya hawa watu ndiyo yanayopelekea kuchukua rushwa kidogo. Watu wa malori hapa wamepanga pesa shilingi elfu mbili mbili au moja moja, kila kituo cha Polisi anatoa mkono tu afande habari yako, wakishikana mkono amemwekeea hapo shilingi mia tano, anamwambia endelea. Sihalalishi rushwa, lakini ndiyo hali halisi. Kwa hiyo, hawa watu maslahi ya Polisi, watu wa Uhamiaji, Magereza, tunalamika hapa madawa yanaingia Magerezani, ni mtindo huo huo na ni rahisi sana kuwadhibiti watu ukishawaboreshea maslahi yao, lakini kama hujawaboreshea unategemea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa Jimbo langu la Kahama. Wilaya ya Kahama ina eneo karibu la kilomita za mraba elfu kumi, ina askari wasiozidi mia moja na ina magari mawili. Wilaya ya Kahama ni mionganoni mwa Wilaya ambazo silaha za kivita zimezagaa, ujambazi ni mwangi, askari hawatoshi. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, tuongezewe askari Kahama na vifaa kama magari ili hawa vijana waweze kufanya kazi ambayo imewapeleka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitoe mwito mwingine kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kahama ahakikishe anashirikiana na Sungusungu. Sungusungu katika Wilaya ya Kahama na Kanda yote ya Ziwa ndiyo tegemeo la wananchi lakini katika siku za hivi karibuni kumekuwana matatizo, sungusungu wameilalamikia Polisi kwamba inashirikiana na majambazi. Sungusungu wakikamata wezi wa ng'ombe majambazi vijijini wakiwakabidhi kwa Polisi kesho asubuhi wako kijijini wana-*harass* sungusungu. Jambo hili sio jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kurudia kusema tena kwamba, Polisi wamewalalamikia Polisi kwamba wanashirikiana na majambazi kwa sababu Sungusungu wakikamata majambazi, wakawakabidhi Polisi kesho yake asubuhi yameachiwa, yanarudi vijijini, yanawatambia wananchi. Sasa hali hii itawakatisha tamaa sungusungu ambao ni tegemeo la wananchi katika Wilaya kama ile ambayo haina Polisi wa kutosha, naomba sana Serikali iwaelekeze Polisi kwamba, wawe na ushirikiano wa karibu na sungusungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kugongewa kengele ya pili, napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie. Kwanza kabisa, nianze na pongezi kubwa kwa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, dosari chache chache haziwezi kukosekana kwa kila binadamu. Pili, niwapongeze Magereza ambao wanafanya kazi nzuri sana, jikaona au kusikia Magereza wanapata lawama nyingi ingawa katika utendaji wao wa kazi wana shida kubwa ya kutokuwa na vitendea kazi, posho za kutosha na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Uhamiaji kwa kazi kubwa wanayoifanya na ni ya makini sana ingawa hapa na pale nao hupata lawama. Zimamoto pia wanafanya kazi nzuri ingawa vitendea kazi hawana, mafunzo mengi hayatoshi na hawana watumishi wa kutosha, nao wanapata malalamiko. Eneo la wakimbizi nao wamefanya kazi nzuri na mtaona sasa hivi wamejitalidi kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali hata wakimbizi wengi wamekwisharudi makwao. Wote hawa nawapa pongezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana, naifurahia. Sasa naomba niende haraka haraka maana yake dakika kumi na tano sio nyingi. Kwanza, naomba niishukuru Wizara na Jeshi la Polisi kwa kupata *solar* katika kituo cha Wilaya ya Polisi pale Namanyere kwa muda mfupi uliopita, nawashukuru sana, lakini nina malalamiko machache, kwa mfano, jengo la Polisi mliniahidi kwamba mngeweza kulimalizia ili kusudi ikiwezekana Makamu wa Rais au Waziri Mkuu aweze kulifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hili limeanza kujengwa mwaka 1983, leo hii lina miaka 23 bado halijakwisha na wala halijafunguliwa. Jengo hili ingawaje limekwishaanza kutumika lakini halina maji wala kisima. Kwa hiyo, ni shida sana na kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na *IGP* waliahidi na Mheshimiwa *IGP* kwa kweli niliongea naye na akasema ahadi hiyo ingeweza kutekelezwa katika bajeti hii lakini jikaona mahali popote palipotajwa jengo hilo la Nkasi kwamba linamaliziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana na namwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo litakwisha kwa sababu najua Mheshimiwa Makamu wa Rais anakuja mwezi ujao, sina uhakika kama litakwisha au vipi. Je, atanihakikishia kwamba litakwisha lini? Pia hawana gari la *OCD*: Je, wanategemea kazi atafanyaje na kwa maana hiyo nasikitika kusema kwamba natoa shilingi na sitaweza kuirudisha. Nadhani Wizara hii ndiyo itakuwa ya kwanza kutoka kwangu kutoa shilingi *and I think you know how serious I am*. Mnanihahamu jinsi gani niko *serious* ninapoamua jambo fulani, huwa sibabaiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende upande wa Magereza. Gereza la kilimo lile la Namteketa ambalo lipo kilomita kumi na sita kutoka Namanyere Makao Makuu ya Wilaya. Nilikuwa naomba lipewe gari kubwa kwa ajili ya kusaidia kusomba kuni, bidhaa mbalimbali kutoka pale mjini na kadhalika na vilevile kwa ajili ya kusaidia wafungwa. Maana yake wafungwa kwenda hospitali pale Namanyere hizo kilomita ni nyingi sana, wanapougu sana wanapata shida na nyumba za askari pale Namteketa naomba zijengwe maana yake hawawezi kuwa na nyumba yoyote ya kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende upande wa uhamiaji. Uhamiaji ni chombo muhimu sana duniani, hakuna Mbunge yeoyote hapa ambaye hajui chombo hiki, maana wote tumekuwa tukisafiri kwenda nje ya nchi.

Chombo hiki kina kazi kadhaa, nitataja chache tu, kama vile kutoa hati za kusafiria, wanapokuwa mpakani kushughulikia watu wanaotoka mpaka wanaoingia kuhakikisha kwamba wanafanya shughuli halali, kuhakikisha wanalinda wageni wote ambaao ni haramu na vilevile kutoa hati za makazi kama vile *residence permit* za aina mbalimbali, *dependant pass* na *exemption* na hati mbalimbali ambazo ni nyingi tu. Wanafanya shughuli za upelelezi kushika, kushtaki na kushughulikia mashtaka Mahakamani na vilevile wanashughulikia suala la uraia, nani ni raia na nani sio raia. Suala hili la kujua nani raia, nani sio raia, popote duniani utakapokwenda ni la uhamiaji tu, sio la chombo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kazi hizo, lakini hawana vitendea kazi kwa mfano hawana magari, magari yao ni ya zamani sana, yamepitwa na wakati na wala hayatoshi, hawana *radio calls* za kuweza kuwasiliana pale wanapofanya shughuli hizo. *Retention* maana yao ili kushughulikia shughuli zao mbalimbali hazitoshi na hapa nilikuwa napendekeza na kuomba angalau wapewe *seventy percent* sio chini ya *fifty percent* ambayo wanapewa leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho unashindikana, unakuta watumishi wanakaa muda mrefu kama miaka kumi, ishirini na kuendelea. Posho zao ni ndogo, kwa hiyo, nilikuwa napenda wajaribu kupewa fedha za kutosha ili waweze kusaidia. Wazalishaji wazuri sana wa kitaifa, hawa ni *revenue collectors* wazuri tu. Kwa hiyo, mkiwapa fedha ya kutosha watazalisha zaidi, hawa wanazalisha zaidi kuliko Polisi, Magereza na kuliko Idara nyingine yoyote iliyopo Wizara ya Mambo ya Ndani. Lakini hivi ni kwa nini mpaka leo uhamiaji haina sera ya uhamiaji? Mnaiendeshaje idara bila kuwa na sera ya uhamiaji? Chombo kikubwa kinachoheshimika na kuaminika duniani hakina sera! Kwa hiyo, waandalieni sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijaribu kuongelea suala la uraia na vitambulisho. Vitambulisho vimecheleweshwa sana na vitambulisho ni muhimu sana duniani. Vitambulisho ni suala la uhamiaji. Kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mtemvu, ni suala la uhamiaji na sio la chombo kingine chochote kile. Vyombo vingine vinaweza kushirikiana na uhamiaji lakini sio chombo kingine kushughulikia masuala ya uraia. Mnataka kutuletea Wanyamlenge wawe raia bila sababu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 1986 ndipo Serikali na Bunge walipitisha suala hili kwamba vitambulisho viwepo na watu wengi walilalamika na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliongoza hasa Kitivo cha Sheria. Nakumbuka wakati ule akina Shivji walikuwa wanalalamika sana, mnataka kutuletea sheria hizo, tunataka kuwa kama watu wa Afrika ya Kusini na vitu kama hivyo. Walipinga kwa nguvu zao na wakataka hata kuandamana ili vitambulisho hivi visije.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Dr. Lamwai peke kutoka kwenye kitivo hicho ndiye aliyeweza kutetea kwamba hapana, vitambulisho ni muhimu na vina faida nyingi na akatoa mifano mbalimbali za Mataifa ambayo yana vitambulisho kwa ajili ya kulinda usalama wa nchi yao. Leo hii wananchi wa Tanzania sasa wanataka vitambulisho na hata wale waliokuwa wanapinga wakati huo wanataka vitambulisho. Nchi jirani wanavyo vitambulisho, katika Afrika Mashariki nadhani bado Uganda na hii Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba *tender* imekwishatoka kwa ajili ya vitambulisho. Najua mambo yanaiva sasa. Sasa vitambulisho kama nilivyosema ni usalama wa nchi, Waziri amesema *tender* yake ni *open tender*. Hili ni kosa kwa sababu vitambulisho ni usalama kabisa mia kwa mia, ni sawasawa na unapotengeneza pesa, unapoagiza silaha, mia kwa mia ni siri ya nchi. Unapotangaza kwa uwazi, ni kosa, ilipaswa iwe ni *restricted tender*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, ulizeni nchi zilizotengeneza vitambulisho wamefanya hivyo, ninyi mnajianika, haya jianikeni kesho na kesho kutwa mtasikia mambo. Nashauri vitambulisho vitengenezwe kwa mtindo wa *smart card*. Ninaposema *smart card* kwa msomi anayejua, anajua *smart card* leo ndiyo teknolojia mpya ya kisasa na ambayo ukiifanyia kazi vizuri mtandao wake ni mzuri, unaeleweka zaidi kuliko ule wa *bar code*. *Bar code* ni mtindo kama ule wa vitambulisho ambavyo vimetengenezwa kama Kenya, Zambia hata wenzetu wa Zanzibar katika kutengeneza wanatumia hiyo *bar code*. Hii imepitwa na wakati.

Ukitaka kupata habari zake ni lazima uende Makao Makuu pale walipo-*install* vyombo, lakini hii ya *smart card* unapotaka kuifanyia kazi mahali popote ulipo hata kama ingekuwa porini unatumia kitu kinachoitwa *reader*. Popote pale ukichomeka ni kama vile wale ambao tuna kisukari, unapochukua damu yako kidogo, unaingiza kwenye chombo fulani palepale inapima tata tatata, unajua leo hii kiasi gani sukari yangu ilivyo, ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, inatakiwa utafiti ambao tayari umekwishakamilika. Naomba muache ubinafsi kwa sababu tayari baadhi ya watu tena wakubwa kabisa wanaanza kubishania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyami naomba dakika moja kidogo, kumetokea dharura kwenye Kamati yangu, nitamwomba Mheshimiwa Job anipokee halafu utaendelea.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyami endelea na dakika zako zitatunzwa.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nilishampongeza Mheshimiwa Waziri na nikasema naomba Mheshimiwa Waziri wale watu wote wenye uchu wa kutaka kuupata huu mradi tena wanaotaka kuupata huu mradi kwa kutumia *bar code* ambayo ni ya zamani ambayo kesho na keshokutwa itatuingiza kwenye matatizo makubwa na kuharibu uchumi wa nchi hii kwa sababu vitu hivi ni gharama, hii *bar code* Watanzania wengi wanaweza kuitengeneza, lakini hii ya *smart*

card Watanzania wanaoweza kuitengeneza hakuna kwa sababu katika nchi ya dunia hii Malaysia ndiyo wanaoongoza na nchi zote nenda Marekani, Uingereza wapi wote wanakwenda kwenye *smart card* na wale wote ambao wapo kwenye *bar code* kama vile Kenya nao wanaachana na hiyo na wametupongeza sana Watanzania kwa sababu tumefanya tafiti zote mbili.

Tumefanya utafiti wa *bar code* na tumefanya na utafiti wa *smart card* kwa kutumia wenzetu wa Chuo Kikuu pamoja na wa Takwimu. Suala hili limekwenda vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba hebu wachunguze sana na wawekee jicho sana wale wanaosema kwamba wanataka *bar code, no, smart card*. Nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekaa Marekani, anakielewa hiki kitu, apige vitu *bar code*, atetee *smart card*, ndiyo maana narudia rudia. Sasa hivi dunia inaelekea kwenye teknolojia mpya. Sasa hivi tuna kompyuta, watu walitaka tubakie na *typewriter*, leo hii zote zimekwishatupwa chini, kila mtu anashughulika na *computer* kwa sababu mambo yote duniani ni ya ki-*computer computer*, tuachane na hiyo ya zamani.

Faida ya mradi huu wa vitambulisho, kwanza licha ya kusaidia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya uhamiaji lakini itasaidia vizazi na vifo, itasaidia upande wa Polisi kwa upande wa *licence* hizi za udereva, itasaidia Halamshauri, *Local Government* kwa sababu gani, wale pia watafanya kazi ya kutambua hawa watu raia ni nani ili kusudi uhamiaji iweze kuchekecha na vilevile Tume ya Uchaguzi kwenye ile *voter registration* watu wa *TRA* katika kukusanya mapato watapata mapato ya kutosha kwa sababu hiki kitambulisho kitakuwa na aina fulani ukikichomeka pale kinaonyesha namba zako zote, kama una *licence* itakuonyesha ulipaji wako wa kodi ulivyo, itaonyesha kila kitu na ni mahali popote patakapokuwa na hizo *reader*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala la uraia wa nchi mbili. Uraia wa nchi mbili hauna sera, kwanza tutengeneze sera ya uraia, halafu ndipo tutengeneze sera ya raia wa nchi mbili na ndipo tuliongelee suala hili. Kwa wakati huu kama alivyosema Mheshimiwa Mtemvu haitusaidii sana, utasaidia watu wachache wachache na hasa weupe, wazalendo hautawasaidia na pesa nyingi zitatoroshwa sana kwenda nje na kama kuna wachache weusi wanaotetea hiki kitu ni wale wachache wenye watoto zao waliopo nje, wanataka tu kwa faida zao ndogo ndogo, lakini madhara yake kwa wakati tulionao ni makubwa, tungoje baadaye, tukishakamilisha vitambulisho, tukiwa na uhakika wa uraia wetu ndipo tuongelee suala hili la *dual nationality*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, siungi mkono kabisa mpaka tutakopofika kwenye vifungu mkinitekelezea yale. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi au watumishi wa Wizara hii wametetewa sana, tumewatetea sana toka jana mpaka leo na tutaendelea kuwatetea lakini shida yetu

kubwa na shida ya wananchi wetu ni haki. Tunachotaka ni kwamba wananchi wetu waweze kupatiwa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamanda wetu Said Mwema ni mwadilifu na hana matatizo ndiyo maana utakuta hata kugombana na wanasiisa hilo hana. Miaka ya nyuma tulikuwa tunasikia wanasiisa wanasema sisi ngangari na wao wanasema sisi ngunguri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo ndiyo kuna matatizo kwa sababu askari hapaswi kujiingiza kwenye masuala ya siasa, wao ni kufanya kazi. Sasa tumeuona uadilifu huo na tunaomba aendelee hivyo, afanye kazi kimya kimya ili aweze kusaidia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Mheshimiwa Dr. Masha nadhani ni wa makusudi kabisa. Huyu mtu ameishi nchi ambayo inatenda haki kwa raia zake na ni mwanasheria, sasa nadhani uteuzi huo ni wa makusudi kuhakikisha kwamba anarekebisha hii hali na ameonyesha katika hotuba kwamba kuna mipango itakayofanywa ili kuweza kurekebisha Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria Jeshi hili ukiangalia toka uhuru hakuna mabadiliko makubwa. Mwaka 1964 wakati yalipotokea maasi ya Jeshi la Wananchi wakati huo linaitwa *Tanganyika Rifles* tarehe 20 Januari, 1964, Mwalimu aliamua kulivunja hilo jeshi, akaliunda barabara kwa misingi ya kwamba linakuwa Jeshi la Wananchi na hilo jeshi limebaki kuwa la wananchi mpaka leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika Idara yetu ya Usalama wa Taifa, hawa watu wamebaki waadilifu, wamefanya kazi kwa uaminifu kabisa kulinda nchi hii lakini bado tuna matatizo makubwa kwenye Jeshi la Polisi na matatizo hayo ndiyo yamezungumzwa. Kwa muda mfupi niliopewa sitatetea sana kama ambavyo wenzangu wametetea kwa sababu nimesema kwamba tumetetea sana. Hii idara ya *DCI* (*Directorate of Criminal Investigation*)- Fungu 7001, sioni sababu kwa nini tunatoa fedha kila wakati kwa idara hii? Hizi fedha badala ya kwenda kuwasaidia wananchi nadhani zinakwenda kuwakandamiza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Trafiki, *Railway Police Division* halafu *Public Safety and Security* tena hii afadhali ingeitwa *Private Safety and Insecurity Monitoring*. Maana *feelings* za wananchi kule, maana turudi nyuma, tusizungumzie hali yetu sisi, sisi ni *percent* ndogo sana ya wananchi wetu, wananchi wetu wanaishi vijijini. Mwulize mwananchi ye yeyote *opinion* yake au mtazamo wake kuhusu Jeshi letu la Polisi. Hii ndiyo *feeling* ya wananchi kwa ujumla, wanasema kwamba Jeshi la Polisi halipo kwa ajili ya maslahi ya wananchi, lipo kwa ajili ya maslahi ya viongozi na watu wachache wenye uwezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri jana niliwaandikia mapema kabisa kwamba, ningeomba nipate majibu ya uhakika kuhusu kesi ya Mwalimu Abraham Mika Mongo wa Mitundu. Huyu mtu tarehe 4 Mei, alikuwa ana-*prepare lesson notes* zake kwa

ajili ya kwenda kufundisha. Ghafla saa mbili asubuhi Polisi wakafika na gari na Polisi watatu wenyе silaha wakamwambia unatakiwa kituoni Manyoni kilometa 100 wakati kuna kituo kingine kipo kilometa saba. Akauliza kwa nini? Wakamwambia unatakiwa kwa mahojiano, wanaita kusaidia Polisi. Unakwenda kusaidia, lakini hurudi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu bwana kachukuliwa kapelekwa kule, lakini kabla ya kufika *destination* hiyo, kuna sehemu moja inaitwa Legeza Mwendo karibu na Doroto, kutoka Mgandu gari lile la Polisi likapinduka. Yule bwana akavunjika mguu, wale Polisi na bunduki zao wakachubuka chubuka, hamadi gari lingine likafika likawachukua, likawapeleka *Gasper Hospital - Itigi*. Kufika Gasper pale wale wenyе *bruises* wakatibiwa, yule bwana akalazwa, akawekewa *POP*. Huyu aliyekuwa anaongoza hicho kikosi, ofisa wa upelelezi akamwambia bwana ukipona urudi nyumbani. Huyu bwana kweli baada ya miezi miwili akatoka pale, kama raia mwema akaenda kituoni kwenda kuuliza kulikoni? Akaambiwa ahaa, bwana tulikosea sio wewe, hii pitcha, hizi sharubu zimefanana na za kwako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakamwambia rudi nyumbani tu. Huyu bwana akawekwa katika *position* hiyo ya kuvunjika mguu na mpaka leo ni kilema, ikabidi hata *the other kind face of Government* (Halmashauri ya Wilaya) ikaanza kumsaidia kumpeleka Muhibili kutibiwa na gharama nyininge. Huyu mtu kwenda kwa wakubwa Polisi anazungushwa, akaenda Tume ya Haki za Binadamu, haki za binadamu akaletewa majibu kwamba inabidi wakufidie, *ana-claim* fidia ya Sh. 20m/= kwa matatizo aliyoyapata. Amezungushwa na sasa anafikiria kwenda Mahakamani, lakini imebidi amwone Mbunge wake, aone pa kukimbilia kwa sababu kwenda Mahakamani ni gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika, wale waliohusika wakapewa adhabu ya uhamisho, tena wamepelekwa kwenda kwenye Jimbo la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma huko Mtware, mbali kabisa. Namwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo gari lililopinduka limetengenezwa kwa gharama za nani? Kwa sababu *OCD* alipoulizwa akakana, akasema hawa jamaa waliiba gari, wakatoka nalo. Kwa hiyo, tunaomba maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka maelezo kuhusu *issue* ya Mosi Mpole wa Muhang'a. Hii kesi sawa na ya Mheshimiwa Misanga, amedhulumiwa ng'ombe 48, wamechukuliwa kwa kisingizio cha ajabu sana na wakauzwa kwa kusema kwamba, ni ng'ombe wa Serikali wakati ni wake. Sasa tunataku kujua kama kweli hawa ng'ombe ni wa Serikali, *details* zake siwezi kuzieleza kwa sababu nitaishiwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka maelezo ya Bwana Mghenyi Senge. Huyu bwana ametoka Marekani, amekuja kushughulikia matatizo yake, ana nyumba ambayo alikuwa anataka kudhulumiwa, Mheshimiwa Waziri anayo barua hiyo. Walipoanza kuona kwamba anajua haki wakamrudishia *passport* yake, wakafuta na ile

kesi, lakini aliwekwa ndani, akazungushwa tena Mghenyi Senge ni Chifu wa Wanyaturu. Kweli mtu kama huyo anaweza kukimbia kwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa pia nataka kupata maelezo kuhusu Ndugu Sylvester James wa Msati Musoma maana msije kusema ni maeneo yangu tu.

Halafu nina kesi mbili za Kisutu ambazo zinasemekana zimefutwa kwa sababu wale watuhumiwa hawakuonekana; *these are murder cases*. Hakimu Mkazi wa Kisutu Hezron Mwakanje aliacha kusikiliza kesi mbili za Mauaji kwa madai zimetajwa kwa miaka kumi bila upelelezi kukamilika. Upande wa mashtaka ulishindwa kueleza sababu za msingi za washtakiwa kufika Mahakamani.

Kesi Na.21 ya mwaka 1998 inayomkibili Hashim Mulaka anayetuhumiwa kumuua Hamisi Mamba eneo la Sinza, kesi ilifunguliwa tarehe 19 mwezi Agosti, 1998, mshtakiwa alifikisha Mahakamani kwa mara mwisho tarehe 18 Mei, 1999 na mpaka sasa hajaonekana. Mahakama imekuwa ikitoa hati za kumwita Mahakamani mara 80, lakini hajawahi kutekeleza maagizo hayo na upande wa mashtaka hauelezi sababu za msingi ni kwa nini mtuhumiwa huyo hafiki Mahakamani. Kesi nyingine ni Na. 26 ya mwaka 1999 Mohamed Hamisi aliyemuua Daniel Hagosti, huyu ameitwa mara 117 lakini hajaonekana. Hao watu ni washtakiwa wa mauaji, wamekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeliomba nipate maelezo ya kina kuhusu masuala hayo ambayo nimeyaelezea. Kuhusu matrafiki wamekwishaeleza wenzangu na matatizo na ubovu wa magari na ajali. Katika ripoti, ukurasa wa nne matukio ya jinai yanazidi kuongezeka na sababu tulizopewa bado haziridhishi. Wamesema ni kwa sababu wanafanya *operation* ya kusaka watu na hivyo unakuta matukio ya jinai yanaongezeka sidhani kama ni sababu za msingi zilizoelezwa ukurasa wa nne. Sasa sisi ni wahanga wa mapungufu hayo ya Polisi. Matatizo yao yanaletwa kwa wananchi. Mimi ningeliomba hao watu wa trafiki, hata juzi hapo Pandambili mwenzetu alipofariki wanassema eneo lile ni mara kwa mara ajali zinatokea. Sasa kwa nini hawazuii kama walikuwa wanajua ajali zinatokea mara kwa mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata magari yenewe yale yanabeba ujumbe gani? Unakuta malori yale yanayosimamishwa ni mabovu na mengine ni mabasi, mengine huku yameandikwa Tenda Wema Nenda zako, lakini mengine yameandikwa Usipime. Sasa usipime ni ujumbe gani? Hawaoni viongozi wa nchi wana kampeni kuhusu masuala ya *UKIMWI* na kuhusu kupima, gari limeandikwa huko nyuma, “Usipime”! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli hii ni halali kweli! Maana yake wao sasa wanaona mbele tu, ni yule dereva na gari lake, lakini nyuma huku hata gari limeandikwa Utajijua, hajui, gari linaondoka anaangalia mbele. Sasa upofu gani huu ndugu zangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba malipo ya posho walipwe Askari wangu wa Manyoni, wamehamishwa wamepelekwa katika Vituo mbalimbali lakini hawajalipwa posho ya kujikimu, wameambiwa nyie ni amri moja, basi wamenilalamikia, sina muda wa kulieleza, lakini hilo lifanyiwe kazi, na ninaomba wapewe kifuta jasho hao Askari

watano waliomua jambazi sugu sana pale maeneo ya Mgandu, Kitaraka pale, huyo jambazi alisumbua watu kwa miaka mingi sana, lakini hao Maaskari niliuliza swali la msingi hapa wakasema ooh, watafuata utaratibu. Hao Maaskari walifanya kazi nzuri kwa sababu sasa hivi wananchi pale ni afueni, huyo jambazi aliua watu, aliteka magari na kuwavua watu nguo, akinamama na akinababa. Sasa unauliza, unaambiwa kwamba ilikuwa kazi yao. Hiyo siyo *fair*, kwa sababu *it is a matter of life and death*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza, kama na mimi nitabambikizwa kesi kwa kuzungumza, basi naiwe maana maisha ya wananchi wangu ndiyo hivyo. Kila siku wanabambikiza kesi, ukiwa na ng'ombe na ukiwa tajiri ni kosa. Wengine wanachukua *advantage za ignorance* ya watu kule. Ana ng'ombe, kwake ni kosa. Ni kengele ya mwisho. (*Makofi/Kicheko*)

WAHESHIMIWA WABUNGE: Ndiyo.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

(*Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa John Lwanji. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mgana Msindai na kama akiokoa muda, nitamwomba Mheshimiwa Faida Bakar, atatumia dakika zitakazokuwa zimebakia. Mheshimiwa Mgana Msindai.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ingawaje ultaka kuninyima haki yangu, lakini nimekusamehe bure. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi hii nichangie Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya fedha kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kukumbusha na mimi nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ni watu wanaofanya kazi kufuatana na misingi maalum na wakitoa ahadi kwa kweli huwa wanatekeleza. Mimi niwakumbushe kwamba wasije wakasahau ahadi walizozitoa kwa Iramba Mashariki. Iramba Mashariki nikianza na Kituo cha Polisi Iguguno ambapo nguzo ya umeme imekaa mita moja kutoka kwenye jengo la Polisi na huu ni mwaka wa tano hawajaunganisha umeme pamoja na ahadi waliyoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri hebu aone aibu uunganishe umeme pale Kituo cha Polisi Iguguno. Jimbo la Iramba Mashariki Mheshimiwa Waziri limekingwa na milima, wananchi wa Iramba Mashariki ni vigumu sana kwenda Makao Makuu ya Wilaya na taarifa yake Mheshimiwa Waziri nimwambie zaidi ya nusu ya Iramba Mashariki inalindwa na sungu sungu na kwetu tunawaita “Nkili” kwa sababu Askari waliopo hawatoshi, Askari waliopo kuna vituo vinne hawana silaha. Kuna Kituo cha Ibanga, Kituo cha Mwagenza, Kituo cha Ikungi na Matongo na sisi

tunapakana na Wilaya ya Hanang, Mbulu, Karatu na Meatu na sehemu ya Nyahaa – Mpambala- Endasiku ni sehemu ambayo wizi wa mifugo unaendelea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliahidi kwamba ingetoa gari kwa Kituo cha Nduguti ambacho ndiyo kikubwa na kiko katikati na kuongezea vifaa vingine. Lakini mpaka leo bado hawajafanya hivyo. Mimi ninawaomba kwa nia njema kabisa na nimwambie Mheshimiwa Waziri Askari ambao wamekaa katika Jeshi la Polisi zaidi ya miaka 15 wanafahamu Iramba ya Mashariki ikoje. Maana mara kwa mara walikuwa wanaitwa kwenda kutuliza vita kati ya wenyeji wa Iramba Mashariki aidha na wa Karatu na Mbulu kwa kuibiana ng'ombe. Kwa hiyo, wanafahamu. Mimi ningeomba wajitahidi sana kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi uliopita mwishoni palitokea tukio mimi nikiwa hapa Dodoma nikapiga simu kwa Mkuu wa Wilaya hakuwepo alikuwa Dar es Salaam, lakini ye ye akampigia simu *OCD* kulikuwa na ugomvi wafugaji wanagombea maji na walikuwa tayari kwa mapigano, *OCD* alijitahidi lakini alifika saa tano usiku akakuta wananchi wamekwishanyamazisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kazi kubwa sana kutoka Kiomboi kwenda Endasiku au kwenda Mwageza ni maeneo yaliyopo zaidi ya kilomita 100 toka Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, ningeomba Kituo cha Nduguti kiongezwe nguvu, kipewe gari na kama magari hakuna, basi kipewe pikipiki Nduguti na Ibaga. Mimi naona niishie hapo. Nina imani sina haja ya kukamata shilingi, lakini ninajua watatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi hapo nilitembelea Mkao wa Ruvuma kwa kweli ninaipongeza sana Serikali kwa kujenga daraja kwenye Mto Mkenda, naipongeza sana. Lakini sasa kwetu bado inataka kutokea kama ilivyotokea Rombo. Wenzetu wa Kenya wakajenga Uhamiaji, wakajenga Kituo cha Polisi na wakajenga *Customs* na sisi kwetu kukiwa hakuna na huko itatokea hivyo. Wenzetu wa Msumbiji wamekwishajenga *customs*, wamekwishajenga Kituo cha Polisi, wamekwishajenga Ofisi za Uhamiaji, lakini kwetu sisi hatujaanza. Hebu hilo jambo lichukuliwe kama jambo la dharura *at least* tulingane na wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo limetuvuruga sana sisi watu wa Mkao wa Singida, sisi Waheshimiwa Wabunge karibu wengi makazi yetu yapo Singida Mjini. Kuna huo wizi wa ng'ombe uliotokea Sepuka. Mwezi uliopita Waziri alisema anakwenda kukabidhi ng'ombe, aseme anakwenda kukabidhi ng'ombe wengine au fedha, lakini ng'ombe hao zilizokamatwa ziliuzwa na Mkuu wa Kituo cha Polisi Singida. Kuna vijana wawili wa Polisi walihusika na bahati nzuri siku ya tukio mimi nilikuwa Singida. Hao ng'ombe walikamatwa Sepuka, tena kijana mmoja wa Polisi alitoka Makao Makuu ya Wilaya na yule mwingine alitoka Sepuka, wakazikamata hizo ng'ombe, wakaenda kuzikabidhi kwa *OCCID* kesho yake wale ng'ombe wakapotea. Vijana wakashtakiwa na tunamshukuru Mungu wakashinda kesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule aliyekabidhiwa ile mifugo alihamishwa baada ya muda mfupi, na mpaka sasa tunasikia yupo Dar es Salaam. Serikali inasema nini juu ya hilo? Kwa kweli ni aibu Serikali inajipaka matope. Kwa hiyo, sisi tunaomba uchunguzi

ufanyike na wale vijana hawakuwa na kosa, wameachiwa na Mahakamam hawana makosam warudishwe kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo tayari kuleta hoja binafsi au kuliomba Bunge tuunde Kamati ya Bunge ikachunguze hilo. Mimi ninajua Polisi ni watu wazuri kabisa na ni wachache wanaolipaka matope Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, ninawaomba sana na hili jambo lichukuliwe hatua haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakwenda kukabidhi hao ng'ombe atapokelewa kwa masikitiko, futilieni na hiyo kazi ifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hapa nchini Jeshi la Nkiri lilipoanza ndiyo Jeshi ambalo lipo na wananchi na ndiyo maana nimesema Iramba ya Mashariki sehemu kubwa inalindwa na hao. Kwa sababu Polisi wamewekwa kule kama picha, hawana silaha, hawana *radio call*. Nenda Matongo, nenda Ibaga, nenda Nkungi silaha zipo Nduguti ambako ni mbali na kwingine. Kwa hiyo, sisi tunaomba Polisi waangaliwe na waache ile tabia ya kusingizia, sungu sungu au Nkiri wanakamata wahalifu wakiwapeleka Polisi wanageuziwa kibao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaanzisha Polisi Jamii, lakini Polisi Jamii ilikwishaanza siku nyingi ndiyo hao sungu sungu na Nkili wanaofanya hiyo kazi. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ijipange upya. Mimi sina ugomvi na watu wa Polisi. Kwanza, kwa miaka 28 nilipokuwa Serikalini nilikuwa nafanya nao kazi katika *operation* mbalimbali na ninajua makamanda wetu na vijana wetu wa Polisi ni watu wanaoipenda kazi yao. Kwa hiyo, naomba sana hao sungu sungu na Nkiri waheshimike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana watu wa Uhamiaji kwa kazi nzuri wanayoifanya. Sasa hivi wanatengeneza *Passport* zetu na sasa hivi hazigushiwi kama kule nyuma na ni watu wanaotengeneza kwa makini sana. Hivi ni kwa nini tuendelee kung'ang'ania kuwapa hii *tender* wengine wakati watu wa Uhamiaji wanaweza kuifanya? Kwa nini wasipewe hii kazi waifanye wao na siri zote watazificha? Kuna nini Serikali inalazimisha kutoa *tender* kwa watu wengine? Wananchi wote wanataka hivyo vitambulisho vitengenezwe na watu wa Uhamiaji na wao ndiyo wanajua jinsi ya kufanya na ndiyo wanaijua nchi yetu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ibadilishe itoe *tender* kwa watu wa Uhamiaji wenywewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uraia wa nchi mbili, jamani tusiwe kikundi kidogo kinatuteka sisi Serikali, Watanzania bado hawataki uraia wa nchi mbili, tunakumbuka mateso tunayopata kutoka kwa wakimbizi mpaka leo. Leo mnataka uraia wa nchi mbili mnatafuta nini? Wakati wa kuwa na uraia wa nchi mbili bado. Sisi tunaomba uraia wa nchi mbili usitishwe labda mpaka mwaka 2020, kwa sasa tuendelee kama ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, ninaunga mkono hoja. Ni hayo tu nilikuwa nayo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mgana Msindai umeokoa muda, sasa Mheshimiwa Faida Bakar atapata dakika zake kumi na tano kama kawaida. Mheshimiwa Faida Bakar tusikie maneno ya Pemba kidogo.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kweli nilikuwa natetemeka hapa, nilifikiri sitapata nafasi, Mungu kanisaidia. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Wizara hii ama kumpongeza Mheshimiwa Masha na Naibu wake Mheshimiwa Balozi Kagasheki kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya katika Wizara hii kwa ushirikiano mzuri na wapiganaji na raia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja kwanza. Vile vile heshima kubwa na pongezi ziwaendee Ma-RPC wangu, Ma-RCOs wote wa Pemba, Kaskazini na Kusini na wa Wilaya zote nne za Micheweni, Wete, Chake Chake na Mkoani na wapiganaji wote wa Pemba na Watanzania nzima lakini mtu kwao kwanza. Mimi kwetu Pemba, kwa hiyo, natetea kwetu Pemba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makamanda hawa na wapiganaji hawa wa Pemba haijapata kutokea. Wewe mwenyewe si unaona amani iliyoko Pemba! Sasa ni kazi nzuri inayofanywa na viongozi hawa kwa ushirikiano mzuri na wapiganaji na raia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwenda moja kwa moja kutetea hoja sasa. Napenda kuongea kuhusu jengo la Makao Makuu ya Polisi Mkoa wa Kusini Pemba. Nilikuwa Mbunge mwaka 2000 wa Jimbo la Wawi. Toka mwaka napata Ubunge wa Jimbo la Wawi miaka ile mitano natetea jengo hili na wenzangu waliokuwepo wanatetea jengo hili na mpaka sasa tunatetea jengo hili, mpaka Mheshimiwa Masoud leo katetea jengo hili, lakini mpaka leo jengo lile ofisi ile ni mbovu.

Mheshimiwa Waziri nawaombeni wote mwende Pemba mkakague jengo lile. Twende pamoja tukakague jengo lile, sisi tunajua ninyi nafikiri hamjaenda nawaomba sana. Askari wetu wako katika hali ngumu katika jengo lile, linavuja. Kweli askari anaweza kufanya kazi kwenye jengo kama lile. Ni kupakwa rangi tu siku mbili tatu, nyufa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana, jengo ni bovu, naomba mlishughulikie jengo kama ni kukarabatiwa ama lijengwe tena jipyka kule Pemba . Lile jengo ni toka enzi za ukoloni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba nimeona hapa kwenye bajeti sijaona hata pesa mbili iliyotengwa kwa kukarabati jengo lile na sijui ni miaka mingapi lakini toka nianze mimi Ubunge huu ni mwaka wa saba natetea jengo. Hivi Mheshimiwa Waziri hamnionei huruma! Nioneeni huruma au mnataka nilie hapa leo? Askari wangu walie kule Pemba! Hatulii, lakini tunajua Serikali yetu ni sikiu na itatusaidia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja kwenye nyumba za askari wa Madungu, ChakeChake Pemba na Mkoani Pemba, Wete Micheweni. Katika ukurasa wa 44 hapa nimefarijika kwamba kuna Madungu. Hapa pameandikwa Madunga, lakini

naamini kama hii ni Madungu. Nyumba za Madungu zitafanyiwa ukarabati na hizi pia tunazitetea toka miaka iliyopita mpaka leo.

Tunashukuru kwamba angalau kwenye bajeti ya mara zimeingizwa. Nyumba zile ni ndogo, mbovu, vyumba viwili, mwenzangu jana alisema. Hata hakuzitetea zile za Madungu, lakini mimi nasema vyumba viwili vidogo askari wanazaa, chumba kimoja, baba, mama humo humo kwa kweli hiyo siyo haki. Tunaomba zikarabatiwe na nashukuru kwamba mara hii imeingizwa hiyo fedha. Lakini naomba hiyo fedha imetajwa hapa, sijaijua fedha ngapi, lakini naamini hii fedha itakuwa ni nyingi kwa sababu nyumba zile si kidogo. Kwa hiyo, zikarabatiwe zile nyumba askari na wao wafarijiwe. Kwa kweli nyumba ni mbovu sana, haziridhishi maskari wetu wanafanyakazi usiku, mchana wanajitahidi kwa kazi. Pemba ina amani sasa. Kwa hiyo, nao wapewe amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia Mheshimiwa Waziri, akija kunijibu aseme ni lini, maana zitakuwa zimewekewa fedha, lakini inawezekana ikapita miaka mitatu mbele au minne hazijakarabatiwa. Ni lini hasa kazi itanza ukarabati wa nyumba za askari Madungu? (*Makofi*)

Vile vile zimeingizwa nyumba za askari Madungu, lakini kuna Mkoani, kwa kweli utashangaa! Ukienda utaona imani! Mheshimiwa Waziri nafikiri hajaenda, naomba twende Mkoani. Vijumba vidogo vile ofisi hapo hapo, yaani inashangaza. Hata mtu akitokewa na mgeni kwa kweli ni aibu. Mheshimiwa Waziri tuwahurumie askari wetu, nyumba zifanyiwe ukarabati ama wajengewe nyumba mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya posho za uhamisho na safari. Kuna baadhi ya askari wa vikosi vya Pemba wanadai posho zao za uhamisho tokeo Julai, 2006 hadi mwaka huu wa 2008 bila mategemeo yoyote hawajalipwa. Naomba Mheshimiwa Waziri akija kujibu anijibu watalipwa lini kwa sababu sio vizuri mtu anategemea analipwa mpaka anakufa halipwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikosi vyote vya Tanzania nzima vitendea kazi kwa kweli ni hafifu. Vinakuwa hafifu kutokana na ufinyu wa bajeti, hatuwezi kulaumu, lakini bajeti inakuja ndogo shilingi bilioni mia mbili inasaidia nini? Isaidie kila kitu mpaka vifaa vya usafiri, magari mabovu hayafanyiwi *service*, vifaa ni vibovu, hakuna *computers*, hakuna simu, yaani ni chache na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wote wameshasema magari hakuna na hata kule Pemba magari hakuna na yaliyoko ni mabovu na sijui hawaingiziwi fedha za *Service*? Nafikiri hawaingiziwi. Kwa sababu ninavyoona askari wakipigiwa simu tu kama mahali pana tatizo saa hiyo hiyo utawaona wameshafika. Tunawapongeza askari kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa kule Pemba. Juzi, limetokea tatizo kule Pemba wakati niko nyumbani, limetokea tatizo tukapiga simu pale pale askari wakafika. Lakini magari mabovu, mwenzangu anasema na Karagwe, lakini hiyo kila sehemu. Lakini ndiyo hivyo, lakini kila aliyeshika kichwa chake natetea kwetu kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Vile vile hata kama hakuna magari, basi wapatiwe pikipiki kwa sababu kuna sehemu nyingine miundombinu ni mibaya, basi magari hayaendi; pikipiki inafika na askari wetu wako tayari kufanya kazi lakini hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Mfikiwa Wawi Pemba, nashukuru askari wetu wamejengewa nyumba nzuri za kisasa, tumefurahi sisi kule kwetu kwa sababu zamani nilikuwa nakwenda kukagua, sasa siku moja walikuwa wapo pale Mwanamashungi, walikuwa wamekaa kwenye mahema tukatetea hapa Bungeni toka siku hizo niko Mbunge wa Jimbo la Wawi, tukajengewa nyumba zile za kule Mfikiwa, lakini nyumba zile ni nyumba tu, umeme upo, tunashukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar kutuletea umeme, maji yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kidogo kinanisikitisha kule sehemu ni mbali sana na mji pale panatakiwa angalau pawe na *dispensary* hata ndogo kwa wale askari kwa sababu wana watoto, wana familia. Vile vile wapatiwe *nursary school* kwa sababu wale askari wana watoto wao watacaa vile mpaka lini ni mbali hawawezi kuwapeleka mjini, kwa sababu mjini ni mbali. Hapa tunaomba wapatiwe na wao *nursary school* hata kama ni ya kuanzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za masomo kwa askari. Askari, wanatakiwa wawe na elimu. Kila binadamu anatakiwa awe na elimu na sera zetu tunaelimisha tuwe na elimu, hata sisi humu tunakuwa na elimu, kila mtu anatakiwa awe na elimu pamoja na utalaam wake wa uaskari, lakini vile vile askari wetu wanatakiwa vile vile wajiongezee elimu ya kuijendeleza haya ya Chuo Kikuu.

Lakini unakuta askari wetu wakiomba nafasi za masomo ya kuijendeleza mfano za Chuo Kikuu hata kama wameshaomba wameshaptiwa nafasi wameshajibiwa kama askari fulani umepatiwa nafasi, Mheshimiwa Waziri hamtoi fursa mnakataza kabisa hata kama mtu akiomba hamuwapi ruhusa askari kwenda kusoma. Mimi hii sioni kama ni haki, haki ya kusoma ni haki ya kila mtu. Kwa hiyo, kama askari anaomba nafasi ya kwenda kusoma kwa nini asipewe nafasi ya kwenda kusoma? Kwa hiyo, hili nalisema na naomba Mheshimiwa Waziri aje utujibu kwa sababu siyo vizuri askari kuwa anafanya kazi lakini elimu yake iko duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za askari Finya na Limbani Kaskazini Pemba, tunaishukuru sana Serikali yetu kutujengea nyumba tumeanzia na tatu, kule Finya ziko tatu zimejengwa sio haba na kule Limbali ziko tatu zinaendelea kujengwa sio haba. Kwa hiyo, tunaomba Serikali yetu vile vile hizi nyumba za *FFU* zilizo Finya, umeme umeshafikishwa pale lakini haujaingizwa kwenye nyumba zao. Tunaomba ufikishwe angalau ndani ya zile nyumba. Vile vile maji yameshafika lakini lile tenki la maji la kuhifadhi maji hakuna. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali yetu ni sikivu na naamini itasaidia askari wetu hawa.

Vile vile kule Finya *FFU* kuna gari lakini wameondoa zile gari nyingine maana vifaa vyenyewe ni kidogo na wale *time* yoyote wanapigiwa simu wanakwenda sehemu yoyote kufanya kazi. Unajua tena *FFU* kazi zao ni nyeti ni ngumu kwa kweli. Kwa hiyo,

nao wapatiwe magari mazuri, magari ya uhakika ili waweze kufanyakazi zao. Sio vizuri *FFU* wanaingia kwenye teksi au daladala, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuchangia kuhusiana na mishahara ya askari. Askari hawana muda wa kufanya kazi, kama walivyosema wenzangu. Wanafanya kazi masaa 24 askari wetu tunaomba askari waongezewe mishahara hata kama Serikali fedha ni kidogo, lakini wapunguze kwenye sehemu moja, lakini waongeze kwenye sehemu za mishahara. Askari wetu kwa kweli wanadhalilika sana, mishahara ni midogo, posho zao hawalipwi, kwa kweli wenzangu wameshasema sipendi kurudia. Lakini Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wanajua hilo.

Kwa hiyo, kwa kuondokana na tatizo hili tunaomba mwaka 2009/2010 mlipangie shilingi bilioni mia mbili hivi tuweke fedha nyingi ambayo tunaweza kuwawezesha askari wetu kuwaongeza mishahara. Hasa wale askari wa viwango vya chini ndiyo kabisa hawapati mishahara kwa kweli na wao ndiyo watendaji. Mishahara labda mikubwa itakwenda kwa wale maafisa wakubwa. Kwa nini askari wadogo amba wanafanya kazi asubuhi mpaka jioni au mpaka siku ya pili masaa 24 mishahara yao haiongezeki? Ndiyo hapo hapo ukiongezeka mshahara ni Sh. 500/=, inakuaje Mheshimiwa Waziri? Naomba sana Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho aweze kunijibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuwapongeza askari wote wa Tanzania wanawake. Askari wanawake tunawaona jinsi ya jitihada zao ambazo wanazifanya. Askari wanawake hawajibagua kama wao ni wanawake askari wanawake wako imara, nawapongeza sana askari wanawake na wazidi hapo hapo, “*keep it up*” wanawake askari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda sana kupongeza Mkoa wa Morogoro....!

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Faida Bakar kwa mchango wako mzuri. Makamanda wa Visiwani wameungwa mkono sana na Waheshimiwa Wabunge akinamama. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, orodha bado ni ndefu kuna Waheshimiwa Wabunge karibu ishirini au zaidi bado hawajachangia na muda kwa kweli haupo upande wetu. Nitawaomba watuwie radhi wale amba mlipenda sana mchangie kwa kusema humu ndani kwa kweli haitakuwa rahisi kupata nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa kuwa muda haturuhusu, tutakaporudi saa 11.00 jioni watachangia Waheshimiwa Wabunge wawili tu, nao ni Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na Mheshimiwa Felix Kijiko. Kwa hiyo, kuwahi ni muhimu kwa hao ambao nimewataja, kama watakuwa hawaonekani humu Bungeni au wamechelewa,

basi kwa akiba Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Diana Chilolo wawe tayari wakati wowote endapo hao watakuwa hawapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo mchangiaji atakayefuata ni Mheshimiwa Naibu Waziri, Balozi Khamis Kagasheki yeye atachangia kwa dakika 35 na baada ya hapo, atakayefuata ni Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hii Wizara inaitwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Lawrence Masha yeye atakuwa na muda wa dakika 40.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii tuliyofikia, naomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni ya leo.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja yetu kwa muda huu wa jioni kabla sijaendelea, ninaomba nimwite Katibu ili atoe Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na kwa mujibu wa Mheshimiwa Mwenyekiti Job Ndugai kabla hajasitisha shughuli za leo mchana aliwataja wachangiaji wawili na tulikubaliana kama hawatakuwepo, basi wale wengine watachukua nafasi yao. Lakini namwona Mheshimiwa Msomi yupo kwa hiyo ataanza, halafu tutaendelea na wale wengine waliotajwa kama watakuwa hawapo, basi tutaona nani achukue nafasi.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba radhi, sauti yangu sio nzuri sana kwa sababu ya mafua makali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuzungumzia suala la Polisi, lakini kabla sijazungumzia suala la Polisi, naomba kutoa pondezi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, kaka yetu *IGP Saidi Mwema* kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa nguvu zao zote kwa hali mpya na nguvu mpya. Pondezi za pekee kwa *IGP Saidi Mwema* kwa kweli Watanzania tunamwona na tunampongeza kwa dhati kabisa adumishe utendaji wa kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji letu la Dar es Salaam tuna muundo wa Kipolisi ambao upo kwa ngazi ya Mkoa na kwa bahati njema Jimbo langu la Kigamboni limepata Wilaya mbili za Kipolisi. Tuna Wilaya ya Mbagala na Kigamboni. Lakini kwa bahati mbaya Wilaya hizi hazina ofisi nzuri za kuweza kuwatendea kazi kwa kiwango kinachostahili hasa Ofisi ya *OCD Mbagala*, kwa kweli inatia aibu inasikitisha, vile vile ofisi ya *OCD Kigamboni* inatia aibu na inasikitisha sana. Nyumba yenyewe inavuja na imekuwa kongwe. Naiomba Serikali mwaka huu kwa bahati mbaya kwenye matarajio

sikuiona. Naiomba sana Wizara ya Mambo ya Ndani kulitazama hili kuwapatia ofisi bora *OCD* wetu ili waweze kufanya kazi vizuri Mbagala na Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana *IGP*, namshukuru Waziri aliyeondoka Mheshimiwa Mwapachu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mohamed Aboud wametusaidia sana suala la usafiri *Landrover* nne, kwa ajili ya Mbagala mbili na Kigamboni mbili. Lakini naomba kuchukua fursa hii vile vile kumwombwa *IGP* na Mheshimiwa Waziri kututazama tena kwa ajili ya kutupatia pikipiki. Tuna maeneo kule ya Mwambao wa fukwe, kule kuna matatizo mengi, kunahitaji kukimbiliwa kwa haraka haraka, kwa hiyo, naomba kutoa wito na ombi rasmi kwa uongozi wa Wizara kutusaidia kutupatia pikipiki kwa ajili ya malindo ya doria sehemu za fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine askari wetu wana matatizo sana ya mawasiliano ya redio takribani siku zote wanatumia simu zao za mikononi kwa ajili ya mawasiliano ya kikazi. Nilizungumza mwaka jana, mwaka juzi, lakini bado utekelezaji wake na mwaka huu narudia tena kuwaomba kutuimarishia mawasiliano ya redio Tarafa ya Kigamboni na Tarafa ya Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kile cha Kigamboni sasa hivi kimezidiwa mno, naomba Serikali ijithidi kutujengea kituo kipyta ambacho kitakidhi na kitakwenda sambamba na maendeleo ya Kigamboni. Daraja hili likijengwa Kigamboni itabadilika kwa ajabu sana.

Naomba Wizara ya Mambo ya Ndani hilo nalo wajiandae basi katika viwanja vinavyopimwa vya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke wachukue kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba za watumishi kuijandaa na mabadiliko hayo makubwa ya mji wa Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji hivi sasa kuna utaratibu kwamba wanategemea kubadilisha muundo wa Utumishi wa Idara hii kutoka muundo wa sasa kuingia muundo wa Kijeshi. Inavyosemekana kwamba muundo huo baadhi ya watumishi Maafisa Uhamiaji italazimika kushushwa vyeo kutoka vyeo walivyonyavyo sasa hivi kuwiana na vyeo vya Kipolisi au vya Kijeshi sijui kama ni Kijeshi *JWTZ* au vya Polisi. Lakini naiomba Serikali jamani, Taifa letu linapiga vita umaskini, leo mtu ameshapata alichonacho baada ya kumwongezea alichonacho mnataka kuwashushia vyeo watumishi wetu hawa mambo hayo mbona yanakwenda kinyume na sera yetu ya Taifa? Naomba kutoa wito kwa Serikali kuacha watumishi wetu kwenye vyeo walivyonyavyo na kama vina tofauti ya uwiano na vile vyeo vya Jeshi muundo unaofuata, basi waongezewe badala ya kupunguziwa. Kwa heshima na taadhima naomba Mheshimiwa Waziri hili alisimamie kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la kusikitisha zaidi kuna watumishi wamekaa kwenye vyeo vyao takribani miaka nane hadi kumi hivi sasa na wameshamaliza *higher examination*, mitihani ambayo wanapaswa kwa ajili ya kupandishwa vyeo awamu kwa awamu, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo wapo watumishi ambao wameishi kwenye vyeo hivyo hivyo wengi tu kwa muda wa takribani miaka kumi na kuendelea.

Kulitokea baadhi ya watumishi wamepandishwa vyeo kwa mserereko, wameruka zaidi ya vyeo vitatu wengine wameruka vyeo vinne, sasa hawa ambao walikuwa na stahili zaidi kufikiriwa kwanza baada ya kumaliza mitihani yao kwa mujibu wa taratibu zilizopo ndani ya Idara ya Uhamiaji hawajafikiriwa, wamefikiriwa hawa wengine, wamerushwa vyeo, lakini waliofanya mitihani na kufuzu bado wameganda pale pale walipo. Naiomba Wizara itujibu juu ya suala hili, imekuwaje na watachukua hatua gani kwa hawa ambao hawajapandishwa vyeo tangu wapite kwenye mitihani yao ya lazima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Zimamoto kulikuwa na mpango wa kila Halmashauri kuwa na Zimamoto yake kwa bahati njema Manispaa yetu ya Temeke tumeanzisha kituo pale *TAZARA* lakini bado pia hakijaanza kazi. Kwanza, naomba kutoa wito kwa Wizara, zisaidie ili kituo hiki kianze kufanya kazi, lakini la pili niliomba mwaka jana vile vile kwamba hali ya mazingira ya Kigamboni hasa ukizingatia kivuko na ukuaji wa Kigamboni tuna haja ya kuanzisha kituo cha Zimamoto Kigamboni. Bado naomba kutoa ombi rasmi kwa Serikali kuanzisha kituo cha Zimamoto Kigamboni. Pia naomba kutoa wito kuitaka Idara hiyo kuendelea kufanya ukaguzi wa taadhari na kinga za moto hasa katika vyombo vya bahari, meli za abiria zikaguliwe. Kwenye taarifa zao humu nimeziona hamna hata sehemu moja zilizotajwa kwenye ukaguzi walizofanya kwenye vyombo vya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vitambulisho. Ninavyofahamu vitambulisho sio kadi, bali ni mfumo. Ni mfumo ambao utawezesha Serikali kupata taarifa za kila mwananchi hatimaye na vyombo vingine vya Serikali kwa makubaliano maalum. Kwa mfano *TRA, Immigration*, Polisi, Benki na kadhalika kuweza kutumia mfumo huu wa vitambulisho kupata taarifa za Mtanzania kwa haraka. Vile vile ninavyoolewa kuwa vitambulisho hivi vitakuwa vya aina mbili, moja kwa ajili ya Watanzania waliozaliwa na pili kwa Watanzania ambao wanaishi Tanzania lakini sio Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki sisi bado tuko nyuma. Sasa hapa naomba kutoa wito kwa Serikali kuongeza kasi ya utayarishaji wa vitambulisho hivi vya raia wa Tanzania. Tumbaki sisi Watanzania kwenye Afrika Mashariki na Uganda. Lakini kama nilivyosema, itasaidia katika mifumo mingine ya Kibenki, *TRA* na kadhalika wenzetu wameshaanza kutumia katika nchi zetu za Afrika kwa mfano *South Africa* wanatumia mtandao huo, Botswana, Kenya, Zimbabwe, Singapore, Malaysia, UK (*Europe*).

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali itoe msukumo zaidi vitambulisho hivi vianze kutengenezwa na hatimaye tuwe na mfumo mzuri wa kupata taarifa za Watanzania. Kwanza, naipongeza Serikali suala hili kuliweka chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu ni Wizara ya Muungano. Sasa hilo ni suala la Muungano lilikuwa kwa kawaida liwekwe chini ya Wizara ya Sheria na Katiba lakini tunavyokwenda mbele huku ni vyema wakafika pale wakaziunganisha hizi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la vijana katika Kata ya Mbagala wanaitwa Mbwamwitu. Vijana hawa ni hatari sana, wanapiga visu raia, wanawaibia, wanawatesa!

Nampongeza sana *RPC*, anajitahidi kwa kadri ya uwezo wake, lakini naomba kuchukua fursa hii kuliomba Jeshi la Polisi, lipeleke Kikosi Maalum ili kupambana na hawa mbwamwitu. Inaonekana kama Serikali haipo. Kuna mateso ya hali ya juu! Pelekeni kikosi kupambana na vijana hawa wa mbwamwitu tena ni vijana wadogo tu wenyе umri kati ya miaka 18, 20 hawazidi 25. Wanasumbua wananchi, wanawatesa, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ijitahidi kupeleka kikosi maalum kupambana na hawa mbwamwitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la usalama barabarani. Kuna mtindo Polisi wa *Traffic* hasa kwenye barabara kuu hizi kujificha kwenye mapori na baadaye kujitekeza kwa ghafla. Sasa hii kwanza inahatarisha hatari kwa gari lenyewe unalosimamisha. Tabia hii ilitolewa wito huu humu kwenye Bunge kwamba waache mara moja, lakini vitendo hivi bado vinaendelea.

Ninaiomba Serikali hasa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya *IGP* ananisikia kukaa na Ndugu Kombe kuona unatolewa wito maalum ili Polisi wakae kwenye vituo vinavyojulikana au angalau, basi woanekane kwa uhakika na gari linalokuja. Lakini kusimamisha gari kwa ghafla ni hatari, linaweza kuleta maafa zaidi kwa raia wetu wa Tanzania.

Katika Zimamoto kuna suala la gari za kuzimia moto kwa maghorofa makubwa. Hili ni tatizo. Tilitokewa na moto pale Wizara ya Nishati na Madini tukahangaika sana. Bahati njema *Ultimate Security* na vyombo vingine vya watu binafsi vilitusaidia tukazima moto huo baada ya wenzenetu kuwa na vyombo vya aina hii. Sasa sijui Serikalini kama tumejiimarisha na kupata vyombo vya aina hiyo, lakini kwa kweli kama bado kuna haja wenyewe ni mashahidi naiona Kariakoo jinsi inavyokwenda na nyumba jinsi zilivyokaliana kwa ukaribu baina ya nyumba na nyumba ukitokea moto na kama vyombo kama hivi hatuna itakuwa ni maafa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaomba Serikali pia Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa mwenzangu Mheshimiwa Mtemvu alizungumza asubuhi Wizara ya Mambo ya Ndani inapewa bajeti ndogo sana. Ni Wizara nyeti haya tunayoyasema kwamba Mheshimiwa Waziri, *IGP* tusaidie tufanye hivi yote yanahitaji fedha na masuala ambayo ni yetu kabisa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia kwako na Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo, waione safari hii Wizara ya Mambo ya Ndani kwenye vipaumbele vyetu vijavyo vya mwaka ujao wa fedha ili hatimaye Wizara hii kwanza iondoe tatizo la nyumba za kuishi za Polisi. Pili, waweze kuongeza nyenzo za kufanya kazi. Kwa mfano, mawasiliano, hali kadhalika na mengineo muhimu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna bahari ya Hindi. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Msomi, Waheshimiwa Wabunge mchana tulisema kwamba kama Mheshimiwa Kijiko atachelewa, basi Mheshimiwa Kabuzi atachukua nafasi yake na Mheshimiwa Kabuzi ameniletea taarifa

hana kwamba wamekubaliana katika suala hilo. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Kabuzi.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nadra ili nami nichangie. Nianze na ku-*declare interest* kwamba mimi kabla sijawa Mbunge mwaka 2000 nilikuwa Tarime napenda niwape pole ndugu zangu wa Tarime kwa matatizo waliyoyapata kwa kifo kilichompata ndugu yetu.

Baada ya hapo nianze na kumpongeza mdogo wangu Masha na ndugu yangu Kagasheki kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini vile vile niwape pole, Wizara hii ni ngumu na nyeti na ndiyo imeshikilia maisha na mali za Watanzania. Nimpongeze vile vile ndugu yangu *IGP Saidi Mwema* ambaye ana hekima na busara na amepewa kazi kubwa. Najua kabisa amepokea kutoka kwenye mazingira mengine na anajaribu *ku-transform* Wizara hii ili iweze kuwa na maadili yake lakini anakabiliana na mambo mengi ambayo yanamkwaza na ndiyo maana hoja zimekuwa nzito na mimi nimeomba kwa nguvu kabisa niweze kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimweleze Mheshimiwa Waziri, nimekuwa nikilalamika pamoja na wenzangu kwa ajili ya maeneo yetu ya machimbo na maeneo yetu ya uvuvi. Tumekuwa tukipata shida sana. Napenda nianze na kueleza hali halisi ya ujambazi katika maeneo yangu. Nitataja Jimbo langu tu, tuna majimbo tatu katika Wilaya ya Geita, lakini nitajielekeza Jimbo moja tu na mwelewe hali ilivyo, kuanzia kwenye mwezi wa Februari mpaka Juni ujambazi ulivyojitekeza. Katika kijiji cha Katoro wamevamia mara tatu wameua walinzi wawili na kuchukua mali nyingi. Juzi tarehe 14 wamevamia kwa muda wa masaa mawili wameiba mpaka askari hawakutoka ndani mpaka askari waliotoka Biharamulo ndio wakaja kuwasaidia.

Kijiji cha Ruhuha walivamia shule wakaua mwalimu kijana kabisa, wakawabaka mama yake, mke wake na dada yake. Bahati mbaya siku hiyo nilikuwa nasafiri nakuja Dar es Salaam nikapigwa simu saa 9.00 ya usiku nimekaribia Sengerema nikaenda kituo cha Polisi Sengerema nikatoa ripoti, nilikuwa naendesha kigari changu cha *Corolla*, nikatoa ripoti wakatoa taarifa Geita na Mkoani, lakini kutoka Sengerema kwenda Geita ni karibu kilomita 50. Nimeanza kuendesha nakwenda mpaka Geita nakuta Polisi hawajaanza safari kwenda kwenye tukio. Ndio tukaanza kukokotana tukaenda kwenye tukio tukakuta Mwalimu ameuawa. Tatizo, gari waliyokuwa nayo ilikuwa mbovu, imekwenda Nkome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Isima walivamia kijiji wakaua mtu mmoja, kuna *ki-centre* cha biashara. Halafu hapo hapo wakavamia shule wakawanyang'anya walimu mali zote. Ni mwaka huu huu! Baada ya pale wakaenda Kijiji cha Kavmema wamevamia kile kijiji wakaua watu wawili na wengine sasa hivi wako hospitali. Wakaenda tena wakavamia Kijiji cha Nyabulolo, wamevamia Kijiji na wakaua mtu mmoja.

Hiyo ni jimbo langu tu mwaka huu huu. Kama walivyovamia juzi, nikapiga simu kutoka huku Polisi kuja kujikusanyisha kwenda pale nashukuru angalau hata helikopta

ilitua pale ikaonyesha kwamba kuna jitihada. Kijiji cha Nyarugusu wamevamia mara sita, mara ya mwisho wamevamia wakawafungia na Polisi ndani hawakutoka kesho yake wananchi wakasema hatutaki Polisi hapa.

Kijiji cha Kaseme wamevamia shule ya Muungano na shule ya Zalawa wakawapora wakawanyang'anya walimu. Huo ni ujambazi. Kijiji cha Mnekezi wakamvamia mwalimu wakachukua vitu vyote majambazi. Kijiji cha Magenge walivamia wakaaua mtu halafu walivamia *bus* wakawachapa viboko wakawanyang'anya mali watu wote. Hilo ni Jimbo moja na ni mwaka huu huu! Sasa tatizo nilipokuja kuchunguza kwamba Polisi wetu kweli, kuna tatizo la wengine kwa sababu ya *discipline*. Lakini Geita tulikuwa tunaomba usafiri, mwaka jana nililalamika hapa, wapeni usafiri. Ikiwezekana hata wale wa Migodi Mheshimiwa Waziri tufanye harambee wakusanye fedha tununue magari kwa ajili ya watu wale, hata pikipiki.

Mheshimiwa Mwapachu ile gari sijaipata ile *Landcruiser* aina ya *pickup* pamoja na pikipiki tatu ulizoniambia humu ndani ya Bunge sasa Mheshimiwa nashindwa kkuuliza kwa sababu umeshaandoka pale uliniahidi ulivaa vizuri na Mheshimiwa Saidi Mwema mliniahidi hicho kitu. Sasa naomba jamani tafadhali watu wangu wanakufa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabuzi ongea na Kiti.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Ndiyo, ni wajumbe waliokuwepo, ahsante nimesikia lakini wamenipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu kuna matatizo makubwa ya ujambazi na hilo ni Jimbo moja tu hata gari yangu na mimi ilivamiwa ikapigwa risasi mwalimu akavunjika mguu na ng'ombe wangu wakaibiwa hata mimi na sizungumzii sana kwa sababu ni mali tu imekwenda wakaibiwa ingawa bahati nzuri niliwarudisha na jinsi nilivyowarudisha nitakueleza maana yake niliona nikitumia Polisi yatakuwa kama yale yaliyotokea Singida. Kwa hiyo, naomba sana mliangalie. Tunaomba ikiwezekana kuwe na Mkoa, umhamishe *RPC*, tunahitaji labda *RPC* kwa Geita ahamie pale kuwe na operesheni ya kukamata majambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia askari wetu, niangalie kwenye maisha ya askari wetu kweli wana viapo vyao na wanaamini viapo vyao, lakini mahali penye njaa kiapo hakifui dafu. Askari sitaki kurudia madai yao ambayo wamesema. Mheshimiwa Limbu amesema, Mheshimiwa N'hunga amesema na wengine wamesema, jamani inashindikana nini? Mimi siamini kwamba Wizara hii kweli hatuwezi kuiweka vizuri tukawawezesha maaskari wetu angalau tuweze kupata namna ya kuwabana kwa sababu mimi kati yao wameniambia tunaomba Mheshimiwa Mbunge, mwambie Mheshimiwa Waziri aje tuanzishe kituo cha Polisi pamoja na kwamba wenyewe wameniambia tuhamishe, lakini ukiangalia hali ya maisha yao askari anakwenda ana njaa, hana usafiri, askari unamkuta ame-*escort* na mvua, akiteremshwa na watu wa mabasi anasubiri na mwamvuli, sasa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie namna ya kuweza kuwawezesha askari wetu angalau tuweze kupata mahali pa kuwabania, sasa hivi ukisema unasema uwezo huko wapi, mimi siku ile natokea Sengerema nilikuwa nimesemsa huyo *OCD* kama hajakwenda akaniambia sasa hivi niende kwa mguu kilomita 30 mpaka Ruhua tukakuta mwalimu ameuawa. Walimu katika Jimbo langu wamehama, sasa hivi wameamua kuhamia Geita, nilipowaambia jamani nivumilieni, wakaniambia tuonyeshe mahali ambapo roho inanunuliwa, wametoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba na wale viongozi mlioko ndani ya *chamber* kule hebu katengenezeni tuangalie maslahi au inashindikana wapi? Kwa sababu ni tatizo na kutoiwezesha Polisi kunaathiri hata uchumi wa nchi, kwa sababu hata hawawezi kufanya biashara. Nitatoa mfano mdogo. Mimi nimeondoka na hizi gari zinazosafiri kwenda Burundi, nimeomba *lift* kutoka Dar es Salaam niko mle ndani, niliyoyaona njiani *traffic* wanavyowafanyia hao jamaa. Hao wana *documents*, wana kila kitu, lakini wao kutoka hapa mpaka kufika Kahama wanatumia siku tatu kwa sababu anasimamishwa kila mahali na ndio una kila kitu! Basi subiri hapo, anatoa Sh.10,000/= ndio anakwenda. Ni kweli sikutaka kujitambulisha mpaka mwisho, kama natania Mheshimiwa Saidi Mwema vaa *T-shirt* upande na wewe uende uone hivyo wanasmamishwa kila mahali, lakini wakati mwingine ukififikiria amekaa pale hajapewa posho na nini yeye amekaa pale taabu tupu, hata ukimfukuza *ha-feel*. Tuwawezeshe hawa wakiwapo kule kule, lakini maadili lazima ya uaskari yawepo, uchumi unaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la watu kusafiri, kwa mfano wenzetu wamezungumza kwamba suala la mabasi kusafiri usiku ni tatizo, kwenye masaa mpaka saa 6.00 mimi nafikiri hilo ni tangazo jema kwa sababu zinazohusika. Tatizo najiuliza: Je, madereva wetu ndio hawawezi kuona usiku? Kwa sababu Kenya na Uganda wanafanya hivyo! Sisi madereva wetu ndio wenye matatizo au kuna nini? Kwa sababu sisi kama tutalala, wenzetu wanafanya kazi saa 24, tunalala. Sisi masaa 18 ndio tunafanya kazi, wenzetu masaa 24, tutawapata hawa watu? Lazima tufikirie hivyo, nafikiri *discipline* ya madereva na askari wetu ndio itakayotusaidia tuweze kufikia mahali.

Mimi nilikuwa nadhani kuna haja ya kulangalia pamoja na kwamba ile amri imetolewa tunaipinga, lakini nadhani nia ya kuangalia watu wafike wapi kwa sababu watu wanaoteseka kwa mfano watu wanaotoka Mwanza ukimtoa Mwanza ukaja ukamlaza hapa ni mateso. Lakini ukimrudisha Dar es Salaam, kesho anafanya biashara anakwenda, anarudi, anakwenda, anarudi kama wenzetu wanavyofanya biashara kutoka Busii anakwenda Mombasa anafanya biashara, anarudi, ndiyo biashara. Sasa sisi tulale! Nadhani kuna haja ya kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu nina Gereza la Butundwa la Kilimo, lakini ukifika pale haifanani hata kama ni gereza, ni kama sijui mji wa mkulima amekusanya watu wengi wanavaa unifomu pale. Kwa kweli hakuna vifaa, hakuna trekta. Niliwahi kuomba trekta nikafuatilia nikapewa trekta kuukuu tukatengeneza kila siku, yaani kwenda shambani inaweza kumaliza siku mbili halijafika shambani, wakanionomba niwazungumzie wanakijiji wapate eneo la kulima mpunga, lipo eneo zuri sana,

nikawabembeleza wanakijiji wakajitolea kutoa eneo. Lile eneo ni kero, halilimiki. Sasa niambieni leo hapa basi tuwarudishie wakulima eneo lao kwa sababu mashamba ya wakulima ni mazuri na lile ni shamba zuri tuwape hivi vifaa wafanye kazi. Hakuna sababu ya Magereza kulialia kwa sababu ni sababu ya uzalishaji lakini tatizo kubwa ni kwamba fedha nadhani ugonjwa ni sisi humu ndani. Hii bajeti tunasema tunaunga mkono, mimi suingi mkono kwa sababu hela tumewapa kidogo na sisi ndio wenye matatizo, hiyo hela yako utakwenda nayo ni kidogo, lakini tuwape fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe kama Kenya. Mbona Kenya kila unaposafiri unakuta Polisi! Ukiwakuta wamesimama wana gari mbili na pikipiki, kila kituo. Sasa sisi tunataka tu watulinde wanakimbia kwa miguu. Wakipata vitambi tunalamika, hatuwapi kazi. Tuwape uwezo wasafiri tuanzie kule Namanga mpaka kule kila kituo hata akiwa porini ametulia tu ni kama mfereji, lakini kilomita mbili kuna gari inasubiri.

Sasa sisi unatoka hapa, ukishatoka tu hapa kwenda mpaka Morogoro ukiona gari ya Polisi ni ndoto, labda mpaka ufile kule kwenye nanihii na wenyewe wanakaa pale sijui ni stahili gani ya *Traffic* kukaa kituo sehemu moja utavizaje mabasi? Stahili gani huko ni kutaka fedha. *Traffic* lazima wahamehame sasa hana jinsi akiwekwa pale mvua ikinyesha itamchapa afanye nini, halafu hata makazi yao askari wetu hawataki kukaa na watu unamwambia kamkamate mtu anaishi naye amepanga kwake atamkamataje kwa nini asishirikiane kwenda kuuza bhangi, kwa hiyo kuna tatizo hapa tuangalie, tuwawezeshe hii sekta hii inatakiwa iangaliwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MUHAMAAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwanza kwa kumpongeza Waziri wa mambo ya Ndani ya nchi kwa hotuba yake nzuri pamoja na wasaidizi wake wote wa Wizara hiyo pamoja na Idara zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangwo wangu kwenye hotuba hii ni kuhusu vifaa vya kutendea kazi kwa askari wetu wa Jeshi la Polisi kama vile radio za mawasiliano, usafiri kwa maana ya magari ya doria na hata kwa ajili ya kusafirisha askari kwenda na kurudi katika majukumu yake ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mafao yao baada ya kusaifu. Jambo hili ni kero ambazo linawasumbua sana askari wetu wastaaifu na imekuwa ni kama kilema katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba pia kuchangia kuhusu mishahara ya askari wetu pamoja na marupurupu yao iboreshwe ili waweze kumudu maisha ya kila siku na kazi zao za ulinzi wa Raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa Afya na kuniwezesha kuchangia kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba yake. Pia nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote waliomsaidia Waziri kutayarisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze *IGP* wa Polisi - Ndugu Mwema pamoja na Makamishna wa Jeshi la Polisi kwa kusimamia vyema utendaji wa kazi katika nchi na Mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu la Polisi linafanya kazi kubwa sana, kazi ambayo inapaswa kuungwa mkono na wananchi wote wapenda amani. Pia napongeza kwa kuongezewa mishahara posho pamoja na kupatiwa huduma nzuri za makazi na vifaa bora ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kama hawakutunzwa vizuri, ni rahisi kurubuniwa na kuliingiza Taifa katika hasara kubwa ya wananchi kutolewana na amani na utulivu tulio nao ukaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu wa Jeshi la Polisi hucheleva sana kupata mafao yao na hutumia muda mwingi kufutilia mafao hayo bila mafanikio. Hali hii sijui inasababishwa na kitu gani! Ninamwomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze ni sababu zippi wakati mhusika amekamilisha kila kitu alichotakiwa na kufika hadi miaka miwili mpaka minne hakuna kilichopatikana? Baada ya kutaka maelezo kwa Mheshimiwa Waziri, pia ningeshauri yafuatayo ili kupunguza usumbufo:

- (a) Kagawa kwa kada masuala ya wastaafu na isiwe Makao Makuu tu;
- (b) Kuunda Kitengo cha kuchunguza wastaafu ambao hawajapatiwa mafao yao; na
- (c) Kukipatia fedha kitengo kilichopo sasa ili kufutilia matatizo Mikoani waliko wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la malipo ya pensheni na Kiinua Mgongo ni suala linalozungumzwa sana na Wabunge wengi na bado ufumbuzi wake hayapatikani. Hili ni kero kubwa na linaleta manung'uniko kwa askari wetu wanamaliza muda na kulipwa kiinua mgongo hasa wakiangalia wenzao wa pensheni wanalipwa mafao mazuri na kila baada ya muda wanaendelea kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu masuala ya baadhi ya wabunge alisema malipo ya pensheni na kiinua mgongo ni hiari na chaguo la askari. Lakini inaonyesha askari hawakuelishwa. Kwa hiyo, hivi sasa imefika wakati mfumo huo uondoshe na askari wote walipwe mfumo mmoja wa pensheni kwa kuzingatia, huo ni mfumo wa zamani na umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanganyika imedai uhuru ili kuondoa ukoloni ambao ulikuwa unamkandamiza mwananchi wa Zanzibar, ikafanya mapinduzi kuondoa dhiki na dhuluma walizofanyiwa wananchi wake na kuahidi kuyaacha yote mabaya na kuyafuata yote mazuri. Hili ni kero na inasumbua. Je, inawekwa hadi lini? Namwomba Mheshimiwa Waziri alitolee kauli ya kulondosha tatizo hili la kiinua mgongo. Waswahili wanasesma: "Mtemewa mate na wengi, hulowa." Suala sio dogo, ni kubwa na lina madhara mbele yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mheshimiwa Lawrence Kego Masha (Mb) – Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri ya kutia moyo kwa jamii ya Kitanzania. Ni maoni yangu kwamba hotuba yake imetupa imani na Serikali yetu na kwamba kama wananchi watatoa ushirikiano wa kutosha, amani na utulivu itazidi kudumishwa.

Kipekee, napenda kumpongeza Naibu Waziri – Mheshimiwa Balozi Khamisi Sued Kagasheki kwa msaada anaoutuo kwa Mheshimiwa Waziri na hivyo kuweka mazingira ambayo yanaleta ufanisi wa hali ya juu. Ningependa pia kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda Raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa hivi sasa Wilaya ya Siha ina Wilaya kamili, baada ya kuhama toka Wilaya ya Hai. Tumekuwa tukiiomba Serikali itusaidie katika suala zima la kujenga Makao Makuu ya Polisi Wilaya. Mheshimiwa Abood Mohammed Abood alipokuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, wakati huo usalama wa raia, alutuahidi kuwa Serikali itahakikisha kuwa inatusaidia kujenga Makao Makuu ya Wilaya hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya hii ya Siha ni Wilaya ya Mpakani ambayo ina matukio mengi ya ujambazi na ujangili.

Mwisho ninaomba sana tusaidiwe vyombo vya usafiri kwa ajili ya Wilaya mpya ya Siha. Kituo cha Sanya Juu, sasa hivi kina gari moja tu la aina ya *Landrover* ambazo ndilo linalohudumia Wilaya nzima. Kituo cha Ngare–Nairobi ni muhimu kwa eneo la *West Kilimanjaro* ambalo uchumi wake ni wa hali ya juu. Hata hivyo kituo hicho kina tatizo kubwa la usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. FATMA OTHMAN ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wa Polisi wengi wanaishi kwenye mazingira magumu sana kwenye makazi yao hasa kwenye vyoo. Naomba wafanyiwe utaratibu wa kupatikana kwa vyoo vingi kwa maaskari wanaoishi kwenye maboma, ukosefu wa vitendea kazi, kwani kwenye vituo vingi vya Polisi haviridhishi, hamna vikalio kama vile viti vya kukalia au mabenchi na hata karatasi za kuandikia maelezo mtu anapofika kituoni hakuna. Kwa hili, naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie kwa makini aone kuna nini huku kwenye Jeshi la Polisi? Hii kasma inayotolewa na Wizara kuhusu mafuta kwa Jeshi la Polisi ni kidogo sana. Kwa hili

naomba Mheshimiwa Waziri aliingilie kati kwani mafuta wanayopelekewa Jeshi la Polisi Zanzibar ni kidogo sana.

Pili, magari yote yaliyokuwepo kwenye Jeshi la Polisi Zanzibar ni mabovu. Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapopata msaada wa magari, asiisahau Polisi Zanzibar. Pia naomba kupatiwa daktari kwenye hospitali ya Ziwan Zanzibar kwani ina ukosefu wa zana za kisasa na daktari mwenye ujuzi mkubwa. Linapotokea shauri lolote kubwa ama askari kuumwa sana au kapata ajali, hukimbizwa hospitali kubwa kwa ajili ya matibabu, laiti angekuwepo daktari mwenye ujuzi isingefika askari kupelekwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Polisi wa kike anapoolewa na askari mwensiwe wakaishi kwenye boma nao hawalipwi posho ya nyumba, kwa nini wakati wale askari wakiume wanalipwa na wa wakike hawalipwi na wao wameoleowa tu? Hawa askari wanaishi kwenye boma wanalipa umeme na wamekekewa mita za Luku na wenzao Bara wanaishi kwenye boma hawalipi umeme. Suala la askari waliotoka mafunzoni Moshi, mafunzo ya awali, wale waliotoka Bara wote wamelipwa posho za kuanzia maisha, lakini wale wote waliookea Zanzibar, hawajalipwa hata kidogo, wengi! Baadhi yao yametilishwa saini kama pesa wamepokea na huku hawakuwalipa. Hii ni hatari! Naomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie kwa makini sana, kwani hicho kitengo cha fedha huko Zanzibar kuna nini? Kwani kuna askari waliokufa tangu mwaka 2000 mpaka hii leo hawajapata fedha zao wale warithi. Je, tatizo liko wapi? Kwenye Jeshi la Polisi au Hazina.

Kuhusu ajira, kwa kweli bado kuna tatizo kwenye ajira za Jeshi la Polisi kwanini sehemu ya ufundi ajira ilipelekwa Dar es Salaam ili wale wote wanaoomba ajira hiyo wakafanye mitihani huko wakati kila Mkoa unao mafundi ambao ni raia, kwa nini wasijaribiwe wale kwanza halafu ndio wapokelewe hao wengine? Kuna vijana askari wanaocheza michezo mingi tu kwenye jeshi kama mipira ya miguu na michezo mingine: Je, kwa nini askari hao wanapoumia kwenye michezo hawalipwi na wala kuhudumiwa na Jeshi la Polisi wakati ameumia kazini?

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa nchi ya amani na utulivu kwa sababu ya kazi kubwa inayofanywa na Polisi wetu, wawe wa usalama wa Taifa, *Traffic* na wengine wote. Kwa mantiki hii, askari Polisi lazima waboreshewe maslahi yao ili waweze kufanya kazi hii kwa uadilifu zaidi. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa askari wetu wanaishi na jamii, jambo ambao sio tu linawavunja heshima, bali pia inakuwa vigumu kufanya kazi zao kwa uaminifu na hivyo kurubuniwa na wahalifu.

Polisi hawa pamoja na kazi ngumu wanazofanya na katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na kutokuwa na *vest* za kuzuia risasi (*protective vests*), watu hawa panapokuwa na hatari zozote zile wanakuwa mstari wa mbele kupambana na hivyo tunaomba Wizara iona suala hili ni muhimu na hivyo kuwapatia vifaa hivyo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa Polisi wanakosa hata gari la kuwasafirisha kwenda vituoni huku wakiwa na silaha. Hivi mwenye gari kama ni

jambazi akawangang'anya, inakuwaje? Sheria inasemaje? Lakini hata sheria kama hairuhusu: Je, usafiri upo?

Polisi hawa wanatulinda, hawalali, lakini viongozi wamelala. Hana sikukuu lakini kikubwa ni posho ndogo wanazopata na mishahara. Kwa hali hii, Polisi hawa wanaweza wakaamua hata kusaliti ili kujikwamua kimaisha, hivyo ni muhimu waangaliwe kwa jicho la imani kutokana na unyeti wa umuhimu wa kazi zao.

Mkaazi ya Askari hawa yanatisha sana. Kwanza kwa utamaduni wa mwaafrika, ni kosa kubwa kwa baba na mama na watoto kulala chumba kimoja! Hii ni aibu na inakwaza na pia inafundisha watoto maadili mabovu. Hivi askari wao hawastahili faragha na wake zao au waume zao? Watakuwa na faragha wapi? Saa ngapi huku watoto wapo? Watoto wa siku hizi hawana dogo, wala hawalali, wanasubiria. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwapatia nyumba kuendana na ukubwa wa familia kama zilivyo sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu kuona nchi yetu mpaka leo haijaleta Muswada kuhusu *dual citizenship* wakati mwaka jana Wizara ilisema ingeleta Muswada huo suala hili ni muhimu na sio tu Tanzania itakuwa ya kwanza. Nchi nyingi sana zina taratibu hizo na wengine hata zaidi ya nchi mbili. Tatizo ni nini?

Kwanza umuhimu wa kuwa na uraia zaidi ya nchi moja ni faraja kubwa kwa nchi kwa mfano kuna Watanzania walio na uraia wa nchi nyingine na wanafanya kazi za kimataifa hivyo anapokuwa hata likizo anapata stahili za *ki-expatriate*, hivyo kupoteza fedha nyingi. Ni lini Serikali italeta Muswada huo ili nchi iweze kufaidika? Watu hawa wanashindwa kuwekeza kwa kuwa hawana uraia wa Tanzania, lakini wangependa sana kuwekeza. Nchi nyingi kama India, Nigeria na nyinginezo zina utaratibu wa kuwa wananchi wao wote walio nje ya nchi wanachangia pato la Taifa. Tanzania ina raia wengi walio nje kwa muda mrefu. Hivyo kuna haja ya kuwatambua na kutambua michango yao ili kuinua pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la kutoa *passport* kutoka 50,309 hadi 73,568 mwaka huu, bado kumekuwa na ukiritimba mkubwa katika utoaji huu wa *passport*. Ikiwemo kusafiri toka mikoani kufuata *pass*. Lakini kibaya zaidi, maswali yanayouliwa sio ya msingi na mengine ni ya udhalilishaji tu. Kwanza katiba inasema Mtanzania ana haki ya kwenda popote alimradi havunji sheria. Sasa anakwenda popote viyi kama hana *passport*?

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Wafanyakazi wa Bunge kwa msaada mliota kwetu wananchi wa Mara kutokana na kifo cha Mbunge Mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Chacha Zakari Wangwe. Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kijana wangu, Lawrence Kego Masha (Mb), Mjukuu wangu Mpandwa, Balozi Khamis Shedi

Kagasheki, Katibu Mkuu, *IGP*, Makamishna, *RPC*, *OCD* na Makamanda na vijana wetu vikosi mbalimbali nchini kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya mpya ya Rarya, natoa shukrani za pekee kwa jinsi Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na *IGP* jinsi walivyoshughulikia maafa yaliyowakumba wananchi wa Rarya. Zaidi ya ng'ombe 3,000 wameporwa kuanzia mwaka 2006 – 2008. Wananchi zaidi ya 10 wameuawa na majambazi. Hali ya usalama na mali zao tangu Serikali kuchukua hatua za kuimarisha ulinzi inaridhisha kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi na shukrani za wananchi, napenda kutoa maombi kutoka kwa wananchi kama ifuatavyo:-

Kamanda *post* ya kampeni hii iko Shirati ambayo ni pembezoni na ni mbali sana. Kwa kuwa *OCD* ameishahamia Kituo cha Utigi ambacho kiko katikati ya Rarya na inafika kutoka pande zote, Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini, wananchi wanaomba kituo kiongezwe, vitendea kazi, simu za mkononi, silaha, pikipiki, magari ili ulinzi uimarike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wezi wengi wa ng'ombe, wanapitia eneo la kijiji cha Bumera na Kata ya Mwema kutoka Wilaya ya Tarime. Vituo vipyta vifunguliwe katika Mirare ambayo ndiyo jirani na Bumera. Kijiji cha Mangore Kata ya Koryo inayopakana na Tarime. Tunashukuru kwa kupata kituo kipyta cha Buganjo.

Hivi karibuni ng'ombe 198 za wizi kutoka Tarime walikuwa wanahamishwa kwenda Mgumu kupitia kijiji cha Benganyo ambapo ng'ombe 300 waliibiwa na vijana wawili walipoteza maisha yao na wawili kupata ulemavu wa kudumu. Wananchi walitambua ngombe 10 kati ya ngombe 188. Hadi sasa wananchi hawajapata ngombe zao. Mpango wa wenye ngombe kurejeshewa ngombe zote unaandalila kupitia Mahakama ya Wilaya. Ulinzi wa kimila uko wazi, ngombe wa wizi wakipatikana katika kijiji au zizi, wanakijiji na mwenye zizi atafidia. Huu ndio utaratibu uliopunguza wezi tangu utawala wa Baba wa Taifa. Leo hii ngombe hao wakirejeshewa wenye we tutakuwa tunahalalisha wizi, tutakuwa tunachochea ugomvi na umwagaji damu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aingilie kati ili ngombe 10 waliotambuliwa wapewe wananchi walioporwa na ngombe waobakia wafidie ngombe 300 walioibiwa. Serikali itoe amri ngombe za wizi 10 wamepatikana katika kundi la ngombe 198 mwenye ng'ombe ndiye mwizi wa ngombe 300 za wananchi wa Bunganzi.

Naunga mkono hoja. Narudia majibu sahihi.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilileta suala langu kwenye Bunge letu Tukufu kuhusu Kituo cha *FFU Matengatwani*, Jimbo la Konde suala hili lilikuja tarehe 4 Julai, 2008 kwa kweli nilivunjika moyo mno na jawabu lililokuja. Kituo cha Matengatwani, kilianzishwa miaka ya 60, mara tu baada ya Mapinduzi ya Zanzibar majengo ya kituo hicho ni makongwe na mabovu mno na yanahitaji ukarabati. Je, ni lini kituo hiki kitapata matengenezo? Mbali na matengezo ya

majengo, askari na wanavijiji wa Matengatwani wanayo kiu kubwa ya umeme. Kituo kipo mita 500 tu kutoka kituo cha kilimo cha Matengatwani ambapo miaka mingi upo umeme na ipo *transforma*.

Kwa tathmini ya Shirika la umeme Zanzibar (*ZECO*) tawi la pemba, kuunganisha umeme kutoka kwenye kituo cha kilimo Matengatwani mpaka kutuo hiki cha *FFU* pamoja na majengo mengine ya makazi ya askari yaliyoko ndani ya kijiji cha matengatwani inagharimu shilingi milioni 7.5. Gharama hizi zinaweza kupungua kwa vile wanakijiji na askari wako tayari kujitolea kufanya zile kazi zisizohitaji utaalamu. Ni aibu ya kuwa leo ni zaidi ya miaka 40 kuwepo kituo hiki, lakini lindo la askari linafanywa kwa taa ya kandili.

Aidha kituo cha Polisi cha Konde kinayo majengo mawili ya ghorofa yaliyojengwa tangu wakati ukoloni. Majengo haya yamechakaa na hayawahi kufanyiwa ukarabati. Vigae (*tiles*) xsx mapaa yameanguka zamani. Mvua ikinyesha inaingia moja kwa moja kwenye vyumba vya ghorofa ya juu hadi kufanya nyumba hizo zisikalike. Mihimili inayozuia paa imechoka kwa kupigwa na mvua miaka nenda miaka rudi. Kuna hatari mihimili hii ikiachia na kusababisha uharibifu wa mali na hata maisha ya askari wetu.

Majengo ya makazi kwa askari yahatoshi, basi angalau tungelianza na matengenezo ya majengo yaliyopo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nalipongeza Jeshi la Polisi na usalama wa Raia kwa kazi kubwa sana wanayoifanya ya kulinda raia na mali zao. Pamoja na juhudhi hizo kubwa, lakini bado vitendea kazi vyao vilikuwepo vyombo vya usafiri ili kurahisisha kazi na kuwahi kwenye matukio bao ni vichache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii muhimu sana ili waweze kupata vyombo vya kutosha vya usafiri. Kila kituo cha Polisi kipatiwe magari ya kutosha na pikipiki za kutosha. Nasisitiza sana vituo vya Polisi kwenye Kata vimesahaulika. *OSS* anafanya kazi kwenye eneo kubwa sana, lakini hana pikipiki, atawezaje kumudu kazi yake kwa urahisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza vituo hivi ni vichache sana. Utakuta *OSS* wa kituo kimoja anahudumia zaidi ya Kata saba mpaka nane, bila usafiri, anafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii kwa jicho la huruma imsaidie *OSS* wa Kata ya Kaliua – Wilaya ya Urambo. Kwa jiografia ya Urambo Kata moja ina vijiji zaidi ya nane na anahudumia Kata nyingi sana, lakini hana chombo cha usafiri. Yeye yuko tayari hata kupewa mkopo wa pikipiki akatwe taratibu kwa sababu ya kuipenda kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vibaka kusumbua sana wakazi wa eneo la *Area 'C'* eneo la *Iringa Road* hapa Dodoma, mimi ni mkazi wa eneo lile, wezi wamezidi, hatulali usingizi. Kila siku amani hakuna kila leo wanavunja na kuiba vitu mbalimbali vya raia. Mwaka 2007 mimi mwenyewe walinivunja nyumba yangu, wameiba kila kitu. Usiku wa leo 30 Julai, 2008 wamekuja tena wanataka kuvunja mlango. Kwa bahati mimi nilikuwa macho nikapiga kelele wakakimbia. Tukiweka ulinzi wanawavamia kwanza wamemjeruhi ndipo wanapata mwanya wa kuvunja milango na kuiba.

Kwa niaba ya wakazi wa eneo lile, naomba sana Serikali kuweka doria eneo lile ili waweze kuwanasa hao wezi ambao wanaondoa amani kwa wananchi. Hatulali usingizi kwa sababu ya hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupandishwa vyeo kwa watumishi wa Jeshi la Polisi na Magereza kuna malalamiko mengi sana kwa baadhi ya askari kukaa kwenye cheo/nafasi moja kwa muda mrefu bila kupandishwa cheo. Askari wengine wamekaa mahali pamoja kwa miaka kumi na nane (18) kama hana mijomba wala mtu mkubwa anayemfahamu hapo kazini. Akistaafu akiwa hapo malipo yake ni kidogo na hayawezi kumudu maisha. Hata kama ana nguvu bado, umri wa kusaafu ni miaka 40 na 45 kwa lazima kiinua mgongo chake ni milioni nne zitamtosha nini? Huku sio kuwafanya watumishi hawa wafe mapema baada ya kustaafu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iweke utaratibu maalumu wa kupandisha vyeo watumishi wake kwa kutenda haki kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuumia kazini, kazi ya askari wa aina yoyote ile ni ya *risk* sana. Wanafanya kazi katika mazingira hatarishi. Inashangaza pale askari anapoumia kwa ajali, kupigwa risasi, kuchomwa kisu hata kupata athari za kiakili, hakuna malipo yoyote anayopewa mwadhrika huyu na kama yapo ni kidogo sana, hayakidhi kupoteza viingo na kupata ulemavu wa maisha. Naomba Serikali iwajali askari hawa pale wanapoumia, tena iwaenzi kwani wanajitoa kwa ajili ya raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wakati wa likizo; Askari hawa wanaposafiri na familia zao hawapewi fedha *Cash*, wanapewa *warrant*, kama sivyo anaambiya ajilipie kisha arudi kudai malipo. Malipo/madai haya hayalipwi kwa wakati. Inachukua miaka mitatu mpaka mitano hajalipwa na wakati mwingine madai haya yanapotelea huko. Hii ni kuwanyima haki watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu wa kuwapa fedha iwe ya safari, ufanywe kabla ya mtumishi kwenda likizo, ili aweze kusafiri vizuri na familia yake kwenda likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aeleze Bunge hili ni kwanini hadi leo askari hawajapewa Bima ya Afya? Ni kwa nini hakuna fedha inayotengwa kwa ajili hiyo? Serikali haioni ni kuwanyima watumishi wa Jeshi Bima ya Afya ni kutowajali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi kwamba baadhi ya watumisi wanapoumia na hata kupooza huwa wanatelekezwa. Hawapewi hata usafiri wa kupelekwa kwenye mazoezi, hawafuatiliwi afya/maradhi yao, gharama zote za kumhudimia zinakuwa juu ya familia yake. Pamoja na hali yake hiyo ataendelea kubaki hapo alipo hadi miaka yake ya kustaa fu ifike hata kama ni miaka ishirini. Hili linakatisha tamaa sana kwani hawa watumishi wanawatumia muda wote wakiwa kazini hata muda wa kujitafutia cha pembeni/mapato ya ziada hawana, hivyo wanapoumia ni jukumu la Serikali kuwatunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za watumishi wa majeshi zinasikitisha. Utaratibu wa kuwaweka kwenye makambi ni mzuri kwa utendaji kazi, lakini nyumba zao ni ndogo sana, hazina hadhi, nyingine ni mbovu na zimechakaa. Familia moja hupewa chumba kimoja, nikutokuwatendea haki kwani wana watoto, kuna wakwe, kuna ndugu na jamaa ndivyo tunavyoishi. Chumba kimoja kinatosha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana la mlundikano wa wafungwa kwenye Magereza yetu. Wafungwa ni wahalifu, lakini pia wanastahili haki zote sawa na binadamu wengine. Suala la hewa ya kutosha na mahali pazuri pa kulala ni la msingi sana kwa wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna hata gereza moja ambalo lina wafungwa idadi sawa na uwepo wake. Magereza haya yote yanajaa zaidi ya uwezo wa majengo yao. Gereza moja tu dogo la Urambo mjini, Mkoa wa Tabora lina uwezo wa kubeba wafungwa 150, lakini sasa limebeba wafungwa 400. Hii ni haki? Huku sio kuathiri maisha ya wananchi wetu hasa kiafya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya wafungwa hawa kuna watu wenye vipaji mbalimbali wakiwepo wajenzi. Serikali iwatumie nguvukazi hii kwenye majengo, vyumba vyta wafungwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie nini msaada wa haraka kwa gereza hili la Urambo ambalo liko kwenye hali mbaya sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la askari kukamata watu na kuwabambika kesi mbalimbali na wakati mwininge wanafungwa bila hatia. Tatizo hili lipo maeneo mengi hapa nchini na hasa maeneo yenye vyama vingi vyta siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kesi zaidi ya nne nimezishudia mimi mwenyewe. Viongozi tukiwapa mamlaka ya kutuongoza wanatumia nafasi zao za kutumia jeshi la wananchi kuwatesa raia. Mkuu wa Wilaya kwa sababu zake za kisiasa anatoa *order* kwa *OCD* naye bila kuhoji anatuma askari waende wakakamate watu wasio na hatia wanawaweka ndani na wanazuia dhamana kabisa bila sababu ya msingi.

Matatizo haya yapo sana Wilaya ya Urambo. Kituo cha Polisi cha Iramba, *OCD* amekuwa mwanasiasa. Nashauri kama kazi ya uaskari imemshinda aache na ajiunge na siasa. Askari anatakiwa kuwa *Neutral*, huyu ameshindwa, ni mwanasiasa *typical*.

Mwisho, yapo malalamiko kutoka kwa askari kuwa ukishtakiwa, kwanini unafukuza kwanza ndipo mashtaka yafuate? Ukishinda kesi hulipwi chochote cha uliyofanya mazuri. Unaambiwa uondoke haraka hata kama Mahakama haijakuweka hatiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunawatendea nini hawa watumishi? Utaratibu gani unatumika hapa pamoja na kazi ngumu wanayofanya siku ikitokea tatizo kidogo tu tunasahau yale mazuri yote! Kama ilivyo kwa raia/waajiriwa wengine, pale askari anaposhinda kesi alipwe haki zake zote ikiwa ni sawa/pamoja na malimbikizo ya mishahara yake na fidia kwa usumbufu kama wengine.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafuli ambao wanapata pensheni kwa limbikizo la miezi mitatu mitatu, wastaafuli hawa wanahitaji utaratibu huu ubadilike, wapewe pensheni kila mwezi ili waweze kukabiliana na maisha kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Muhamed Abdu alikuwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia alipokuwa akijibu maswali hapa Bungeni, alimjibu Mheshimiwa Maida kuwa kutajengwa nyumba za ghoroga Tanzania Bara na Visiwani. Unguja na kule Pemba je, ujenzi huu utakuwa katika bajeti hii au vipi? Kama ni kwa bajeti hii, posho hizi mbona ni kidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi vinahitajika kwa askari wetu pia na kivazi kama sweta, raintoti, blanketi ili vifaa hivi viweze kuwasaidia askari wetu wanapokuwa kazini hasa nyakati za usiku. Askari wetu tuwajengee mazingira mazuri ya magari ya doria ili waweze kufanya kazi kwa uhakika zaidi kwani wakiwashika wahalifu waweze kuwafikisha kituoni bila ya matatizo yoyote ambayo yanaweza kujitoneza. Baada ya kusema hayo, naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

MHE. MCHUNGAJI DR. GERTRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu wengi kwa kumpongeza kwa dharti Waziri, Naibu Waziri na timu ya watendaji wake wote kwa hotuba nzuri inayotupa matumaini ya usalama wetu Watanzania.

Ninaomba nimpongeze *IGP* - afande Saidi Mwema kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya kuwadhibiti majambazi nchini hasa Dar es Salaam. Tunamshukuru Mungu kwa juhudhi hiso, sasa Dar es Salaam tuna amani na tunalala vizuri. Kukiwa na tukio la ujambazi, ukipiga simu mara moja wanafika mahali pa tukio. Kwa kweli tunawapongeza sana!

Nimefurahishwa sana na uteuzi wa Afande Kova Suleiman kutoka Mbeya kuja Dar es Salaam. Nina uhakika sasa Mheshimiwa Mwema amepata kiungo kizuri sana katika juhudhi yake ya kudhibiti ujambazi. Afande Kova anastaili ya ulinzi shirikishi ambayo imefaulu sana ule Mbeya. Nimeona unatiliwa mkazo Dar es Salaam. Nina uhakika sasa amani na usalama nchini hasa Dar es Salaam. Pongezi zetu ni nyingi sana, mnafanya mengi ya kujituma bila nyenzo muhimu bila manung'uniko. Mungu awabariki sana. Naomba nitoe ushauri wa maboresho kuboresha nyumba za maaskari. Ni chache,

hafifu na nyingi chafu. Hata rangi au hata nyiru zingekuwa zinapakwa. Ukarabari wa *sewage systems* ili kuonyesha tunawajali kwa marekebisho madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya ujenzi wa nyumba za maaskari, zijengwe nyingine kwa sababu askari ni wengi. Watumie vikosi vya wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya mishahara. Mishahara ya askari wetu iko chini sana ndio maana askari wachache wanajiingiza kwenye vitendo vya rushwa. Tuwathamini kama *TRA* au *DRS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba askari wapewe vitendea kazi jamani, huwezi kufukuza mwizi na miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba ulinzi wa maalbino uongezwe na elimu itolewe katika sehemu hizo za machimbo.

Mhesimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara idhibiti wawekezaji feki. Wachina wanauza *cream*, maua, wana *garage*. Hizi ni kazi za Watanzania. Naunga mkono hoja mia kwa mia

MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kabisa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Wazi, Katibu Mkuu na Watendaji was Wizara nzima kwa kutuletea hotuba nzuri yenye kutia moyo kwa wananchi wote.

Aidha, nawapongeza kwa kazi ngumu ya kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao. Naiomba Serikali kuongeza fedha katika bajeti ya Wizara hii. Sasa kuna upungufu mkubwa wa Askari (*policemen and women*), vitendea kazi, makazi (*housing*), Ofisi za kutosha katika Wilaya setu (hasa Utete/Rufiji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zangu ni ukosefu wa ofisi ya Polisi Wilaya pamoja na nyumba za Maafisa na *barracks* za askari katika Makao Makuu ya Wilaya Utete/Rufiji.

Kwa jambo hili, nilipata kusikilizwa na *IGP* na akaonekana kunionea huruma, yaani alikubali nyumba za maofisa, Ofisi ya Wilaya na *Barracks* kule Utete/Rufiji lakini mpaka sasa sijapata taarifa ya maendeleo ya jambo mpaka sasa. Naomba maelezo ya kina kuhusu habari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upelelezi dhaifu katika Jeshi la Polisi Wilaya ya Rufiji kwa mfano katika uchaguzi Mkuu wa 2005 kulitokea mauaji ya mpiga kura mmoja. *RPC* Pwani anafahamu habari hii, lakini hadi sasa hakuna matokeo yanayoridhisha kabisa. Naomba majibu ya kisa hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari bubu ya Kijiji cha Mohoro Rufiji ni bahari haramu. Bandari hii inaingiza vitu mbalimbali, kama nguo, dizeli, vyombo na vifaa, *spare* na kadhalika kutoka Zanzibar Pemba na Arabuni. Wengi wao ni *CUF* wanauza bidhaa hizo kwa bei ya chini. Vile vile, wanunua bidhaa nyingi kwa njia ya haramu

kama mbao, mikoko na nyara za Serikali. Viongozi wa Mkoa (*RC, RPC, RSO*) wanayo taarifa, lakini upelelezi wa bandari hii haujaleta tija yoyote. Biashara haramu inaendelea na Taifa linazidi kupoteza mapato yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa kuwahamisha baadhi ya askari kutoka pale Mohoro/Rufiji. Naomba Wizara itupie macho hii bandari buba ya Mohoro. Mauaji ya hivi karibuni ya raia watatu katika *Selous Game Reserve*, watu hawa walikuwa wanavua katika mabwawa yaliyo ndani ya *Selous* bila kibali. Watu hawa waliuawa kwa kupigwa risasi na askari wanyama pori na walikuwa hawana silaha. Jeshi la Polisi lilitazamiwa lifuutiliye mauaji haya.

Pamoja na ukweli kuwa hawa wafu walikuwa wahalifu, lakini utawala bora unahitaji watu wenye makosa ya jinai wakamatwe na kupelekwa Mahakamani wala sio kuwamiminia risasi na kuwauwa. Naomba Jeshi la Polisi wapeleleze vifo hivi na tupewe matokeo ya upelelezi huo. Mbaya zaidi wauwaji hawa hutembea tembea katika kijiji cha Mloka/Rufiji. Yaani ni kijiji cha biashara nje ya *Selous Game Reserve*. Wale ndugu wa Marehemu wana hasira sana. Tafadhalii Noamba Mheshimiwa Waziri adumishe utawala bora kwa kuwachukulia hatua thabiti ya kuwakamata wauaji (askari wanyamapor) hawa na kuwaleta mbele ya vyombo vyanya sheria (Mahakama)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wachache Wilaya ya Rufiji tunaomba Jeshi la Polisi kwanza liwahamishe askari waliokaa Rufiji zaidi ya miaka mitano na kuletwaa askari wapya, hatua hii itapunguza kufanya kazi kwa mazoea na mianya ya kufanya kazi kwa kuombaomba kila kidogo (rushwa). Tusaidieni Rufiji jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja mia kwa mia, lakini naomba Wizara izingatie maombi yangu.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima kwa siku ya leo na kuniwezesha kuchangia hutuba hii ya mambo ya Ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi Nzuri walioifanya kwa kutayarisha hotuba hii yenye mwelekeo na inaendana na Ilani ya Chama Tawala CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Makamishna wote wa Polisi na Magereza kwa kazi kubwa na nzuri bila kujali wakati na siku na namna wanavyosimamia askari wao na ufanini mzuri unaopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na wanafanya kazi hiyo bila ya kinga inayomlinda askari, ni mara nyingi askari hufukuzwa kazi kwa uwongo wa wananchi. Suala hili linatokea baada ya askari kufanya kazi nzuri pengine amekataa kupokea rushwa fulani na baadaye yule mwenye hatia humzunguka askari na askari anakuwa yeye ndiye mwenye hatia na kwa kuwa hakuna kinga ya askari, askari huadhibiwa bila ya uchunguzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inavunja moyo na kupunguza rari za utendaji wa askari wetu. Mheshimiwa Waziri lazima afahamu, hakuna mhalifu yeyote anayempenda askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya Mkoa wa Kusini Pemba ili aje ajionee mwenyewe. Kituo cha Polisi Madungu ni kibovu na ni muda mreru hakijafanyiwa matengenezo yoyote na Waswahili wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivi sasa Serikali inajenga nyumba za Askari, lakini walisahau kukarabati vituo kwani ndio ofisi ya askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kiinua mgongo limeulizwa mara nyingi na kutakiwa lirekebishwe lakini bado lipo linazidi kuumiza ndugu zetu. Tunataka kusafisha Jeshi letu la Polisi na rushwa na kama kweli tuko makini na hili, basi jambo la mwanzo kuondoa malipo ya kiinua mgongo na tuweke pensheni kwa askari wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu ni zuri na linafanya kazi nzuri, lakini matatizo yako Serikalini kwa kutowaondolea kero zao na matatizo yaliyo moyoni mwao. Naomba Mheshimiwa Waziri aliondoe tatizo hili. Kama tatizo ni fedha, askari hawa hawastaa fu siku moja. Sasa sijui kuna tatizo gani hebu Mheshimiwa waziri atueleze, Serikali ina kigugumizi gani kuondoa tatizo hili linalotumika katika Jeshi la Polisi tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu mdogo, naunga mkono hoja.

MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii. Kwa kiasi kikubwa hotuba hii ina lengo la kuimarisha Wizara hii na watumishi wote walio chini ya Wizara hii. Aidha, Wizara imeifanya nchi yetu kuwa na usalama zaidi na kuwa kisiwa cha amani katika Afrika na Dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, naanze kuchangia hotuba hii kwa kuanzia na suala la Gereza la Kibiti. Kwa miaka miwili mfululizo, nilikuwa nachangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii kuhusiana na Gereza hili la Kibiti. Naishukuru sana Wizara hii na hasa aliye kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi Mheshimiwa Joseph Mungai kwa kwenda kuliona gereza hili hapo 2007 na kuweza kutoa fedha za ujenzi wa mabweni ya kulala wafungwa ambayo yapo katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhakikishia Waziri na Serikali kwa ujumla kuwa ujenzi wa bweni hilo unaendelea vizuri sana. Aidha, Gereza hili limepewa gari pamoja na fedha za ujenzi wa vyoo vya ku – *flash*. Ni matarajio yangu kuwa Serikali itaendelea kutoa fedha za ujenzi na kukamilisha mabweni ambayo yanatarajiwa kujengwa katika gereza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, bado naiomba Wizara iliangularie kwa jicho la huruma Gereza hili la Kibiti hasa kwa upande wa nyumba za askari. Nyumba zote za askari ni za udongo na zimejengwa miaka zaidi ya 30 iliyopita.

Nyumba hizo ni mbovu zinavuja na hazifai kukaa askari. Ni vizuri sasa wakati Serikali iwe inajenga mabweni ya wafungwa, kazi hiyo iende sambamba na ujenzi wa nyumba za askari wanaofanya kazi katika gereza hili. Kwa kufanya hivyo, kutawafanya askari hao waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusiana na vifaa vya kilimo kwa ajili ya Gereza hili la Kibiti. Gereza hili ni la kilimo na lina eneo kubwa la mashamba ambalo lina rutuba ya kutosha, lakini halilimwi kutokana na ukosefu wa zana za kilimo kama vile matrekta pamoja na pembejeo za kilimo. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kulipatia gereza hili trekta angalau moja ili waweze kufanya kazi zao vizuri kulingana na madhumuni yaliyowekwa ya kuanzishwa kwa gereza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusiana na mahabusu wanaokaa katika gereza hili wakisubiri kesi zao kusikilizwa. Nilipotembelea gereza hili juni mwaka huu nilishangaa kuona mahabusu ni wengi zaidi kuliko wafungwa. Wengi wa mahabusu hao ni vijana chini ya miaka 18. Nilipowahoji baadhi ya mahabusu hao sababu za kukaa rumande, walinifahamisha kuwa walikuwa na kesi za aidha, kuiba simu au mazao ya wakulima. La kushangaza zaidi ni kumwona mtoto mmoja chini ya miaka 18 amewekwa mahabusu kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa kosa la kuiba simu ha Sh. 30,000/=. Hali hii sio nzuri. Namwomba Mheshimiwa Waziri aende Gerezani Kibiti kuona ni namna gari ya kuwasaidia mahabusu, hao watoto ambao wanakaa katika mazingira magumu na kuwafanya walelewe gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Kituo cha Polisi Kitibi. Kituo hiki kipo umbali wa takriban kilometra 90 toka Makao Makuu ya Wilaya. Kituo hiki ndicho kituo cha pili kwa ukubwa na ndicho chenye kesi nyingi. Kutokana na kuwa na kesi nyingi na kuhudumia zaidi ya watu 140,000 katika Jimbo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kina matatizo mengi yakiwemo ya kukosa gari wala pikipiki ya kufanya kazi. Aidha, kituo kina ukosefu wa nyumba za kuishi, askari na kuwafanya waishi uraiani. Hali hii ni hatari na hasa ukizingatia kuwa kituo kina askari zaidi ya saba wakiwemo wale wa usalama barabarani. Naiomba Serikali itoe angalau pikipiki mbili ili ziwasaidie watumishi hawa waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, kituo hiki cha Kibiti kilicho jengwa miaka mingi iliyopita, kina matatizo ya jengo la ofisi. Jengo hili lipo katika eneo la barabara (*Road reserve*) na hivyo kwa sasa wanahangaika kutaka kuhamisha, lakini fedha hazipo. Ni vizuri Serikali ikalionna hili ili kuhakikisha kuwa jengo jipya linajengwa kwa ajili ya Kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. FELIX KIJKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya Wizara hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na watalaam wote kwa kuandaa hotuba nzuri sana. Ni wa mantiki hiyo, napenda kuiunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono, ninapenda kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipengele cha kuboresha maisha ya Askari, hiki napenda kutoa ushauri kuwa maisha ya askari ni duni sana kutokana na mshahara mdogo. Kazi inayofanywa na watu hao ni ngumu na isiyokuwa na muda wa kumaliza kazi. Ninashauri kwa makusudi mazima Wizara ijipange kuwaongeza mshahara na pia kuangalia uwezekano wa kulipa *risk allowance* kwa kila askari. Aidha, katika kuboresha hali hiyo, ni vyema pia kuangalia kiwango kinachotolewa kama *ration allowance* kwa kila askari kuwa ni kidogo mno. Vile vile wapo askari wanaokaa nje ya “*barracks*” ambao hawalipwi malipo ya *house allowance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fedha za likizo yamekuwa yakilalamikiwa kwa sababu wakati mwangi askari wamekuwa wakijigharimia nauli waendapo likizo kwa kuahidiwa kurudishiwa pindi wanaporudi. Malalamiko yaliyopo ni kuwa mbali ya kwamba wamekuwa wakifanya hivyo, lakini bado kurudishwa fedha hizo kunachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi la Polisi na hususan Idara ya Uhamiaji kwamba Idara hiyo imekuwa ikijitahidi sana kuwakamata Wahamiaji haramu na kuandaa utaratibu wa kuwarudisha walikotoka. Hali ambayo imekuwa ikikwamisha juhudzi za Idara hiyo kushindwa kuwarejesha kutokana na kukosekana kwa fedha. Ninashauri Idara hii itenye fedha kwa ajili ya kazi hiyo na fedha hizo zimilikiwe moja kwa moja na Mkuu wa Idara hiyo ili kurahisisha kazi za namna hiyo kufanyika pasipo kucheleweshaji ambao ni kutokana na maombi ya fedha kutoka Wizara hii. Sasa hivi kwa Dar es Salaam tu wapo wahamiaji haramu wapatao 1,500 ambao wako rumande wakisubiri kurejeshwa lakini kutokana na uhaba wa fedha imeshindikana. Hali hiyo inasababisha msongamano katika magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa kuhusu usafiri kwamba Wilaya za kwenye Mikoa iliyoko Mikoani kama vile Kibondo kwenye ujambazi wa kutisha, *OCD* hawana magari mazima ya kuwawezesha kupambana na ujambazi. Kwa Wilaya za Mikoa wa Kigoma yenye wakimbizi, magari ambayo yamekuwa yaktumika kupambana na ujambazi, ni yale magari ambayo wamekuwa yakifadhiliwa na *UNHCR*. Sasa hivi wakimbizi wanaondoka kurudio kwao na magari yaliyokuwa yaktumia yamechoka sana. Ninaomba Wizara hii iweke utaratibu wa kutoa magari kwa *OCD's* ili kuwawezesha kupambana na ujambazi. Hiyo ndio njia pekee ya kuokoa maisha ya wananchi wa Mikoa yenye ujambazi kama Mikoa wa Kigoma na Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wakimbizi wameingia katika Mikoa wa Kigoma wapo wananchi ambao waliharibiwa miradi yao kama vile kupigwa marufuku kuendelea kurina asali. Wananchi wa Wilaya ya Kibondo na hususan wa vijiji vilivyo karibu na zilipokuwa kambi za wakimbizi kama vile Nengo, Mtendeli, Kifura na Busunzu, walihidiwa kulipwa fidia. Hadi leo wakimbizi wanaondoka bila maelezo ya kamili ya malipo hayo. Ni vyema Wizara itoe hofu wananchi wa vijiji kwa kufanya mawasiliana na uongozi wa *UNHC* ili walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo sugu la askari kufanya kazi bila kupumzika. Hali hii inatokana na uchache wa askari ambapo suluhu yake ni kupanga kozi ya kuwafundisha vijana wengi na hatimaye kuwasambaza kwa nchi nzima. Kwa kufanya hivyo, askari watapata muda wa kupumzika. Kwa mtindo wa kubadilisha *shift* kwa masaa yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyenzo za kutendea kazi kwa maana ya magari kwa kikosi hiki hayakidhi mahitaji. Kazi kubwa ya kikosi hiki ni kupambana na dharura ya moto. Kumeibuka hali isiyo ya kawaida ya kuwepo kwa ongezeko la matukio. Kwa makusudi mazima kitengo hicho kipewe uwezo huo wa kuboreshewa utendaji kwa kupelekewa ombi rasmi kwenda Serikalini ili kuvezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Nyaronga kilijengwa na Serikali kwa makusudi ili kuweza kupambana na ujambazi unaofanywa na wananchi kutoka Burundi. Ndiyo maana kituo hicho kilijengwa mpakani kabisa mwa Tanzania na Burundi. Kituo hiki kwa muda mrefu kimekuwa kinatakiwa kukarabatiwa kwa muda mrefu pasipo mafaniko. Sasa hivi kuta zake zinakaribia kuanguka chini wakati askari wanafanya kazi humo. Ninaomba kituo hicho kifanyiwe ukarabati wa haraka kabla jengo zima halijaanguka chini.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, naomba nimpongeze wewe kwa uteuzi wa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii. Kubwa na nyeti. Aidha, kwa hotuba nzuri uliyowasilisha leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa kupitia kwako kumpongeza sana *Comrade Balozi Kagasheki* kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Uwezo anao na utashi wa kidiplomasia anao. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu Muya na watumishi wake.

Hoja, nampongeza sana *IGP Mwema*, Makamishna wote hasa Mtweve, Chagonja, Munisi, Mangu, Mama Mkumbi na wengine wengi kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa Wabunge na wananchi hususan Kilindi. Naomba nirejee tena ahadi ambazo zimetolewa mara kadhaa kwa miaka ya nyuma hadi sasa.

Kituo cha Polisi Kikunde: tangu enzi ya Chiligati alihadi wananchi wajenge kituo yeye ataleta bati 120 na misumari. Nilipokumbusha wakati wa Mheshimiwa Aboud alisema wanashubiri mvua zikatike, baada ya jitihada za wananchi kujenga kwa kasi na mvua kwisha, naomba hatimaye turudishe imani ya wananchi kwa kuleta hizo bati mapema. Naamini sasa litatekelezeka baada ya kuandika barua tatu kwa ofisi yako, sasa litatekelezwa bila kuchelewa. Natanguliza shukrani za awali.

Tunashukuru kwa kupata *OCD, OCS, OC – CID*, maaskari, lakini tatizo hatuna kituo, kuna posti ndogo tu, ambayo imetubidi tugeuze chumba cha mahabusu kufanya ofisi. Mheshimiwa Aboud akiwa Naibu Waziri, Wizara hii aliasema tusubiri tathmini ambayo ilikuwa inafanya pindi tutakapomaliza fedha zitatolewa ingawaje kazi ilikamilika, hadi leo tunasikia matatizo ya fedha. Je, hamwonni kama fedha za wapiga

kura zimetumika bure kufanya tathmini ambayo haitekelezeki? Naomba tusaidiwe tupate Ofisi ya Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya pamoja na ukubwa wake, hatuna gari la Polisi kwa takriban miezi mitatu licha ya kwamba tupo pembezoni jamani hapo sidhani kama ni sahihi kwanza nikuwatesa watendaji kwa kulazimika kutembea kwa mguu, njia ndefu na kutukanwa kwa kushindwa kufika kwenye maeneo ya matukio kwa wakati. Hii inakwenda sambamba na madeni lukuki waliyonayo ya mafuta. Kwa vile huku ni pembeni sana, basi tuisiwavunje moyo Polisi hawa kwa kuwatesa licha ya kwamba wanaishi katika mazingira duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hatua za awali kama tulivyoelezwa, lakini kama nakumbuka vizuri, hizo ni za ukarabati na ununuvi wa vifaa. Hivi zabuni tulizotangaza fedha ziko wapi? Hebu tuwe *practical* na angalau jambo lione kane. Tusingoje muda ambapo fedha hazipatikani. Hebu tuangalie angalau tuongeze fedha hata nusu ya shilingi bilioni 58.

MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba siungi mkono hoja. Haki ya Mungu siungi mkono hoja. Huu ni mwaka wa nne naomba usafiri kwa Wilaya ya Geita naahidiwa uwongo. Nimetembelea ofisi za Wizara hiyo mara nyingi. Waziri anafahamu, Mama Nyoni anajua tangu Waziri aliyetoka wanafahamu. Mwaka jana na mwaka juzi niliahidiwa Geita kupewa gari na pikipiki tano. Hadi leo hatujapewa. Tunaomba Geita kuangushwa Mkoaa wa kupambana na uhalifu. Geita ina matatizo mengi kwa sababu ya mvuto wa machimbo. Majambazi yote yako Geita.

Mheshimiwa *IGP* katika bajeti iliyopita, alisema kwa mdomo wake kuwa atatupatia gari na Mheshimiwa aliye kuwapo aliahidi kutupa gari aina ya *Land Cruiser pick up* na pikipiki tano.

Geita ina Majimbo matatu. Naomba nilete matukio ya ujambazi katika eneo langu Busanda, mwaka huu mauaji yametokea kijiji cha Katiro wamevamiwa mara tatu na watu wawili kuuawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ruhuha wamevamiwa mwalimu akauawa na wengine wakabakwa. Kijiji cha Isima, wamevamia mara mbili na kuua watu wawili. Nyanaguzu wamevamiwa mara sita na kuua mtu mmoja Kamena wamevamiwa mara moja na kuua watu wawili; Nyabalolo wamevamiwa mara moja na kuua mtu mmoja. Walivamia na kupora na Madiwani kuchapwa viboko; Kaseme Shule ya Muungano na Shule ya Nyamalulu, waalimu walivamiwa; Nyamalulu pia albino aliuawa. Mnekezi walivamia walimu na kumkatakata, walidai pesa; Magenge walivamia wakaua mtu, walivamia gari yangu kwa risasi na kumvunja mwalimu mguu. Haya ni matukio ya toka Januari hadi Julai. Wananchi hawana imani na askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mambo kukithiri, kuna mmoja wa kijiji cha Ibondo alimwona mtu ambaye alimshtukia na kaamua kupambana naye. Alimudu

kumpiga chini na kumnyang'aya silaha iliyokuwa na magazine yenye risasi 24. Ndipo wananchi wakaja wakamsaidia. Hivi sasa huyu kijana anatafutwa na majambazi. Pamoja na kazi hii nzuri Serikali imeahidi nini katika kumlinda na kumsaidia? Nadhani kuna haja ya kumpa tuzo ya ajira kwa ujasiri wake. Ni askari wangapi wamewahi kuwa jasiri kama yeze pamoja na usomi wao? Nashauri Wizara itusaidie kumhifadhi huyu kijana kwani atauawa na chama cha majambazi, anaishi kwa mashaka.

Katika jimbo langu nina gereza moja la Kilimo, Butundwe. Nasikitika kusema kwamba sioni na sielezi kinachoendelea. Waliomba niwatafutie eneo la kulima mpunga. Nikashawishi Serikali za vijiji zikawapa eneo zuri. Hilo eneo wameshindwa kulilima. Naomba tuwarudishie shamba hilo wananchi kwani wananchi wananailaumu mimi. Niliwahi kuja Makao Makuu ya Magereza kuomba trekta na ndani ya Bunge, niliahidiwa kuwa gereza hilo litapewa trekta. Badala yake tukapewa trekta bovu. Naomba vitendea kazi kwa Gereza hili.

Mwisho, Askari waache kunyanyasa wanaosafirisha magari kutoka bandari kwenda nchi za jirani. Niliwahi kupanda magari hayo karibu mara tatu na sikupenda kujitambulisha. Huwa wana *document* zote ila kila wanapokutana na askari lazima waache pesa. Vinginevyo hawa waruhusiwe kuendelea.

Matajri wengine wanaamua kuitishia Bandari ya Mombasa wanatunyima uchumi na wanatia aibu nchi yetu.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Waziri na Wasaidizi wake kwa hotuba nzuri sana. Aidha, naipongeza Wizara na majeshi yaliyoko chini yake kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wa Jeshi la Polisi wanaishi katika mazingira magumu sana. Polisi walio hapa Dodoma ni mfano mzuri. Askari wanaishi kwenye mabana ya mabati kukikotekea baridi, kama ilivyo sasa ni ya kwao na likiwapo juu ni lao. Haya ni mateso kwa askari na familia zao. Baadhi ya askari wamejjengea vibanda vyta tope. Tatizo ni nini? Jeshi la Polisi lina kikosi cha ujenzi, Jeshi la Magereza lina kikosi cha ujenzi ambacho wamekitumia vizuri sana kujenga nyumba za askari wao. Kwanini vikosi hivi visitumiwe kujenga nyumba za askari Polisi? Wakati huo huo Magereza wana wafungwa ambaa ni mafundi wa ujenzi uashi, useremala na kadhalika. Iwapo uwezo uliopo kwenye majeshi yaliyoko chini ya Wizara yatatumika inawezekana kupunguza tatizo la makazi ya askari. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ashughulikie suala la malazi ya askari kwa juhudhi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Dar es Salaam - Morogoro kipande cha Ubungo hadi Kibanda kina ajali nyingi sana na wananchi wengi wamepoteza maisha yao kwenye eneo hili. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwahi kujibu swali langu hapa Bungeni ambapo alitoa takwimu za kutisha sana za ajali kwenye eneo hili, yapo matatizo kwenye barabara hii ambayo yanapaswa kushughulikiwa. Tatizo la kwanza ni lile la kudhibiti mwendo (Kazi) wa magari. Tunaomba yawekwe matuta katika maeneo ambako ajali hutokeea mara kwa mara (*Black sports*). Wizara ya Miundombinu na RCC

wamekwishaagiza viwekwe vidhibitit mwendo kwenye maeneo hayo. Naomba Jeshi la Polisi lihimize kutekelezwa kwa uamuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mbezi Luis pana matatizo mawili pana kituo cha daladala chenyenye msongamano mkubwa wa magari na watu. Ilikwishakubaliwa kukipanua kituo hicho na kukiweka mbali na barabara. Hiki ni kituo cha ajali. Ni hatari tupu! Mbele kidogo kuelekea Morogoro penye Kanisa la Wakatoliki, kimewekwa kituo cha (*customs* cha kukagua mizigo) mahali hapo panakuwepo msongamano mkubwa wa malori makubwa ambayo yanameegeshwa kwenye barabara ya Dar es Salaam – Morogoro. Tunaomba sana kituo hili kiondolewe na tunaomba ushirikiano wa Jeshi la Polisi katika kuhimiza utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FUYA GODWIN KIMBITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Wilaya ya Hai, ninawapongezeni sana kwa hotuba nzuri, nikianza kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wengine wote Wizarani na kwenye Idara mbalimbali zilizomo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Nisiingie kwenye kuwarushia lawama askari wetu wote kwa maana ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto kwa baadhi yao kujihusisha na mambo ya rushwa, bali nishauri/napendekeza tuangalie na kuijuliza: Je, ni sababu zipi zinazowapelekea kudai/kuomba rushwa ili tukijaribu kutibu wale ambaio sio kwa sababu yoyote bali ni hulka yao, hao lazima tuwadhibiti na kukomesha vitendo hivyo.

Nashauri adhabu kali sana kwa wale wote wanaojulikana na vitendo vyatya muuaji kwa watu, wenzetu maalbino kwa sababu ya imani chafu za kushirikiana pamoja na wale wote wanaowafanyia vitendo watoto wadogo/wachanga kwa imani hizo. Ninapongeza Jeshi letu la Polisi kwa kazi mbalimbali wanazozifanya/kutenda ikiwa ni pamoja na *operations* na doria zote pamoja na hili wazo la Polisi jamii kwa mafanikio yake yameonekana na ni mazuri.

Ninashauri yale mashamba makubwa (maeneo) ambayo yako chini ya Jeshi letu la Magereza utaratibu ufanyike yapewe taasisi/watu wengine wenye uwezo wa kuyaendeleza badala ya hivi yalivyoachwa na kuwa mapori na wengine vichaka vyatya majambazi.

Ninashauri tuwe na uangalifu wa ziada kuhusu wageni na wakimbizi wanaoomba uraia wa nchi yetu kwani mengine huko watokako hawakuwa na sifa nzuri na baadhi yao waliingia hapa nchini kinyume kwa njia ambazo sio za halali.

Hivi hii kazi ya kusajili vyama/vikundi vyatya kijamii bado ni sahihi iendelee kuwepo ndani ya Wizara hii ikiwa kuna ofisi/Wizara nyingine zinafanya kazi hizo hizo na kwa kuzingatia majukumu mengi, makubwa na muhimu yanayoikabili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi wa vitambulisho vya Taifa ninaungana na waliopendekeza mradi huo ufanywe na Idara yetu ya uhamiaji na siyo kupewa makampuni binafsi.

Ninashauri kwenye Magereza yetu vyuo vya Polisi na uhamiaji kwa shughuli za kupika na taa tutumie *biogas technology* ambayo tayari Mtanzania mwenzetu aliwafanya nchi jirani na hivyo kuokoa gharama na kulinda mazingira yetu kwa maana ya kutotumia kuni.

Katika kitengo cha kushughulikia malalamiko, ninaomba wakati wa kuhitimisha nipiatiwe majibu ya ni nini au hatima ya kesi iliyokuwa *ikiwakabili Askari Polisi* na Kituo cha Mabatini Kijitonyama waliomtesa na kumnyanyasa kijinsia binti mdogo aliyepelekwa pale kituoni kwa kisingizio cha kumwibia aliyekuwa mwajiri wake na hatimaye ikagundulika ilikuwa uonevu, kwa hiyo, binti anayeitwa Alice Nahumu, bado anaumwa hadi leo hii kutokana na mateso aliyoypata.

Mwisho, ninapendekeza kwa wale Polisi na Askari wengine kwenye idara mbalimbali wanaofanya kazi vizuri na kwa uadilifu wapewe zawadi na kupandishwa vyeo ili tuwatie moyo zaidi kikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhanu wale wote wenye utovu wa nidhamu na waisofuata/kutii maadili kazi zao.

Kwa mara nyingine ninaunga mkono hoja.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaunga mkono Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *the IGP* na viongozi na watumishi wote wa Wizara hii. Uongozi mpya umeanza kuonyesha kuwa taswira ya matumaini na hii imeelezwa vizuri na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maeneo ya kutilia mkazo zaidi: Kwanza, maslahi ya Jeshi la Polisi ni Jeshi ambalo linahitaji mtazamo wa kipekee. Maslahi haya ni pamoja na mishahara, makazi, posho, nguo, likizo, elimu na kuthaminiwa na viongozi pamoja na Taifa kwa ujumla, wananchi wanaowalinda na mali zao. Maslahi haya ni pamoja na vitendea kazi na fedha za matumizi (*OC*) katika ofisi za Wilaya na Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetanguliza haya, kuelezea kwamba chanzo cha matatizo yanayozungumzwa, msingi wake ni mazingira duni ya Jeshi la Polisi. Kule Bariadi watu wanauawa mno. Gari la Polisi likitoka halirudi tupu. Ndiyo kusema lazima lirudi na mahabusu au fedha. Kama wananchi wana mtazamo huu, ni vipi wataliamini Jeshi? Bariadi pakitokea tukio la uhalifu, kituo kinadai wale wananchi walioomba huduma ya Jeshi walipie mafuta ya gari ya Polisi. Jambo hili nimeliona na risiti ya petroli nimeiona, hili limewezekana kwa sababu (*OC*) fedha ya matumizi haipo.

Ukimwuliza *RPC* anasema haifanyiki. Ukimwuliza Waziri anasema hili halipo. Hii ni kuficha ugonjwa na utaumbuliwa na kilio. Ni vizuri Serikali ikubali hili lipo na likatafutiwa dawa. Ushauri wangu, kwa kuwa tumeamua kuhamasisha ulinzi shirikishi,

basi sioni sababu ya kuzuia, kushirikisha Halmashauri katika kulinda wananchi wake. Tunahitaji mtazamo mpya wa kushirikisha Halmashauri katika matumizi ya Polisi. Huduma ya ulinzi wa wananchi na mali zao haiwezi kuachiwa Serikali kuu tu. Imeshindikana na matokeo yake ndiyo haya na kuomba wananchi kulipia gari kwa siri. Jambo hili liangaliwe kwa kina. Wananchi wako tayari kulipia kodi ya kulindwa kama Polisi watakuwa waaminifu na watenda haki.

Aidha, tatizo lingine ambalo hata Mheshimiwa Waziri amelisema ni hili la kubambikiza kesi zaidi kesi ya mauaji isiyo na dhamana. Wilaya yetu ya Bariadi, tatizo hili ni kubwa na zaidi jambo linapohusisha siasa, mtindo wa kubambikiza kesi kwa misingi ya ushiriki wa kisiasa ni aibu kwa jeshi zima. Naomba uchunguzi ufanywe Bariadi juu ya tatizo hili zaidi katika Idara ya upelelezi. Wasukuma hawataki bugudha. Ukimpa kesi ya kuua atalipa hongo tu. Udhifu huu wa msukuma unatumika sana Bariadi. Kwa hatua ya haraka Polisi wetu wa upelelezi pamoja na dreva upelelezi wahamishwe kwani wamekaa muda mrefu mno.

MHE. DUSTAN MKAPA: Mheshimiwa mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Masha na Naibu Waziri - Mheshimiwa Kagasheki kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Wizara hii. Aidha, napenda nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na *IGP* kwa kuchapa kazi zao kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Wilayani Nanyumbu wanaishi kwa taabu sana. Wilaya ya Nanyumbu hakuna nyumba za kuishi askari Polisi. Polisi wanaishi uraiani. Hivyo ninaiomba Wizara iwaonee huruma Polisi wa Nanyumbu kwa kuwajengea nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Nanyumbu hakuna kituo cha Polisi cha maana. Nyumba ya kuishi askari imegeuzwa kuwa Kituo cha Polisi. Hivyo, naiomba Wizara ijenge kituo cha Polisi Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu ina gari moja tu la Polisi. Wilaya hii eneo lake ni kubwa sana na inapakana na nchi jirani ya Msumbiji. Gari hilo moja la Polisi halikidhi mahitaji ya Wilaya nzima. Matukio ya uhalifu ni mengi, gari moja kuhudumia eneo kubwa la Wilaya ya Nanyumbu halitoshelezi. Ombi hili nilimfikishia Mheshimiwa Masha na aliahidi kulishughulikia, lakini naona mpaka hivi sasa naanza kukata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaoiomba Wizara itupatie pikipiki Wilayani Nanyumbu ili Polisi waweze kufika maeneo yasiyopitika kwa gari kwa haraka na pia kuweza kufanya doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya narudia kuunga mkono hoja hii na kuomba Wizara isikilize maombi yangu hapo juu ili Wilaya ya Nanyumbu ambayo ni mpya iweze kuimarika na Polisi wake waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Lawrance Kego Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri - Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Inspeka Jenerali Said Mwema pamoja na Makamanda wote. Wanastahili pongezi kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu mradi wa vitambulisho vyta Kitaifa. Waziri amelieleza Bunge lako Tukufu matarajio ya Wizara yake ya kumpa mkandarasi atakayesimika mtandao wa ukusanyaji wa takwimu kwa mwaka huu wa fedha. Kwa kuwa zoezi hili nyeti, gumu/gharama kubwa na endelevu kutokana na ukweli kuwa binadamu wanaangaliwa kila siku, sioni mantiki ya kukabidhi zoezi hili kwa wakandarasi. Pengine Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwanini Serikali isifanye kazi hiyo nyeti badala ya kukabidhi wafanyabiashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tume ya Uchaguzi imeweza kutumia mtandao wa watendaji wa Serikali kikamilifu na kwa mafanikio, kwa nini Serikali isitumie idara zake ikiwemo idara ya uhamiaji wakisaidiwa na mtandao wa Serikali kama Serikali za Mitaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa ni zaidi ya mwaka mmoja sasa tangu majambazi waliovamia na kupora magari mapya mawili mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ambapo gari moja lilipatikana nchi ya jirani, hadi sasa gari hilo halijarejeshwa Simanjiro na taarifa ya gari lingine bado ni kitendawili. Je, Serikali itarejesha lini gari hilo kwenye Halmashauri ya Simanjiro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu limekwishapoteza Wabunge wenzetu watano wakiwemo watatu waliopoteza uhai wao kwa njia ya ajali. Wabunge hao ni Marehemu Salome Mbatia, Marehemu Juma Akukweti na Marehemu Chacha Zakayo Wangwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhali yapo madai au ushauri unaodai kufanyiwa uchunguzi wa kifo cha Marehemu Chaha Z. Wangwe, naishauri Serikali ifanye uchunguzi wa kifo hicho na iwapo taarifa zimekamilika, umma upatiwe taarifa kupitia Bunge lako Tukufu. Mimi siamini ukimya pale umma unapohitaji kupatiwa taarifa. Binadamu huzaliwa na hufa lakini mkanganyiko wa taarifa za awali zinadai taarifa za ziada.

Naunga mkono hoja.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana, mchakato wa ajira kwa vijana ajira katika Jeshi la Polisi hutekelezwa katika Mikoa. Hii ina maana kila Mkoa hupewa idadi maalum ya vijana wanaohitajiwa kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mchakato wa kuwapatia hao vijana unalazimisha kila Mkao upewe idadi maalum ya kuwapata vijana hao ili waweze kuajiriwa. Mfano kwenye Mkao wangu wa Kusini Pemba, kijana hawesi kufika kwenda kwenye mafunzo ya upolisi kama hajakubaliwa na sheha, Kamati ya Ulinzi ya Wilaya na hatimaye Kamati ya Ulinzi ya Mkao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo ni mzuri, kwani unahakikisha vijana watakaoajiriwa ni wenye tabia nzuri kama haukupita ubinafsi ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana inapotokea kukubaliwa kupata ajira, vijana wanaotoka nje ya Mkao huo hususan kutoka Unguja na Tanzania Bara na kuchukua nafasi ambazo kimsingi sio zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inadhihirisha kuwa baadhi ya viongozi wa Polisi wanaashiria katika zoezi hilo la kuwapandikiza vijana kutoka maeneo mengine yasihohusiana na Mkao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inatokana aidha na rushwa au ujamaa (undugu) umefanya kazi, lolote lile kati ya hayo mawili, uajiri wa aina hiyo haukuliki. Huko ni kutowatendea haki vijana wa Mikoa ambayo imepandikizwa vijana kutoka Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo au jawabu la maswali haya. Je, yuko tayari kuchunguza kashfa hiyo? Je, atakapobaini wale vijana ambaa wamechukua nafasi sio zao wataondolewa kwenye mafunzo? Je, wale viongozi wa Polisi walioshiriki katika zoezi hili baya kwa ajira ya kwanza 2008 Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria za nchi kanuni za Jeshi la Polisi (*PGO*)? Je, Mheshimiwa Waziri anatuahidi nini ili suala hilo lisitokee tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuacha utaratibu huo uendelee unaweza kuleta hisia mbaya mionganoni mwa vijana wa nchi hii.

MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri na yenye maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa ya waajiriwa wa Jeshi la Polisi kwa upande wa Zanzibar ni maonevu ya askari wa ngazi ya chini (wasio na vyeo) kumekuwepo na kufukuzwa kazi kiholela kwa baadhi ya askari bila ya kufuata utaratibu wa bila ya Makao Makuu kujua chochote.

Kuna mifano hai kwa baadhi ya askari kufukuzwa na kuwepo nje kwa muda wa miezi kadhaa hata mwaka na wakati huo huo mishahara yao ikiipelekwa Zanzibar na baadaye kupandishwa cheo na Makao Makuu. Inakuwaje matukio kama haya yanatokea? Mheshimiwa Waziri anaweza kunithibitishia kwamba haya hayatatokea tena? Matukio

kama hayo yameigharimu Serikali, wanapowarudisha askari hao kazini na kuwalipa malimbikizo yao ya mishahara bila ya kufanya kazi.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupakana Wilaya ya Geita na Wilaya zilizopokea wakimbizi: Wakimbizi waliokuja Wilaya za Ngara, Kibondo, Kasulu baada ya kurudi kwao wapo ambao wamebaki katika Wilaya za Bukombe, Kahama, Biharamulo na Geita kwani wanachanganyikana na ndugu zao ambao wanaishi huko kama Watanzania, hawa wengine wana silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Wilaya ya Geita: kuwapo kwa miundombinu inayowezesha majambazi kujificha. Geita ina misitu mingi pamoja na visiwa ambavyo ni maficho ya wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za kiuchumi: kuwapo kwa migodi mikubwa na wachimbaji wadogo wadogo (migodi midogo midogo) pamoja na makambi ya wavuvi kunasababisha mikusanyiko mikubwa ya watu ambayo ni sehemu ya maficho ya wahalifu/majambazi. Geita ina watu milioni moja sasa.

Operations zinazofanyika Mikoa ya Kagera na Kigoma mara kwa mara kumewafanya majambazi kukimbilia Wilayani Geita. Kwa kuwa *RPC* Mkoa wa Mwanza hivi karibuni aliongeza maaskari (kwa muda) kuimarisha hali ya usalama Geita (mjini), majambazi sasa yamekimbia/yamegeukia maeneo ya vijiji ambapo mara nyingi yanashirikiana na wenyeji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujambazi kufufuka kuwa mradi – *Investiment*: Vijana ambao wamekuwa wakishirikiana na majambazi wamekuwa wakibadilika kiuchumi. Hii imewafanya hata wale vijana wema (baadhi) kushawishika kufanya biashara hii inayolipa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maaskari kushirikiana na majambazi: Askari waliokaa Wilayani humo kwa muda mrefu wanajenga mazoea na baadhi ya watu wabaya, kuwalinda. Kuna ushahidi kwamba baadhi ya majambazi (watuhumiwa) wanapofika Polisi huachiwa baada ya kutoa pesa (hili nina ushahidi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya *OCD* kutokuwa na usafiri: Kuna gari moja tu *Land Rover* ya siku nyingi iliyochakaa na ambapo hulazimika kutembea zaidi ya kilometra 500 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba, wizara ipeleke magari mawili Geita kwa *OCD* ili magari mawili yawe ya *patrol* na moja *standbay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ipeleke angalau pipipiki kwa vituo vya vijiji ili Kuimarisha kujenga majengo (*armery*) vituo vya vijiji kwa kutumia nguvu ya wananchi. Wanasiwa, Serikali kuu, *DC/Makatibu Tarafa* wanawenza kuhamasisha, kusimamia hili na ku-overhaul maaskari Wilaya ya Geita.

Ngazi za juu Mkoa/Taifa kufanya vikao elekezi kwa maaskari hao mara kwa mara kwani wengi wamejisahau na kwao ujambazi ni “mgodi”/ deal/neema.

Naomba maelezo ya Wizara juu ya haya.

MHE. MAULIDAH A. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa pamoja na kujadili Wizara hii nyeti ya ulinzi wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ni Wizara muhimu sana kwa nchi yoyote duniani, kwani ndiyo inayolinda maslahi ya usalama wa raia ndani ya nchi yao pia kuwa na usingizi mzuri kwani huwa tunahakikisha tuna ulinzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali machache tu kwa Mheshimiwa Waziri.

Wananchi hawana raha ndani ya nyumba zao, ifikapo usiku, ulinzi umekuwa kitendawili kisichoteguka. Je, kuna nini? Ina maana mpaka leo haikuweza kupata njia ya ulinzi thabiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwamba tujitahidi kuwapa maslahi mazuri askari wetu, tujitahidi kuwapa vitenda kazi vya kutosha, tujitajidi kuwaweka kwenye mazingira mazuri, tuondokane na kuwaacha askari wetu kwenda kulinda na virungu na kuishi kwenye nyumba za kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho wa askari wetu uzingatiwe sana hususani wale viongozi wasikae kwenye kituo kimoja zaidi ya miaka mitatu au mitano

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ufisadi ni jambo ambalo linachangia sana wananchi kukosa imani na Serikali zao. Je, wale Askari usalama waliokuwa wakifuatilia kwa karibu sana wananchi wasioeleweka wako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma wakati wa utawala wa Serikali ya awamu ya kwanza, yoyote aliyekuwa akionekana maisha yake yanabadilika haraka haraka kwa kujenga majumba mazuri na kumiliki magari ya fedha nyingi kinyume na mapato yake, alikuwa akifuatiliwa na mpaka kupatikana na hushikwa na kuulizwa mali hizo amezipata wapi. Je, leo vipi? Kuna nini? Naogopa kusema hawapo, lakini inatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimamoto: kuna mambo mengine yanatisha nchi hii, kila siku tunaimba nyimbo ya hakuna fedha, hii nyimbo sio nzuri, kwani wazee wa zamani walisema wimbo mbaya habembelezewi mtoto. Lakini Serikali yetu watubembeleza kila siku hakuna fedha, nchi maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moto umeshawaka, ndipo simu hupigwa kuitwa gari la Zimamoto, lakini likifika kwenye eneo, hamna maji wanaondoka kwenda kuweka maji na hapo moto ndipo unamaliza mali inayowaka. Je, lini Serikali itakuwa na fedha ya

kujenga ofisi nzuri na kununua magari ya Zimamoto ya kutosha na askari wapewe nguo zinazohitajika kwa moto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi wa kesi au kwa maeneo mengine upelelezi wa kezi umegubikwa na harufu ya rushwa kwani ukiangalia, kesi zinazochunguzwa mpaka zikifikishwa Mahakamani kwa kweli hairidhishi. Mpaka leo wananchi wanalamika kuhusu wanavyokamatwa, vituo vya Polisi vinavyowatesa na kesi zinazofuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu, hebu tubadilishe namna ya ufuutiliaji wa kosa na pia kutoa elimu ya kutosha kwa askari wetu wanaopeleleza makosa kabla ya kuyafikisha Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Polisi viwe ndio vya kutoa hukumu kwa kuwatesa wanaodhaniwa ni wakosaji. Mtuhumiwa anapolalamika asikilizwe, siyo kudharauliwa na kuonekana yeye ni mkosa. Narudia, tujitahidi kwa njia yoyote kuwapa maslahi mazuri askari wetu – labda itapunguza rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamiaji ni chombo cha kukiangalia kwa udhabiti kwani hapa ndipo tunapopokea wageni wazuri na wabaya. Ofisi za mipakani bado zina utata, kwani watu wanapita kama sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa *passport* bado hatujaweza kuudhibiti. *Permit* za wageni wanaotaka kukaa nchini kibashara au kufanya kazi bado kuna malalamiko kwamba wasio raia wapo, wamejaa wanafanya kazi ambazo raia wangezifanya na biashara ambazo haziruhusiwi wageni kuzifanya – tuiangalie tena uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uhamisho wa wafanyakazi uzingatiwe. Sio vizuri kuacha Askari Uhamiaji kukaa kwenye eneo moja kwa muda mrefu (anazoea vibaya na kujenga urafiki).

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya mara kwa mara inahitajika kwa askari wetu wote, inasaidia kwani dunia inabadilika ya jana sio ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pamoja na hayo, napenda kusisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Heru Ushingo Wilaya ya Kasulu ni eneo muhimu sana kiusalama kwa sababu linapakana na mpaka wetu wa Burundi na kuua vijiji zaidi 11 katika eneo hilo kupitia ulinzi shirikishi (Polisi jamii) naomba sana Wizara itenye fedha au kwa kupitia marafiki zetu wa upendeleo au/na bajeti ya mwaka 2009/2010 ili kupanua kituo kidogo kilichopo ili kifanane na hali ya eneo husika (nyumba za askari, ofisi kuu na vitendea kazi) idadi ya askari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu tutaoa ushirikiano mkubwa baada ya uamuzi wa Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamisha Gereza kuu la Kasulu lililopo katikati ya Mji wa Kasulu, hapo nyuma zilikuwepo fikra za Jeshi la Magereza kuhamisha gereza na kulipeleka maeneo ya Heru Ushingo, Kagera Nkanda, Rungwe Mpya, maeneo yenye rutuba safi na maeneo makubwa yenye nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo/Ombi langu ni kwamba Gereza hili lihamishwe na lifanywe gereza la Kilimo. Hii itasaida sana katika uzalishaji wa chakula na kupunguza Mgogoro wa Msongamano gerezani. Aidha, Gereza la Kasulu mjini linaweza kutumika kwa Mahabusu au makosa madogo madogo. Tuanze mchakato sasa ili mwaka 2009/2010 tutenge fedha katika bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama katika Mikoa ya Kigoma na Kagera, pendekezo/ombi/ushauri wangu ni kwamba iundwe kanda maalum ya Kigoma/Kagera ya kipolisi kama ilivyo Kanda ya Dar es Salaam. Hali ya usalama ya Mikoa hii na hasa Kigoma ni tete (*unpredictable on and off*). Sababu kubwa ni nchi za DRC, Burundi na Rwanda hazina usalama wa kutosha. Kanda hii itasaidia sana kudhibiti hali katika eneo hilo. Naomba Wizara ya Mambo ya Ndani/IGP wafanye utafiti na pengine tuanze kwa miaka miwili ili tuone hali itakuwaje. *Give it a thought and get started.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha mamlaka ya Usalama Barabarani, (*Traffic and Roads Authority*) kama ilivyo katika nchi nyingine duniani kama Australia, New Zealand na nchi nyingi za Caribbean, mamlaka hii itakuwa inaongozwa na Raia na sio Jeshi la Polisi, Polisi watakuwa kazi yao ni kutekeleza sheria tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida zake: *Police Force* itapunguziwa mzigo na taasisi itafanya kazi kama ilivyo kazi ya TRA na hata TPH.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka hii itaanzisha utaratibu wa kuwatahini madereva wote nchi nzima. Madreva wa magari ya abiria, malori makubwa na mitambo watafanyiwa utaratibu maalum wa mafunzo na mitihani. Akishindwa asiruhusiwe kuwa barabarani kabisa, utoaji wa leseni utafanywa na mamlaka na siyo *Traffic* Polisi tena. *Police will only enforce the law.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali barabarani zitapungua na magari yote yatakaguliwa na mamlaka kuitia gereji maalumu zenye viwango nchi nzima ambazo zitabainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa barabara kubwa *highways* itasimamiwa na mamlaka hii kwa kushirikiana na *tanroads* (Wizara ya Miundombinu), *Police Traffic* na watumiaji barabara wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo tayari kutenga muda wangu au Kata kuandika andiko (*paper*) endapo vitaombwa na Wizara yako kufanya hivyo. Aidha, ninaweza kukutana na wewe/Wizara yako tukazungumza ili nifafanue dhana hii (*I am available*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa askari Polisi Wilaya ya Kasulu: Wilaya yangu ni kubwa sana katika Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma. Aidha, ina wakazi zaidi ya 760,000. Uhaba wa askari ni mkubwa. Naomba Wizara na Ofisi ya *IGP* itoe kipaumbele katika maeneo yenyewe watu wengi na tete, yaliyo katika mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Askari Kituo Kikuu cha Kasulu (*OCD Office*), ni chakavu sana. Naomba Mheshiiwa Waziri atenge fedha za ukarabati wa nyumba hizo na kujenga nyumba mpya za gharama nafuu kwa askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pikipiki kwa askari, vituo vidogo vya Reusesa, Heru Ushingo, Rungwe Mpya Wilayani Kasulu.

MHE. DAMAS PASCAL NAKEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kutoa salaam zangu za rambirambi kufuatia kifo cha ghafla cha Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe Mbunge wa Tarime. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake Marehemu kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi ni kama kioo cha kuonyesha kuwa nchi yetu inazingatia utawala wa sheria na wananchi wanahakikishiwa usalama wao. Kwa nini tumefikia hatua ya wananchi kujichukulia sheria mikononi? Kwa nini Watanzania wengi sasa hawaogopi kuvunja sheria kwa maana nyingine hawaogopi kuwakosoa wenza? Mfano dereva wa basi la abiria anapokwenda ovyo haogopi kwamba anawakosea na kuwaudhi na kuwahatarishia maisha abiria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo langu la uwakilishi, Jimbo langu la Babati Vijijini tumekuwa tukisikia vituo kadhaa vya Polisi kujengwa ili kuleta karibu huduma za kipolisi. Tunaomba kituo cha Polisi Bashanet, Dareda, Galapo na Duru. Kila mara tumeambiwa wananchi wajenge wenyewe. Je, hiyo ni sahihi? Je, Serikali haiwezi kusaidia suala hili muhimu kwa usalama wa raia wa babati vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja ili Serikali iweze kutekeleza ahadi zake.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya inanipassa kwenda Jimboni kwa ajili ya ujio wa Rais na kwa hiyo, naandika mchango wangu bila kuona hotuba yako. Nina machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kituo cha Polisi Makao Makuu ya Tarafa ya Kalenga yaliyoko Kalenga, sasa hivi kiko Ipamba Hospitali. Hapo Kalenga pamekuwa na matukio ya uhalifu bila wahalifu kukamatwa mauaji yapatayo sita katika miaka minne/mitano iliyopita yanahitaji uwepo wa kituo *Lockup* ipo na tunaweza kusaidiana kupata ofisi. Nyumba za kuishi kwa kupanga zitapatikana.

Pili, kuna mashirika mawili ya kitapeli ambayo nitapenda kuona Polisi inawashughulikia. Moja, likiitwa *HEA (Heal Environment in Africa)*. Liliwatapeli kama

shilingi milioni 20, wananchi wa Kata ya Magulilwa. Niliiarifu Polisi miaka miwili iliyopita na Polisi (*Advocate Nyombi*) aliniarifu kuwa viongozi wao walikamatwa, lakini sikusikia zaidi. La pili linaitwa *COEL*. Lilitapeli fedha zisizojulikana katika Tarafa ya Kalenga, Ifunda na Ipengine Kiponzela. Mkoaa na Wilaya walipiga marufuku, wakawaruhusu na kuwapiga marufuku mara ya pili. Waliwataka watu walipe Sh.18,000/= ili wapatiwe kazi, lakini walitokomea baada ya kushtukiwa na wananchi. Sijui kama Polisi walifanya lolote, lakini mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kalenga na hususan wale walioliwa hela zao, ningependa kuona wanachukuliwa hatua, uchunguzi ukidhihirisha utapeli wao.

Tatu, suala la madawa ya kulevyaa linakera wote wanaolitakia mema Taifa hili. Kutokana na taarifa za vyombo vya habari, kila mara ni vigumu kuelewa kwa nini wahalifu hawachukuliwi hatua. Bila shaka, Polisi inawajua *Drug kings* na *drug pushers* walio wengi. Kwa nini wasishughulikiwe, ikiwa ni pamoja na kushikilia *passport* zao? Taifa hili litakuwa la mazeza katika miaka 20 mpaka 30 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala hili, nimeshindwa kuelewa kwa nini kuna kitengo katika ofisi ya Waziri Mkuu cha kupambana na madawa hayo. Maana yake ni nini? Polisi hawawezi? Nashauri kama ifuatavyo:-

- *Drug Dealers/pushers* wanaofahamika wapelekwe katika vyombo vya sheria pamoja na kuwapokonya pasi za kusafiria;
- Sioni sababu ya kuwa na kitengo nje ya Polisi, hivyo kirejeshwe; na
- Vita dhidi ya madawa haya ihamie pia mashulenii, kuwe na mitaala katika shule zote za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sitakuwepo kupiga kura, naitakia Wizara hii kila la kheri ili makadirio ya Wizara hii yapite bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuzungumzia mishahara na marupurupu ya Askari Polisi. Inasikitisha sana kuona maisha ya Askari Polisi ambao kwa kweli sasa wanafanya kazi nzuri sana, hayaboreki. Askari wetu wanafanya kazi usiku na mchana wakiwa wamebeba silaha lakini maslahi yao hayaangaliwi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu hawana nyumba, mishahara midogo, hawana marupurupu mengine hata yale ambayo ni stahili yao kisheria. Askari hawa wanalinda mabenki yetu, naomba Serikali/Waziri aniambie wanalipwa kiasi gani cha fedha kwa kutoa huduma hiyo ya ulinzi?

Aidha, napenda kujua pia kwa faini tu (*notification*) kutokana na usalama barabarani ambazo hulipwa na madereva wanaofanya makosa na wanaotembeza magari mabovu ni kiasi gani cha fedha kinachopatikana? Je, kiasi hicho hakiwezi kuboresha

maisha ya askari wetu, hata kwa marupurupu tu? Naomba maelezo ya kina juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati aliyejewa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia -Mheshimiwa Aboud alipokuwa akijibu swali langu jinsi ya kuweka umeme kituo cha Kibakwe cha Polisi. Naomba nifahamu kama Wizara katika bajeti yake imeweka fungu hilo, ambapo ni kiasi cha takriban shilingi milioni nne tu.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka niridhike na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri atatoa.

MHE. MOHAMED ABOUR MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja. Naomba kutoa pongozi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji na hasa *IGP* kwa kazi nzuri kutekeleza majukumu yenu. Mchango wangu unagusa Jeshi la Polisi pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi, lakini katika kulifanya Jeshi la Polisi liwe la kisasa linahitaji mambo matatu muhimu ambayo ni vifaa vya kisasa, taaluma na maslahi ya askari.

Naomba Wizara iangalie umuhimu wa kuwapatia vifaa vya kisasa askari, kuimarisha taaluma zao, aidha, kuona umuhimu maslahi ya askari hasa katika mradi wa kujenga nyumba za askari. Aidha, kutazama utaratibu maalum kupewa viwanja vya ujenzi Askari Polisi katika eneo moja ili iwe rahisi kupatikana wakati wa dharura kwa kukaa eneo moja.

Naomba pia uangaliwe mpango maalum kupatiwa maji ya bomba katika makambi ambayo yana upungufu wa maji, kwani hili linakuwa tatizo sana kwa askari hasa wanawake ambao wanapaswa kuhudumia Jeshi pamoja na familia zao. Aidha, kufikiria kuanzisha shule za chekechea kila kambi ili watoto wa askari wapate masomo ya awali katika makambi yao.

Kutokana na umuhimu wa afya kwa askari hasa na mazingira yao ya kazi, naomba pia kuwe na mpango maalum wa dharura kuimarisha hospitali za Jeshi la Polisi pamoja na kujenga vituo vya afya kila kambi na kuifanya hospitali ya Kurasini Mjini Dar es salaam kuwa Hospitali ya Rufaa ya Jeshi la Polisi.

Naomba pia kuwe Idara ya Upelelezi ya Polisi ipewe upendeleo maalum kutokana na umuhimu wake katika Jeshi la Polisi hasa kuendeleza ujenzi wa Chuo cha *CID*, Dodoma pamoja na kukarabati majengo ya Kidatu yatumike pia kuwa Chuo cha *CID*. Pamoja na kujenga Makao Makuu ya Polisi *CID* Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. DR. WILBROD PETER SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya ya Karatu na hasa Miji ya Karatu, Kibaoni na Barazani kuwa na mchanganyiko mkubwa wa watu kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo za kitalii, biashara na hata za kijamii kumekuwa na matukio mengi ya uhalifu na hata ujambazi na kwa kuwa Polisi Wilaya ya Karatu ina gari moja tu, tena zee na limechoka lenye usajili No.STJ.3413 la mwaka 2000 jambo ambalo limefanya Jeshi la Polisi kupata wakati mgumu katika kufanya kazi zake kwa ufanisi: Je, ni lini *OCD* wa Karatu atapelekewa angalau gari moja jipya ili Jeshi la Polisi liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ilianzishwa rasmi mwaka 1995. Kwa muda wote huo Jeshi la Polisi limekuwa likitumia majengo ya makazi ya askari yaliyojengwa wakati wa ukoloni ambako Wilaya ya Karatu yote ilikuwa *Division*. Majengo hayo yamechoka, hayajawahi kufanyiwa ukarabati na wala hayajaongezeka hata baada ya Karatu kuwa Wilaya na wakati huo huo viongozi wa jeshi akiwemo *OCD* na *OC-CID* wakiishi mbali na Kituo cha Polisi jambo linalofanya wafanye kazi katika mazingira magumu kwa kukosa usafiri wa uhakika, magari ya watu binafsi jambo linalofanya Jeshi letu kupata picha mbaya na kwa kuwa *OCD* wa sasa ameanza mpango wa Harambee wa kujenga nyumba ya *OCD* kwa kuanzia na hatimaye nyumba ya *OC-CID*.

Je, Serikali iko tayari kuchangia jitihada hizo za *OCD* na wananchi wa Karatu kufanikisha zoezi hilo na katika bajeti hii inaweza kuchangia kiasi gani pamoja na kilio cha jumla cha ufinyu wa bajeti?

Serikali ina mpango gani wa kujenga makazi ya askari, angalau kwa awamu baada ya nyumba chache zilizoko kuwa *condemned*? Kama kwa mwaka huu haiwezi kufanya lolote, Waziri anaweza kuahidi mpango huo utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Karatu imetua ardhi ya uhakika kwa ujenzi wa Magereza ya Wilaya ya Karatu kuondoa kero ya watuhumiwa kupelekwa Manyara au Arusha kwa kuwekwa *lockup* na au wafungwa kupelekwa Gereza la Kilimo la Mang'ola ambalo liko mbali sana na au kupelekwa Arusha na kwa kukosekana gari haki za walioko rumande zinaminywa sana kwa kukosekana usafiri wa uharaka na kwa uhakika,

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itaanza lini ujenzi wa Magereza ya Wilaya ya Karatu katika eneo lililotengwa na Serikali? Imeishalipia fidia tayari eneo hilo? Maandalizi ya ujenzi huo mathalan ramani yamefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa gharama za ujenzi zinapanda kila leo. Je, kwa kuchelewesha ujenzi huo, Serikali haioni kuwa itafika mahali hata ujenzi huo utashindikana kutohana na gharama za ujenzi zinazopanda? Ni kwa nini Serikali isijitose kufanya ujenzi kwa sasa kuepuka athari ya upandaji huo wa gharama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile maaskari magereza wa Geraza la Kilimo la Mang'ola wanaishi maisha magumu, kukosa makazi ya hadhi ya askari, jambo linalowafanya askari wetu waishi maisha kama ya wafungwa wao pamoja na familia zao.

Je, ni lini Serikali itajenga makazi yenyé hadhi ya binadamu kwa vijana wetu hao pamoja na familia zao? Ni kwa nini Serikali isiweke mkakati maalum angalau mapato yanayotokana na shughuli za kilimo za gereza hilo lisitumike kwa mpango wa *Retention* kujenga nyumba za askari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha.

MHE. DR. GERTRUDE MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kazi na ya kuishi ya Polisi ni duni na yanahitaji kuboreshwa hasa kwenye maeneo ya pembezoni mwa nchi. Mfano mzuri ni Kituo cha Polisi Murutungulu, Ukerewe ambako Polisi wanatumia majengo ambayo ni magofu yaliyokuwa wa *Ginnery* ya Pamba iliyojengwa karne ya 20 (1920's) na sasa tuko karne ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani - Mheshimiwa Seif Khatibu wakati huo alitoa ahadi ya kujenga Kituo cha Polisi huko Mwitu ambacho kingehudumia Tarafa ya Urangala na visiwa visivyozungua 20. Ni sehemu hii ambayo wavuvi huathirika kwa uvamizi wa majambazi. Wananchi walitoa ekari sita kwa ajili hiyo. Hivi sasa kituo hicho kiko kwenye nyumba ya mtu binafsi. Ninaomba nihakikishiwe ni lini kituo hicho kitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujambazi Ziwani ni tatizo. Kama Polisi waliweza kushinda majambazi yaliyolenga mabenki, kwa nini majambazi yanayosumbua wavuvi yasikomeshwe? Tatizo ninini?

MHE. OMARI S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa raia na mali zao ni jambo muhimu na nyeti kwa uhai wa Taifa lolote.

Pia haki na wajibu wa raia ni muhimu kwa maendeleo ya raia na Taifa. Kwa misingi hii, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ili aendelee kutekeleza majukumu hayo muhimu. Nawatakia kila la heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea Geraza la Babati tarehe 11 Machi, 2008 kama *visiting Justice*. Nilipata malalamiko yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutopelekwa kwa mahabusu Mahakamani kwa tarehe wanazohitajika na mfano ultolewa kwa mahabusu wanaopelekwa Mahakama ya Mwanzo – Magugu. Mahabusu wengi walilalamika kuwa wamebambikiziwa kesi na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano ni mkubwa ndani ya Gereza la Babati kwani uwezo wa gereza ni watu 115 nami siku hiyo ya tarehe 11 Machi, 2008 nilikuta wafungwa na mahabusu 572, hali ambayo kwa vigezo vyovoyote inakiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa majengo ya gereza, mahitaji ya wafungwa na mahabusu kama ule matandiko, vyombo na kadhalika. Askari wa ngazi za

chini kulalamika kuwa posho za aidha zinacheleweshwa au kuna mchezo mchafu wa kutokuwapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo nilichukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, kumwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa barua ya tarehe 10 Aprili, 2008 ili Mahakama ichukue hatua za kuondoa tatizo la kupunguza msongamano kwa kusikiliza kesi za mauaji za mahabusu 90 ambao kesi zao upelelezi haujakamika, wakati huo mahabusu 36 waliofungwa *PI* lakini bado hawajawahidi kwenda Mahakamani. Mahabusu sita ambao tayari walifungwa *PI* na wana kesi za kujibu na walikwishapelekwa kwa Jaji kujibu kesi zao, lakini hadi nilipofanya ziara hawajapelekwa tena kwa Jaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kama sasa hatua zimechukuliwa ili nitakapofanya ziara tena mara baada ya Bunge hili niweze kujibu kero hiyo ya msongamano na matatizo niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakala ya barua yangu na orodha ya wahusika wote nilimpelekea Mheshimiwa Waziri, *IGP*, Jaji Mkuu, Waziri Mkuu na wahusika wengine.

Nitapenda kujua jinsi Wizara itakavyofanya ukarabati wa Gereza la Babati ambapo pia natazamia kupata majibu kuitia swali linalosubiri majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Gallapo - Babati wanasubiri ahadi ya *IGP* kuhusu Kituo cha Polisi Gallapo. Naomba ahadi itekelezwe.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wengine wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukumbusha mambo kadhaa ambayo Wizara huko nyuma iliahidi kuyatekeleza Iramba Mashariki, lakini mpaka leo hayajatekelezwa. Kwa kuwa kijiografia Iramba Mashariki imejitenga na milima inafanya ugumu sana kwa usafiri. Serikali iliahidi kutoa gari ambalo lingekuwa linakaa kituo cha Polisi Nduguti kusaidia panapotokea matukio makubwa kama ya wizi wa mifugo ambao mpaka sasa bado unaendelea.

Pia lingesaidia sana matukio ya ujambazi na kadhalika. Ilitolewa ahadi ya kuimarisha Vituo vya Polisi Nduguti na Ibaga kwa kujenga vituo vipyta na pia kutoa silaha kwa askari wa Ibaga ambao mpaka sasa wanaendesha kituo hicho bila kuwa na silaha. Pia ahadi ilitolewa kupeleka *radio calls* za kisasa kubadilisha zile za kizamani hivyo kurahisisha mawasiliano. Pia ahadi ilitolewa kuwapatia vitendea kazi vingine zikiwepo sare. Napenda tu nifahamishiwe kama ahadi hizo zitatekelezwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa ng'ombe uliotoka eneo la Sepuka na Mheshimiwa Waziri aliahidi ndani ya Bunge hivi karibuni, bado linawasumbua sana

wananchi wa Singida. Ng'ombe hao walikamatwa na Askari Polisi wa Sepuka wao wakakabidhi kwa *OCD* wa Singida.

Polisi wawili waliohusika kuwapeleka ng'ombe hao Makao Makuu ya Polisi Wilaya walifukuzwa kazi na kuchukuliwa hatua kwa kisingizio cha kwamba walihuksika na upotevu wa hao ng'ombe. Wananchi wanauliza kila siku, Mkuu wa Polisi Wilaya kwa nini hakuchukuliwa hatua kwa kuwa ye ye ndiye aliyekabidhiwa hao ng'ombe? Badala ya kuchukuliwa hatua alihamishwa haraka haraka na kupewa cheo. Ningependa kuuliza, hivi kweli Polisi Mkoa na Makao Makuu walifanya uchunguzi wa kina juu ya tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iramba Mashariki kuna Gereza la Singa ambalo huko nyumba lilikuwa linajihuisha sana na kilimo, lakini sasa hivi kilimo kimesimama kabisa kwa ukosefu wa vitendea kazi kama *tractor*. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atumie busara zake gereza hili lipatiwe *tractor* na zana nyingine za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuwahamisha Askari wa Usalama Barabarani ambao wanakaa kwenye vituo vyao kwa muda mrefu na utaratibu wa kuwabasilisha vituo vyao kazi uwe endelevu. Hii itapunguza sana malalamiko kwamba askari hao wamebobea kwenye kupokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. LUCY FIDELIS OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Jeshi la Polisi. Napenda kuchukua nafasi hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Mkoa wa Kilimanjaro hata katika ulinzi na (*petroli*) wakati wote ukizingatia kipindi hiki kuna wageni wengi sana (watalii) pamoja na kutokuwa na vitendea kazi vyao kutosha lakini wanafanya kazi nzuri.

Vitendea kazi pamoja na makazi ya Polisi, Wizara hii inahitaji bajeti kubwa zaidi ya waliopewa. Kwa mfano hata Pingu za kufungia wafungwa hazitoshi? Nyumba za Polisi hasa mjini Moshi zinatisha. Nyumba zile zilijengwa enzi za mkoloni na ni za zamani sana. Polisi hawa ni binadamu, jamani wanazo familia zao vijumba vile ni kama *store* ya kuhifadhi vitu, ichukuliwe kama jambo la dharura kuwajengea Polisi hawa nyumba nzuri za kuishi ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na hili linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Jeshi la Polisi huwa linafanya kazi katika kulinda mabenki. Je, Wizara huwa wanalipwa kiasi gani kwa kazi hii? Basi pesa hizi zitumike kwa ajili ya kuwajengea nyumba za Polisi hawa. Je, mapato haya yanaonekana wapi katika mapato ya bajeti au kufungu kipi?

Mheshimiwa Mwenyekitii, mauaji ya kikatili ya kuchomwa moto Ndugu Peter Swai, ambaye aliuawa kwa kuchomwa moto na mfanyabiashara wa Moshi Mjini ajulikanaye kwa jina la J.J. na anaitwa Jaffa Abubakar na Haruna Yusuph walimwagia matufa ya taa kwa kumsingizia aliiba Sh.150,000/= zilizoibowiwa ndani ya hoteli, Moshi pale kwa hatia lakini baada ya kuchomwa moto Marehemu, walikwenda kupekua ndani ya hoteli ile na kukuta fedha zile ndani ya mto. Aliyeibiwa alikuwa ametoka kwenye harusi na ulevi wake akaficha fedha zile kule na kusahau alipoziweka na kwa kuwa

walijuana na wakubwa wakati huo J.J. alichukua sheria mkononi na kumchoma kijana Swai.

Harusi ya dada yake Jafair Abubakar (J.J.) ilihudhuriwa na wakubwa wakati huo *IGP* (Mahita, *RPC* Kilimanjaro (Chico) huyu kuna hisia, haki isingetendeka kwa kesi ya Marehemu. Aliyekuwepo, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai wakati ule Adad Rajabu baada ya watuhumiwa kukimbilia kusikujulikana, aliagiza atafutwe. Je, hakuna tangazo lolote lenye picha za watuhumiwa zinazosema wanatafutwa? Yawezekana kabisa labda wapo ndani ya nchi, lakini bila picha zao watu watajuaje wanatafutwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwa kitendo cha Jeshi la Polisi kutuletea mpango wa Polisi. Jamii (kushirikisha jamii katika ulinzi), lakini mpango huo ulikuwepo wakati Mheshimiwa Augustine Mrema alivyoanzisha na kujenga vituo vyta Mrema. Swali mpaka sasa ni kwamba, ni vituo vingapi hadi sasa vinafanya kazi au vinaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Kuna tetesi hata vituo alivyofungua majina yanafutwa. Je, ni kweli au ni maneno ya Mitaani tu? Kuna kituo kilichopo barabara ya *Rose Garden* pale *TPDC flat Mikocheni* leo hii Kituo kile cha Polisi kinatumika na *private security company* (walinzi binafsi) na bado kituo kile kimeandikwa Kito cha Polisi kuna haki hata majambazi kutumia kituo kile. Nashauri kwamba Wizara ifufue kituo kile ukizingatia katika eneo lote lile hakuna kituo chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Jeshi la Polisi likiteketeza mashamba ya bangi kwa kuyachoma moto. Je, hii ndiyo njia sahihi ya kuteketeza bangi hiyo kwa kuchoma? Je, kuna utafiti umefanyika? Kuna madhara gani kwa Polisi wanaovuta moshi ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza yetu yapo kwenye hali isiyoridhisha na haya pia yalijengwa wakati wa mkoloni ni madogo, machafu hata tunasikia kule Lindi wanapewa vyakula vibovu. Ni wakati muafaka kuwa na mkakati wa kuyapanua Magereza haya na kuyajenga ili kukidhi watu wote. Kwa kweli kwa sasa hivi hayakidhi matumizi ya binadamu.

Mwisho kabisa, (*Traffic Lights Dar es Salaam*) kama tujuavyo Dar es Salaam kioo cha nchi yetu, lakini inatia huruma jinsi *Police Traffic* (wakati wa mvua, juu kali) unamkuta amesimama anaongoza magari kwenye taa za barabarani. Polisi hawa ni binadamu. Ni kwa nini Wizara hii haina miundombinu wasiwasiliane na (*Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* ili wa-up-grade taa zile ziendane na ongezeko la magari? Ni lini mara ya mwisho taa hizo zilikuwa up-graded? Labda Polisi hawa watumike tu wakati umeme umekatika, lakini zinaweza kutumika taa zenye kutumia *solar* (juu).

Mwisho, Jeshi la Polisi bado lina mfumo dume, ongezeni wanawake kwenye uongozi na mishahara iboreshwe, wale wote mfano waliopigana na majambazi benki wapandishwe vyeo kama motisha.

MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Inspekte Jenerali wa Polisi, Makamanda wote wakiwemo Makamanda wa Polisi Mikoa na Wilaya na Kamishna Mkuu wa Magereza, Maafisa Magereza Mikoa na Askari wote Polisi na Magereza kwa kazi nzuri wanayofanya ya kupambana na uhalifu hapa nchini pamoja na kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti, vitendea kazi havitoshi kwa mfano magari, kwenye vituo vya Polisi. Kikiwemo Kituo cha Polisi cha Kibakwe na Chipogoro Wilayani Mpwapwa na gari la Gereza la Mpwapwa ni bovu, gereza halina usafiri muda mrefu, vifaa vya kisasa vya mawasiliano. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha matatizo hayo yanatatuliwa pamoja na ufinyu wa bajeti?

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya skari na kuwajengea nyumba za kuishi ikiwa ni pamoja na kukarabati nyumba zilizopo za askari zikiwemo nyumba za askari wa Mpwapwa ambazo zimechakaa na hazijafanyiwa ukarabati miaka mingi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Gereza la Mpwapwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa nyumba za Askari Magereza zilizojengwa miaka miwili iliyopita na hazijakamilka hadi leo? Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati gari la Gereza la Mpwapwa ambalo limeharibika muda mrefu na gereza hilo sasa halina usafiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana *IGP* Saidi Mwema kwa kupeleka askari wengi *CCP* na Chuo cha Polisi Kurasini ili kuwaendeleza kitaaluma na baadaye kuwapandisha vyeo.

Je, katika kipindi cha 2007/2008 ni askari wangapi wamepelekwa kozi na kupandishwa vyeo? Je, maslahi yao yameboreshwa?

Je, ni sababu gani za msingi zinazofanya wahamiaji haramu kuingia katika nchi yetu na kwa kuwa mipaka yetu yote ya nchi ina ulinzi wa kutosha? Je, wahamiaji haramu na hasa Wasomali na kadhalika wanapitaje katika mipaka yetu? Je, hawahatarishi amani na utulivu wa nchi yetu kwa kuingiza silaha nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivi sasa kuna ongezeko kubwa la ajali hapa nchini na ajali hizo zinasababishwa na madereva wazembe, hawana leseni, magari mabovu, kuendesha gari wakiwa wamelewa: Je, serikali imeweka mikakati gani ya kudhibiti hali hiyo? Je, katika kipindi cha 2007/2008 ni ajali ngapi zimetokea na watu wangapi wamepoteza maisha na mali kiasi gani zimeharibika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na wale wote ambao wameipongeza Wizara hii kwa kazi njema, lakini kwa juhudzi za Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na pia *IGP* na Watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kifupi tu, tumeona namna Jeshi la Polisi ilivyobadilika na kuwa jeshi rafiki kwa wananchi na kuonekana kama jeshi la watu badala ya kuwa chombo cha dola cha kusimamia na kutekeleza matumizi ya nguvu dhidi ya wananchi, kwa mabadiliko haya wananchi wamekuwa tayari kuisaidia Polisi katika mpango wake wa Ulinzi shirikishi. Natoa pongozi kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni za Jeshi la Polisi ni za muda mrefu na nyingine zinahitaji kupitiwa upya hasa katika maeneo ya mishahara, posho na mafao ya askari. Nadhani pia inawezekana hata kwa Jeshi la Magereza. Mfumo wa kufikia kikomo katika mshahara inawavunmo moyo na ari ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kusoma na kupandishwa vyeo kwa askari uwe wazi na unaoelewaka kupunguza malalamiko na hatua za makusudi za kuwasaidia wale ambao walijiunga na jeshi katika mfumo ambao wakati uele vyeo vilitolewa kwa utendaji kazi, uaminifu na ujasiri wa askari na siyo elimu pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wa Polisi wa Idara ya Upelelezi kwa muda mrefu wamekuwa wakilipwa *Outfit allowance* ya Sh. 50,000/= kwa karibu sasa miaka 20 bila ya kuona hali ya maisha ilivyobadilika kwa muda wote huu, kiasi hicho hakitoshelezi hata kununua kaunda suti ya mtumba. Pamoja na hilo, lakini lipo tatizo katika Idara hii inahitajika hatua za haraka na makundi ya askari wa idara hii kupewa mafunzo ya mara kwa mara ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi hasa wakati huu mbinu mpya za uhalifu zinabuniwa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mashaka na uwezo wa Idara hii kwa namna kesi nyingi ambazo zinafukuzwa Mahakamani kwa Polisi kushindwa kukamilisha upelelezi au ushahidi dhaifu unaotoa fursa ya washtakiwa kuachiwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa wazi ni ile kesi ya fedha za Polisi kituo cha Polisi msimbazi, fedha zimepokelewa kituoni, zimehifadhiwa kituoni, zimeibiwa kituoni, lakini Polisi wameshindwa kukamilisha upelelezi hatimaye watuhumiwa kuachiwa huru. Huu ni udhaifu wa wazi namna Polisi wanavyofanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya askari wetu wa Jeshi la Polisi na Magereza ni aibu. Aibu na hayafai labda kama tunayaacha kama kumbukumbu namna wakoloni walivyowaweka askari nasi kwa miaka 46 bado askari anaishi katika nyumba ya chumba kimoja na sebule na wengine katika makambi ya mabati ya msonge kama vile Dodoma, Tabora na mingi mingine kwa miaka 46 tunashindwa kuboresha makazi ya askari wetu. Aidha, hata fedha wanazolipwa kama *house allowance* kwa wale ambao hawapo kambini ni ndogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya askari ya mafao au masufuru yao hadi sasa hayalipwi kwa wakati na ni kero na usumbufu kwa wahusika hata madai ya Wazabuni kwa Jeshi la Magereza yawe yanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Magereza yetu na idadi ya wafungwa au mahabusu havina uwiano wala hakuna mpango wa kupanua magereza hata mazingira ya

gerezaji lenyewe inatisha sana hayafanyiwi matengenezo ya mara kwa mara kwa kuwatumia wafungwa hao hao na pato kutokana na kazi zao za magereza, wanaweza sana kama kutakuwa na mpango shirikishi wa kutengeneza magereza na kuyaongeza. Kwa sababu hata chakula katika yale magereza ya kilimo yakipewa vitendea kazi ili yaweze kuzalisha kwa matumizi yao na ziada kwa ajili ya kuuza na kuboresha makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama barabarani na ajali. Ni matumaini yangu kama askari wa *Traffic* wataongeza juhudini katika kusimamia kazi zao vyema. Inawezekana sana kupunguza ajali za barabarani. Ajali nyingine ni kwa sababu hatuna alama za barabarani ni vyema sasa yakawepo mshirikiano ya karibu kati ya Wizara ya Miundombinu na Idara ya *Traffic* alama zipo wazi, hasizomeki, zimebekwa karibu sana na amri au ishara mfano ni alama za *lumps* na *bumps* katika barabara kuu hata ukubwa na muundo wa hayo matuta, rangi zinazotakiwa kuwepo na zenye kufanana nchini ili maana ya kuwepo kwa hayo matuta ilete mafanikio. Aidha, matuta haya yawe salama yasiletie athari kwa magari kwa maana gharama za kutunza hayo magari ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa mikanda katika magari ni lazima sasa elimu itolewe na siyo elimu tu, tuhakikishe kila anayetumia gari anawajibika kufunga mkanda wa kiti (*safely belt*) dereva pia abiria na kila askari wa *Traffic* atakapoona sheria hii haijatekelezwa anatoza faini ya papo kwa papo na kutoa stakabadhi, anza tu na adhabu ya Sh. 5,000/= kila anapoonekana hajafunga mkanda akilipa mara mbili/tatu atafunga mkanda. Utamaduni huu upo duniani kote ila Tanzania Bara tu. Inashangaza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu sasa kusimamia na kujenga tabia ya kutumia mikanda. Inawezekana kama tukiamua tukisimamia vyema hata wageni wanatushangaa kuona hatujui hata maana ya hiyo mikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuwa muhtasari tu, kuhusu suala la wakimbizi katika makazi hususan yaliyopo Mpanda pamoja na zoezi linaloendelea ila kuwarudisha makwao kwa hiari wala sina tatizo hata kidogo pamoja na kwamba tumekuwa nao kwa zaidi ya miaka 40, tulipowapokea wakimbizi wa Rwanda katika miaka ya mwanzo ya 1960.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo ni idadi ya wakimbizi watakaorejea ni wachache sana kuliko wale ambao wanataka kuendelea kuishi Tanzania na kupewa uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uraia ni wa nchi, ni kwa mujibu wa sheria zipo taratibu na kanuni za kuwezesha mtu kupata uraia wa nchi yetu. Masikitiko yangu ni pale tunapoamua kuzingatia sheria zetu. Sheria inamtaka mtu anayetaka uraia wa nchi hii kupeleka maombi kwa Mheshimiwa Waziri kujaza fomu zinazohusika, kuwepo wadhamini wanaofahamu, kujitangaza katika magazeti kama litakuwepo pingamizi na kulipa ada kwa viwango kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakimbizi hawa maombi yao hayazingatii matakwa haya ya sheria, wote wanajaza fomu kituoni. Wadhamini ni wale wale kwa maombi yote,

hawajitangazi ili kama kuna mtu anazo sababu au mashaka ya mtu huyo kupewa uraia, kibaya zaidi, ada inalipwa na *UN* (sawa kwa sababu lazima walipe).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nionavyo mimi, tunauza uraia kwa sababu ya umasikini wetu, tupate fedha. Hawa wanaonunuliwa uraia, watathmini vipi uraia huo wakati wanaupewa tu? Wangepaswa kulipa wenyewe tungeweza kugundua wale wenye dhamira ya kweli ya kuwa Watanzania. Uraia wa nchi hii una thamani siyo wa kuza kirahisi kiasi hicho kwa sababu *UN* wanalipa na wanatupa fadhila na misaada mingine, lakini mambo haya naomba sana yawe yamezingatiwa kwa sababu hatuvezi kurudi nyuma na zoezi linaendelea.

Athari za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiusalama kama wakimbizi hawa kwa maelfu kesho watakuwa Watanzania na haki sawa na raia mwingine pia uwiano kati ya idadi ya wakimbizi na wakazi wa Mpanda, nini athari zake, mipango ya baadaye baada ya kupewa uraia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili linasimamiwa na maafisa Watanzania na washiriki wakuu ni watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana Polisi na Uhamiaji, lakini inasikitisha watumishi wa Wizara moja wanafanya kazi (*operation*) kwa pamoja lakini malipo yao hayafanani. Polisi wanalipwa kiasi kidogo sana na hii imeleta manung'uniko kwa washiriki wa zoezi hili. Naomba maelezo, kwanini malipo yao yametofautiana tena kwa kiasi kikubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataraji kupata ufanuzi kwa mchango wangu. Nashukuru sana.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri zinazofanywa sasa na Majeshi yetu ya Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwapongeza polisi wa Wilaya ya Muheza kwa jitihada kubwa wanazofanya na kufanikiwa kupambana na majambazi na wahalifu wengine waliojitekeza kwa kasi kati ya mwaka 2007 na 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri, mapendekezo na maombi yafuatayo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza nilimwalika Waziri wa Mambo ya Ndani kutembelea Muheza mwaka 2003/2004 na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati huo alifika Muheza. Napenda kuishukuru Wizara kwa kukubali na kutekeleza ujenzi wa Kituo Kipywa cha Polisi Wilaya ya Muheza na jinsi Wizara yenye ilivyojitelea kugharamia kufikisha umeme na maji kituoni hapo baada ya *TANESCO* na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kushindwa kutekeleza. Pamoja na shukrani hizo sasa niendelee kutoa maoni na ushauri.

Pili, ujenzi wa nyumba za polisi, kama nilivyojeza mwaka 2004/2005 na 2006/2007, kituo cha zamani cha polisi Wilaya ya Muheza na nyumba za polisi zipo

katika eneo la Shirika la Reli na kihistoria ni mali ya Shirika la Reli. Kwa msingi huo naishauri Wizara ya Mambo ya Ndani kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba za polisi, Muheza.

Tatu, kuimarisha Kituo cha Polisi cha Amani Muheza kipo wastani wa kilometra 35 kutoka Muheza Mjini. Kituo bado hakina gari na nyumba zilizopo zinahitaji ukarabati. Amani ni eneo kabla, Tarafa yenyé Kata tatu za Kisiwani, Misalai na Zirai. Amani ina mashamba makubwa matatu ya chai, hakuna benki na hivyo fedha husafirishwa umbali wote huo bila ulinzi, Amani ni eneo la utalii na idadi ya watalii kwenda katika hifadhi ya Misitu ya Amani imeongezeka. Amani ni eneo la uvunaji wa madini ni miti ya biashara, Amani ni eneo la vyanzo vikuu vya maji mto Ziggi na chanzo cha Derema. Kwa hali hii Kituo cha Polisi Amani kinahitaji kuimarishwa kutokana na uhalifu wa ujambazi imelazimika mabasi ya abiria kutoka Muheza kwenda Amani kusindikizwa na polisi yote hayo yanaonyesha umuhimu wa kuimarisha kituo hicho na kukipatia gari.

Nne, kuongeza kituo cha polisi Wilaya mpya ya Muheza. Awali Wilaya ya Muheza ilikuwa pamoja na Jimbo la Mkinga ambalo sasa ni Wilaya. Mgawanyiko huo unafanya Wilaya mpya ya Muheza kuwa na vituo viwili tu vya polisi ambavyo ni Muheza Mjini na Amani kutokana na ukubwa wa eneo la Wilaya ipo haja ya kuongeza kituo kimoja zaidi cha polisi. Mapendekezo ni kujenga kituo katika kata ya Kwafungo. Kituo kitakuwa katikati ili kuhudumia kata jirani za Songa, Potwe na Mtindiro. Kata hizo zina watu wengi na biashara nyingi pamoja na kuongeza kwa uzalishaji wa machungwa. Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi ifikirie ujenzi wa Kituo hapo ili kuboresha ulinzi wa wananchi.

Tano, ujenzi wa Gereza na nyumba za Maofisa wa Magereza Muheza. Mwaka 2004 Naibu Waziri wa Wizara hii alipotembelea Muheza aliona fedheha kubwa ya hali ya gereza na nyumba za maofisa wa Magereza Muheza. Nyumba za fito, tope na viezekeo vya makuti na mabati yaliyojaa kutu. Aliahidi kusaidia lakini hadi sasa hakuna lililofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 Julai, 2008, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Wilaya ya Muheza alielezwa hali mbaya ya Gereza na nyumba za Magereza kule Muheza. Mheshimiwa Rais aliahidi kusaidia kuangalia hali hiyo. Ni dhahiri sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi italazimika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza ahadi hii ya kuona umuhimu wa kuboresha hali ya Gereza, Nyumba za Polisi, Magereza na kupunguza gharama za usafirishaji wa mahabusu kila siku kutoka Gereza la Maweni Tanga hadi Muheza kwenda na kurudi. Gharama hizi ambazo zimekuwa zinatumika kwa zaidi ya miaka 50 sasa zingetosheleza ujenzi wa Gereza la kisasa na nyumba za maofisa wa Magereza Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tutaendelea kutumia fedha hizo hadi lini? Je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza gharama hizo? Pamoja na ushauri na maoni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 wananchi wa kijiji cha Mchinga kupitia nguvu zetu tulifanikiwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha polisi kijijini hapo. Kituo hiki kimejengwa kwa kuzingatia mchoro uliyotolewa na Jeshi la Polisi.

Kwa bahati mbaya kituo hiki haijafunguliwa kutokana na kutokuwepo nyumba za askari. Kwa niaba ya wananchi wa Mchinga ninaleta ombi la kupatiwa vifaa vyta ujenzi na wananchi tutajenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuwepo kwa kituo hiki Mchinga kwa sababu kijiji hiki ni kikubwa na kina wakazi wengi. Kijiji hiki kina shule za msingi mbili, kituo cha walimu, shule ya sekondari moja, mahakama ya mwanzo, zahanati na kituo cha uvuvi. Aidha, Mchinga ni Makao Makuu ya Jimbo, Tarafa na Kata. Mchinga pia ni kituo muhimu cha magari ya abiria wa barabara ya Mtwara – Lindi – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri amwombe *IGP* kutembelea Mchinga ili kwanza ajionee hali halisi na pili tuone namna bora ya kulitatu tatizo hili.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba kutanguliza shukrani.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, viongozi wote wa Wizara *IGP* na majeshi yote yaliyo chini ya Wizara hii kwa hotuba nzuri. Naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Nimefurahi sana kusoma kwamba Wizara imeanzisha Kikosi cha Ujenzi. Mimi siku zote nashauri Serikali Kuu na Halmashauri kutumia vyombo vyta Serikali kama SUMA JKT na Kikosi cha Magereza kutekeleza miradi mbalimbali kwa kuwa mimi nasimamia miradi ya maji na umwagiliaji, ni vyema tuangalie nini kifanyike ili kikosi cha ujenzi cha Magereza kihusike pia na ujenzi wa miradi ya umwagiliaji. Kwa mfano, ujenzi wa bwawa la kumwagilia la Mang'ola ungeweza ukafanywa kwa gharama ndogo kama kikosi chenu kingetumika. Lakini je, Kikosi cha ujenzi cha Magereza kinavyo vifaa vyta Ujenzi kwa mfano, *construction equipment* kama vile *bulldozers, mortorgrders, concrete mixers, compactors* na kadhalika? Mnahitaji kujenga uwezo huo.

Kituo cha Polisi cha Nyaronga – Kakonko katika Wilaya ya Kibondo, kituo hiki kina nyumba nyingi nzuri sana lakini kimechakaa na nyingi zimepata *cracks* kiasi kwamba zinahatarisha maisha ya askari na familia zao. Kwa kuwa kituo kiko mpakani na wakati mwingine kinatumika kuhudumia askari (kwa kuwapa nyumba) nashauri Wizara iangalie upya namna ya kutumia kituo hicho kwa ufanisi zaidi.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na hatimaye kuiwasilisha hotuba ya Bajeti kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza sana jeshi letu la polisi kwa utendaji wao uliotukuka wa kuitumikia nchi hii. Kuhusu ongezeko la wahalifu, kuna dhana ya ongezeko la wahalifu nchini kwa mwaka uliopita 2007/2008. Hii inaonyesha ama ni kweli wahalifu wamezidi au jeshi la polisi limejikita zaidi kuwasaka, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, basi tulipongeza jeshi letu. Aidha, tunaipongeza hatua ya kukipeleka kitengo cha mashtaka kwenda kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili kuharakisha usikilizwaji wa kesi mbalimbali. Tunaomba hatua hii iwe chachu ya kupunguza mrundikano wa kesi ili kesi zisikilizwe haraka na wananchi wapate nafasi kufanya shughuli nytingine za kimaisha.

Pia tunaipongeza hatua ya kuanzisha polisi jamii ili wananchi wasaidiane na polisi kuwatambua wahalifu. Katika mchakato huu kunahitajika usiri mkubwa ili kuwanusuru raia wema wanaotoa taarifa za wahalifu. Kuna tetesi kuwa wapo askari polisi wanaoshirikiana na wahalifu kwa tamaa ya fedha kwa kuwapa taarifa zinazowasaidia kufanikisha uhalifu wao katika mabenki na sekta mbalimbali za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza yanegera na mahali pa kuwapa mafunzo wahalifu ili wamalizapo adhabu zao magerezani wawe raia wema. Najua hivi sasa kuna miradi mingi ya kilimo na mifugo nchini, lakini miradi hiyo haipo kwa lengo la mafunzo bali ipo kwa lengo la mateso (adhabu). Tukiwafunza wahalifu fani mbalimbali kama kilimo cha kisasa na ufugaji wa kisasa, ufundu wa umeme, uashi, uchongaji na kadhalika, tutaweza kuongeza idadi ya Watanzania wenye elimu ya kujitegemea.

Aidha, Magereza yanapaswa kutumia hali ya upungufu wa chakula duniani na kuongezeka kwa bei ya chakula kwa kujikita kuzalisha chakula kwa wingi kwa kuuza ndani na nje jambo lisilokubalika kwa Serikali kutenga Bajeti kwa ajili ya chakula cha wafungwa wakati ardhi ya kulima ipo na uwezo wa kulima upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utendaji wa Idara ya Zimamoto hauridhishi hata kidogo. Hata kama vifaa vyao ni kidogo lakini hawafiki katika eneo la tukio kwa wakati. Wizara ijipange vizuri zaidi ili Zimamoto wachache waliopo wafanye kazi za kuokoa maisha na mali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji iondoe urasimu wa upatikanani wa *passprt* kwa kuwa hiyo ni haki ya kila Mtanzania. Pia iharakishe vitambulisho vya Mtanzania.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuwapongeza Wizara hii hasa kwa kuongoza mapambano dhidi ya majambazi. Kwa kuwa hivi karibuni imanzisha dhana ya polisi jamii na kwa kuwa maeneo ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Magharibi kuna ulinzi wa jadi (Sungusungu/Usalama) ambao kwa sasa

kwa kiasi fulani umezorota; nashauri kuanzia sasa polisi iwachukulie sungusungu kuwa ni wadau muhimu katika kusaidia ulinzi wa raia na mali zao hasa vijijini.

Kwa kuwa usafirishaji wa mizigo kwa sasa hufanywa na magari makubwa (malori) na utaratibu wa sasa kulazimika kuyapima mabasi kwenye mizani jambo ambalo ni usumbufu kwa wasafiri. Je, pangewekwa utaratibu wa kuwa mistari ya malori na maalum wa mabasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nzega ina vituo polisi vitatu ambavyo vipo katika Tarafa. Tatizo kubwa linaloathiri utendaji ni usafiri kuwa na gari moja tu. Naomba huruma yako walau nipate magari hasa katika Tarafa ya Puge ambayo ipo mbali na ni kubwa kijiografia.

Madeni ya wazabuni mbalimbali yalipwe haraka ili kutowapa adhabu wananchi hawa. Naomba pia ujenzi wa nyumba za watumishi (Polisi/Magereza/Uhamiaji) uende hadi ngazi ya Wilaya. Nawapongeza kwa kujenga katika ngazi za Miji Mikuu. Pelekeni huduma hiyo Wilayani. Nawatakia kazi njema.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kama ifuatavyo hasa baada ya kuisoma vizuri hotuba nzuri iliyosomwa vizuri sana na Waziri, Mheshimiwa Lawrence Kego Masha. Niruhusu niwashukuru na kuwapongeza uongozi mzima na Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya hasa la kusimamia usalama wa raia na mali za Watanzania chini ya *IGP*, Saidi Mwema na makandama wote mikoani. Kama nilivyoanza kusema naomba nishauri na kuomba kama ifuatavyo:-

Kwanza, vitendea kazi kama vile magari, yanayofanana na maeneo husika, pili, pikipiki, balskeli, *radio call*, kamera za kisasa pamoja na mafuta na tatu, sare za askari wote polisi, Magereza, *FFU*, Uhamiaji, viatu na soksi, kofia zenyenye ubora unaofanana na thamani ya pesa inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazabuni wanaoteuliwa huleta vifaa visivyokuwa na ubora hasa sare ambapo sare nzuri yenye ubora hupewa viongozi wa juu wale wa ngazi ya chini ili mradi wamewapa, hazina ubora unaofanana na pesa zilizotolewa, viatu askari hulazimika kucaa viatu vya mitumba kama inaruhusiwa sawa kama sivyo basi liangaliwe upya na hapo naomba nipate maelezo ya kina kuhusu uteuzi wa wazabuni Idara ya Polisi, vinginevyo wakati vifungu nitasimama kuhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wafungwa wengi hasa ikizingatiwa kuwa wengi wao ni wataalam, wenye fani zao ambazo endapo tungeamua tungeweza kuwatumia katika uzalishaji mali. Kitendo cha kuwafuga na kuwalisha Januari hadi Januari na kwa idadi inavyozidi kuongezeka hauleti tija. Naomba niiombe Wizara tuachane na dhana ya haki za binadamu. Wafungwa hao sasa watumie na kazi za ujenzi, kilimo ufundi na kadhalika. Tukifanya hivyo zile pesa ambazo zingetumia kuwalipa wakandarasi pesa hizo zitafanya kazi nyingine.

Katika Wilaya ya Kwimba, Ngudu hatuna jengo la polisi, linalotumika siyo lake na halina hadhi, naomba niiombe ofisi yako tutumie wafungwa kujenga ofisi lakini ofisi yako itupatie vifaa vingine vyote yaani mabati, mbao misumari na milango na mengine yatakayowezesha kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Wilaya ya Polisi ni aibu Wilaya iliyozaa Misungwi, Magu na Maswa haina ofisi ya polisi yenye hadhi.

Kwa niaba ya ofisi ya Wilaya, naomba tuhurusiwe kutumia wafungwa tulionao kwa kufanya kazi za uzalishaji mali hasa katika kufyatua mawe na mengine kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Wilaya.

Naomba kuuliza ni kwa nini makosa ya jinai yaliyori potiwa mwaka 2007 Mkoa wa Mwanza na Dar es Salaam unaongoza na Mkoa wa Pwani unaripotiwa kuwa na makosa madogo, je, ni sababu gani kinachosababisha Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza kuongoza katika makosa ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama katika Wilaya ya Kwimba ni nzuri lakini siyo vizuri sana kwani mauaji ya vikongwe, maalbino, uchomaji moto wa watuhumiwa kwa wanaotuhumiwa kudokoa au kuiba bado unaendelea. Naomba kuleta ombi ofisi hasa ya *IGP* Saidi Mwema kwa kunisaidia kuipatia usafiri wenyewe uhakika. Kwimba ni Wilaya kubwa, gari moja halitoshi, mafuta tunayopata hayatoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RPC* aliyehamia Mbeya nilimweleza kuhusu viongozi wa ngazi ya juu Wilayani kuhamasisha kuua watuhumiwa wanapokamatwa hali iliyopelekeea ongezeko la kuuwawa kwa watuhumiwa. Ofisi ya *IGP* iwe macho, masikio na mikono mirefu naomba hili litafutiwe ufumbuzi. *RPC, RCO* taarifa wanazo.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri Mheshimiwa Lawrence Masha na Naibu wake Mheshimiwa Khamis Kagasheki na Katibu Mkuu wa Wizara Mheshimiwa Muhammed Muya kwa maandalizi mazuri ya Bajeti.

Nawapongeza Mheshimiwa Saidi Mwena, *IGP* na Makamanda wake pamoja na *RPC* Mkoa wa Singida kwa kazi nzuri. Naomba waongeze jitihada zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16 Julai, 2008 niliuliza swali kuhusu wizi wa ng'ombe 25 za Mzee Mahola ambazo zilikamatwa katika Kijiji cha Mnangana, Kata ya Sepuka, Wilaya Singida Vijijini na katika majibu yake Waziri Mheshimiwa Masha, aliahidi kuwa ng'ombe hao 25 watarejeshwa kwa Mzee Mahola na kwamba atakwenda Singida kutekeleza ahadi hiyo. Nasubiri kujua siku tutakayokwenda Singida na Mheshimiwa Waziri kufanya kazi hiyo.

Katika majibu yake alieleza kuwa askari wawili Ndugu Julius na Ndugu Tungaraza walifukuzwa kazi na kupelekwa mahakani. Askari hawa walikabidhi ng'ombe 25 na wezi kwa *OC CID* wa Wilaya ya Singida ng'ombe wamepotelea mikononi mwa *OC CID* baada ya kukabidhwu vipi askari wafukuzwe kazi na *OC CID* wachiwe na kupewa cheo. Huu ni uonevu kwa askari hao. Mahakama iliwaachia huru askari hawa kwa kuwa hawana hatia/kosa. Kwa hiyo, katika utawala unaojali sheria, askari hawa ni

vema wakarudishwa kazini na *OC CID* achukuliwe hatua vinginevyo sitaunga mkono hoja na kisha itabidi nilete hoja binafsi kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utaratibu wa ulinzi shirikishi na polisi jamii hautaeleweka vizuri kwa wananchi. Nashauri elimu itolewe hadi vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Dar es Salaam wageni haramu wapo wengi sana. Ipo hoteli moja Kariakoo wageni hao wapo wengi. Naomba wafuatiliwe.

Kuhusu huduma za Zimamoto ziimarishwe mijini hasa Singida na Dar es Salaam.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane nawe katika kutoa salaam za rambirambi kwa msiba wa Mbunge mwenzetu Chacha Wangwe. Sote tuliguswa sana na tukio hilo. Tuzidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aipokee roho yake Marehemu Chacha Wangwe.

Pili, naomba nimponeze Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Mkuu wa Jeshi la Polisi, *IGP* akiwemo Mkuu wa Magereza na askari wote kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi chote hiki cha 2007/2008. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo kwangu mimi yamekuwa ni kero na kunifanya nichangie hoja hii kwa kusema kwa kuwa ninaonekana kupoteza muda wangu bure na kunakowezekana nikaonekana mtovu wa nidhamu ndani ya Bunge lako Tukufu. Mambo yenye ambayo yananikera ni pamoja na kilio changu cha zaidi ya miaka 15 Bungeni, bila mafanikio.

Kwanza ni kuhusu ujenzi wa ofisi ya polisi Wilaya ya Sumbawanga. Leo hii Sumbawanga ni Manispaa yenye Wilaya yenye Wabunge watatu. Unawezaje kuendelea na ofisi ndogo ya tangu ukoloni? Nini mpango wa Wizara kwa hili?

Pili, ujenzi wa mahabusu mjini Sumbawanga na ukarabati wa nyumba za askari katika Mkoa wa Rukwa. Kuonekana hakuna mpango wowote ulio wazi juu ya hatma ya jambo hili maana kazi yake ni ndogo sana. Kusua sua kwa hili nini tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ombi la kuongezewa wafungwa kwenye gereza la Mollo ni wanaofungwa Magereza mengine yasiyo na shughuli za kiuchumi wahamie kwenye maeneo ya uzalishaji kama Gereza la Mollo Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara hii kwa kutupatia zana za kilimo katika Gereza la kilimo la Mollo. Hatua hii imesaidia sana kwa Gereza hili kuongeza uzalishaji wa chakula na kuwapa molari watumishi wa gereza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto, sehemu nyingine linatia aibu, aibu yenye inatokana na tabia ya kuchelewa kufika kwenye tukio na baya zaidi wanafika kwenye tukio, kunakuwa hakuna maji kwenye magari yanayoletwa. Suala hili lifuatiliwe kwa karibu na kutoa mafunzo ya uhakika kwa watumishi wa jeshi hili. Tusikubali

magari ya zimamoto ya makampuni binafsi yaonekane ni bora kuliko ya taasisi za umma,
why?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshi la polisi lishirikiane na polisi (*traffic*) na *TRA* ili kubaini leseni feki za magari. Hapa jijini Dar es Salaam kuna utaalami wa kuchapisha leseni feki; *insurance* feki; *road licence* feki na kukosesha mapato ya Serikali. Namtaka Waziri alione hili ili kukomesha vitendo hivi viovu ambayo ndani ya *Bongoland* lazima tushinde maovu ya aina yoyote ya kukwepa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa magari umeshamiri na hasa baada ya kuwa na *show rooms* nyingi za magari mitumba toka Dubai au Japan naona Dubai imehamia hapa Dar es Salaam. Ni vizuri tuendelee kuzichunguza vizuri *show rooms* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mheshimiwa Waziri atusaidie kutupatia ufanuzi wa kina kuhusu vitambulisho vyta Kitaifa hasa kwa kuzingatia kuwa kazi iliyo mbele ni kubwa sana. Ni kwa msingi huo ndiyo maana nashauri kuwe na utekelezaji kwa awamu kwa awamu. Awamu ya kwanza tuanze na mikoa ya mipakani hasa Kagera, Mara, Rukwa, Ruvuma na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kulipongeza Jeshi la Polisi likiongozwa na *IGP* Saidi Mwema kwa kazi nzuri wanayoifanyia nchi hii. Tuzidi kuwaomba waendelee kushirikisha jamii kama Kamanda wa Kanda Maalum ya Dare es Salaam Kamanda Kova, anavyojitahidi kuwahuisha wananchi katika kazi hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. NURU A. BAFADHIL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Chacha Zakayo Wangwe, aliyejewa Mbunge wa Tarime kwa tiketi ya Chama cha Chadema kilichotokea juzi tarehe 28 Julai, 2008. Tukumbuke kuwa; “Bwana ametoa na Bwana ametwa, jina la Mungu libarikiwe.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli polisi wanajitahidi kufanya ulinzi wa raia lakini tatizo ni uhaba wa polisi na uhaba wa vitendea kazi.

Miaka ya 1980 Serikali ilihamasisha kujenga vituo mbalimbali katika Kata, vituo hivi vilisaidia sana uimarishaji wa ulinzi. Kidogo uhalifu ulipungua. Baada ya hapo majengo hayo sasa hivi yamekuwa ni nyumba za kulala vibaka na wahalifu wengine. Naiomba Serikali iandae utaratibu wa kuvifungua vituo hivyo na viweze kufanya kazi. Vituo hivi vingi vilijengwa ili kuhamasisha wananchi kupeleka malalamiko yao katika kituo cha polisi cha Wilaya, badala yake watumie vituo vyao vya kata ili kupunguza msongamano katika vituo vya Wilaya. Katika Jiji la Tanga wananchi walijitahidi kujenga vituo hivyo lakini sasa vimebaki tu ni makazi ya wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutokana na kuanzishwa kwa polisi jamii, wananchi wahamasishwe umuhimu wa polisi jamii na jinsi gani linasaidia Serikali kupunguza uhalifu katika makazi ya raia.

Kuhusu huduma za uhamiaji, Mikoa wa Tanga kwa upande wake wa Kaskazini unapakana na nchi jirani ya Kenya. Kuna wimbi la wageni wanaoingia kuititia njia za panya na kuingia nchini mwetu. Wageni hawa baada ya muda wanajifanya ni raia wa Tanzania. Hii yote inasababishwa na ukosefu wa vitambulisho kwa wananchi wetu.

Naiomba Serikali itueleze ni lini Watanzania wataanza kupata vitambulisho ili kuzuia waingiaji haramu nchini kwetu. Tukichukuliwa mfano wa wenzetu jirani, nchi ya Kenya unapotembea barabarani polisi anaweza kukusimamisha akakuuliza kitambulisho na kama sio raia wa Kenya utaonyesha hati yako ya kusafiria. Hii inapunguza wimbi la uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Tanga polisi wetu wana matatizo ya nyumba za makazi. Nyumba za Chumbageni, Mabawa na Msambweni ni nyumba zilizojengwa toka miaka ya 1940. Nyumba hizi zimechoka hazifai kabisa, mashimo ya choo yamejaa, mabovu ni hatari kwa usalama zaidi watoto wadogo ambao huchenza katika mashimo hayo ya maji taka yanayo julikana kwa jina la kejeli *SACCOS*. Je, Serikali haioni pia hata kama nyumba hazijajengwa lakini kambi hizo zenyenye nyumba za kuishi polisi ziingizwe kwenye mfumo wa maji taka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa maeneo, je, Serikali haioni huu ni wakati muafaka kujenga nyumba za ghorofa maeneo yale yale yenye nyumba hizo za kizamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia jeshi la polisi lina mafundi katika fani mbalimbali, je, haiwezekani kuwatumia mafundi waashi kujenga nyumba hizo? Serikali itafute vifaa tu, mafundi watakuwa wale wafungwa ambao ni mafundi waashi ili kupunguza gharama za fedha za kulipa mafundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati za kusafiriria, kuna usumbufu mkubwa sana katika ufuatiliaji wa hati za kusafiria, je, Mtanzania hana haki ya kuwa au kumiliki hati ya kusafiria mpaka awe na safari. Mfano safari ya Hijja au anaenda kwa ajili ya matibabu. Rushwa kubwa imetawala katika eneo hili la upatikanaji wa hati za kusafiria. Serikali iliangalie sana tatizo hili.

Kuhusu ajali za barabarani zimekuwa ni tishio sana kwa wasafiri. Ajali nyingine chanzo ni sisi wenye tunaosafiri katika mabasi. Abiria akielezwa kuwa basi halina nafasi anadai yeye atasimama. Matokeo yake kuna mabasi ambao yanaweza kubeba watu zaidi ya waliokusudiwa. Maoni au ushauri wangu, basi litakalokutwa limesimamisha abiria, basi kondakta na abiria waliosimama bila kupata nafasi kitini wote wawe na hatia. Kama ni kulipishwa faini walipe wote. Hili litasaidia abiria kutokubaliana na kusafiri ikiwa amesimama kwa vile ataona uchungu naye atatoa pesa za uvunjaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii atatoa usafanuzi kuhusu hatua nzuri na za haraka kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa vitambulisho vya uraia ili kudhibiti waingiliaji haramu katika sehemu za mipaka yetu ambao pia ni chanzo cha wimbi la ujambazi.

Mwisho, nalipongeza jeshi la polisi kwa kujituma na kulilinda Taifa letu kwa uadilifu.

MHE. ATHUMANI S. JANGUO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri Balozi Khamis Kagasheki, Katibu Mkuu, na wasaidizi wa Wizarani. Katika Majeshi ya Polisi, Magereza na Uhamiaji kwa jinsi wanavyochunga usalama wetu na mali zetu. Nawapongeza pia kwa hotuba nzuri.

Nianze na Jeshi la Polisi ambalo lina kazi kubwa sana ya kulinda usalama. Tunathamini sana jinsi jeshi linavyopambana na majangili wakati mwingine kuhatarisha maisha yao. Lakini ipo kasoro moja pale baadhi yao wanaposhirikiana na majambazi na wakati mwingine wao wenyewe kufanya ujambazi, wakaua watu wasio na hatia kwa kisingizio kuwa wameua majambazi. Nashauri Wizara iwe imara kuwadhibiti askari kama hao. Inapotokea askari amepatikana na hatia, hapana budi wapewe adhabu kali zikiwemo kufukuzwa kazi, kufunguliwa na hata kifo kutegemea na makosa yenyewe.

Suala la huduma za Magereza, ni kweli kuwa jukumu la Magereza lina sura mbili au tatu, kwanza ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu, kutoa adhabu kwa wahalifu na kurekebisha tabia za waovu ili wawe raia wema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majukumu haya mimi naamini kuwa Taifa, litafaidika sana kama Magereza yatatilia mkazo urekebishihi wa tabia kuliko mengine yote kwani hatimaye tabia za watu wetu wote zikiwa nzuri, tutapunguza uhalifu na Magereza hayatahitajika yawe mengi kiasi kuwa hata uwezo wa kuhifadhi wafungwa 22,660 tulionao utakuwa mkubwa zaidi kuliko mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naipongeza Serikali kwa progamu za urekebishihi zinazoleenza katika Ibara ya 32 hadi 37 ya hotuba kwani baadhi ya wahalifu wanasukumwa kutenda uhalifu kwa sababu ya hali ngumu ya maisha, hivyo wakifundishwa shughuli zinazoleenza hapo wakitoka wataweza kuajiriwa na kujajiri, hivyo kuachana kabisa na uhalifu. Lakini nashauri Magereza kuwa na utaratibu wa kutoa vyeti na shahada za kuhitumu katika mafunzo wanayoyapata katika fani mbalimbali wanazofundishwa kwa vitendo ili wakubalike katika ajira au kwa wale watakaojajiri ujuzi wao utambulike kwenye kupewa zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wafungwa 39,951 waliopo katika Magereza hadi tarehe 1 Juni, 2008 ni kubwa, kinyume na uwezo wa Magereza kuwahifadhi wafungwa 22,669. Hapana budi tujitahidi kuzuia wingi huo. Njia kubwa ya kuipunguza ni kuwafanya watu wetu waache uhalifu. Hili litawezekana tu kama Taifa litabuni miradi itakayozalisha ajira za aina mbalimbali yaani zinazohitaji taaluma na nguvu kazi.

Kuhusu msamaha wa Rais unasaidia kupunguza msongamano, lakini njia hii ina madhara yake. Wafungwa 7,696 kuruhusiwa kutoka gerezani na iwapo bado tabia zao hazijabadilika tunaongeza sumu ya maovu katika jamii. Isitoshe baadhi yao hawachukui muda wanarudi tena Gerezani. Kwa hiyo, dawa kubwa ni kubadili tabia za wahalifu wawe watu wema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakimbizi. Tatizo la wakimbizi linatuathiri kwa njia mbalimbali, tunatumia mali zetu finyu kuwahudumia badala ya kuwahudumia watu wetu, baadhi yao wanaharibu mazingira, wanatusaliti dhidi ya Serikali zao pale wanapofanya vitendo vyta uchokozi dhidi ya Serikali zao na wanaathiri tabia na mila zetu pale baadhi yao wenye tabia mbaya wanapoeneza tabia zao kwa vijana wetu. Kwa hiyo, naishauri Serikali kuwachuja vizuri sana wale wanaoomba uraia ili wale wenye tabia mbaya wasipewe uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Zimamoto. Huduma ya zimamoto ni muhimu sana hasa wakati huu ambapo matukio ya moto, mafuriko na kuperomoka majengo yamekuwa mengi. Kwa ufupi idara ina matatizo mawili, kwanza zana mbou na pili, uzembe au uwezo mdogo wa wahudumu kushindwa kuwahi kwenye matukio. Naishauri Serikali iyasimamie haya kimakini. Naunga mkono.

MHE. SAMUEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza hotuba nzuri hii kwa kuleta mbele ya Bunge hotuba nzuri. Ninayo mambo makuu mawili tu ambayo naiomba Wizara hii iyafuatilie na kuyatekeleza nayo ni kuwa mnamo tarehe 29 Juni, 2008. Muda wa usiku jimboni kwangu Buchosa katika Kata ya Nyehunge na kijiji kitiwacho Nyehunge palivamiwa na kundi la majambazi yaliyokuwa yamesheheni silaha mbalimbali, bunduki pamoja na mabomu, yalivamia na kuteka mji mzima wa Nyehunge na kupora mali za wafanyabiashara kinyama na kusababisha kifo cha mfanyakibashara mmoja aliyepigwa risasi zaidi ya saba mwilini kwake na akiwa nyumbani kwake vita iliyokuwepo pale hata askari wa kituo kilichopo hapo walishindwa kujibu mashambulizi kutokana na uchache wao hata silaha zao kuwa duni.

Je, hatua zipi zimechukuliwa na jeshi la polisi baada ya tukio hilo la fedheha kwa wananchi wangu kukaa bila amani sasa, mimi napendekeza kuwa kutokana na sehemu hiyo kuwa ya biashara kubwa wakati mwingine ukifanya hesabu pale pana biashara kubwa kuliko hata Sengerema Mjini. Hivyo naomba kituo cha polisi kilichopo Nyehunge kipandishwe hadhi ili kiweze kupatiwa askari wa kutosha na sihala za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinzi uimarishwe katika Ziwa Victoria, wavuvi kila siku na kila mara wanauawa sana na kuporwa mali zao kinyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga hoja mkono asilimia mia moja. Naomba kujibiwa kwa maandishi.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa Bajeti nzuri mawaziri wawili Mheshimiwa Lawrence Masha na

Mheshimiwa Khamis Kagasheki, tuna matumaini makubwa pia watendaji wote wachapakazi safi.

Napenda nitoe pongezi na shukrani kutoka kwa wananchi wangu wa Kawe wanashukuru sana idara ya Uhamiaji wameimarika vizuri. *Passport* mnatoa kwa uharaka bila urasimu. Namtaja kipekee ndugu Shayo, Afisa Uhamiaji. Naomba apongezwe sana. Pia jeshi la polisi kwa ujumla wanatoa huduma za kupambana na uhalifu jiji la Dar es Salaam vizuri sana.

Napendekeza, ofisi za vituo vya polisi vya Wazo na Kawe viboreshwe. Pia wapatiwe vitendea kazi kama gari la ziada vituo hivi vinahudumia watu wengi.

Mheshimiwa Waziri, naona hukutaja kuhusu uraia wa nchi mbili. Hili suala limechukua muda mrefu na linarudisha maendeleo ya nchi yetu nyuma. Kuna watu wako tayari kuleta mali na uwekezaji hapa nchini kama watapewa *dual citizenship*. Naomba Waziri anijibu ni lini Serikali itatekeleza? Zanzibar sio mbali kaeni pamoja myamalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kutoa salaam za pole kwa kifo cha Mbunge wa Tarime, Marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, kwa Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, familia ya Marehemu na wananchi wa Jimbo la Tarime.

Napenda sasa nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Lawrence Masha na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Balozi Khamisi Kagasheki, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali. Naunga mkono hoja.

Mchango wangu ni kama ifuatavyo, jimbo langu la Tandahimba lina tatizo kubwa la askari polisi. Polisi ni wachache kuliko mahitaji. Ombi langu kwa Wizara ni kuongeza askari kwa Wilaya hii. Lipo tatizo kubwa la kuwahamisha watendaji kama vile *OCD*, *CID* bila nafasi hizo kuzibwa kwa haraka.

Napenda nipate maelezo chanzo cha viongozi hao kuhamishwa bila nafasi hizo kuzibwa. Hivi sasa *OCD* Tandahimba amehamishwa lakini nafasi hiyo haijazibwa/kujazwa na hivyo kuleta matukio na maafa kwa wana Tandahimba kwani wahalifu wanatumia mwanya huo. Hadi sasa Wilaya ya Tandahimba haina Magereza kwa maana ya ofisi ya Magereza na majengo ya wafungwa.

Napenda nipewe maelezo ni lini Idara ya Magereza itazidisha shughuli za jeshi hilo jimboni kwangu kwa kuwa na ofisi na majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo shamba lililokuwa linatumwa na Magereza Newala lililoko kata ya Maundo, Kijiji cha Mbuyuni Chiumo. Shamba hili sasa halitumiki kwa nini kama Magereza hawalihitaji lisirudishwe kwa wananchi. Jeshi la

Polisi liongeze idadi ya mafunzo kwa vijana ili kuongeza ajira ya askari na pia askari walioko kazini wapewe motisha kwa vyeo vya mafunzo.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi katika Bajeti hii ili niweze kutoa mawazo yangu ambayo naiomba Wizara yako iyachukulie hatua madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa matumizi ya silaha, Mheshimiwa Waziri najua kitengo hiki kina majukumu makubwa na kina kazi nyeti na muhimu sana ili wahakikishe silaha zinazotolewa hazifikii kwenye mikono ya maadui. Kitendo cha kupokea rushwa kwa watendaji wa sehemu ya mwisho ya kuthibitisha raia wa Tanzania anapatiwa silaha kwa matumizi binafsi. Sehemu hii ambayo watendaji wake wengi ni askari polisi imekuwa ni hatari kubwa kwa usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Waziri nafahamu vizuri kwamba kabla ya hujapewa silaha inabidi fomu yako iwe imepitia kujadiliwa katika sehemu mbalimbali hadi ifike kiwango cha kuipata silaha hiyo, kuna ushahidi wa kutosha kwamba baadhi ya askari huwa wanafika kiwango cha kubadilisha majina ya watusika amba fomu zao zimepita katika maeneo yote ya mchakato mzima. Askari wanaobadilisha majina halisi ya walioomba na badala yake wanaandika watu waliota rushwa kati ya shilingi milioni moja hadi mbili, hili ni jambo la hatari kwa usalama wa nchi yetu kwa tamaa za watu binafsi.

Jambo la pili ni lile linalofanywa kinyume na watendaji wa jeshi la polisi wakati wa kuajiri askari wapya, kwani huonekana waandishi wa askari hao ni lazima watoke Bara je, Zanzibar hakuna watu wenye uwezo wa kuifanya kazi hiyo. Waandishi hawa wanaotoka Bara wanakuwa tayari wameshachukua vijana wao kutoka Bara na wanakuwa wakiandikisha majina ya vijana hao hii sio halali kwa upande mmoja wa Muungano. Nategemea kuunga mkono.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenyewe mwelekeo wa kuboresha idara zote zilizomo ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchangu wangu ninamuomba Mwenyezi Mungu awe kiongozi wao wakati wakitekeleza malengo yao ili yalete tija kwa Watanzania. Naunga mkono hoja hii nikiwa na matumaini kuwa hoja zangu zitatolewa ufanuzi wakati Waziri anafanya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza askari wa Idara ya Zimamoto Singida. Napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali kutupatia Manispaa ya Singida gari la Zimamoto ambalo litasaidia sana endapo kutakuwa na tatizo la moto tutaweza kuzima ili usilete madhara makubwa kama ilivyotokea miaka iliyopita wananchi walipata hasara ya nyumba zao kuteketea pamoja na mali zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupatiwa gari la zimamoto bado gari hilo halina kazi maana Mkoo wetu hauna askari wenyewe fani ya zimamoto. Hivyo basi naiomba Serikali kutupatia askari wenyewe kusomea fani ya zimamoto ili waweze kutumia gari hilo la zimamoto. Kwa huruma ya Mheshimiwa Waziri nina matumaini wakati wa majumuisho atatufikiria kupata askari wa zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari waliofukuzwa kazi kwa upotevu wa ng'ombe walioibiwa, naishukuru sana Serikali kwa kukubali kumfidia Mzee aliyeibiwa ng'ombe na kupotelea kituo cha polisi. Vile vile naipongeza mahakama kwa kuwaachia huru askari wawili waliohusishwa na upotevu wa ng'ombe hao baada ya kuridhika kuwa hawakuwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa askari hawa wameachiwa huru na mahakama baada ya kuridhika kabisa kuwa hawana hatia, kwa nini Serikali haijawarudisha kazini mpaka sasa badala yake wanaendelea kutishwa hadi wamekimbia familia zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kupidia raia wema wanaolijua tukio hili wanaendelea kukiri kuwa Mkuu wa kikosi cha Upelelezi Wilaya aliyeuwepo wakati huo alihusika kupotea kwa ng'ombe hao lakini ye ye hajaguswa na bado anaendelea kupanda madaraka. Naiomba Serikali kuwarudisha askari hawa kazini kwani hawana hatia.

Kuhusu nyumba za askari Magereza Singida, napenda kukiri kuwa Serikali siku zote haina nia mbaya na askari wake bali kinachowakosanisha ni ufinyu wa Bajeti. Vile vile nampongeza Mkuu wa Jeshi la Magereza (*RPO*) Singida kwa jinsi anavyojitahidi kutumia nguvukazi aliyonayo ya wafungwa kujenga nyumba za askari wake pamoja na kukarabati Magereza kwa kutumia matofali yenye gharama nafuu yanayofyatuliwa kwa kutumia mashine ya *Interlocking bricks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tofali hizi ni nzuri na zinatumia simenti kidogo sana kwani mfuko moja hutoa tofali 120. Nashauri Serikali kupelika askari Singida kujifunza namna ya kufyatua tofali hizi ili Serikali iweze kujenga nyumba za askari magereza na polisi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kumwezesha *RPO* wa Singida ili mradi huu uweze kuzaa matunda haraka kwani kupidia nguvukazi aliyonayo anawenza kufyatua matofali ya kuza ili apate fedha za kununua simenti kwa kuendelea kujenga nyumba za askari wake.

Kuhusu magari na mafuta ya doria, napenda kuijulisha Serikali kuwa baada ya Singida kuwa *highway* sasa inahitajika doria madhubuti ili kuweka tahadhari ya matukio yanayoweza kujitokeza mfano ajali na kadhalika, hivyo basi naiomba Serikali kutuungezea magari ya doria kwa Wilaya zote kwa mgawo wa gari moja kila Wilaya ya Manyoni na Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana Wilaya hizi zote kupambana na matukio. Vile vile naiomba Serikali kuongeza mgawo wa mafuta kuliko ilivyo sasa kwani sasa hvi magari hupewa lita tano hadi kumi kwa siku bila kuweka tahadhari yoyote. Hii ni sawa na kuwa na gari la zimamoto linalokaa bila kuwa na maji ya tahadhari. Ni vyema magari yaye yanawekewa mafuta ya kutosha ili tatizo lolote likitokea waweze kulikabili haraka iwezekanavyo. Nitafutarahi Waziri akieleza hili.

Suala la uhamisho wa askari, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana askari wote nchini kwa kuwa na kauli ya nidhamu kwa viongozi wao. Kwani siku zote wamekuwa tayari kupokea amri halali kwa wakuu wao. Mfano wapatapo amri ya kuhama, huondoka mara moja bila kujali amelipwa fedha ya uhamisho au sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauru Serikali sasa kubadilika, iwe inatoa amri ya kuhama pia askari huyo alipwe fedha za uhamisho haraka kwani kukaa hata miaka miwili ndipo analipwa jamba ambalo linatenganisha askari na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya polisi ya jamii, ni ukweli usiojificha utaratibu huu wa polisi jamii ni mzuri sana kwa kuboresha ulinzi kwa askari kushirikiana na wananchi hata katika kujenga nyumba au vituo vya polisi. Tatizo ambalo bado linakwamisha hapa ni elimu hajapelekwa vijijini kwa wananchi. Naiomba Serikali itoe elimu ya kutosha hadi vijijini sio mijini tu. Itasaidia sana mpango huu kuzaa matunda.

Suala la vitambulishao vya uraia, Watanzania walifurahi sana waliposikia kuwa Serikali imepokea ombi la kutengeneza vitambulisho vya uraia. Naiomba Serikali itoe maelezo mpango huu umefikia wapi na kwa nini unachukua muda mrefu kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya mazingira magumu kwa askari matumaini yangu Serikali itakubaliana nami kuwa askari wakati mwingine hufanya kazi katika mazingira magumu mfano askari wanaoshiriki misafara ya viongozi na kadhalika hupata vumbi, upopo mkali na kadhalika, ukimuuiliza umepata posho kiasi gani atakueleza shilingi 20,000/= kiasi hicho ni kidogo sana kulingana na adha wanayopata. Naishauri Serikali kuwapa sasa posho ya mazingira magumu sio posho ya kawaida tu. Ninaunga tena mkono.

Kuhusu kiinua mgongo cha askari, ni suala la kusikitisha sana tunapoona askari anakuwa na thamani wakati tu anapokuwa kazini lakini anapostaafu hukosa thamani. Naiomba sana Serikali kuwalipa askari kiinua mgongo mapema mara wanapostaafu kwani anapocheleweshwa hufikia hatua ya kuchakaa sana pia hata wale wanaobaki kazini wakiona hali hiyo huona bora kupokea rushwa ili atakapostaafu imsaidie hiyo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile fedha wanayopata ya kiinua mgongo ni ndogo sana kulingana na hali ya maisha inavyopanda, naishauri Serikali kuongeza kiwango cha kiinua mgongo na kulipwa mara wanapostaafu.

Kuhusu askari kuchelewa kupanda vyeo, napenda kukiri kuwa askari wetu wanafanyakazi vizuri sana, lakini wapo askari wengi hadi kufikia hatua ya kustaafu bila

cheo kabisa. Nashukuru Serikali awamu mbili zilizopita walipelekwa kozi askari ambao wamekaa miaka mingi bila ya kupandishwa vyeo. Naiomba Serikali utaratibu huu uendelee ili wote ambao walisahaulika wapate kozi ili wapande vyeo. Baada ya hapo basi askari wawe wanapata nafisi mapema ya kozi ili tabia ya kushaulika iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la askari kukaa kituo kimoja kwa muda mrefu, matumaini yangu Serikali itakubaliana na mimi kuwa askari akikaa muda mrefu kituo kimoja ni matatizo makubwa kwani huzoleka sana na ni rahisi kutumia nafasi yake vibaya. Sio hayo tu hupata pia maadui kutoikana na kutimiza wajibu wao hali ambayo inaweza kumsababishia kupata matatizo ya kukosa usalama. Ninaishauri Serikali iwe inawahamisha askari anapoonekana kukaa muda mrefu sana kituo kimoja cha kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ni ndogo sana. Ni kweli usiojificha kuwa Wizara hii ina majukumu mazito sana. Hivyo ni vyema ikafikiriwa namna ya kuongeza Bajeti yao. Nina uhakika wanafanyakazi katika mazingira magumu sana kwani kazi yao ni kulinda watu na mali zao kwa watu wabaya hasa majambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwendo kasi kwa magari ya abiria inasikitisha sana tunapoona ajali za magari ya abiria bado zinaendelea siku hadi siku. Magari haya ya abiria kwa uelewa wangu huwa ya gia tano tu yale ambayo yanamwendo mzuri lakini yako magari ya abiria aina ya *scania* yanagia hadi kumi na mbili. Ni wazi magari haya pale dereva anaendelea kuongeza gia huzidi kuwa mepesi na mwendo huwa kasi sana hivyo likipata ajali sio rahisi kupona abiria. Naishauri Serikali kuchunguza magari yenye gia nyingi yasitumike watu wataendelea kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa vituo vya polisi mpakani natambua wazi kuwa mpakani kuna vituo vya polisi lakini ni vichache sana njia nyingi ni za panya ambazo biashara nyingi zinapitia humo, suala ambalo linapoteza mapato mengi ya nchi yetu.

Naishauri Serikali kujenga vituo vya kutosha mpakani ili kuondoa njia za panya. Vituo hivi watafanyakazi askari wa uhamiaji, afisa wa *TRA* na askari wa kawaida, hii itasaidia sana kulinda mapato ya nchi yetu na kuzuia majambazi toka nchi jirani kutoingia nchini mwetu ovyo. Ninarudia tena kuunga mkono hoja hii nikisubiri ufanuzi wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti , ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni, napenda kurejea swali langu nililouliza hapa Bungeni juu ya kuchakaa na kuvuja Kituo cha Polisi ya Wilaya Manyoni wakati Mheshimiwa Bakari Mapachu, alipokuwa bado Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii. Mheshimiwa Mapachu alinipa maandisi ya *note* ambayo bado ninayo kuwa angepeleka fedha za kununua bati kwa kukarabati majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhafamu endapo fedha hizo zimeshapelekwa Manyoni ili kuwanusuru watendaji na kumbukumbu zisivujiwe masika yakianza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi hiyo. Mheshimiwa Mapachu, jibu la msingi nilijibiwa kuwa azma ya Serikali ni kujenga kituo kipyä cha Wilaya hiyo ya Manyoni na fedha za awali kupima kiwanja ziliishapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu kupitia Bajeti hii zimetengwa, shilingi za Kitzanzania ngapi ili zoezi la kujenga kituo hicho cha Wilaya lianze moja kama ilivyo azma ya Serikali kwani kituo hiki kilikuwa ndani ya eneo la hospitali ya Wilaya hiyo. Nategemea Mheshimiwa Waziri mwanangu Lawrence Masha atafuta machozi ya wananchi wa Wilaya ya Manyoni wakati akifaya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kutamka tena kuwa ninaunga mkono Bajeti hii na nawatakia utekelezaji mwema.

MHE. DR. LUKE J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe na kwako wewe na Bunge la Jamhuri ya Muugnano wa Tanzania kutokana na kifo cha Mbunge huyo shupavu, ambaye ameacha pengo kubwa si kwa familia yake na Jimbo la Tarime tu bali kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake iliyoandaliwa kwa umahiri mkubwa. Napenda pia nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Makamanda na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa jumla kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutayarisha makabrasha ya Bajeti ya Wizara hii.

Napenda niwapongeze kwa dhati Wakuu wa Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji kwa ushupavu wao katika kuongoza majeshi hayo. Napenda pia, kuwapongeza kwa dhati askari wa watumishi wote wa Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto ambao pamoja na mazingira magumu ya kazi, uhaba wa vitendea kazi kwa uchache wao ikilinganishwa na umma wa nchi hii, wanaofanya kazi bila kuchoka na kwa kujituma kwa moyo wote ukiachia wachache wao suala ambalo hutokea katika kundi lolote kubwa la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba nielekeza hoja yangu katika mambo yafuatayo, kwanza, uchache wa vituo vya polisi Jimbo la Mbozi Magharibi, upungufu wa vitendea kazi kwenye vituo vya uhamiaji mipakani, ukosefu wa huduma za Zimamoto sehemu nyingi za mijini na ukosefu wa magari/pikipiki Wilayani Mbozi kwenye vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbozi hususan Jimbo la Mbozi Magharibi lenye Kata 11 zenye jumla ya eneo la kilometra za mraba 6,275 ambalo pia linapakana na nchi za Zambia na Malawi na pia ni njia kuu ya kwenda na kutoka nchi za Kusini mwa Afrika na *Congo DRC*, lina vituo vidogo vya polisi viwili tu ambayo vinatenganishwa na umbali wa kilometra takriban 200. Kati yake kuna misitu minene ambayo hutumika kama maficho ya majambazi na wahalifu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Tunduma, kwa uwepo wake mpakani unakabiliwa na tatizo kubwa la ujambazi amba ni wa Kimataifa. Kuwepo kwa kituo kidogo cha polisi kimoja tu mjini hapo na maeneo ya inayozunguka kufanya mazingira ya utendaji kazi ya askari wetu kuwa magumu sana. Hali hii inafanywa kuwa ngumu zaidi kutokana na kituo hicho kutokuwa na gari, suala ambalo ni gumu kwa Wilaya nzima ya Mbozi, kwani hata polisi Wilaya haina gari la uhakika kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wa Tunduma mwaka jana kwa kuhamasishwa na Kamanda Kova, aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya na Mbunge wa Mbozi Magharibi waliweza kuchanga fedha na kununua pikipiki sita kwa ajili ya doria pale Tunduma, na kwa muda wimbi la ujambazi lilipungua sana. Bahati mbaya, hali hiyo kwa sasa nimerudia kuwa mbaya kutokana na uchache wa askari na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kata za Kapele, Myunga, Ndalambo, Msangano, Chitete, Chilulumo na Ivuna ambako kuna misitu minene kwa umbali mkubwa kuna ujambazi mkubwa wa uporaji mali za wasafiri na utekaji nyara magari, kiasi cha kuathiri hali ya maendeleo ya wananchi wa kata hizo. Wananchi wa Kata kadhaa ikiwemo kata ya Msangano walijenga vituo vidogo vya polisi toka mwaka 1997 lakini mpaka leo hakuna askari hata mmoja aliyepelekwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya vituo vya uhamiaji mpakani yana upungufu mkubwa wa vitendea kazi yakiwemo magari ya doria, vifaa vya kupimia dawa za kulevyta na zana zingine za ukaguzi. Pia kuna watumishi wachache sana. Hali hii inaathiri sana shughuli za uhamiaji wa forodha. Mfano halisi ni Tunduma ambapo kutokana na uchache wa watumishi hao na vitendea kazi kuna msongamano mkubwa wa magari ya mizigo na abiria na pia kuna uvunjaji wa mipaka, kwa maana ya kwamba watu wanavuka mpaka bila taratibu.

Suala la upungufu au ukosefu wa vifaa vya zimamoto, hususan mijini. Sihatiji kuongea kwa kirefu kuhusu suala hili kwani kila linapotoka tukio la moto tumeshuhudia mali zikitekeketea kutokana na ukosefu wa zana za kuzimia moto yakiwemo magari ya kubeba vifaa vya kuzimia moto. Pia ukosefu wa gari Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi na kwenye vituo vya polisi vya Tunduma na Kamsamba, Jimboni Mbozi Magharibi. Kwa upande wa gari la polisi Wilaya ya Mbozi hii imetokana na gari lililokuwepo kupata ajali mwaka juzi. Kwa Kamsamba ni muhimu kuwe na gari kutokana na umbali wa zaidi ya kilometra 130 kutoka makao makuu ya Wilaya, kwa Tunduma ni ule uwepo wake mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi zao wanazozifanya na wale wote walioshirikiana kwa kutunga hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara inayofanya shughuli zake katika mazingira magumu, inahitaji kuangalia wafanyakazi kwa kupewa maslahi yaliyoboreka kwa hivyo, tunaiomba Serikali iwaongeze, maslahi yao ni madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi natokea katika Shehia ya Finya, jimbo Mgogoni hapo ilipo kambi ya *FFU*. Kwa kweli kambi hiyo ina matatizo ya tenki la kuhifadhia maji, nyumba tatu zilimalizika kujengwa bado hazijaungwa umeme na vile vile gari zilipo ni mbovu na nyingine zimehamishiwa vituo vingine na zilipo sasa hazikidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wakati akitoa majumuisho yake anijubi je, ni lini matatizo hayo yatatatuliwa kwani Waziri aliyepita nilimweleza haya na akaniahidi lakini mpaka leo bado hasa tatizo kubwa la tenki la kuhifadhia maji, kwa sababu katika ujenzi unaoendelea maji ni usumbufu kuyahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha kuna askari wa Zanzibar waliokwenda kusoma mafunzo mpaka leo askari hao hawajalipwa posho zao na wewe binafsi umekiri kuwa fedha hizo tayari Wizara imepokea. Kamishna mwenyewe kakiri kuwa amepokea. Nataka unijibu kuna kigugumizi gani mpaka leo ikawa hawajapata fedha hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomwombea Waziri na Naibu Waziri afya njema na maisha marefu na awape nuguvu za kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia hoja hii kwanza naunga mkono hoja hii asilimia mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba hii kwa jinsi ilivyokuwa nzuri yenye maboresho mazuri ya Jeshi la Polisi pamoja na idara zote zilizo ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kuwa Wizara hii ina mzigo mkubwa sana kwa sababu ni Wizara ambayo imebeba Idara sita ambazo zote ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo ni dunia ya wajuuji wawe wananchi wa askari wa aina yoyote kwa Wizara hii ni Wizara inayotizamwa na wananchi wote. Kwa hiyo, lazima iwe na mbinu za dunia ya leo ndani ya umma na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshi la polisi ni dira kwa nchi yoyote ile. Jeshi hilo ndilo la mwanzo kufika kwenye matatizo na penye faraja. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kuliwezesha jeshi hili kwa kuwapa vifaa vya

kisasa vinavyoendana na wakati. Askari wa *traffic* wapewe usafiri wa kutosha kama pikipiki kwa ajili ya *patrol* kwa barabara zetu ambazo mara nyingi huwepo na makosa ya madereva na msongamano hata ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, doria za askari polisi ziimarishwe ili wananchi wazidi kuwa na imani na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafuta, petroli au dizeli vituoni. Jambo linaloturejesha nyuma ili kazi za jeshi la polisi zisiende haraka vituoni mwetu wakati wa matukio kutoka ni kukosa magari vituoni au kukosekana petroli kwa magari yaliyopo. Hivyo hufanya kazi kutofanyika kwa wakati. Hata Jeshi la Polisi likifika sehemu ya tukio hukosa ushahidi au hata waliosababisha tukio hilo kwa sababu wahusika na tukio hilo huondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Magereza naomba Serikali hivi sasa isimamie kupunguza msongamano magerezani kwa sababu karibu magereza yote hivi sasa yana msongamano mkubwa sana hali inayofanya wafungwa kukosa hewa inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zimamoto na uokoaji. Zimamoto iwe na vifaa vinavyoendana na hali ya nyumba zilivyo, kwa sababu hivi sasa majengo yanayojengwa yana ghorofa nyingi na marefu sana wakati inapotokea moto kwenye majengo hayo basi vifaa huwa havikidhi haja kutokana na majengo yetu kuwa marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uhamiaji wawezeshwe kuwa na vifaa vinavyoweza kukabiliana na jambo lolote linalotokea. Wawe na pikipiki ambazo zinaweza kufanya doria mipakani pamoja na kuwa na gari za kuwarahisishia kazi zao hasa mikoani kwenye mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ili kuziweka vizuri idara zetu zote ndani ya Wizara hii ni kupata mafunzo mara kwa mara kwa kukabilaina na lolote lile.

Mwisho nazidi kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu nazidi kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Napongeza hasa juhudzi za kujitegemea kwa majeshi ya polisi na Magereza, ikiwa ni pamoja na kujijengea nyumba zao wenyewe na kujilisha. Nilipotembelea Gereza la Rombo Mkuu nilifurahishwa sana na utawala bora ulidhahirika hapo (*Professional Competent*).

Nilihuzunishwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu wanaume. Iko haja ya kupanua majengo (mabweni). Nilikuta ucheleweshaji wa hukumu au watuhumiwa mahabusu kutokana na uhaba wa magari ya polisi, Waendesha Mashitaka na Mahakimu. Hata washitakiwa waliokiri makosa hawapati hukumu kwa wakati.

Aidha, liko jengo hapo lililokuwa linajengwa kwa michango ambalo ni la Serikali. Naomba fedha kidogo zinazotakiwa kulikamlisha litolewe ili askari wafanye mambo mengine. Nafurahi kusoma leo kwamba jengo la utawala Rombo limekamilika sasa. Nilipotembelea lilikuwa bado.

Kuhusu mpango wa Wizara wa kuteua maofsia wa Mikoa na Wilaya. Nashauri kuwa wapewe pia ukamanda wa mipaka ya nchi, hususan vituo vya mipakani na nchi jirani. Mipakani kuna utawala wa kila mtu na lwake, hakuna kiongozi wa kituo. Hii ni kasoro kubwa kiutawala na kiusalama. Ndiyo sababu Afisa Forodha anaweza kuruhusu mali za magendo bila kuulizwa na yule wa uhamiaji au hata wa Usalama wa Taifa. Wasomali/Wahabeshi wakiingizwa kinyemela hakuna wa kuuliza au hata kuwarudisha! Suala hili lilikuwa likishugulikiwa na Wiziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Sumaye; nadhani bado halijaamuliwa na utumishi. Naomba lifuatiliwe. Zingatia kuwa *TRA* walipofuta utawala wa kila mtu na lwake, Wilayani na mikoani waliongeza sana sana ufanisi na ukusanyaji wa mapato. Nilihuksika na uamuzi huu

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa hatimaye kutumia utaratibu wa *visa stickers* ambaa uliamuliwa hapa Bungeni miaka ya nyuma lakini utekelezaji ukasua sua. Ni chanzo kizuri cha mapato ya Serikali na *retention* Wizarani kama ukisimamiwa vizuri. Kuna uwezekano wahamiaji wa mipakani wakadaiwa hela taslimu (magendo) na hivyo kupoteza mapato hayo. Je, viwanja vidogo vidogo vya ndege wanamo tua watu kama watalii toka nje au watafiti/wachimba madini wanahuishwa vilivyo kwenye utaratibu wa *stickers*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwaunga tena mkono kwa kazi nzuri ya majeshi yetu katika mazingira magumu na pia kwa hotuba nzuri ya leo.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kabla ya yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba nzuri sana, yenye malengo yanayotia matumaini, hata katika kuboresha mazingira ya kufanya kazi na makazi ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara wakati wa kuweka vipaumbele hasa vya kuboresha makazi ya askari. Nyumba za askari mjini Lindi, Mkoani Lindi zipewe Kipaumbele, kwani nyumba hizo zipo katika hali mbaya sana ukilinganisha na baadhi ya maeneo ambayo nimefanikiwa kutembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja kwa mara ya pili.

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usalama wa raia uko katika mikono ya Serikali lakini jukumu kubwa liko hatika Jeshi la Polisi ambalo linafanyakazi usiku na mchana, hivyo ni lazima kulipongeza jeshi hili kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa jeshi hili wanafanyakazi katika mazingira magumu, ikiwa pamoja na mishahara na posho kuwa halitoshi, nyumba za kuishi, vitendea kazi duni kukabiliana na wahalifu pamoja na majambazi. Hivyo ili kufanikisha utekelezaji mzuri wa kazi lazima mambo yote ya msingi yatekelezwe ili kuweza kukabiliana na changamoto zote wanazozipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna madai ya malimbikizo ya madai kwa wanajeshi wetu hao hivyo imefika wakati kwa Wizara kumaliza malimbikizo ya madai hayo ili wanajeshi wetu wafanye kazi kwa ari kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya askari wetu kuchukua hatua mikononi mwao kuwapiga watuhumiwa bila sababu ya msingi hivyo ifikie wakati sasa hao wenye tabia mbaya wachukuliwe hatua pale watakapobainika. Vile vile pamoja na wale wanaowabambikia kesi wachukuliwe hatua ili kuondo tabia mbaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vingi ni chakavu ambavyo vinatishia usalama wa wafanyakazi, majengo mabovu na bado hayajafanyiwa ulkarabati kwa kipindi kirefu hivyo Wizara ijitahidi kuyafanyia ukarabati yapendeze na kuonekana kama ni sehemu nyeti na nadhifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano katika Magereza bado ni tatizo kubwa pamoja na kurundikana kwa mahabusu hivyo Wizara iendelee na mpango wa kupanua na kujenga Magereza mapya na ya kisasa kwani mfungwa ni binadamu kama binadamu mwingine anahitaji mambo yote ya msingi, hivyo Magereza yaimarishwe vizuri pamoja na wafungwa kupatiwa burudani na kufanya ibada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara ya zimamoto ipatiwe vifaa vyta kisasa ili waweze kukabiliana na majanga ya moto ambayo yanatokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara ya uhamiaji nayo iache ukiritimba pale raia wanapohitaji *passport*, wajue kuwa hiyo ni haki ya raia. Ahsante.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Majeshi, Wakuu wa Idara na wataalam wengine wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kwa hotubu nzuri na jitihada nzuri za kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkinga ina kero nyingi zinazohusiana na Wizara hii. Awali ya yote, Wilaya ya Mkinga haina makao Makuu rasmi ya polisi. Mpaka sasa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (*OCD*) na wasaidizi wake wanatumia kituo cha polisi cha Duga Mtandikeni kama makao makuu ya muda. Kuna umuhimu mkubwa wa kujenga Makao Makuu ya Polisi katika Makao Makuu ya Wilaya, Kasera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijibanda cha polisi kilicho mpakani Horohoro kinatia aibu. Alipofika ziarani Mkoani Tanga hivi karibuni, Mheshimiwa Rais aliagiza kituo

imara na chenye hadhi ya hapo mpakani kijengwe kwa hadhi na uimara unaolingana au kupita kile kilichopo upande wa pili nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kidogo cha polisi na nyumba chache za kukaa askari kule Maramba zipo katika hali mbaya sana. Haja kubwa ya kujenga kituo imara na nyumba bora na za kutosha kwa askari pale Marimba nimeeleza kwa muda mrefu sana. Naiomba Wizara ilifikirie hii kwa Bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukubwa wa jiografia ngumu ya Wilaya ya Mkinga kuna haja kubwa ya kujenga vituo vidogo vya polisi katika maeneo mengine yakiwemo Mtimbwani, Mwakijembe na Jasini. Aidha, kutokana fukwe ndefu za Bahari ya Hindi zinazopakana na nchi ya Kenya pamoja na bahari ndogo nyingi ipo haja ya kuweka angalau boti moja ya doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufinyu wa Bajeti uliopo, uimarishaji wa usalama wa raia na mali zao Wilayani Mkinga hauwezi kuimariika bila ya kuwa na idadi ya kutosha ya askari pamoja na vifaa vya mawasiliano pamoja na gari za 999 na pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa ulinzi wa Shirikisho, ipo haja kubwa ya kuhamiasisha na kuwapa wananchi mafunzo ya polisi jamii. Kwa hili, nashauri motisha za kuwazawadia wanaofanikisha kupambana na uhalifu ziboreshwé na kuwekwa wazi zaidi ili wananchi wengi zaidi waweze kufanikisha zaidi ufichuaji wa uhalifu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji inatumia ofisi pamoja na mamlaka ya kodi (*TRA*) na taasisi nyinginezo pale Horohoro mpakani jengo linalotumika ni finyu na halina hadhi stahiki. Ni wakati muafaka sasa kwa azma ya kujenga jengo moja la kisasa chini ya mpango wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki likaanzwa kujengwa ama pamoja au sambamba na kituo cha polisi stahiki cha mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Mkinga ina mipaka mirefu na nchi ya Kenya, wenye njia za panya nyingi ni muhimu Wizara ikaishawishi Wizara ya miundombinu na pia Wizara ya Ulinzi kuimarisha barabara za mipakani ili kuimarisha ulinzi wa mipaka na pia ulinzi dhidi ya uhamishaji bidhaa isiyo halali (*smuggling*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

MHE. COL. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nina heshima ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kazi wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 ambayo imejaa hekima na mipango mizuri ya kukabili kazi za Wizara na Idara za Ulinzi zilizoko chini ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maeneo yafuatayo, hali ya ulinzi jamii/shirikishi (polisi). Naupongeza sana mpango huu kwani umeonesha mafanikio makubwa sana na kuna haja kubwa ya kuuendeleza kwa juhudhi kubwa. Ushauri wangu

juu ya ulinzi shirikishi ni mambo yafutayo, kwanza ni elimu juu ya ulinzi wa aina hii uimarishwe na wananchi waelimishwe zaidi juu ya kutochukuwa sheria mikononi mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya uraia uimarishwe zaidi. Kuhusu polisi wanamaji, hali ya kikosi cha wanamaji ni mbaya kwa kweli si ya kuridhisha. Nashauri sana Serikali sasa iwekeze nguvu kubwa katika kikosi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunaeleweka umuhimu wa ulinzi mwambao mwa bahari yetu aidha, ulinzi wa maziwa yetu makuu. Hivi sasa kuna upungufu wa kukabili hali ya malindo hayo ambayo baadhi ya wahalifu kutoka nchi jirani za Mwambao wa Maziwa yetu Makuu wanavamia wavuvi wetu na kuwanyang'anya mali mbalimbali za wavuvi hao. Nazidi kushauri kupatiwa vyombo vya ulinzi ili waweze kukabili majukumu yao.

Kuhusu magereza, jeshi la magereza linajitahidi kutekeleza kazi zake na nawapongeza sana, lakini napenda kushauri mambo yafuatayo, kutokana na hali mbaya ya bei ya chakula duniani na kuongezeka hali ya njaa hasa nchi zetu za Afrika, nashauri Jeshi la Magereza sasa tuwapatie zaidi matrekta na zana zaidi za kilimo, pembejeo na kadhalika ili kuhakikisha kupatikana chakula cha kutosha kwa jeshi lenyewe na kupatikana ziada ya kulisaidia Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauru Serikali hasa Wizara katika kulitaka jeshi la Magereza kutoa elimu ya amani na tabia njema ya kuishi uraiani ili watakapotoka gerezani wawe na taaluma na ujuzi wa kazi ya kumsaidia maisha bora akiwa uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP* na Makamanda wote walio waadilifu na wanaojituma.

Napenda kuchangia yafuatayo, kwanza ni kuhusu majengo, ukarabati wa ofisi kuu ya polisi Wete; bora kuziba ufa kuliko kujenga ukuta. Jengo hili zuri Bajeti hii lipatiwe kasma ya kuliboresha (Wete Pemba). Pia jengo la *garage* na ofisi ya madereva wote Pemba lijengwe upya, lilivyo linahatarisha maisha ya wafanyakazi wake (lipo Wete Pemba). Makazi ya *FFU* – Matongatuwani hebu yaoneni! Yako katika hali mbaya, makazi ya *FFU* – Kwale yaendeee kuboreshwa na majengo ya ofisi kuu za polisi Chake Chake yanasononesha na ni hatari.

Jengo lililopo karibu na ofisi hiyo libomolewe au lijengwe/ukarabati mkubwa kabla halijaleta maafa kwa wapitao, askari kukaa sehemu moja kwa miaka mingi, inawafaya baadhi waonekane kutokuwa na toafuti na raia katika utendaji wao, wengine kujiingiza katika siasa, kuzorota katika utendaji wao na haya yapo yameota mizizi polisi Wete.

Kuhusu upandishwaji vyeo, polisi wengi hawapandishwi vyeo, au wanaganda na cheo kimoja hadi wanapostaafu hii ina *emolarise* utendaji wao, hili liangaliwe. Polisi waendesha mashtaka kula njama katika kesi bila kutoa haki, naelewa sasa suala hili litatatuka kwa vile hatohusika tena, ila wanashirikiana na wenye pesa na kuwanyima wanyonge haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuwa na kituo cha polisi Makangale Wilaya ya Micheweni, eneo la Makangale liko mbali na kituo cha Polisi Konde, linafikika baada ya kupita katikati ya msitu mnene. Uhalifu wa uporaji mali (misitu, mbao) unafanyika bila mtu kujua. Aidha, kwa vile *remote* watu waovu wanafika na kuondoka bila polisi kujua. Wakati wa uchaguzi watu toka Mombasa walifanya ndio *route* yao ya kuingia Pemba kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa wafanyabiashara wasio waaminifu bado wanasafirisha bidhaa toka Mombasa kupitia maeneo hayo muafaka ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *passport* na uraia, uadilifu unahitajika katika utoaji pasi hasa sasa unasikia kila mara mtu amekamatwa na pasi tatu za kugushi. Wapo wanaoomba uraia wakapewa baadae wakajihuisha na masuala ya uovu. Je, upo uwezekano wa kuwanyang'anya *passport* zetu?

MHE. ANIA SAID CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangaia kwa maandishi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote kwa kuleta hotuba hii yenye mikakati endelevu na uboreshaji wa Wizara nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo sugu katika baadhi ya Wilaya ambalo linaendelea hivi sasa la baadhi ya polisi wanashirikiana na baadhi ya watendaji wa Serikali kuwabambikia kesi wanasiasa na kuwafungulia kesi za ujambazi au mtu kuambiwa si raia. Kwa kweli jambo hili si zuri na kudhalilisha kwa kumuweka katika wakati mgumu mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia uliyopo katika Jiji la Dar es Salaam katika baadhi ya vituo ukienda kutoa ripoti ya tatizo, mfano unafanyiwa fujo nyumbani kwako unaambiwa humna usafiri au polisi wako wachache au mlete mtuhumiwa. Utaratibu huu hauwatendei haki wananchi, ni vyema vituo vidogo (*police post*) viongezwe idadi ya polisi na vitendea kazi ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya uraia vya Kitaifa napenda kuweka msisitizo Serikali iangalie isije wageni ndio wakapatia vitambulisho badala ya raia halisi, maana hivi sasa pamoja na juhudhi kubwa za uhamiaji kukamata wahamiaji haramu, bado kuna wimbi kubwa la wavamizi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naupongea utaratibu wa hivi sasa wa polisi kuwaelimisha abiria kuhusu uendeshaji vibaya wa dereva wanapokuwa safarini na kutoa namba zao za simu ili kutoa ripoti inapotokea tatizo la uendeshaji mbaya. Nashauri ni

bora elimu hiyo itolewe katika vituo vya mabasi badala ya mtindo wa sasa kusimamisha basi njiani na kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maoni haya naunga mkono hoja.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri inayofanywa na hasa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi limekuwa linapambana vyema na wimbi la wahalifu na majambazi yanayotumia silaha. Lakini ni lazima tukubali kwamba kadri ya ulimwengu unavyobadilika kisayansi na teknolojia ni hivyo hivyo nao wahalifu wanaboresha mbinu za kutenda uhalifu.

Hali hii inapelekea ulazima wa kulipatia Jeshi letu la Polisi mafunzo ya kisasa ili kukabiliana ipasavyo na ongezeko la wimbi la uhalifu. Aidha, ni lazima jeshi letu la polisi liimarishe taaluma katika fani ya *Forensic Examination*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma hii ni nyeti na muhimu sana katika kukabiliana na wahalifu wanaotumia sayansi ya kisasa. Tukiweza kuimarisha kitengo hiki sina shaka tutaweza kukabiliana na uhalifu kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko makubwa kwa askari wetu wa Jeshi la Polisi, Zanzibar. Askari hawa wana madai yao ya muda mrefu ya malimbikizo ya madai mbalimbali. Madai ya malimbikizo haya sasa yameshafikia miaka mitatu lakini bao hayajalipwa. Nina taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri jambo hili amelishughulikia na fedha hizo nasikia zilitumwa kwa Kamishna wa Polisi, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba Kamishna wa Polisi Zanzibar amekiri kupokea fedha hizo lakini hadi leo wahusika hawajalipwa malimbikizo yao.

Ningependa kujua ni kwa nini hadi leo fedha hizo hazijalipwa kwa wahusika? Na aidha, ninamwomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua za ziada kumtaka Kamishna wa polisi Zanzibar walipe haraka askari ambao wanadai malimbikizo mbalimbali ili kuondoa aibu hii ya Jeshi letu kudaiwa ovyo ovyo pasi na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uraia wa nchi mbili limekuwa ni la muda mrefu. Najua mchakato wa kupata maoni kwa upande wa Tanzania Bara umefika mahala pazuri. Tatizo lipo upande wa pili wa Muungano, Zanzibar. Mpaka sasa mchakato wa kupata maoni ya uraia wa nchi mbili kutoka Zanzibar bado haujapiga hatua.

Mimi nadhani, na kwa kweli huu ndio ushauri wangu juu ya suala hili kwamba kwa kuwa suala hili linaungwa mkono na wananchi walio wengi hapana budi Serikali sasa iandae Muswada wa Sheria na kuuwasilisha Bungeni na kwa kuwa suala uraia ni la Muungano bila ya shaka baada ya Waheshimiwa Wabunge kuujadili Muswada huo kwa

niaba ya wananchi wanaowawakilisha na hatimaye Bunge litapitisha iwe ni sheria na sheria hiyo italazimika kuheshimiwa na pande zote mbili za Muungano.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kujitahidi kutimiza majukumu yao kama inavyotakiwa. Mwenyezi Mungu awape nguvu na uwezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhalifu limekuwa tatizo sugu nchini pamoja na juhudu kubwa zinazochukuliwa na jeshi hili. Naomba niishauri Serikali kuongeza vitendea kazi zaidi na kuwaboreshea mishahara yao na posho zao askari wa Jeshi la Polisi ili iwe rahisi zaidi kukabiliana na jukumu hili zito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya wakati askari wanapopewa taarifa ya uhalifu ama uvamizi wa aina yoyote kwa raia hucheleva kufika katika eneo la tukio kwa kisingizio cha kukosa ama usafiri ama hudai hawana mafuta mpaka wanafika kwenye tukio wahalifu wameshaondoka, je, tutamaliza tatizo la ujambazi? Naomba tatizo hili lishughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Kwa upande mwingine askari hao hao wanapopewa taarifa ya kwenda kuwapekuwa wananchi saa saba usiku hawakosi magari wala mafuta. Namwomba Waziri arekebishe watendaji wake ili haki itendeke kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wa *FFU* Finya wana tatizo kubwa la maji, ambapo walihidiwa kuwekewa tanki ya maji, jambo ambalo hadi leo limeshindikana, je, kulikoni?

Pia kuna nyumba tatu hadi leo hazijaungwa umeme jambo ambalo limewalazimu askari hao kutumia vibatari kwa kuonea na pia kukosa mahitaji muhimu yahusuyo umeme kama vile kukosa habari muhimu kupitia luninga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kuongeza ajira kwa jeshi la polisi, bado katika vituo vingi kuna upungufu wa aksari wa kike. Tatizo hili nimelisema mara nyingi ndani ya Bunge hili lakini bado hali ni mbaya na bado wananchi wanaendelea kusachiwa majumbani mwao bila ya kuwepo askari wanawake hilo ni kosa na udhalilishaji wa kijinsia. Pia linapotokea tatizo la ama ubakaji ama mimba za watoto/wanafunzi, kule vituoni pengine kuna askari wa kike mmoja tu na hayupo zamu, hulazimika afuatwe nyumbani jambo ambalo hupoteza muda wa kupata ufumbuzi naomba tuongeze ajira za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya askari wetu ni mabaya mno kiasi ambacho ni aibu kwa jeshi letu. Nyumba zao hawa mara nyingi hupewa chumba kimoja tu hata kama ana familia. Je, hii inaendana na mila na silka zetu. Ili kurekebisha hii hali basi pamoja na kujenga hizo nyumba kwa ajili ya jeshi letu basi na zile nyumba kongwe zifanyiwe ukarabati ili zisaidiwe kuondoa hii kero. Hebu Mheshimiwa Waziri aziangalie nyumba za *police line* Wete, Konde na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye magereza yetu. Magereza yetu hayaridhishi hata kidogo. Usafi wa Magereza ni hafifu mno. Jambo linalochangia kuathiri mazingira na afya za wafungwa na mahabusu, hata mlo wao haqidhishi. Je, wafungwa kuwapa chakula kibaya, Kibichi kisichofaa kuliwa na binadamu huwa ni jumla ya adhabu au vipi.

Mwisho, naomba nimuulize Mheshimiwa je, inakuwaje kule gerezani wafungwa na mahabusu wanapata bangi na kuvuta kama kawaida. Je, huo ulinzi inakuaje. Hicho kitengo cha dawa ya kulevyia kinafanya kazi gani.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa familia na wananchi kwa kumpoteza mtetezi wao aliyekuwa Mbunge mwenzetu Marehemu Chacha Zakayo Wangwe. Namuombea Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali panapostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima iliyoandaa hotuba hii inayoendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze *IGP*, Ndugu Saidi Mwema pamoja na Jeshi lake kwa kazi nzuri wanayoifanya licha ya hali ngumu waliyokuwa nayo. Jeshi la Polisi nchini kutokana na kazi ngumu wanayoifanya ni vyema kutunzwa kuwapatia huduma, vifaa, pamoja na kuwezeshe kimaslahi ili kuwapa moyo na kutokushawishika na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wa jeshi la polisi wana malalamiko mengi ambayo ni kikwazo ambacho kinawafanya baadhi ya askari kuona wanaonewa na kubaguliwa na ufanyaji kazi wao kushuka na kupoteza maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ni malipo ya *pension* na kiuunua mgongo. Suala hili lilishaulizwa mara nyingi katika Bunge lako Tukufu na majibu ni kuwa ni jambo lililochaguliwa na askari mwenyewe, nakubaliana nalo lakini hivi sasa imefika wakati kuondosha utaratibu huo na askari wote walipwe kwa mfumo mmoja tu wa *pension*. Kwa sababu kuna aibu kubwa ya askari wetu kiutendaji, kazi zao na wakati wa kustaafu, kama hatuwalipi vizuri ni rahisi kushawishika kujinga na kambi za matukio ya hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ni sikuvi na inajali wananchi wake. Mfano wa hayo Serikali ilikubali kuwalipa wastaaful kwa mkupuo na baadaye ikawasaidia tena waliokuwa hai na kuendelea kuwalipa kama kawaida, Serikali ilipata sifa kwa kuwajali wastaaful wake. Je, kwa hili la askari polisi Serikali inakigugumizi gani kurekebisha au kufuta utaratibu wa kibaguzi na kero kwa jamii pia wa aibu kwa Taifa? Mheshimiwa Waziri atuambie ni kasoro gani itapatikana kwa Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wa polisi pia wanapata taabu sana wakati wakifuatilia malipo yao wakati wa kustaafuli huchukua muda mrefu na hufatilia hadi anachoka na wakati mwigine huona asamehe kwani hicho anachostahili ni kidogo kuliko gharama zake alizotumia bila mafanikio. Kwa hivyo, nashauri Serikali ili kupunguza kero hizo basi kitengo cha kushughulikia wastaafuli kigaiwe kwa kanda badala ya kitengo hicho kuweko Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhamisho, Jeshi la Polisi hivi sasa wanatekeleza kauli za Wabunge katika Bunge lako Tukufu la askari kutokukaa kituo kimoja kwa muda mrefu. Katika kutekeleza hayo kunatokea usumbufu mkubwa wa makazi kule wanakopelekwa, fedha za uhamisho hawapati na zikipatikana zitalipwa nusu na nusu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inapaswa kuzingatiwa na kuangaliwa kwa sababu wanahamishwa wanafamilia zao na huleta usumbufu mkubwa kwa familia hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba jeshi linapokusudia kuhamisha askari kumpeleka sehemu nyingine ya kazi kuzingatia yale yote yanayomhusu askari atimiziwe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu polisi jamii na upotoshwaji unaofanywa. Katika ukurasa wa 7 Mheshimiwa Waziri amezungumzia huduma za polisi yaani kuwashirikisha wananchi katika suala zima la kulinda usalama wao na mali zao ambayo ndiyo dhana ya polisi jamii ambayo historia yake inajulikana zamani sana tokea mwaka 1829 ilioanzishwa na Bwana Robert Peel na kanuni zake 9 za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana hii inapotoshwa hasa Kisiwani Pemba ambapo imedakwa na Masheha na kutaka kuteua baadhi ya watu kufanywa ndio wao wawe polisi jamii. Kitendo hiki ni mithili ya baadhi ya watu kufanywa askari kanzu na kutaka kuhasimiana na watu kwa kuripoti kwa Sheha kitendo ambacho kinaleta ufitina mkubwa.

Naliomba Jeshi 1 Paolisi waje Pemba hasa Jimboni kwangu tufanye mkutano pamoa na kuwaeleza wananchi dhana halisi ya polisi ya jamii sio hivi inavyoelezwa visiwani. Hali ikiachiliwa ilivyo itahatarisha amani kwa sababu imedakwa na Masheha ambao wanatumikia Chama Tawala na sio jamii yote kushirikiana na polisi kwa karibu na wananchi bali wako karibu na Masheha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi katika Visiwa vya Unguja na Pemba na mwambao wote wa Tanzania hasa Tanga, Bagamoyo, Lindi, Mtwara na visiwa vya Mafia, wimbi la ujambazi hasa visiwa vya Pemba na Unguja sasa hivi ni vikubwa sana. Yawezekana kuna sababu nyingi zinazosababisha lakini sisi wa visiwa vya Unguja na Pemba linajua moja kati ya sababu ni kuondoshwa kwa pasi ya kusafiria ambayo kwa

kiasi fulani ilikuwa kila mgeni anayeingia inajulikana anakwenda wapi, mwenyeji wake nani na atakaa kwa muda gani. Sasa hivi ni vurugu hajulikani anayeingia, wala anayetoka ili mradi ni Mbantu na sura huwezi kujua kwamba unatoka Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Somalia au Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nililolisema lakini jambo zito zaidi kwa nini baadhi ya wahalifu hawa wanaingia katika visiwa vya Pemba na Unguja kwa kutumia boti zenye mashine usiku lakini hakuna doria ya Serikali na kuwakamata wahalifu hawa? Tunapouliza hapa Bungeni tunaelezwa polisi wanashirikiana na vikosi vyote vilivyopo nchini kwa ajili ya ulinzi wan chi yetu. Lakini kama hayo ni kweli mbona ushirikiano huu huonekana siku za uchaguzi tu? Ndio tunaona makundi ya KMKM, Polisi JKU, KVZ, Zimamoto na kadhalika. Ikiwa polisi wanashirikiana mbona boti za KMKM zipo kituoni kuwakamata wahalifu hawa isipokuwa wale wanaosafirisha karafuu tu ndio hukamatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Chuo iliyoko Ziwani Zanzibar, kuna habari za utatanishi kuhusiana na ubadhirifu au wizi wa fedha nyingi zilizoibiwa katika Zahanati ya Chuo cha Polisi iliyopo Ziwani Zanzibar inasadikiwa shilingi milioni 15 zilizopelekwa kwa ajili ya dawa na uendeshaji wa Zahanati hiyo shilingi milioni 12 zimeibiwa au haijulikani zilipo na kupelekea Zahanati hiyo kufungwa. Pia zipo habari kwamba Mkuu wa Chuo hicho anayejulikana kwa jina Maulid Almasi Mabilura ndiye anayeshukiwa kuhusika na upotevu wa fedha hizo.

Pia kuna habari kwamba kuna Tume iliyoundwa kuchunguza upotevu huo iliyomuisha akina *DCI* Kayuga na *RPC* Ameir aliyekuwa Pemba wakati huo. Lakini hadi hivi leo muda mrefu umepita hapajajulikana chochote wala hakuna taarifa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri afanye juhudzi za haraka kabla ya siku ya majumuisho kutupatia ukweli wa suala hili limefikia wapi na hatua gani zimechukuliwa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumpongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu wake, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki na viongozi wengine wa Wizara hii kwa mikakati mizuri ya kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama vilivyoko kwenye Wizara hii kama waliyoionyesha kuititia Bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri kaiwasilisha leo.

Katika kuunga mkono Bajeti hii, napendekeza mambo yafuatayo yapewe kipaumbele. Kwanza kuwa Bajeti ya Wizara ni ndogo, naomba sana Wizara hii iweke vipaumbele vyake kwenye maeneo yenye matatizo zaidi na pia izingatie ukubwa wa Wilaya.

Katika hili, naomba kipaumbele kiongezwe Kahama. Wilaya hii ina watu 800,000 na pia yenye shughuli nyingi za kijamii na kiuchumi, zinazosaidia kuwepo uchumi mzuri kwa wananchi, kama madini (migodi mikubwa ya Bulyanhulu na Buzwagi), Kilimo hasa pamba na tumbaku na mawasiliano hasa uwepo wa bandari ya

nchi kabu Isaka. Hatari ya kuwepo ujambazi ni kubwa kwani watu/wageni ni wengi sana. Kwa sasa naomba Wilaya iongezewe yafuatayo:-

(a) Bajeti ya mafuta, kwa sasa polisi hawawezi kufanya kazi zao vizuri kwa Bajeti ya lita 200 kwa mwezi. Wilaya ni kubwa sana na matukio ni mengi. Mara kadhaa polisi wamekuwa wakilazimisha wananchi waliopatwa na majanga kuchangia mafuta. Hili Serikali ililipiga marufuku hapa Bungeni hivi karibuni. Lakini je, mmeongeza Bajeti? Unapozua polisi wasiombe msaada kwa wananchi bila kuwaongezea Bajeti, je, unataka wafanyeje? Hivi sasa polisi wanatumia zaidi ya saa sita kufika kwenye matukio ya ujambazi! Sababu gari hakuna/mbovu, mafuta hakuna!

(b) Vitendea kazi viongezwe, tunaomba Kahama iwe Mkoa wa kipolisi. Matukio ya uhalifu ni mengi sana na eneo ni kubwa. Tunaomba magari na pikipiki ziongezwe Kahama. Jeshi la Polisi liombe msaada kwa makampuni ya madini yaliyoko Kahama ili yasaidie. Najua Bajeti ya Wizara ni ndogo, lakini ukishirikisha wadau wanawenza kutusaidia.

(c) Idadi ya askari polisi iongezwe Kahama.

(d) Idadi ya vituo vya polisi iongezwe. Naomba, maeneo ya mbali na Mjini Kahama ya Kabondo (Kata ya Kinaga) na Bulige (kata ya Bulige) yajengewe vituo vidogo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iimarishe mahusiano yake na jamii. Kwa sasa kuna tatizo kubwa sana Kahama la Polisi kunyanyasa sungusungu. Polisi Kahama wanatuhumiwa kushirikiana na majambazi. Kila tukio linapotokea, polisi Kahama wanakwenda kwenye tukio na kuwanyanyasa Sungusungu. Aidha, kuna tuhuma kwa Jeshi la Polisi Kahama kushirikiana na wahalifu kuwabambikizia kesi wananchi wasio na hatia, hasa viongozi wa sungusungu. Hivi sasa kuna sungusungu wengi wako mahabusu au wana kesi mahakamani ambazo nyingi ni za kubambikiziwa. Naiomba Wizara ifute kesi zote zinazowahusu viongozi wa sungusungu ambao wengi wao wamembambikiziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana pia Wizara ijizatiti kuondoa tatizo la ujambazi Kahama ambalo linaongezeka kwa kasi. Hivi karibuni, katika kipindi cha miezi sita iliopita, kumekuwapo matukio zaidi ya 30 ya ujambazi. Kwa bahati mbaya, matukio yote yamekuwa yakilenga watumishi, hasa walimu wa vijijini kwa sababu walimu hawakai vijijini Kahama! Hali ya usalama imeanza kuathiri elimu. Naamini matokeo ya mtihani darasa la saba mwaka huu hayatakuwa mazuri kwa sababu ya usalama wa walimu! Naomba sana walimu Kahama walindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba Wizara iboreshe huduma za magereza na mahabusu Kahama. Kama nilivyosema, Kahama ni Wilaya kubwa, watuhumiwa ni wengi, hivyo huduma wanazopata wakiwa mahabusu ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba kusisitiza Wizara itoe majibu kwa hoja zangu zote. Kwa kuwa siwezi kuchangia wala kusimama kwenye vifungu,

naiomba Wizara inijibu walau kwa maandishi (si lazima leo, lakini) nipate majibu nitakayoenda ambayo kwa msingi wa *collective responsibility*, nitawajibika kwenda kuwaeleza/kuwajibu wananchi wangu ambao ndio hasa wanahitaji majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kibaigwa ni mji mdogo unaokuwa haraka, Kibaigwa tuna soko la Kimataifa na biashara kubwa zinafanyika zenye kuhusisha fedha nyingi. Pamoja na yote hayo hakuna kituo cha polisi na jambo hili linafanya Kibaigwa pasijengwe mabenki kwa kukosa usalama.

Kwa kuwa ni miaka kadhaa sasa Wizara inaahidi kufungua kituo hicho cha polisi lakini haifanyi hivyo. Je, ni kwa nini nisisimame wakati wa vifungu kukamata shilingi ya mshahara wa Waziri wa Mambo ya Ndani hapo kesho? Mara kadhaa nimelalamikiwa na vijana *ex-form six police* kuwa wakiomba ruhusa ya kuijendeleza baada ya mkataba wa kazi wa miaka miwili hapewi ruhusa ya kwenda kusoma.

Kuhusu mabasi ya abiria huwa na gia sita, mabasi ambayo ni malori yana gia kumi na mbili je, ajali zitaisha nchi hii? Kituo cha Polisi Kongwa kimechakaa ni cha siku nyingi sana ukarabati ufanywe na nyumba mpya zijengwe.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kupata nafasi ya kuchangia japo kidogo kuhusu hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ya Jeshi la Polisi kwa kweli ni jambo la kushangaza na kusitika kuona kwamba huu ni zaidi ya miaka 40 tangu Uhuru, lakini bado askari wetu (Polisi) hawajapatiwa nyumba kwa ajili ya makazi kwa maana ya nyumba za kutosha zinazokidhi haja kwa wingi na ubora kulingana na mahitaji ya Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kwa sababu gani suala hili la nyumba za polisi linasumbua? Tuseme ni ufinyu wa Bajeti ya Wizara ni kwamba hapana mikakati maalumu au ni suala la kipaumbele katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati sasa Wizara itoe kipaumbele kwa makusudi katika kushughulikia ujenzi wa nyumba zilizobora kwa kila Wilaya ili kuwezesha askari wetu kuondokana kuishi mitaani, jambo ambalo si jema kwa wao kuishi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wahamiaji haramu, suala hili limekuwa likiongozeka mwaka hadi mwaka na inaonekana kwamba tatizo hili sasa limekuwa la dunia nzima. Hapa kwetu kuna aina mbili za wahamiaji haramu, wako wale ambo nia yao ni kukaa hapa nchini na wako wale ambao nia yao ni kukaa kwa muda lakini madhumuni hasa ni kuendelea na safari nao nchi nyingine kama vile Afrika Kusini na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamtaka Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho atueleze ni mikakati gani wameandaa katika kukabiliana na tatizo hili. Kama kweli Serikali imejidhatiti vilivyo kwa hili, kwa nini tatizo hili linaongezeka badala ya kupungua?

Kuhusu mishahara ya Jeshi la Polisi, ni jambo lisilopingika kwa kuwa na mjadala kwa askari wetu wa jeshi la polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa kweli wanastahili pongezi kubwa kwa juhud ya hiyo tunawaomba wasichoke na waendelee na moyo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko ya muda mrefu kwamba mshahara wa askari polisi ni mdogo sana na kutokana na kupanda gharama za maisha. Kwa kuwa tunatarajia kazi nzuri kutoka kwao na kutokana na mazingira yao ya kazi, ipo haja Serikali kuliona hilo na hivyo kuweza kupandisha mishahara yao na hata posho zao za kawaida. Pamoja na kuangalia kupanda kwa maslahi yao, basi suala la kucheleweshwa kwa maslahi hayo lizingatiwe sana kwani nalo linawakatisha tamaa askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa upandishaji vyeo katika jeshi la polisi, kuna malalamiko kuhusiana na suala la utaratibu wa kuwapandisha askari polisi vyeo yaani kutoka nafasi (ngazi) moja kwenda nyingine. Hivi ni vigezo gani (vipi) vinavyozingatiwa katika kuwapandisha vyeo askari wa jeshi la polisi? Napenda kujua ni utaratibu gani unaotumika katika kuwahamisha askari kutoka kituo kimoja kwenda kingine. Maana wako baadhi yao wamekaa muda mrefu katika kituo hicho bila kupata uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya Magereza nchini, hali ya Magereza nchini hairidhishi kwa maana ya majengo yake, huduma muhimu je, ni juhud zipi zinachukuliwa ili kuondokana na mapungufu hayo? Hali ya msongamano wa mahabusu, je sasa ikoje? Muda wa upelelezi wa kesi je, sasa umepungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hali ya wafungwa Magerezani sasa inaridhisha kwa maana ya chakula, malazi na hduma nyingine muhimu? Naomba maeleo kuhusiana na hayo. Ahsante sana.

MHE. ABDALLAH SALUM SUMRY: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shurani za dhati kwako kwa kunipa nafasi ya kuchangia juu ya hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Kego Masha, nampongeza yeze mwenyewe Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maafisa wote wa Wizara *IGP* Mheshimiwa Said Mwema, Mkuu wa Magereza nchini na Maafisa wote wa vyombo vya usalama ndani ya Wizara. Ni Bajeti inayoleta matumaini na usalama wa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza pia Wizara zote tulizopitisha hadi wakati huu Bajeti zao zinaugusa umma, tunawatakia utekelezaji mwema kwa kile walichokipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuishukuru Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi wanazozifanya katika Mkoa wangu wa Rukwa Wilaya yangu

ya Mpanda na katika kata zangu za Karema, Ikola Mishamo na Mwese. Maeneo haya yalikuwa yakisumbuliwa kwa ujambazi mara kwa mara, ushirikiano uliopo kati ya Jeshi la Ulinzi na Polisi katika vituo vyetu vya mpakani vya Karema na Ikola kando ya Ziwa Tanganyika wametusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 na 2006/2007, nilifikisha malalamiko yetu juu ya vijana wetu waliotekwa nyara kule kando ya Ziwa Tanganyika maeneo ya Kawela Mayaga na Kasangatongwe na kupelekwa upande wa pili wa Ziwa Tanganyika huko Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Vijana waliotekwa ni Tunu Wasenka, Saimon Feruzi, Maganga Sokolo, John Paul Kilimo na Gervas Pima. Walipotekwa hao vijana walitekwa pamoja na mali zilizochukuliwa zikiwa na thamani ya shilingi milioni mbili na nusu katika kipindi hicho. Vijana hao walitumiwa kwa kusoza hadi upande wa pili wa Ziwa na hadi leo hii vijana hawajapati, pamoja na ahadi ya Wizara ya Usalama wa Raia na pia Mheshimiwa Inspeksa Jenerali wa Polisi kuahidi kwamba watafuatilia na watapata taarfa ya kina lakini hadi leo hii hakuna taarifa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Wizara hii iweze kutuarifu juu ya hatima ya vijana wetu hao walioko huko. Vile vile ni muda mrefu sasa tangu Wizara ilipoahidi kutoa *speed boat* katika maeneo yetu ya Ziwa Tanganyika hilo halijatekelezwa. Ulinzi ziwani unahitaji *Marine Police* pia *speed boat* iendayo kasi kukabiliana na majambazi ndani ya Ziwa. Ziwa ambalo linautajiri mkubwa wa dagaa na samaki pia ni kiungo cha mipaka ya nchi tatu, Zambia, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Ni wakati sasa wa kuleta mageuzi ya ulinzi katika eneo hili ili watu wetu waweze kutumia fursa ya utajiri iliyomo ndani ya Ziwa hili kama ajira ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliweza kuchangia juu ya shamba la Gereza la Kalilankulukulu ambalo limezungukwa na vitongozi vya wakulima wa Sijonga, Mbogwe, Kamakuha, Ilebula, Ikaka, Gengeni, Wankulu, Kawanzige, Mbugani na Kakese. Shauri hilo nililileta Wizarani kwa maandishi.

Naiomba Serikali kupitia Wizara hii na mwenyewe Mheshimiwa Waziri Masha, wananchi hawa watazamwe ili waweze kumegewa maeneo waweze kutumia kwa kilimo kama walivyokuwa wakutumia zamani kukuza kipato chao ili kuondoa umaskini. Eneo hili lina ukubwa wa hekta elfu kumi sawa na hekta elfu ishirini na tano tangu Gereza lilipoanzishwa hawajalima hata hekta mia moja. Kwa ajili hiyo tunaiomba Serikali kwa makusudi iruhusu wanavijiji hao kutumia ardhi hiyo kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuomba Serikali iweze kuongeza vituo vidogo vya polisi kule kata ya Mpanda Ndogo, Kata ya Katuma na Kata ya Kabungu hususan Kahese ili kupunguza msongamano mkubwa wa huduma hii kutolewa kituo cha polisi cha Mpanda Mjini. Kwani maeneo niliyotaja yana umbali wa kuanzia kilometra sitini na kuendelea. Pia tunaomba msaada wa gari kwa ajili ya huduma ya ulinzi na usalama huko Karema Mwese na Mishano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya ujambazi katika Wilaya ya Ngara. Hali ya usalama wa raia katika Wilaya ya Ngara ni mbaya. Majambazi wamezidi katika Wilaya ya Ngara. Watu wanavamiwa majumbani kwao. Vijiji vya Mururyagira, Mabawe, Ngundusi, Kabanga, Kilushya, Mukikomero watu wengu wamehama toka vijiji hivi kuwakimbia majambazi. Hawa majambazi wengi wao wanatokana na wakimbizi kutoka Burundi. Huko Burundi ni rahisi sana kupata bunduki. Hizi bunduki zinatumika kufanya ujambazi katika vijiji vya jirani na nchi ya Burundi kama nilivyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Serikali ni kwamba polisi wafanye doria ili ujambazi ufutike kabisa katika Wilaya ya Ngara. Kuhusu upungufu wa magari ya polisi Ngara, wananchi wa Ngara wanaomba Serikali ipeleke kwa haraka sana magari kwa ajili ya vituo vitatu vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kabanga Border Polisi Station*. Kituo hiki ni kikubwa na kipo kwenye barabara ya kwenda Burundi. Hapa kuna uhalifu mwingi sana. Wananchi wa Kata ya Kabanga, Kata ya Mabawe na Kata ya Mugoma wanaomba gari ya polisi kwa kituo cha polisi ya *Kabanga Border* ili wawezwe kuwasaidi wananchi wa Kata hizi wakati ujambazi unapotokea.

Rusumo Border Polisi Station, wananchi wa Kata ya Rusumo na kata ya Nyamiyaga na Kata ya Ntobeye wanaomba Kituo cha Polisi cha Rusumo wapewe gari ili wawezze kukabiliana na majambazi katika kata hizo tatu. *Murusagamba Polisi Station*, kituo hiki cha polisi hakina usafiri.

Majambazi wanapovamia Kata za Murusagamba, Uganza na Keza, askari hawa hawana usafiri wa kuwakamata hawa majambazi. Wananchi wa kata hizi tatu wanaomba Serikali iwapatie magari kituo hicho cha polisi cha Murusagamba ili wawezze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magari ya *UNHCR* ya zamani Ngara. *UNHCR* inayo magari ya zamani ambayo wanayauza kwa watu binafsi kwa sababu ofisi yao ya Ngara inapunguziwa kazi. Ombi la wananchi wa Ngara wanaomba angalau magari matatu aina ya *Land Cruiser* wapewe hawa polisi wa vituo hivyo vitatu ambavyo ni Muruasagamba, *Kambaga Border* na *Rusumo Border* ili wawezze kukabiliana na ujambazi ambaeo umekithiri katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *operation* ya kusaka majambazi, kwa niaba ya wananchi wa Ngara naomba marudio ya ile operesheni ilioongozwa na Kamanda Venance Tossi mwaka 2006 irejewe tena. Mwaka huo kikosi maalum cha askari toka Mkoani Kagera waliweka Kambi Ngara wakawashika majambazi wengi na ujambazi ukawa umepungua kwa kiasi kikubwa. Operesheni ya aina hiyo iwe inafanywa mara kwa

mara katika Wilaya ya Ngara ili majambazi wakose nafasi ya kuvamia wananchi wa Ngara.

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongozi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara yao pamoja na kazi nzuri na ngumu ya majukumu yao kila siku wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wa polisi bado wanaishi katika mazingira magumu na wanafanya kazi ngumu zikiwemo za kupambana na wahalifu. Serikali iboreshe makazi ya askari hao kwa kuzifanyia ukarabati wa mara kwa mara nyumba wanazoishi wakati Serikali inachukua jitihada ya kujenga nyumba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna umuhimu wa kuwapatia vitendea kazi (pikipiki, gari, *walk talks, stationeries* na kadhalika). Vituo vingi vya polisi kwa upande wa Tanzania Zanzibar hawana baadhi ya vitendea kazi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufinyu wa Bajeti naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kuweka umeme kwenye jengo wanaloishi askari polisi ambalo kwa miaka mingi jengo hilo halina umeme pamoja na kuwa nguzo ya umeme iko jirani sana na jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kufanya uhamisho wa askari wake hasa wale wa Tanzania Zanzibar kuletwa Tanzania Bara. Zoezi hilo lisiishie hapo liendeleeli ili askari wetu wapate uzoefu mbalimbali katika maeneo tofauti nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa askari wetu wa Jeshi la Magereza husimamia wafungwa ambao baadhi yao watakuwa wameathirika kwa maradhi mbalimbali kwa mfano kifua kikuu, UKIMWI na kadhalika. Je, Serikali ina mpango gani kwa askari ambao wanaishi na kufanyakazi na wahalifu ambao uhakika wa afya zao hazijulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ISSA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Waziri pamoja na Naibu Waziri, vile vile nampongeza *IGP* Ndugu Saidi Mwema kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tabia ya baadhi ya askari hasa *traffic* hawana lugha nzuri kwa wananchi. Ni bora kuwe na taratibu juu ya askari wanaokaa kipindi kirefu kutuoni. Kuhusu utaratibu wa ajira, ni bora utaratibu wa zamani urejeshwe, utaratibu uliotumika mwaka 2008 ni mbovu, kwa sababu ajira ya polisi inahitaji uangalifu mkubwa kwa sababu wanaojiriwa wanahitaji waanzie nchini kuchunguzwa ili wajulikane uaminifu wao.

Mheshimiwa Waziri, naomba unipe maelezo kamili juu ya watumishi wa uhamiajji juu ya malipo ya nyumba wanazopangishwa kulipa kodi na kukatwa asilimia 10

ya mshahara wake wakati wenzao polisi nyumba hizo wanaishi bure. Uhamiaji wanalipa umeme na maji nao wote wako kwenye Wizara moja, naomba maelezo kamili. Naomba nielezwe kwa nini askari wanaoishi Ziwan Polisi ndani ya Boma waweze kulipishwa deni la umeme walilolirithi ndani ya Kambi ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya jeshi la polisi nyumba wanazoishi hazitoshi. Ni bora wakapewa jukumu la kujenga nyumba hizo *NSSF* ili askari waishio kwenye makazi mazuri. Suala la uwekwaji wa askari kwenye kituo kimoja muda mrefu sana na hasa kikosi cha *FFU*. Kwa nini askari anawekwa kikosi hicho muda mrefu bila ya kubadilishwa.

Mheshimiwa Waziri, naomba askari wa vyeo vya chini waangaliwe upya juu ya mafao au marupurupu ili wasiombe kwa sababu maslahi ya Jeshi la Polisi ni madogo, wanashindwa kufanya kazi kwa sababu maslahi ni madogo sana.

Suala la upandishwaji vyeo polisi, utaratibu gani unaotumika kwa upandishaji vyeo vijana wetu wanazo sifa za kupandishwa vyeo. Lakini vijana wanakaribia kuacha kazi bila kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu wa jeshi pamoja na waliofariki kuna ukiritimba juu malipo yao tunayo maelekezo kamili juu ya malipo ukifuatilia unaambiwa faili halionekani hatimaye malipo warithi wanasmabuliwa. Mheshimiwa Waziri, naomba kitengo cha malipo ya wasaafu tumeomba kifunguliwe na Zanzibar ili kuondosha manung'uniko ya malipo yao ili kuepukana na usumbufu wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kukupongezeni kwa jitihada kwa ajili yule askari ameondoka na kuelekea kwenye matibabu India.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, katibu Mkuu, Wakuu wa Idara zote tisa na vitengo sita kwa hotuba yenye mlolongo mzuri wa utekelezaji wa shughuli za mwaka 2007/2008 na malengo ya utekelezaji kwa mwaka 2008/2009.

Mchango wangu utahusu maeneo mawili au matatu, kwanza ni huduma za polisi. Gari kituo cha polisi mji mdogo wa Mlimba, katika Mkutano wa Saba wa Bunge niliuliza swali ambalo lilijibiwa tarehe 13 Aprili, 2007 (Rejea *Hansard* ya tarehe 13 Aprili, 2007 ukurasa 13 – 15).

Katika swali langu ambalo nilieleza taabu, adha wanayopata askari polisi wa mji mdogo wa Mlimba katika Wilaya ya Kilombero, katika kukabiliana na uhalifu kutokana na kuhudumia Kata yenye eneo kubwa pamoja na kata za jirani za Utengule (kilometra 35 kutoka Mlimba), Taweta (kilometra 56 kutoka Mlimba) na Uchindile (kilometra 80 kutoka Mlimba). Kata yenye we ya Mlimba ina vijiji zaidi ya saba ambayo ni Mlimba A, Mlimba B, Matema A na /B (kilometra 18, kilometra 20) Viwanja sitini (kilometra 6), Msolwa (kilometra 8) Kalengero (kilometra 6) Ngwasi (kilometra 10) na Kamwene (kilometra 4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata ya Mlimba ina vitongoji 47 na idadi ya watu wasiopungua 25,000 na kuna stesheni kubwa ya *TAZARA*. Jeshi la Polisi katika kituo hicho halina gari la kuwawezesha kumudu kazi zao kwa ufanisi na huwafuata wahalifu kwa baiskeli katika umbali mrefu. Waziri akijibu swali langu, alitambua umuhimu wa mji mdogo wa Mlimba kuwa na usafiri wa gari kwa ajili ya kuzuia uhalifu. Wakati mimi nauliza swali hali ya gari namba *STJ 974 Land Rover 110* ambalo Waziri alisema tayari amewishalitoa kwa ajili ya kituo cha Mlimba lilishakuwa bovu na halitembe ndiyo sababu ya kuomba gari katika kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri katika majibu yake alikiri kuwa gari hilo ni bovu na ndiyo maana alisema; “kutokana na hali ya gari hilo, jeshi la polisi limelazimika kulifanya matengenzo ili liweze kutoa huduma katika eneo hilo.” Mwisho wa kunukuu.

Aidha, Waziri aliendelea kwa kusema; “Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Castor Ligallama, kuwa kituo cha polisi Mlimba ni moja katika vituo ambayo vitapewa upendeleo maalum mara tutakapopata magari mapya kwa ajili ya vituo vya polisi nchini.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ahadi hizo nzuri ambazo zilishangiliwa na Wabunge wote, wananchi wa Jimbo langu, taarifa nilizonazo ni kwamba ni jana tu tarehe 29 Julai, 2008 ndipo afisa kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi alifika Mlimba na kuomba aorodheshewe vitu vilivyocharibika katika gari hilo takriban muda wa mwaka mmoja na miezi mitatu tangu swali langu lijibiwe kwa matumaini makubwa.

Naomba Waziri anapofanya majumuisho yake awaeleze wananchi wa Tarafa nzima ya Mlimba ni lini watapata gari ya kuhudumia kituo cha polisi Mlimba yaani gari jipya.

Sidhani kuwa tangu niulize swali magari haya hayajaingizwa nchini, nikiwa na maana ya mwaka mzima wa 2007/2008. Afadhali basi gari hilo *STJ 974* lingetengenezwa kipindi kile kile alichoahidi Waziri ningeweza kuelewa kuwa tunasubiri magari mapya kama alivyoahidi Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za uhamiaji. Ofisi ya Uhamiaji Mji wa Ifakara katika Wilaya yangu inashughulikia pia Wilaya ya Ulanga, iko kwenye jengo ambalo ni *condemned*. Jengo lile ni hatari kwa maisha ya wafanyakazi wake ambao wameshanitolea malalamiko nami nililitembelea na kuona jinsi lilivyo. Jengo lina nyufa nyingi, ambapo pamoja na miaka ya nyuma kufanyiwa ukarabati mdogo, bado nyufa zinajirudia kutokana na uchakavu wa jengo lenyewe. Watumishi wanafanya kazi kwa uoga na ningeishauri idara ikodi jengo mahala ili mahala pa kufanya kazi pawe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yale ni ya bomani, katika mji wa Ifakara kuna majengo ya watu wengi ambao wenye wako kwenye miji mikubwa wakifanya kazi au kuna uwezekanao wa kuiomba Idara ya Ardhi ya halmashauri, kutenga Kiwanja kwa ajili ya Ofisi ya Uhamiaji kwa ajili ya kujenga ofisi mpya. Sidhani kwamba kuna tatizo la viwanja katika mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za polisi, dhana ya polisi jamii, dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika jeshi la polisi ni dhana nzuri sana kama itaendelezwa mpaka chini kwenye Wilaya, Kata na vijiji. Kwa sasa dhana hii inatekelezwa zaidi mijini na elimu yake iko zaidi kwa watu wa mijini wenye bahati ya kuwa na luninga na redio. Juzi juzi yametokea matukio ya ujambazi katika Wilaya yangu ambapo Mkandarasi ambaye alikuwa anatujengea barabara ya kilometra saba kwa kiwango cha lami kutoka Kibaoni hadi Lipangalala katika mji wa Ifakara Wilaya ya Kilombero, aliuawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya polisi jamii inafanana kabisa na Sera ya Chama cha Mapinduzi ambapo kwa kutumia wajumbe wa nyumba kumi (Mabaloz) kila mgeni aliweza kufahamika, wapi anatoka, amefuata nini na mwenyeji wake ni nani? Nina imani elimu ya polisi jamii ikisambaa uhalifu nao utapungua. Naisihi idara kama vile ilivyoahidi kuongeza mikoa katika mpango huu ifike mpaka ngazi za chini za kijiji.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Lawrence Masha na Naibu wake kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama ufuatao:-

- (a) Wizara iongeze kasi ya kujenga nyumba za Askari, tatizo ambalo ni la muda mrefu.
- (b) Upandishwaji wa vyeo kwa Maafisa na Askari usiwe upendeleo. Ufuate utaratibu wa kozi zao na wanayopewa. wa mafunzo

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi yafuatayo:-

(a) Jimbo langu la Mbinga Magharibi na hasa kwa mwambao wa Ziwa Nyasa, Askari Polisi wapo Mbambabay pekee. Naomba Askari katika miji midogo ya Liuli na Lituhi ambayo iko mbali sana na mpakani mwa Tanzania na Malawi.

b) Uhamiaji – Mbambabay, naomba Maafisa Uhamiaji katika mji huo, naona ni bandari ambayo inaunganisha Tanzania na nchi za Kusini mwa Africa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Nawapongeza watendaji wote wa Wizara. Pia nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kufanya kazi nzuri na kujituma na kuleta mabadiliko ya kitendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo gani la vitambulisho kupatikana? Hili ni tatizo na ndilo linalochangia kiasi kikubwa kuwasumbua wananchi wanaohitaji kupata

Passport zao, kwani huyu ni Mtanzania haeleweki pamoja na kuwa anapeleka cheti chake cha kuzaliwa na kuapa Mahakamani bado maeneo mengine haeleweki kama ni Mtanzania na kusababisha usumbufu kwa wananchi. Swali:-

- (1) Passport ni bidhaa adimu ya kiasi gani?
- (2) Serikali inaamua/au inatoa kauli gani ambayo ni sahihi kwa upatikanaji wa *passport* hizo kwa wananchi? Naomba taratibu hizo ziwe bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama barabarani. Watendaji wa usalama barabarani hufanya kazi zao kwa wakati mgumu sana na pia hupata matatizo ya kugongwa na magari kulingana na kazi zao lakini wanapofanya wajibu wao huo, wajitahidi kusimamisha magari kwa kufuata sheria pembezoni mwa barabara ili kupunguza ajali hizo zinapotokea wao kusimamisha magari barabarani ni mengi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba wanazoishi Askari. Majengo huko Wilayani na Mikaoani zikarabatiwe na ziwekwe katika mazingira mazuri ya kuishi binadamu kwani mnaweza kufanya majengo hayo kubadilika na kutumia kiwanja kidogo kama yatajengwa magorofa na pia kupata mkopo na kutumia wafadhili mbalimbali kama ilivyo taratibu kwa sasa ninazoziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makazi bora, maisha bora na kazi bora.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Lawrence Kego Macha (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara na wasaidizi wao wote, pia nichukue fursa hii kuwapongeza makamanda wote wa Jeshi la Polisi, Uhamiaji, Magereza na Kikosi cha Zima Moto, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuweka hali ya amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kutoa mchango ufuatao katika kuboresha Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakiri Jeshi la Polisi linalo sura ya kuridhisha sasa kiutendaji, mwonekano huu ni ule wa ngazi ya Makoa Makuu na pengine kwa baadhi ya Mikoa (*RPCs*) fulani fulani, lipo tatizo kubwa sana ngazi ya Wilaya na kuendelea ngazi za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ma-*OCD* wengi, uwezo wao wa kiutendaji ni mdogo sana. Inasikitisha kuona baadhi ya Ma-*OCD* kufunikwa na watendaji wadogo wadogo kimaamuzi mfano, *OCD* wa Iramba. Nathibitisha kwamba *OCD* huyu uwezo wake ni mdogo sana, sina hakika kama angepewa Wilaya yenye matukio makubwa kama angemudu. Inashangaza tukio lolote likitokea, unapajaribu kumuulizia basi yeze anaeleza hajui anasema labda pale kituoni ndio wanajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa sana juu ya maamuzi yanayofanywa tena na Askari wa chini sana aitwae *Detective Ismael*, masuala mazito ya Kiwalaya. Ninao ushahidi juu ya ng'ombe walioibiwa wa mzee Shaban Mohamed wa Shelui. Ng'ombe wale walikamatwa na baadaye alijitokeza mtu kumdhampuni yule aliyejamatwa na wale ng'ombe baadaye yule aliyejamini aliamua kulipa ng'ombe wale tena kwa hati ya Polisi, lakini siku mbili baadaye, Polisi ilibadili uamuza na kumrudia Mzee Shabani, kumtisha awarudishe wale ng'ombe. Ng'ombe walioibiwa ni nane (8) gharama ya usumbufu alifidia ng'ombe wawili (2) na Polisi Shelui ikaamua aongeze wawili (2) kwa ajili ya kituo kama fidia jambo ambalo ni rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya siku tatu, Polisi ile ile tena bila aibu na huku ikiwa imetoa hati ya makabidhiano juu ya wizi wa wale ng'ombe, ikarudi kinyume nyume na kumnyang'anya yule mzee wale ng'ombe tena wakimpa vitisho vyta kumkamata usiku huku wakimwambia watamfungulia mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wziri anipe majibu ya kuridhisha kwa maana ya kumrejeshea yule mzee wale ng'ombe wake na wale Polisi wachukuliwe hatua akiwemo *OCD* na *OC-CID* kwa kuwa ndio vinara wa usimamizi wa matukio yote yaliyojitekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Polisi Iramba imewahi kutoa kibali kwa mmiliki wa gari aina ya wa Kiomboi aitwae Farijalali ili lori lake libebe wanafunzi kwenda Singida kwa ajili ya michezo. Lori hilo lilipata ajali na wanafunzi watatu kupoteza maisha na wengine kujeruhwa vibaya. Polisi hawa akiwemo *OCD* walitoa kibali huku wakijua hilo ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na Polisi wa aina hii ni tatizo kubwa, wameweza kuleta maafa makubwa sana Wilayani Iramba. Kadhalika *OC-CID*, ni mlevi sana na mara nydingi anaanzisha fujo yeeye mwenyewe kutokana na ulevi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nashukuru Magereza Kiomboi kupatiwa gari. Naomba sasa Magereza za Kitibu na zile za Ushara 1 & 2 zipewe gari moja kubwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na kusafirishia kuni kwa ajili ya mahabusu na wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, shughuli ya vitambulisho vyta uraia ni muhimu sana. Umuhimu unatokana na hali ya kutenganisha/ufahamisho wewe ni raia wa nchi yetu hasa kuzingatia na hali ya ushirikiano wa kikanda kama ulivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii nzuri yenye kuleta matumaini kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongozi hizo nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la idadi ya watu hapa nchini, ni vema kungekuwa na mpango maalum wa kujenga vituo vya Polisi kwa kila Kata, pamoja na nyumba za MaAskari angalau watano kwa kila Kata. Hii itasaida kudhibiti uhalifu wa aina mbalimbali kama ujambazi, ulevi wa madawa ya kulevyta, mauaji ya maalbino, uchawi, mauaji ya wazee na kadhalika na kwa kuwa hali ya fedha katika Serikali si nzuri, ingefaa Wizara iruhusiwe kukopa kwa udhamini wa Serikali. Faida ya kujenga vituo hivi ni:-

- (a) Ajira ya Askari itaongezeka;
- (b) Kutapunguza gharama za *operation*; na
- (c) Nchi itakuwa na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa eneo la Chanika limekuwa na wahamiaji wengi, kunahitajika kituo kikubwa cha Polisi. Ofisi husika iwasiliane na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ili watenge eneo la Kituo cha Polisi huko Chanika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana kwa kazi nzuri, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa rambirambi kwa ndugu wa Marehemu Chacha Wangwe, aliyetutoka jana. Mungu ailaze mahali pema peponi, Amen!!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nisiache kumshukuru Waziri na MaNaibu Waziri pamoja na viongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Mungu kwa kutuwezesha leo kuwa katika Bunge hili la leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa huu wa Dodoma, kuna Gereza la Isanga, wafungwa wale wanlishwa na aliyechukua tenda ya kuwalisha wagonjwa hao ni mfanyakishara mmoja ambaye ni *Juwa Company*. Mzabuni huyo alikuwa akichukua tenda katika Gereza la Isanga, lakini mpaka sasa Mkuu wa Gereza hilo la Isanga bado pesa hajjalipwa tangu mwaka 2006 mpaka leo. Kwa hiyo, katika bajeti hii basi amliche pesa hiyo anayodaiwa ambayo ni Shillingi millioni nane na laki sita (8,600,000/=).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna MaAskari wa Polisi ambao walishafariki lakini mirathi yao hajjalipwa, kwa mfano kuna Askari mmoja jina lake P/C Hasani M. Luya, *Force No. – ESSS2*, alikuwa tarehe 27 Mei, 2006, mirathi No.48/1/2001, mwenye kudai mirathi hiyo ni mama yake mzazi na hati zote zinazotakiwa, za mirathi zilikamilika. Mwaka 2006 mimi mwenyewe Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, niliamua kufuutilia suala hilo mpaka Makao Makuu ya Polisi – Dar es Salaam. Nikawasilisha hati zote za Marehemu mpaka nikafika Hazina – Dar es Salaam. Nilikutana na Afande Tomasi na Mande hao ndio wanaoshughulikia mirathi ya

Askari waliokufa. Nimefika mara kadhaa hapo Makao Makuu Polisi na ninakutana nao majibu yao siyo mazuri, mpaka nikachukua jukumu la kufuutilia mpaka Hazina nikokuta taarifa za marehemu zilishafikishwa Hazina tangu tarehe 22/7/2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo wale Askari wakanipa taarifa kwa simu, wakiniarifu kuwa mama yake marehemu aende Hazina Ndogo Kigoma. Yule mama alikwenda lakini hakukuta jina hilo bali ni la Askari ambaye naye alikuwa anaitwa Hasani, Force Number siyo zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo niandikapo hoja hii, hajalipwa mirathi hiyo. Je, huoni kama huo ni usumbufu tangu mwaka 2004 mpaka leo mwaka 2008 hajalipwa, inavyoonekana, cheki hiyo ilishatoka tangu mwaka 2002 na haijullikani ilipopelekwa, je, Serikali inasemaje kwa hilo na ni lini huyo mama atalipwa mirathi hiyo? Au Serikali ndio imeshadhlumu haki ya marehemu? Naomba kama kuna mtu aliyechukua mirathi hiyo achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna Askari waliopigana vita vya Nduli Idd Amini mwaka 1978 –1979, vita vilipokwisha waliolipwa ni wale Askari waliokuwa na vyeo vya juu tu na kwa kuwa kuna vikosi mbalimbali vya Askari vikiwemo na Wanamgambo ambaa ndio walikuwa mstari wa mbele lakini baada ya vita hiyo Mgambo hao waliachwa hivi hivi, badala ya kuwapeleka Jeshi au Polisi Chuoni wakapata mafunzo, waliwaacha bila chochote.

Wale Mgambo waliopigana vita hivyo wanasema Serikali itawasaidiaje? Hali zao ni duni na kwa kuwa kuna Askari Polisi ambaye ni EXC 5299 PC HAMIS, alipigana katika kikosi cha Brigade 207 ya Marehemu Walder (Brack Mamba), Mkuu wa Kikosi 26 KJ akiwa Luteni Kanali Bayeke, Mkuu wa *Support*, Captain akiwa Msabaha – viongozi wote hao walipandishwa vyeo na kulipwa pesa iliyotengwa ya ahsante, lakini Polisi huyu anasema hawakulipwa chochote bali walipewa malimbikizo yao ya mishahara tu!! Wale Askari wote waliotoka *Brigade* ya Polisi hawakulipwa, je, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha na Naibu wake, Mheshimiwa Kagasheki pamoja na timu yao katika kufanikisha hali ya utulivu na amani katika nchi hii.

Mchango wangu leo ni mkubwa kwa kuwa napenda kuwalisha kero na maoni ya wadau wenyewe kama ambavyo waliniandikia kuitia anuani ya hapa Bungeni. Pamoja na kwamba hawakupenda kutaja majina yao pamoja na anuani zao labda kutokana na woga na taratibu ambazo wamepaswa kuzifuata na labda zimekuwa hazizai matunda, wameona wanitumie mimi ili kuhakikisha kuwa ujumbe wao umefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, naomba nikukabidhi maswali yao 23 pamoja na kero zao nikitarajia wao kupata majibu wakati utakapohitimisha bajeti yako, kwa vile majibu yao sina njia nyingine ya kuwfikishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua yao inasema hivi:-

“Mheshimiwa Shikamaoo (Stella Manyanya) pole kwa kazi ngumu ya ujenzi wa Taifa letu kwa ukweli usiopingika ni kweli umekuwa mstari wa mbele katika kutetea maslahi ya Taifa letu.

Awali ya yote, tunapenda kutuma pongezi zetu za dhati kwa kazi kubwa mliyoifanya kuhusiana na suala zima la Richmond. Kwa kifupi tunasema kazi nzuri Mheshimwa imewatia faraja Watanzania wote kwa ujumla bila kujali itikadi za kisiasa na imeonesha kwamba wanawake wanaweza kufanya mambo makubwa wakiwezeshwa.

Baada ya kuongea hayo, Mheshimiwa ngoja sasa tukupe kero na dukuduku zetu, zinazotukabili hususan ni sisi Askari Polisi ambao tumebahatika kupata madaraja mbalimbali ya elimu hususan katika madaraja ya Astashahada, Shahada, *Post Graduate* na Shahada ya Uzamili katika fani zote mfano, Sheria, Elimu, Utawala na Uongozi. Tunakero katika masuala ya upandishwaji vyeo na maslahi nikiwa na maana ya mishahara, malalamiko yetu ni kama ifuatavyo:-

Katika mfumo mzima wa upandishwaji wa vyeo katika Jeshi la Polisi upo mara mbili au tatu. Mfumo wa kwanza ni ule ambao Askari hupandishwa vyeo kutohana na kufanya kazi muda mrefu bila kupanda cheo na hii imefafanuliwa katika Sheria ya Polisi (*PGO – Police General Order*) inayoeleza kwamba bila kujali elimu, Askari atapanda cheo kimoja kwenda kingine ndani ya miaka mitatu (3) ikiwa Askari mlengwa hajashitakiwa kiJeshi.

Mfumo wa pili, ni ule wa upandishwaji wa vyeo ambao unafanyika kwa kigezo cha elimu nikiwa na maana kwamba Askari mara amalizapo mafunzo fulani katika nyanja fulani ya elimu, analazimika apandishwe cheo mfano ngazi ya Diploma, *Advance Diploma, Bachelor Degree au Master*, katika fani zinazoendana na Jeshi la Polisi na kwa mujibu wa taratibu za Polisi. Askari akiwa na elimu ya Chuo Kikuu – Shahada – Shahada ya Uzamili, anastahili kupanda cheo mara tu amalizapo kozi yake na utaratibu huu ndio unaonyika hata kwa Wizara/Idara nyingine za Serikalini.

Sasa mapungufu na kero nyingi zinazoibuka katika mfumo huu wa upandishwaji vyeo kwa vigezo vya elimu ni pale unakuta Askari amemaliza Shahada yake au Shahada ya Uzamili, anatakiwa apandishwe cheo mara amalizapo lakini matokeo yake anawekwa kando unakuta anakaa miaka miwili mpaka mitano hajapandishwa cheo na huku amepata elimu inayostahili apandishwe cheo na hii mara nyingi inatokea pale bosi anayetakiwa akuandikie, anapindisha maeleo na kupelekea kukosa *promotion* pale inapotokea. Huku watu wasio na sifa wa kupata cheo hicho ndio wanapewa ukijaribu kuhoji unaambiwa

wewe unaringia elimu lazima usote kwanza na ikitokea ukipata cheo hicho. Basi utasota nacho hata miaka minne (4) hadi mitano ndio unakumbukwa.

Mheshimwa katika kipengele hiki kuna upendeleo wa hali ya juu sana unakuta wanaopandishwa vyeo ni watoto wa wakubwa au ndugu wa wakubwa kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa katika taratibu za Jeshi la Polisi upandishwaji vyeo kwa kigezo cha elimu unafanyika kwamba kama Askari amepata Shahada yake mara baada ya kusajili vyeti vyake inatakiwa aanze na cheo cha Ukaguzi Msaidizi (yaani *Assistant Superintendent of Police (ASP)*) na kupita utaratibu huu inatakiwa ndani ya miaka minne – mitano, msomi huyu wa Polisi awe amefikia ngazi ya *Assistant Superintendent of Police (ASP)* kutoka kwenye cheo cha Ukaguzi Msaidizi yaani *Assistant Inspector (A/I)* lakini matokeo yake utaratibu huu haufanyiki ila unapindishwa na kupeleka Askari asiyestahili kupandishwa vyeo kutohana na urasimu huu wa kutowajali wasomi ndani ya Jeshi la Polisi husababisha matokeo yafuatayo:-

Ndugu Mheshimiwa napenda kwanza kukueleza kwamba Polisi hawa wasomi wanajisomesha kwa gharama zao wao wenyewe kupitia vijimishahara vyao wenyewe. Sasa katika hali hii, inapelekea kushuka kwa ufanisi na utendaji mzima wa kila siku wa Jeshi la Polisi kwa sababu mtu anajiuliza kuna haja gani ya kuongeza ufanisi wakati sijaliwi wala kuthaminiwa. Kwanza nimekopa, nimeuza vitu vyangu vya thamani ili nikapate *degree* nije niongeze ufanisi ndani ya Jeshi matokeo yake sipandishwi cheo kama matarajio yangu niliyoyapanga kutohana na ukweli kwamba upandishwaji cheo huenda sambamba na upandaji wa mshahara.

Ndugu Mheshimiwa matokeo ya pili ya kutopandishwa cheo kwa wakati, hupelekea vijana au Askari wengi wasomi kuacha kazi kwa sababu Askari huyu msomi anaona hakuna maana ya kusoma ukiwa ndani ya Jeshi la Polisi kwa sababu ya kutothaminiwa ni bora mtu aende kutafuta kazi sehemu nyingine ambapo atapata maslahi mazuri yatakayomfanya yampe motisha na kufurahia kazi yake. Mfano hata ingekuwa ni wewe una Shahada/Shahada ya Uzamili unalipwa mshahara wa Tshs.113,550/= wakati kuna ofisi nyingine analipwa T.Shs.300,000/= . Sasa ni kweli utaendelea kung'ang'ania hapo kweli? Kwanza mazingira ya kazi ni magumu halafu lawama ni nyingi sana. Sasa kutohana na Askari kuacha kazi kwa wingi inapelekea nguvu kazi kupungua (*shortage of Human Resources*) kwa kiasi kikubwa na matokeo yake ni kushuka kwa ufanisi na utendaji na hapo ndipo utendaji wa kimazoea unapoibuka kwa sababu *competent personnel* wameondoka na nguvu kazi iliyobaki kwa kiasi fulani inashindwa kukabili changamoto zinazoibuka hususan katika kipindi hiki cha utandawazi, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa kwa tafiti tulizofanya ndani ya Jeshi la Polisi wanaothaminiwa, ni wale Askari ambao wamesoma Cheti cha Sheria miezi tisa, sasa Mheshimiwa hivi inaingia akilini kumpa kipaumbele mtu mwenye Cheti cha Wheria au Cheti cha kozi nyingine ukaacha mtu/Askari mwenye Shahada au Shahada ya Uzamili? Sasa kwa udhaifu huu, unafanya Askari wasomi ndani ya Jeshi kuacha na kutafuta sehemu

nyingine kwa sababu mtu hawezi kukubali kuona bosi ana cheti cha kozi fulani ambazo amesoma miezi sita (6) mpaka nane wakati Askari amekwenda kusoma miaka kati ya mitatu mpaka mitano (5) na sio hivyo tu unakuta hawa mabosi wenye ngazi ya cheti wanaowaongoza hawa wenye Shahada/Shahada za Uzamili wakijitamba na kutoa maneno ya kejeli kwamba pamoja na kupata madigirii yenu, mtakuwa chini yangu na mshahara nawazidi. Sasa katika mazingira haya, hata ukimpelekea bosi *Transcript/provision result statement* ataweba kuisoma? Matokeo ni Askari wasomi kuacha kazi.

Mheshimiwa kwanza mazingira ya kazi ni magumu sana unakuta huyu Askari mwenye elimu anapewa kazi za kumkatisha tamaa kuendalea na Jeshi, mfano kutokana sasa na nguvu kazi kupungua baada ya Askari kuacha kazi, unakuta Askari wawili au watatu wanasantikiza mahabusu wa mada kesi kama thelathini (3) kwa umbali wa urefu wa kilomita 50 – 102, wewe niambie ni hatari ilioje? Halafu hauthaminiwi matokeo yake unaambiwa unaringa kwa sababu una digrii au *masters*. Sasa katika hali hii, je, uzalendo utakuwa nao? Huku unaona mwenzako uliyemaliza naye chuo yupo katika nafasi nzuri na mazingira ya kazi ni mazuri sana.

Ndugu Mheshimiwa, sikitiko letu ni kwamba vyeo vinatoka kwa upendeleo, undugu, ukabila, sio kama tunaongea majungu ndio hali halisi, urasimu umejaa ndani ya Jeshi na upendeleo ambaa hauna mantiki na manufaa yoyote. Hivyo basi Mheshimiwa tunaomba kero hii uifuatilie na uhakikishe inapatiwa ufumbuzi wa haraka wa muda mfupi, wakati mrefu ili kuongeza ufanisi ndani ya Jeshi letu kwa kuondoa huu udhaifu wa kupandishana vyeo kwa kujuana kwani ni hatari sana kwa sababu hata utendaji wa kazi utapungua.

Ndugu Mheshimiwa tunaomba kupitia huu mfumo wa pili wa maboresho ya utumishi wa umma suala la *professionalism* ndani ya Jeshi uangaliwe kwa mapana na mrefu kwa mfano kuwe na tofauti ya malipo kati ya Askari na Taaluma au elimu ya Chuo Kikuu/Vyuo Vikuu vinavyotambulika na Serikali. Mfano utakuta Askari X – elimu ya msingi au sekondari na Askari Y mwenye elimu ya Chuo Kikuu hawa wawili (2) utakuta wanacheo sawa na mshahara sawa sasa, je, kwa hali hii ni uungwana? Tunaomba Mheshimiwa ulishawishi Bunge, Wizara ya Mambo ya Ndani, Ofisi ya Rais Utumishi kwamba Askari walipwe kutokana na elimu kama ilivyo kwa Idara na Wizara nyingine za Serikali na hii inaweza kuingizwa kupita Tanzania *Police Force Reform Program* ambayo yanaendelea kufanyika.

Ndugu Mheshimiwa, hivi kweli ni halali mtu umesota kwa miaka mitatu – mitano, unapata Shahada na ukichukulia ugumu wa masomo halafu ukija kuripoti unawekwa kanda halafu hauthaminiwi hata kidogo huku ukipata kejeli kutoka kwa wenye vyeo wasio na taaluma wakidiriki kusema kwenda kusoma ni kiherehere watu hatusomi na vyeo tunalingana na mshahara pia sasa kwa hali kama hii ni kweli tutafika?

Mheshimiwa jambo lingine la kushangaza na kusikitisha ni kwamba Jeshi letu la Polisi lina vyuo vyake vitatu – Chuo cha Polisi Moshi (*CCP*), Chuo cha Maafisa cha Dar es salaam na Chuo cha Zanzibar, utakuta Walimu wa vyuo hivyo wengi wao wana elimu

ya Astashahada na Shahada ni wa kuhesabu na watu hawa wenyewe elimu hizi utakuta wanawafundisha watu/Askari wenyewe Shahada mbalimbali pindi waendapo kwenye mafunzo sasa Mheshimiwa, hii si fedhea iliyopitiliza? Wewe mtu ume-*graduate* labda Shahada ya Sheria, *Administration* halafu ufundishwe miezi sita – tisa na mtu mwenye elimu ya cheti kweli si dharau ya hali ya juu na si hivyo bali ni kudhalilisha taaluma na chuo husika mtu ulichosomea hiyo Shahada yako.

Sasa matukio haya mtu akiyaunganisha unakuta anaamua kuacha kazi na aishii hapo Walimu hawa hujitapa kwa kusema tuna vyeti lakini tunafundisha watu wenyewe *Degree* zao pamoja na *Masters*. Je, Mheshimiwa unaridhika na hali hii? Ni tatizo hili linasababishwa na *poor human resources planning* kwa sababu kama kuna *clear human resource planning* huwezi kukuta udhaifu kama huu.

Mheshimiwa jambo la kushangaza, Askari wanajisomesha kwa gharama zao wenyewe kwa ngazi ya digrii lakini tunachojiliza mbona Idara nyingine za Serikali, wafanyakazi wao wanasomesha na Idara husika iweje sisi Polisi tujisomeshe bila kurudishiwa gharama zetu? Halafu matokeo yake wanasemwa hakuna kuacha kazi, sasa nimejisomesha mwenyewe, cheo sipandishwi kwa wakati, nanyanyaswa na watu wenyewe vyeo na elimu yao kiduchu, sasa kwa nini nisiache kazi na niende kutafuta sehemu nyingine?

Mheshimiwa, tuna mambo mengi ya kukueleza ili uyafakishe Bungeni na Wizara husika lakini kwa leo ngoja tukupe hayo tunategemea uyafakishe Bungeni mwezi wa nne – sita kwenye vikao vyenu, hii imetulazimu tukutumie wewe kwa sababu tumefarijika katika hotuba yako uliyolezea kuhusu mambo ya Utumishi wa Umma na jinsi mambo yalivyo kwenye Utumishi wa Umma (udhaifu wa viongozi).

Mheshimiwa, tunaomba kwa niaba yetu utuulizie maswali haya na kupatiwa majibu katika Bunge letu Tukufu.

(1) Je, kwa Askari ambao wamejisomesha *Degree* kwa gharama zao, Serikali (Wizara) ina mpango gani wa kuwarudishia gharama zao kama si zote hata nusu?

(2) Hadi kufikia leo, je, Jeshi la Polisi lina Askari wangapi wenyewe elimu ya Shahada (*Bachelor Degree*) na je, ni Askari wangapi wenyewe Shahada ya Uzamili (*Masters*)?

(3) Je, kati ya Askari wenyewe elimu hizo tajwa hapo juu hadi kufika leo ni Askari wangapi wameacha kazi kutokana na mazingira magumu ya kazi?

(4) Je, kipindi kati 1998 – 2008, ni Askari wangapi wamepata elimu za Vyuo Vikuu vinavyutambulika na Serikali? Je, kati yao ni wangapi wameacha kazi?

(5) Je, Askari hawa ni kwa nini wameacha kazi baada ya kutoka vyuoni?

(6) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hawa Askari wanarudishiwa gharama zao waliojisomesha vyuoni?

(7) Je, uongozi wa Jeshi la Polisi, lina mipango gani ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya kuhakikisha Askari hawa waliomaliza vyuo wanapewa vyeo kulingana na elimu kwa wakati kama ilivyo kwenye Idara nyingine za Serikali?

(8) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wahitimu hawa kati ya 2005 – 2007 baadhi yao kutopandishwa vyeo?

(9) Je, Jeshi la Polisi kupitia *promotion board* ina maelezo gani ya kulishawishi Bunge kuhusiana na udhaifu walioufanya na kupelekea Askari wengi kuacha kazi baada ya kukosa promosheni?

(10) Je, Serikali (Wizara ya Mambo ya Ndani), ipo tayari kuwapandisha vyeo Askari hawa vyeo na pamoja na malimbikizo ya vyeo ambavyo walistahili kuwa navyo?

(11) Je, hadi leo hii ni Askari wangapi ambao wapo masomoni katika ngazi ya Shahada na Shahada ya Uzamili au Uzamivu?

(12) Je, Serikali ipo tayari kusomesha Askari ambao wanataka kusoma Shahada ya Pili, ndani na nje ya nchi?

(13) Je, ni Askari wangapi ambao wameomba ufadhili wa Wizara kwa ajili ya kusoma *Masters* nje na ndani ya nchi? Kama ni ndani ya nchi ni vyuo gani ambavyo wameomba?

(14) Je, uongozi wa (Jeshi la Polisi unaweza kutueleza ni kwa nini vijana/Askari wengi wasomi wanaacha kazi?)

(15) Je, Wizara ina mpango gani wa kuanza kuwalipa Askari kutokana na taaluma zao? Je, kama kuna mpango kama huu ni lini mpango huo utaanza kutekelezwa, hususan ni hawa *graduate*?

(16) Je, uongozi wa Jeshi la Polisi upo tayari kubadilika kiutendaji kutoka kwenye utendaji wa kimazoea na kutumia mfumo mpya wa kisasa kupitia *Tanzania Police Force Reform*?

(17) Je, Wizara ipo tayari kuwaomba radhi Askari hawa kwa kutopandishwa vyeo kwa wakati kutokana na taaluma walizozipata vyuoni?

(18) Je, huu mpango wa Askari wanapostaafu na kuomba mkataba mpya hasa unahusisha Askari wenye vyeo vipi?

(19) Je, ni kwa nini Askari wenyе vyeo vya *OCD, OCS, RPC* na wasipewe mikataba? Je, kama wanapewa ni mkataba wa miaka mingapi?

(20) Je, kuanzia mwezi wa saba mwaka huu ni *OCS, OCD's* na *RPC's* wangapi wanaotegemea kustaafu? Je, kati ya hao ni wangapi wamepewa mikataba?

(21) Je, Serikali ipo tayari kuwaruhusu Askari hawa kuhamisha ajira kwenda sehemu nyingine ya Idara ya Serikali?

(22) Je, ni maofisa wangapi wa Polisi wenyе vyeo vya *ASP, SP, ACP* ambao wapo masomoni nje kwa kozi za *Master's*?

(23) Je, Serikali (kupitia Jeshi la Polisi), lipo tayari kuwatunuku vyeo Askari ambao wametoka masomoni kuwekwa kando kama sehemu ya kuwafariji kuwa kutopewa kwa cheo kwa wakati?

Mwisho tunapenda kukutakia kazi njema kwa ujenzi wa Taifa letu. Tunatarajia ujumbe wetu utatufikishia kwa wahusika nasi kupatiwa majibu.

Ni sisi Askari wako watiifu.

NB: Mheshimiwa ikumbukwe tumeandika barua hii kwako si kwa kumpiga mtu majungu, la hasha, bali tumeeleza udhaifu uliopo, hatuna chuki wala nia mbaya na mtu yeoyote”.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kuwashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara, kwa kazi kubwa ambayo wamefanikisha kuandaa mpango wa bajeti ya 2008 – 2009 ambayo ikipitishwa na ikatekelezeka, itaongeza ufanisi na utendaji kazi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuchangia katika Wizara hii kwa kuzungumzia uingiaji holela wa wageni kutoka nje katika nchi yetu. Kwa kweli, nchi yetu ina wageni wengi sana toka nje ambao huingia nchini kiholela na wengine huingia kwa utaratibu lakini muda wao unapoisha hubakia nchini na hakuna anayewafuatilia wala kuchukuliwa hatua kitu ambacho kwa Mtanzania anapoenda nje hufuata taratibu na wachache ambao wamekuwa wakienda kinyume, wamekuwa wakipata matatizo makubwa na tumeshuhudia wengine wakirudishwa nchini. Je, ina maana sisi sheria yetu ina upungufu kiasi kwamba tunashindwa kuwabaini hawa wageni na kuwachukulia hatua? Au kuna upungufu wa kiutendaji katika mipaka yetu? Au mipaka yetu inaingilika kiholela? Naomba Wizara ichukule suala hili kwa uzito mkubwa sana kwani hata baadhi ya matukio ya ujambazi, mengine wao hushiriki kwa kushirikiana na wenyeji wao hata kuhujumu uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya 2007 – 2008, Wizara iliahidi kuboresha shughuli zake hasa kwa kuongeza vitendea kazi. Nichukue nafasi hii, kuipongeza Wizara kwa kuboresha vifaa vya usafiri hasa katika Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza, ni muhimu sana lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, mishahara midogo, hawana marupurupu, nyumba za kuishi katika Magereza nyingi nchini hasa Mtwara pale Lilingu, Newala na Masasi ni chache, mbovu zimepitwa na wakati na Askari wengine hulazimika kupanga nyumba za raia. Wizara haioni kwamba kwa kuwatumia Askari wenyewe fani ya ujenzi na wafungwa, Serikali ingetenga bajeti na kushirikiana na Halmashauri husika kuanza kujenga nyumba za kisasa na zenye hadhi ili kuboresha hadhi ya Askari na kuwaondolea adha wanayoipata hivi sasa? Pia katika kuboresha maisha yao kwa nini wasiwe wanalipwa fedha ya usumbufu hasa wanapofanya kazi za nje hasa au wanapowasimamia wafungwa katika kazi za nje?

Kwa mfano, kilimo, kukata kuni, anapolazwa mfungwa hospitalini na kadhalika. Naomba hili kwa sababu mfungwa akilazwa Askari hulazimika kuwepo hospitalini kwa ulinzi hivyo na yeze huwa kama ni mgonjwa, akienda kukata kuni au kuwasimamia kilimo, nao hulazimika kushinda juani kutwa, mvua ikinyesha nae hunyeshewa lakini mfungwa akitoroka Askari huyu huwajibishwa, hivyo naona iko haja kwa Askari hawa wawe na malipo ya ziada wanapokuwa katika majukumu kama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie pia katika Jeshi la Polisi, nao pia wana majukumu makubwa sana lakini mazingira yao ya kuishi hayatofautiani kabisa na Askari Magereza. Hivi ni kwa nini Askari aishi uraiani ni kweli tumeshindwa kuandaa mpango mzuri wa kuhakikisha tunakuwa na nyumba za kutosha? ufile wakati tatizo hili litatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara hii kwa kukabiliana na matukio ya ujambazi nchini hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa matukio hayo na kuendelea kusimamia usalama wa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitengo hiki, maelekezo makubwa au usimamizi wa mara kwa mara kwa Askari wa Barabarani (*Traffic*), kwa kweli hawa ni tegemeo kubwa katika kusimamia usalama wa barabarani ili kupunguza ajali za barabarni na ulinzi kwa ujumla lakini wamekuwa kero kubwa barabarani. Wamekuwa wakijali maslahi haramu wanayowatoza madereva wenyewe makosa na kuingiza mifukoni mwao na kuwaacha madereva hao wakiendelea kutenda makosa, kuendesha magari mabovu na kadhalika. Tunaomba sana Askari hawa warudi katika maadili ya kazi na kuwajibika ili kuleta imani, matumaini kwa wananchi ili kuondokana na matatizo wanayopata madereva na abiria wawapo safarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kutayarisha na kuwasilisha bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza watendaji wako wote wa Wizara kwa kazi nzuri hasa kupunguza uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri kwa vituo vya mipakani – Wilaya ya Karagwe. Tunaomba vituo vilivyo mpakani na Uganda na Rwanda, vikihudumia maeneo makubwa na mbali sana toka makao ya Wilaya, wapewe usafiri wa angalau pikipiki kwa kila kituo. Vituo hivi ni Murongo, Kaisho na Rubwera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa Kituo cha Polisi – Kaisho. Tunaomba kituo hiki kifanyiwe ukarabati.

Naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, IGP na viongozi wote wa Wizara na taasisi zake, kwa hotuba nzuri sana, naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri katika maeneo matatu yafuatayo:-

(1) Wizara inatoa maelekezo gani kwa kata ambazo zimejenga, zinajenga, zinapanga kujenga *police posts* kama vile vya Mlola na Kwai ambavyo vinaomba Askari vianze kutoa huduma?

(2) Ni lini Wizara itatekeleza ahadi yake ya kujenga ofisi mpya ya Polisi Lushoto badala ya magofu yaliyoachwa na Wajerumani yaliyopo?

(3) Ni lini Wilaya ya Lushoto itapatiwa gari, zana na Askari wa zimamoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Lawrence Masha, (Mb,) Waziri na Mheshimiwa H. Kagasheki (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalamu mbalimbali wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri na mikakati mizuri ya kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka rasmi kwamba ninaunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaelekeza katika mambo yafuatayo:-

(1) Tatizo la usafiri wa gari la Polisi Karogwe. Korogwe ni Wilaya yenye matukio mengi ya uhalifu, hali ya usafiri hairidhishi kabisa – Polisi wangu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Bila kuwa na gari la uhakika, hawezu kufanya kazi kwa ufanisi. Ninaomba kupatiwa gari. Ninasisitiza Korogwe ni mahali nyeti sana kupatiwe gari la uhakika.

(2) Majengo ya Polisi Korogwe. *OCD* Korogwe hana nyumba. Mkuu wa Kituo cha Polisi Korogwe hana nyumba. Sio sahihi kwa *OCD* kuchukua nyumba ya Mkuu wa Kituo. Ninaomba Polisi wajenge nyumba ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya. Hii yote imeletwa na *OCD* aliyeama kununua nyumba ya *OCD*. Aidha pia ninashauri nyumba za Polisi na Afisa Magereza Korogwe zijengwe mpya. Hali ya nyumba za Polisi na Magereza Korogwe zinatisha hazifai.

(3) Bado lipo tatizo sugu sana la upelelezi wa watuhumiwa kuchukua muda mrefu hebu jitihada zifanywe kwa upelelezi uchukue muda mfupi. Upo mrundikano wa mahabusu wengi sana Magerezani hasa Korogwe.

(4) Vituo vya Polisi. Kwa muda mrefu nimeshauri Kituo cha Polisi kata ya Mashewa Mjini kiimariswa na kipatiwe usafiri. Eneo hili ni la machimbo Kalalani mara kwa mara kunatokea matukio mabaya ya uhalifu, lakini matukio hayo yanapotokea inakuwa vigumu sana kupata huduma ya haraka kutokana na umbali. Ninashauri Mashewa paimarishwe.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hotuba ya Waziri kwa hotuba yake nzuri. Wizara hii ni ngumu sana kwani kuna mambo mengi yanayotokea kuleta hali ya amani na utulivu nchini siyo kazi rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wana kazi ngumu kupambana na wahalifu wengi wanaotokea kila siku. Mafanikio yanaonekana kila majambazi wanapokamatwa hata wakati mwingine kuuwawa. Wananchi wanategemea Jeshi la Polisi kwa ulinzi wao na mali zao ambao wameutekeleza kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuelezea kwamba Jeshi la Polisi likishirikiana na wananchi wahalifu hawatashinda kwa uhalifu wao kwani wananchi watatoa taarifa mara watakapoonekana.

Napenda kutoa baadhi ya matatizo yaliyoko kwenye Jimbo langu:-

(1) Kwanza eneo la mpaka toka Rombo mpaka Lake Natron ni eneo la Longido, kituo kilichoko Namanga ni mbali sana na ukanda wa Lake Natron. Kwa hiyo, naomba Wizara yako kumalizia kituo cha Gilay Lumbwa kwani imejengwa muda mrefu bila kumalizika ili wananchi wapate ulinzi eneo hilo.

(2) Wilaya ya Longido ni mionganini mwa Wilaya mpya kabla ya kuundwa Wilaya makao makuu ilikuwa Monduli. Kwa kuwa tumepata wilaya, naomba Wizara yako waweke Wilaya ya Longido kwenye mipango ya kujengewa Makao Makuu ya Polisi kwani ni Wilaya mojawapo ya Wilaya.

(3) Kituo kidogo cha Kamwanga ambayo kimejengwa na wananchi. Kituo hiki kimejengwa kabla ya barabara ya lami kufika kijiji cha Kamwanga lakini kwa sasa kituo hicho kinabomolewa kupisha barabara hiyo kujengwa. Naomba Serikali watakapotoa fidia fedha zitolewe kwa ajili ya kujenga kituo kingine kipyaa kwani kuna

umuhimu mkubwa kuwa na kituo hicho kwani kuna uhalifu mkubwa sana kutokana na eneo hilo kuwa mpakani.

(4) Napenda kueleza kwamba eneo la Longido ni kubwa na kuwa ni Wilaya ya pembezoni na mpaka mrefu wa Kenya na Tanzania na kuwa na njia nyingi za panya. Naomba Polisi waongezwe kwenye vituo vya Polisi vilivyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja, ahsante.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha bajeti ya Wizara humu Bungeni. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia.

(1) Hali mbaya ya Kituo cha Polisi Vwawa – Mbozi. Hivi karibuni niliuliza Serikali kuhusu ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Vwawa, Wilayani Mbozi pamoja na nyumba za kuishi Askari. Hata hivyo, majibu ya Serikali hayakuwa ya kuridhisha kwani niliambiwa kwamba kituo hicho hakijatengewa pesa kabisa kwa mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Serikali iliwahi kutoa tamko hapa Bungeni kwamba kituo hicho kipo kwenye mpango wa miaka mitano wa kukarabatiwa, sasa ni miaka miwili tangu tamko hilo, hakuna kinachoendelea, inasikitisha! Kwa mara nyingine tena namwonga Waziri anieleze ni lini sasa kituo hicho pamoja na nyumba za Askari ambavyo vipo kwenye hali mbaya sana vitakarabatiwa. Vinginevyo sitaunga mkono bajeti ya Wizara hii kama sitapewa majibu ya kuridhisha.

(2) Gari na pikipiki kwa vituo vya Polisi. Nchi hii ni kubwa sana kwa maana ya idadi ya watu na eneo. Kwa msingi huo, hata mtandao wa Vituo vya Polisi, ni mkubwa sana. Wilaya ya Mbozi yenye jumla ya wakazi 600,000 kata 26, tarafa 6 na eneo la ukubwa wa kilometra za mraba zaidi kidogo ya 9000 ina Vituo vya Polisi zaidi ya vitano (5). Pamoja na yote hayo, Wilaya kubwa namna hiyo ina vifaa vichache sana vya kazi na hususan magari na pikipiki. Wilaya ina magari yasiyozidi matatu na hivyo kufanya utendaji wa kazi hasa za ufuatiliaji na uchunguzi kuwa vigumu sana. Wizara ione namna ya kuipatia Wilaya (Polisi) magari na pikipiki kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi.

(3) Rushwa Polisi wa *Traffic*. Pamoja na kazi nzuri ambayo Askari Polisi wa Kikosi cha Barabani wanafanya, lakini kazi yao nzuri huchafuliwa na Askari wachache wanaodai rushwa kwa Madereva wa magari yale ya abiria na mizigo. Magari mengi yanayotembea barabarani siyo mazuri sana “not worth road going”, hata hivyo, kwa sababu ya tamaa ya MaAskari wetu, hupokea rushwa na kuachia magari hayo yatembee baada ya kupewa kitu kidogo yaani rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na viongozi wa Jeshi la Polisi, kukomesha hali hiyo, bado jitihada hizo hazijazaa matunda mazuri. Nashauri wazidishe jitihada hizo, aidha, Askari *Traffic* wanaokamatwa na kutuhumiwa kupokea rushwa wafukuzwe kazi mara moja. Jambo la msingi zaidi ni kwamba *Askari Traffic* wa

Barabarani wasikae kwenye kazi hiyo muda mrefu ili wasijijengee himaya kwa kuzoenana na Madereva wa magari kupita kiasi.

(4) Gereza la Mbozi liimarishwe. Mapema mwaka jana nilitembelea Kituo cha Gereza Mbozi na kujionea hali halisi ya Gereza. Jambo muhimu linalohitaji kufanyiwa kazi mapema ni kusakafia ukuta. Ukuta wa Gereza ambao umejengwa kwa tofali na matope. Ilivyo ni rahisi sana kwa wafungwa kuchimba ukuta na kutoroka. Hivyo basi ili kuzuia hali hiyo isijitokeze, naomba Wizara itengete pesa kwa ajili ya kuimarisha ukuta wa Gereza Vwawa – Mbozi. Aidha, Wizara itengete pesa za kuliwezesha Gereza kusambaza umeme (taa) kwenye ukuta wa Gereza kwa kufanya hivyo tutafanya hata kazi za Askari wetu kuwa rahisi zaidi.

(5) Ulinzi Shirikishi Jamii. Ni wazi kwamba Askari Polisi tulionao nchini, hawezi kuhakikisha kwamba wakati wote kwa usalama wa wananchi na mali zao nchini kote. Askari wetu ni wachache na wanazidiwa.

Dawa pekee ya kuimarisha ulinzi kwa wananchi wetu na mali zao ni kuhakikisha kwamba ulinzi shirikishi unaimarishwa zaidi, pamoja na jitihada za viongozi wa Jeshi la Polisi kusisitiza sana ulinzi wa namna hivyo. Ni vema viongozi hao wakausimamia mpango huo kwa nguvu zao zote. Hivyo, ndiyo pekee ambayo itahakikisha kwamba jamii yetu tnakuwa salama zaidi. Ahsante sana.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imejipanga vizuri juu lakini kuna matatizo mengi ngazi za chini. Jeshi la Polisi halijamudu kuendana na wakati hasa zama hizi za utawala bora na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi bado wanalamikia maonevu, rushwa na unyanyasaji kutoka Jeshi linalopasa kuwalinda wao na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu bandia (*artificial shortage*) ya Askari Polisi kunakoletwa na Serikali kutoajiri Askari wa kutosha ili kulinda raia na mali zao. Hakuna sababu ni kwa nini Serikali isiajiri Askari wa kutosha wakati mwaka uliopita wa fedha (2007/08) Shs.3 billion zililipwa kwa watumishi hawa! Vijana wengi wanamaliza JKT na kukaa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ratio* ya Askari kwa watu anaowahudumia hapa Tanzania, ni Askari mmoja kwa watu 1,339 wakati nchi zinazojali utawala bora ni Askari mmoja kwa watu 400 kwa mwaka. Je, Askari wa Tanzania atamhudumia nani vizuri na amwache nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, '*Artificial shortage*' hii huwanufaisha MaAskari kwa sababu wananchi hununua kipaumbele cha kupata haki na hivyo wenye uwezo ndiyo wanaohudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Upelelezi (*CID*), ni Idara inayopaswa kubeba lawama nyingi kwa kuhodhi haki, rushwa na maonevu kwa wananchi. Wananchi wanakosa imani na Jeshi la Polisi na wamefikia hatua za kujichukulia Sheria Mikononi

(*Mob Justice*) kwa sababu haki huchelewesha kuanzia Kituo cha Polisi na Upelelezi huchukua muda na wamefikia hatua za kujichukulia sheria mikononi (*mob Justice*) kwa sababu haki huchelewesha kuanzia Kituo cha Polisi na upelelezi huchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kwa *case zifuatazo*:-

(1) Kituo cha Polisi Manyoni:

Mwalimu Abraham Mika Mongo wa shule ya msingi Mgandu ambaye alikamatwa na Polisi nyumbani kwake tarehe 4/5/2007 saa mbili asubuhi na Askari kutoka Manyoni. Akawekwa chini ya ulinzi, akasafirishwa katika gari la Polisi PT.0845 LR.110 lakini kabla ya kufika Manyoni, gari likapinduka na mtuhumiwa kuvunjika mguu. Wote, Askari watatu na mtuhumiwa, wakapelekwa hospitali ya Mt. Gaspar Itigi, wale Askari walitibiwa wakaruhusiwa siku hiyo hiyo akiwemo Afisa Upelelezi wa (W). Lakini mtuhumiwa ndiye aliyeumia zaidi na akalazwa na kuwekewa POP (2 months). Kabla Afisa Upelelezi hajaondoka hospitali alipita kumwaga mtuhumiwa kuwa akimaliza matibabu basi aende nyumbani!

Baada ya kupata ahueni kidogo, Bwana Abraham Mika Mongo, aliona ni vyema aende kituoni akajue sababu ya yeye kuwekwa chini ya ulinzi mkali na Askari watatu wenyе silaha na ni kwa nini baada ya kupata ajali alitekezwa. Alipofika kituoni akaambiya kwamba walikosea kwa sababu picha waliyokuwanayo inafanana na sura yake. Huyo aliyekuwa anatafutwa alikopa vifaa vya ujenzi M/S Tunakopesha Ltd – Dodoma, hivyo yeye hakuwa na kesi aende nyumbani.

Ndipo Bwana Abraham alipoanza kudai fidia kwa kilema alichopata na gharama za matibabu, nauli, posho za St. Gaspar na Muhibili. Hata mwajiri wake Halmashauri ya (W) Manyoni alimwonea huruma akagharamia sehemu ya safari zake za kwenda Muhibili kwa matibatu zaidi. Hadi leo hii Bwana Abraham Mika Mongo bado hajapona sawasawa mguu wake wa kushoto. Polisi wanamzungusha ingawa wanamwonea huruma! Baadaye aliomba ushauri Tume ya Haki za Binadamu wakaipitia *issue* yake na kumshauri kuwa mwenye gari (Polisi/Serikali) inapaswa kumlipa. Aliomba fidia ya Sh.20m/= Anazungushwa na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo:-

(a) Polisi imechukua hatua gani kumfidia Bwana Abraham? Hata kama Serikali haiweki bima kwa magari yake, je, uonevu aliotendewa bwana huyu na kumtia kilema bila sababu uishe hivi hivi?

(b) Ni kwa nini *OCD* Manyoni aliruka kuwa hakutoa kibali cha gari hilo litoke Manyoni Kilomita 100 kwenda Mitundu kumfuata Bwana Abraham Mika Mongo? Anadai Ofisa wa *CID* ndiye alichukua gari bila kibali chake.

(c) Ni kwa nini Bwana Abraham Mongo hakupelekwa kuhojiwa kituo cha jirani cha Kayui kilomita tano kutoka Mitundu na hasa kutokana na aina ya kosa la

kukopa na badala yake akasafirishwa chini ya ulinzi mkali kilomita 100 kwenda Manyoni kuhojiwa?

(d) Ni hatua gani zilizochukuliwa dhidi ya MaAskari hao watatu akiwemo Afisa Upelelezi (W) na hata *OCD* mwenyewe?

(e) Uhamisho walioupata Maafisa hao ni hatua zilizochukuliwa kutokana na sakata hili?

(2) Kesi ya Mosi Mpole kijiji cha Muhanga - Manyoni

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Manyoni. Naomba kujua ni kwa nini Polisi walimfilisi Bwana Mosi Mpole ng'ombe wake? Alibambikizwa kesi baada ya kukutwa na kipande cha ngozi ya Boko. Boko huyu aliuawa na Askari wanyamapori 2005, bwawa la Itigi na nyama yake kugawiwa kwa wananchi. Bwana Mosi naye alipata "share".

Baada ya muda alikutwa nyumbani kwake akakamatwa kwa madai ya kuwa na nyara na gobore. Akafunguwa mwaka mmoja (kifungo cha nje) nje ya jela, lakini wakati yuko ndani bado ng'ombe wake 48 waliibiwa, alipotoka aliwatafuta ng'ombe wake. Akafanikiwa kuwakuta ng'ombe 16 katika zizi la mtu mwininge (mwizi wake) ambaye alikimbi na kuacha ng'ombe hao 16 na wengine 30 jumla 46. Bwana Mosi Mpole alipoitaarifu Polisi, walimpa barua kuwa atunze/afuge ng'ombe hao 46. Lakini baadaye Polisi walifika kwake wakachukua mifugo yote 46 na kumwaarifu kuwa ng'ombe hao ni mali ya Serikali na kwamba watauzwa na fedha ziingie Mfuko wa Serikali! Bwana Mosi Mpole sasa ni maskini, hana la kufanya. Naomba maelezo juu ya hili.

(4) Naomba kupata maelezo kuhusu Bwana Sylvester James wa Msati, Musoma aliyekatwa goti na Polisi alipotoka kuangalia luminga (mpira). *Issue* hii iko kwenye magazeti muda mrefu.

(5) Naomba kujua juu ya kesi ya jinai iliyofutwa Mahakama ya Mkoa wa Singida CR:22/2008 inayomhusu mwananchi Mghenyi Senge. Ni kwa nini alifunguliwa kesi ya jinai na kunyang'anywa *passport* yake wakati ndiye mmiliki halali wa nyumba/kiwanja kilichozua mgogoro huo. Ni kwa nini ilifutwa kama alikuwa na kosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo, ni hatua gani zimechukuliwa kwa *PP* na Hakimu wa Mahakama ya Mkoa waliokula njama na mlalamikaji kumwonea Bwana Mghenyi Senge, mara alipofika tu kutoka Marekani, Bwana Senge ni raia mwema wa Tanzania, na ni Mtemi wa kabile la Wanyaturu na mwenye hadhi na heshima kwa watu wake.

(5) Naomba kupata maelezo ni kwa nini *OCD* Manyoni hajawalipa posho za uhamisho watumishi wake waliohamishwa kwenda vituo vyta kazi ndani ya Wilaya. Wote wanalamika kuwa waliohamishwa bila posho yoyote na kuambiwa hamna posho, ni amri moja tu wahame!

(6) Naomba kupata maelezo juu ya Kituo cha Polisi reli Itigi, ni kwa nini wizi/uvunjaji wa mahehewa umekithiri kati ya Itigi na Chaya? Majambazi mara kwa mara wanafanya *operation* za wizi bila kizuizi chochote toka kwa Askari wa kituo hiki, je, wanakula sahani moja?

(7) Tunaomba ‘*armory*’ Kituo cha Polisi Mitundu

(8) Kuhusu kesi ya mauaji Na.21 ya 1998. Upande wa mashtaka ulishindwa kueleza sababu za msingi za mshtakiwa kushindwa kufika Mahakamani. Mahakama imekuwa ikitoa hati za kumwita Mahakamani X 80 lakini hajawahi kutekeleza maagizo hayo na upande wa mashtaka hauelezi sababu za msingi za kwa nini mtuhumiwa huyo hafiki Mahakamani.

(9) Kesi ya mauaji Na.26 ya 199. Kesi hiyo ilifunguliwa Mahakamani tarehe 8/10/1999 ambapo mara ya mwisho mshtakiwa alifikishwa Mahakamani tarehe 11/12/2002. Mahakama ilitoa hati 117 za kumwita mshtakiwa Mahakamani lakini mtuhumiwa aliendelea kukaidi amri ya Mahakama, hakufika mara zote hizo.

Tafadhali, napenda kupata maelezo ya kina walipo washtakiwa hawa wa kesi No.21/1998 na No.26/1999.

MHE. MOHAMMED ABDI ABDALAZIZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ningependa nizungumzie kwa ufupi hoja zifuatazo:-

(1) Nyumba za kuishi Askari: Kwa muda mrefu tatizo la nyumba za kuishi Askari limekuwa kubwa Askari wanaishi nje ya makambi na hata hao wachache wanaoishi katika kambi za Jeshi la Polisi wanaishi katika mazingira duni yasiyofanana na hadhi ya Askari. Kwa vile bajeti ya Serikali inayotolewa kwa Wizara kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari. Ninapenda kutoa ushauri kuwa, Serikali izungumze ni mifano ya hifadhi ya jamii ili kupata mkopo mkubwa wa kujenga nyumba za Serikali kwa mfano Serikali ikikopa shillingi bilioni 25 inaweza kujenga nyumba zaidi ya 1000 ambayo ni karibu na wastani wa nyumba 40 kwa kila Mkoa.

(2) Hali ya uhalifu nchini. Ninapenda kutoa pungezi zangu za dhati kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi katika kukabiliana na uhalifu. Tumeshuhudia namna Jeshi la Polisi lilivyopambana kwa ujasiri na umakini mkubwa katika kupambana na wimbi la ujambazi ambalo lilianza kuota mizizi. Kwa kazi hii nzuri natoa pungezi zangu za dhati kwa mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspeksa Jenerali Saidi Mwema na watendaji wenzake kwa kazi yao nzuri.

(3) Jeshi la Magereza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi hili, kumekuwapo na matukio ya wahalifu kutoroka wakiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Magereza. Tabia hii inapunguza ari ya utendaji kwa Jeshi la Polisi ambao ndio wenye jukumu la kuwasaka na kuwakamata wahalifu. Rai yangu ni kwamba, inapotokea mhalifu kutoroka akiwa chini ya Jeshi la Magereza, basi kazi ya kumtafuta mhalifu huyo

isiachwe kwa Jeshi la Polisi pekee bali iwe ni kazi itakayofanywa kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na Magereza.

MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla maslahi ya Jeshi la Polisi na Magereza yanatakiwa yaboreshwe.

Mazingira wanayoishi, Karibu Tanzania nzima mazingira ya makazi ya Jeshi la Polisi si yakupendeza. Nashauri, Wizara itiliane mkataba na *NSSF*, *PPF*, *NHC* na hata Wizara ya Miundombinu wa kujenga nyumba za watumishi hao na ofisi. Nina hakika kwa kutumia mishahara yao wanaweza kumudu kulipia nyumba hizo iwapo zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu likizo baada ya miaka mitatu ya kazi, utaratibu huu umelalamikiwa na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza. Hivyo utaratibu ubadilishwe ili watumishi hawa wapate likizo sawa na utaratibu wa watumishi wengine wa mwaka mmoja, likizo ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo, kumekuwa na malalamiko kuhusu mafunzo kwa wale ambao hawajamaliza mwaka mmoja au miwili tangu waajiriwe. Elimu ni haki ya msingi ya kila mtumishi. Ushauri, waruhusiwe kwenda masomoni (Chuo Kikuu) wale ambao wako tayari kujilipia (kujigharimia) wenyeve mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho vya uraia, tunahitaji tuambiwe ni lini tarehe na mwaka hasa vitambulisho hivi vitakuwa tayari? Nini hasa kipingamizi cha mradi huu? Ni tenda haikamiliki au tatizo ni nini?.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu katika uchangiaji hoja hii. Napenda kumpongeza Waziri kwa kazi ngumu na nzito ambayo kwa ukubwa wa Wizara hii inampa kufanya kazi kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kusema katika bajeti ya mwaka jana, Wizara iliahidi kujenga magorofa kwa ajili ya makazi ya Askari, ninapenda kujua ujenzi huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika ajali za barabarani zinaongezeka na watu wengi kupoteza maisha, sababu ambazo tunapewa ni mwendo kasi wa magari ya abiria na uzembe wa madereva. Napenda kuuliza hivi zoezi la vizibiti mwendo uliishia wapi au ulikuwa mradi wa mkubwa au nguvu ya soda? Kwani tulishuhudia ufungaji wa vizibiti mwendo na ukaguzi ulifanywa mara kwa mara. Lakini hivi sasa hatuoni vizibiti mwendo hivyo na hata kupo lekea ajali mbaya kwa gari zibebazo abiria. Naomba Waziri wakati wa majumuisho yake aniambie ufungaji wa vizibiti mwendo katika gari zibebazo abiria uliishia wapi au ulikwamishwa na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuulizia ahadi za boti ziendazo kasi kwa ajili ya patro ndani ya ziwa Victoria, cha kusikitisha ni kwamba, Wizara haikuleta boti mpya ila ilikarabati vyombo ambavyo tayari vilikuwepo jijini Mwanza. Hivi kweli boti hizo zilizopo Wizara haioni kama boti hizo mbali ya ubovu, ni vya kizamani na haziwezi kwenda sambamba na vyombo ambavyo wanatumia maharamia katika Ziwa Victoria.

Majambazi hawa wanatumia boti za kisasa ambazo hufanya ujambazi na kukimbia kwa kasi na vyombo vya Polisi kutoweza kuwakamata majambazi hao hivyo, naomba niambiwe ni lini Wizara itaona ni muhimu kutupatia boti za kisasa katika Ziwa Victoria ili kuweza kupambana au kukabili ana na ujambazi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari mengi pia ni mabovu sana na hayafai kabisa kutembea barabarani, kwani yamechoka na mengine kutoa moshi mwingi. Hapa Dodoma, nimeshuhudia zaidi ya mara mbili, magari ya Polisi yakitembea usiku na yakiwa hayana taa, hivi utawezaje kukamata gari bovu wakati na lakwako ni bovu?

Pia katika barabara iendayo Dar es Salaam eneo la Ipagala huwa kuna (gofu) gari la Polisi hupaki hapo, lakini hupita magari mabovu na mengine hayana taa na mengine eneo la mbele lipo barabarani na maeneo ya nyuma yako pembeni. Wataalamu husema limekata Engaraini, lakini gofu hiyo halisimamishi na wala hawachukuliwi hatua yoyote. Je, gari hilo hapo linafanya nini au husubiri maroli ya mizigo tu? Tunaomba wawajibike Askari ambao wanashindwa kukemea maovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kushauri Askari wasiweze kuachwa kwenye eneo moja kwa muda mrefu mpaka akaota mizizi. Pia nashauri madereva ambao wanapewa leseni za kuendesha gari, wachukuliwe alama za vidole kwani, wasababishapo ajali awezenyang'anywa leseni hiyo na kupewa adhabu ya muda bila kuendesha kulingana na ajali aliyoifanya. Huenda ikawa msaada wa kulinda Sheria za Barabarani. Namaliza kusema kuwa nakutakieni kazi njema, ahsante.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri. Pongezi za kipekee kwa Jeshi la Polisi kwa kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama. Kazi inayofanywa na Jeshi la Polisi ni kubwa, muhimu na yenye changamoto nyingi nzito, Polisi imefaulu sana kutimiza wajibu wake licha ya upungufu wa vifaa na mahitaji mengine, pongezi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Jimbo la Shinyanga Mjini ambayo ni Manispaa, kuna vituo vichache sana vya Polisi; naomba viongezwe kwa mfano Kata ya Kizumbi (Nhelegani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nyumba za kuishi za Askari pamoja na juhudi za Serikali kuanza kuboresha nyumba za kuishi za Askari, ambazo nazipongeza, bado Askari wengi (Polisi, Magereza, na kadhalika) wanaishi katika nyumba duni, zingine zikiwa zimejengwa wakati wa ukoloni na/au mara tu baada ya uhuru. Hali hii haikubaliki, hakuna sababu ya Askari wetu kuishi maisha duni. Nyumba bora ni muhimu kwa Askari nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nashauri mpango kabambe wa ujenzi wa nyumba bora za Askari upanuliwe na kutekelezwa haraka. Hata pale Shinyanga Mjini, Askari wanaishi katika nyumba duni sana, zingine zilijengwe wakati wa ukoloni. Nauliza basi kuwa lini nyumba bora za Askari zitajengwa hapo Shinyanga Mjini? Naomba jibu. Nyumba zote duni za Askari zivunjwe na kujengwa nyumba bora zenye

ukubwa wa kutosha na mazingira ya kutosha palipo na nafasi, katika makazi ya Askari pawepo pia maduka ya biashara ili kuwezesha kujipatia mahitaji ya lazima katika umbali mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Vituo vya Polisi, naomba vituo vyote vya Polisi viwe vya kisasa kuwezesha Askari kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, mimi siyo Mbunge wa Arusha, lakini naomba Kituo cha Polisi kikamilishwe kujengwa sehemu ya Njiro (Kontena); ujenzi ulianza zamani lakini ukakwama hadi leo. Kwa kumalizia ujenzi huu, usalama utaimarika Njiro, na kadhalika, kwa manufaa hata ya watalii wengi wafikao Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, yote niliyoyataja hapo juu yanahitaji fedha, hivyo naomba sana Wizara hii iongezewe fedha ili hayo na mengine muhimu yafanyike. Huwezi kuwa na Askari bora na kazi bora bila ya kuwa na fedha za kutosha. Usalama ni moja ya mihimili mikuu ya kuwezesha harakati za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Shinyanga Mjini. Naomba kijengwe upya Kituo cha Polisi cha Manispaa ya Shinyanga kilichopo ni kituo kilichoengwa wakati wa ukoloni na majengo machache mara baada ya uhuru. Majengo yaliyopo sasa, ni chakavu sana hayatoshi na yalijengwa kizamani. Naomba bajeti ya 2009/2010 ijumuushe kazi hii. Ahsante.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yake. Hata hivyo, naomba ufanuzi katika maeneo yafuatayo:-

(a) Uhamisho wa Askari. Nyaraka za Serikali (*circulars*) zinataka kwamba Watumishi wa Serikali wakae katika vituo vyao kazi si chini ya miaka mitatu na si zaidi ya miaka mitano. Nia ya Serikali katika hili ni kupunguza kuzoleka kwa mtumishi na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Je, utaratibu huu unawajumuisha pia Askari walio chini ya Wizara yako? Kama jibu ni ndio kwa nini Askari anakaa katika kituo kimoja zaidi ya miaka kumi (10) hadi kushindwa kutofautisha kat i ya Askari na mwanakijiji wa kawaida kwa tabia na vitendo?

(b) Ajira ya Askari katika Mashirika ya Umma na Makampuni, kumezuka mtindo wa Askari Polisi kuomba kazi na kuajiriwa katika mashirika ya umma/makampuni kwa mishahara mikubwa. Je, hii ni sawa? Kwa nini wasifanye hivyo baada ya kustaafu kazi katika Jeshi la Polisi hasa ikizingatiwa kwamba Polisi nchini ni wachache na hawajawahi kukidhi mahitaji ya wananchi ya ulinzi na usalama wa maisha yao na mali zao! Kwa nini wasipate kibali cha kuajiriwa kwingine kutoka kwa mwajiri wake yaani Jeshi la Polisi?

(c) Ujenzi wa Kituo cha Polisi Jema (Oldonyosambu). Kitongoji cha Jema ni “corridor” ya wahalifu wa aina zote kwenda nchi jirani ya Kenya. Naomba ramani na usimamizi wa ujenzi wa kituo hicho kikubwa kutoka Polisi kwa sababu fedha zipo kwa

ajili ya miundo mbinu ikiwemo kituo hicho cha Polisi. Kiasi cha TShs.1.1 bil. zilitengwa na *NCAA* kwa miundombinu hapo Jema.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa wazima na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi niliwasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani, sasa nitakuwa sina maneno mengi sana isipokuwa nitazungumzia baadhi ya mambo ya Jimboni kwangu na Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa kuzungumzia uhamisho wa Jeshi la Polisi. Kuna MaAskari wamekaa muda mrefu sana katika kituo cha Wete kwa mfano kuna Askari Mwinyi Mselem, amekaa pale zaidi ya miaka ishirini (20) tokea aajiriwe. Amejitahidi kuomba uhamisho lakini hakufanikiwa akaniomba mimi MBunge nikamuombee kwa Waziri wa Usalama wa Raia na nikafanya hivyo Waziri akanielekeza niandike barua nikafanya hivyo na akaniomba barua nikafanya hivyo na akaniomba nimkumbushe kuwa hajapata huo uhamisho nikamkumbusha na akaniuliza apelikwe wapi nikamwambia Arusha lakini mpaka Mheshimiwa Mwapachu anaondoka pale na mpaka leo kijana huyu anasota hapo hapo sasa je, Mheshimiwa Waziri mpya unasema nini kuhusu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Polisi wa Mikoa ya Pemba wanawekwa sana nyuma kielimu pamoja na maendeleo kwa sababu jana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alisema kuwa Askari wengi wamepatiwa elimu ndani na nje ya nchi. La kusikitisha ni kuwa Askari hawa wamepata masomo ya ndani tu lakini hakuna aliyepekwa nje ya nchi, je, kwani wao hawastahili kupelekwa nje? Kama wanastahili kwa nini na wao wasipelekwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Askari hawa wanadai malimbikizo mengi ya fedha kwa Serikali na kunataarifa kuwa baadhi ya fedha zao zinakwama Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, je, Serikali ina jibu gani kuhusu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya tarehe 11/5/2008, saa saba za usiku, nilipigwa simu na wapiga kura wa Jimbo langu wakanieleza kuwa wamevamiwa na Polisi. Nikawauliza wanatafuta nini, wakaniambia eti wanamtafuta mtu mmoja anaitwa Jirani nikauliza amefanya nini wakaniambia hawajui, wakaniambia saa kumi na moja nifike kule na nikafanya hivyo. Niliposikia Jirani alikuwa amekimbia lakini nikawaambia wanakijiji cha Shumba Mjini wakamtafuta tukampleka Polisi tulipofika Polisi wakamchukua wakampeleka Chake Chake na baadaye wakamsafirisha Unguja. Sasa ninaliuliza Jeshi la Polisi kuitia kwako Mheshimiwa Waziri je, huo ndio utaratibu wetu wa Jeshi la Polisi wa kukamata watuhumiwa saa saba za usiku? Je, wanakijiji wangerusha mawe usiku angejibu nani hoja hiyo, huu si utaratibu mzuri wa kazi za Polisi, ahsante.

MHE. FAIDA M. BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara hii, pamoja na watendaji

wote na wapiganaji wote wa Tanzania, napenda kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia yafuatayo:-

(1) Jengo la Makao Makuu ya Polisi Mkoa Kusini – Pemba:-

- Jengo ni bovu sana na linahatarisha maisha ya wapiganaji wetu.

- Linavuja na lina nyufa.

- Huu ni mwaka wa saba (7) nalisemea toka 2000 – 2008 lakini hakuna kinachoendelea. Bajeti kila mwaka ni ndogo lakini Askari ni muhimu sana. Endapo litaanguka litaleta hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jengo hili kwa vile kipindi hiki halikutengenezwa fedha lakini naomba mwaka wa 2009 – 2010 liweze kutengewa bajeti liweze kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akija kujibu hoja aweze kunijibu nini mpango wa kusaidia Askari wetu wa Mkoa Kusini – Pemba kuhusiana na jengo lao la kufanya kazi.

(2) Nyumba za Askari za Madungu Chake Chake – Mkoani – Pemba. Mheshimiwa Sipa, napenda kuishukuru Serikali kwa kupanga kufanyiwa ukarabati nyumba za Askari zilizopo Madungu Chake Chake Pemba. Kama ukurasa wa 44 unavyooleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iona pia ubovu wa nyumba za Askari zilizopo Mkoani – Pemba, nyumba hizi na Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani, ni mbovu sana na ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wengi wanaishi uraiani jambo ambalo sio zuri kwa Askari kuishi uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba njibewe nyumba za Askari Wilaya ya Mkoani zitafanyiwa ukarabati lini?

(3) Madai ya posho ya uhamisho na safari. Kuna baadhi ya Askari wa vikosi vya Pemba wanadai posho zao za uhamisho tokea July, 2006 hadi sasa bila kulijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kunijibu ni Askari hao wa Pemba watalipwa fedha zao za posho za uhamisho na safari?

(4) Vitendea kazi. Vikosi vya Pemba wana matatizo ya usafiri. Gari walizonazo ni mbovu sana na zinahitaji kufanyiwa matengenezo ili ziweze kusaidia kazi za Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vingine ni pikipiki kufuatilia sehemu zisizofika gar, simu za upemo na kadhalika.

(5) Kamati ya Mfikiwa, Wawi – Pemba. Naishukuru Serikali kwa kuwajengea majengo Askari wetu. Lakini kwa kuwa Askari wanaoishi hapo wana watoto, naomba wajengewe *dispensary* na chekechea (*Nursery School*).

(6) Mishahara ya Askari. Kwa kuwa mishahara ya Askari wetu, bado ni ya hali ya chini na hasa pale inapoonekana ina tofauti kubwa na Maafisa. Askari wa kiwango cha chini (*privates*) na wenye vyeo vya chini wanapaswa waongezwe mishahara inayoridhisha maana ndio watendaji wakubwa na hawana muda wa kufanya kazi nyingine za binafsi, kulingana na kwamba wao wanafanya kazi muda wote.

(7) Fursa za Masomo kwa Askari. Kuna tabia kwamba hasa Askari amepata nafasi ya kusoma (kujiendeleza hasa kwa elimu ya juu) basi ofisi haimruhusu Askari huyo kwenda kusoma. Je, ni kwa nini? Naomba jibu kwa sababu sera ya Serikali yetu ni kutafuta elimu, elimu ni ufunguo wa maisha na kila Askari anapopata elimu sasa basi anakuwa mzuri zaidi.

(8) Nyumba za Askari Finya na Limbeni – Kaskazini Pemba. Naishukuru Serikali kwa ujenzi wa nyumba tatu katika Wilaya ya Wete – Pemba lakini katika nyumba tatu (3) za Askari F.F.U. Finya – Wete bado umeme hujafikishwa kwenye nyumba na hasa maji yamefikishwa lakini hakuna *tank* la maji ambalo ni muhimu sana kwa kuhifadhi maji ambayo yanaweza kuwasaidia Askari wetu.

(9) Pongezi kwa Askari wanawake. Natoa pongezi kwa Askari wetu wanawake wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi hii.

(10) Michezo. Bajeti haikuelekea habari ya michezo kwa wapiganaji wake, kwa hiyo, naomba Serikali itilie maanani suala la michezo kwa Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini kwenye bajeti hii hakuna suala la michezo na fungu lake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni kazi, ni furaha na ni dawa kwa binadamu. Bajeti ijayo michezo ipewe kipaumbele. Ninawapongeza Askari wanamichezo wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa wakati wa bajeti ya Waziri Mkuu, nilichangia hoja inayohusu gari la zima moto la Halmashauri ya Kibaha, kwamba lilipangiwa pesa tangu bajeti ya 2005/2006 lakini

mpaka bajeti ya 2008/2009 wakati ninachangia hoja ya Waziri Mkuu gari hilo halijaonekana katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Siku ya pili kwa taarifa niliyopata kwa wananchi wa Kibaha na Diwani wa kata ya Mailimoja, gari hilo la zimamoto lilionekana likipita lilipokuja Kibaha viwanja vya Mailimoja na viongozi wakawambia wananchi kuwa, wasisikilize maneno ya watu wasiokuwa na nia nzuri maendeleo ya Kibaha wanaosema kuwa gari hili ni bovu. Wananchi walishangilia sana. Baada ya siku mbili tangu *demonstration* hiyo ifanyike, nyumba ya Bi. Rukia Mohamed Ngulengule Mbonde ilishika moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diwani wa Mailimoja, Ndugu Hassan alipiga simi kuomba gari la zimamoto ili lije kuzima moto nyumba ya huyu mama, lakini wakaambiya gari hilo la zimamoto liko gereji kwa hiyo nyumba ya Bi. Rukia iliteketea kabisa. Wananchi waliponitaarifu, nililifuatilia tatizo hilo kwa Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Mwanaidi Kiongozi, ye ye alinitaarifu kuwa ni kweli gari hilo liko gereji. Pia nilipata taarifa dereva wa gari hilo na baadhi ya wafanyakazi wa Idara ya Zimamoto wanaishi Dar es Salaam. Kuwa tukio lililojitokeza kwenye gari hilo kufika Kibaha na baada kushindwa kufanya kazi yake kwa sababu liko gereji. Hii imethibitisha kuwa gari hilo halikuwepo Kibaha mpaka baada ya hoja yangu Bungeni. Pia gari hilo halikuwa zima wakati lilipoletwa Kibaha.

Je, Mkurugenzi wa Zimamoto Wizarani aliliruhusu vipi au kuthibitisha uzima wa gari hilo kusababisha Wizara ya Miundombinu kuruhusu lipewe namba na lije kuanza kazi, wakati gari hilo baada ya siku chache kufika Kibaa likapelewa gereji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, “uongo unaweza kumuongopea binadamu lakini huwezi kumuongopea Mwenyezi Mungu”. Ndio maana Mwenyezi Mungu amedhihirisha usemi usemao “lisemwalo lipo, kama halipo linakuja” na “kwenye ukweli uongo hujitenga”.

Je, Mheshimiwa Waziri unaweza kuwatumia wataalamu wa Nyumbu, *PCCB* na wataalamu wa Wizara ya Miundombinu walikague gari hilo na kama ikidhibitika kuwa gari hilo ni bovu na si jipya, Mkurugenzi wa Zimamoto na watendaji waliohusika kununua gari bovu wawajibike?

MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri yenye kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo yote yaliyomo na zaidi kuhusu usalama wa nchi, pia nawapongeza kwa kuamua kuwa na vikosi vyao wenyewe vya kushughulikia mambo ya ufundi ujenzi na kadhalika. Pia ninashauri viwepo pia vya kushughulikia mambo ya Uadtari, mahebabu, uuguzi, kilimo, ufugaji, mazingira, pia na aina za utaalamu mwingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi na mimi nasisitiza kuhusu makazi ya Askari Polisi na Magereza, wapatiwe nyumba zilizobora na za kisasa, ili wapate kufanya kazi zao kwa uhakika na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya PPolisi vidogo dogo viongezwe ili kupunguza matatizo yanayojitokeza kama vile ajali, uhalifu na masuala ya mshahara na posho waongezewe ili kupiga vita rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uhamiaji, mbona wahamiaji haramu wanazidi kuingia nchini kila siku inakuaje? Hakuna wahuksika huko mipakani, kwa hiyo ulinzi wa mipakani uzidi kuimarishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madawa ya kulevya yanaingizwa kwa wingi nchini, je, hii ina maana walinzi wetu wanahusika? Hivyo iwekwe mikakati ya makusudi kwa walinzi wetu hasa wa uhamiaji na mipakani, bandarini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nawatachia kila la kheri.

MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja iliopo mbele yetu katika maeneo yafuatayo:-

(1) Uhamiaji. Hiki ni chombo muhimu sana kwa usalama wa Taifa letu kama vyombo vingine vya ulinzi. Yapo malalamiko makubwa mionganoni mwa watendaji wake. Kama inayojitokeza kwa waajiriwa wa Jeshi la Polisi na Magereza, wafanyakazi wa uhamiaji na wanalamikia juu ya mishahara isiyokidhi mahitaji halisi ya maisha ya kila siku, hakuna utaratibu mahsususi unaotambulika wa upandaji vyeo ndani ya Jeshi la Uhamiaji jambo ambalo linalalamikiwa na wengi.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Polisi, yapo malalamiko kadhaa yanayolalamikiwa na Askari wa Jeshi letu hilo. Mishahara wanayolipwa Askari wa Jeshi la Polisi ni midogo ikilinganishwa na uzito wa kazi zao ambazo takriban ni za masaa ishirini na nne. Mshahara usiokidhi mahitaji wakati mwingine ni chanzo cha kujiingiza katika vitendo vya rushwa. Aidha posho za mlo na usafiri ni ndogo sana zisizoendana na hali halisi ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari pia wamekabiliwa na tatizo la kucheleweshewa viinua mgongo vyao wanapostaa fu ambapo sambamba na hili hata stahili zao nyingine kama fedha za uhamisho hucheleweshwa au kukosekana kabisa. Lipo tatizo la nyumba za kuishi jambo ambalo linadhalilisha Jeshi letu na kupunguza kasi ya uwajibikaji wao. Ukosefu wa mavazi na vifaa vingine kama viatu ni tatizo lililojichimbia katika vyombo vyetu hivi. pamoja na hayo machungu yanayowakabili Askari wetu kwa upande wao wanayoyafanya ambayo si mazuri kwa raia wa Tanzania. Kwa kupokea chochote ni kuwaacha madereva wa magari ya abiria na kasoro kubwa. Upukuzi unaofanywa kwa taratibu zisizo sahihi ni jambo lisiloridhisha na linalowadhalilisha wananchi, ahsante.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, usafiri kituo cha Chwaka. Hivi sasa kutokana na ujenzi wa shughuli za kitalii ikiwa ni sehemu moja ya uchumi wa Zanzibar, matukio mengi hujitokeza na Askari kushindwa kufuatilia maeneo ya matukio. Hali hii inarejesha nyuma wawekezaji. Usafiri wa kituo cha Mwera kwamba utumike hadi sehemu za Chwaka ni vigumu sana. Usafiri kituo cha Chwaka utatumika maeneo ya kanda za pwani na za juu kwa mfano Dunga, Kiboje Uzini Pangwe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Vituo vya Polisi (Chwaka na Dunga), Kituo cha Polisi hapo Chwaka kimezungukwa na nyumba pembezoni za kiraia na kituo cha zamani sana hivyo inakuwa sio jambo la busara kwa sababu sehemu ya kituo inawajibika kuwa faragha. Kituo hakina *CELL* ya kuhifadhi watuhumiwa ambao wanasikiliza kesi zao. Kituo hakina muundao wa kituo kwa sababu ni nyumba ambayo imerithiwa toka ukoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Dunga. Kituo hiki kimejengwa kwa ufadhili. Lakini la kusikitisha Serikali haishughulikii kwa matengenezo ya aina yoyote. Wakati wowote kinaweza kuanguka kwa sababu kimeshafanya mpasuko. Hata dari yote imeshatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Askari. Katika vituo vyote hivyo viwili vilivyoko Jimbo la Chwaka hakuna nyumba za Askari. Askari wanaenda na kurejea kazini. Nyumba zilizopo kituo cha Chwaka za ukoloni, chumba kimoja wanalala wazee na watoto wao humo humo hii pia inajenga hisia potofu ki-ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, malindo binafsi, kuna mikataba gani ya malindo binafsi kama:-

- (a) Shell ya Chwaka
- (b) Pongwe Hotel Beach. *PGO* ya Polisi lindo lilindwe kwa masaa sita hadi nane (6 – 8) na hayo hulindwa masaa kumi na mbili (12.00).
 - (i) Je, hii *allowance* inakwenda wapi au wanapewa nani?
 - (ii) Utaratibu gani unatumika hususan wakati wa maafa katika eneo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu za dhati iwapo nitapatiwa ufanuzi wa maelezo yangu pamoja na maswali niliyouliza. Ahsante Sana.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri sana. Aidha, ninampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongozi hizi, ninaomba kuchangia machache katika Wizara hii:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, gharama za kushughulikia watuhumiwa vijiji. Kumekuwa na malamiko mengi kuhusu gharama nyingi na kubwa wanazoingia walalamikaji kuwashughulikia watuhumiwa wao. Gharama hizo ni zipi? Gharama hizi ni zifuatazo:-

(a) Gharama za kumkamata mtuhumiwa. Mlalamikaji yeote anapotaka kumfikisha mtuhumiwa wake kwenye vyombo vya haki analazimika kumgharamikia mgambo wa kwenda kumkamata na kumpeleka kwenye chombo cha kutoa haki. Kwa sasa gharama haipungui shillingi elfu kumi (10,000/=). Bila hivyo mtuhumiwa hawezi kushughulikiwa.

(b) Gharama ya chakula. Mlalamikaji, analazimika kutoa huduma ya chakula kwa mtuhumiwa wake akiwa mahabusu ya kijiji au kata.

(c) Gharama ya ulinzi wa Mahabuusu. Mlalamikaji analazimika kutoa gharama za ulinzi wa mahabusu anamowekwa mtuhumiwa wake akiwa mahabusu ya kijiji au kata.

(d) Garama ya usafiri. Endapo mtuhumiwa atapatikana na hatia akapewa adhabu ya kifungo ni wajibu wa mlalamikaji mtuhumiwa na mgambo hadi Gereza la Wilaya. Je, ni Watanzania wangapi wanaweza kumudu gharama hizi? Jibu ni kwamba Watanzania wengi wameshindwa kwa sababu gharama ni kubwa na nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake:-

(a) Watuhumiwa wengi hawashughulikiwi wakiwemo majambazi, vibaka, wezi, wauaji na wahalifu wa aina mbalimbali nchini.

(b) Kutokana na jibu la (a) wahalifu na uhalifu umeongezeka sana nchini hususani vijijini.

(c) Kuhatarisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani ametufikisha nani hapa? Jibu ni “Serikali”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Serikali ilikuwa na utaratibu mzuri sana wa kushughulikia watahumiwa.

- Askari wa kukamata wahalifu - tarishi;
- Kulikuwa na mlinzi wa mahabusu;
- Kulikuwa na lishe kwa kila mahabusu; na
- Mtendaji wa Kata aliwezeshwa kugharamia usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ndiyo iliyofuta utaratibu mzuri uliopo huko nyuma na kumtupia mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendezo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kurudisha ajira ya Askari Mgambo katika ngazi ya kata na kijiji;
- (b) Kurudisha huduma ya lishe katika mahabusu zote nchini;
- (c) Kuajiri walinzi katika ngazi ya kata na kijiji; na
- (d) Ofisi ya Kata iwezeshwa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kushughulikia matukio ya mauaji. Serikali inadai kuwa matukio ya mauaji yanapotokea Idara ya Polisi ndiyo inayogharamia mafuta na posho kwenda kwenye matukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa kinadharia ndivyo inavyotakiwa lakini katika hali halisi ni ndugu wa marehemu ndiyo wanabeba gharama zote kwa madai kuwa Polisi hawana fedha kwa ajili ya matukio ya aina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali itupie macho eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, ninaomba kuunga mkono hotuba hii.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa uongozi wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kulinda raia na mali zao. Naomba utaratibu huu uendelee wakati wote kwani imejitokeza kwamba wakati wa uchaguzi mkuu, Jeshi hilo huwa ni adui wa baadhi ya raia na mali zao pamoja na kuwanyanyasa na kuwadhalilisha hasa wale wa vyama vyaa upinzani. Baadhi ya Sheria za Jeshi la Polisi zimepitwa na wakati. Zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linahitaji kupatiwa vitendea kazi kama vile magari, pikipiki na kadhalika kwa Askari wanaopangiwa kazi za ulinzi kama kwenye mabenki, mipakani wanaopambana na majambazi wapatiwe silaha pamoja na makoti ya kuzuia risasi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa umakini zaidi. Askari wanapofanikiwa kuwashinda majambazi wapewe motisha kwani kupambana na majambazi wengi silaha ni kazi ya kufa na kupona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya Jeshi la Polisi hayaridhishi kwani wengine wanaishi katika majumba yaliyochakaa au katika chumba badala ya vyumba wakiwa pamoja na wake zao, watoto wao ambao wengine ni wakubwa. Huu si utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya uraia ni muhimu sana katika kuwatambua raia halali wa nchi hii. Vitambulisho vinasaidia kuwajua wageni au wakimbizi wanaoingia nchini kinyume cha sheria na hivyo kuweza kuwachukulia hatua za kisheria. Naiomba Serikali ione umuhimu wa vitambulisho na ihakikishe kwamba kabla ya 2010 wananchi wote wanapatiwa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wa Zimamoto wapatiwe vitendea kazi kwani majanga ya moto yanatokea mara kwa mara lakini kutokana na upungufu wa vifaa vya kuzimia moto wakati mwengine wanashindwa kufika katika maeneo ya majanga kwa wakati na hivyo kushindwa kuokoa maisha ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wanakuwa wepesi kuchukua hatua mara moja ya kuwahoji au hata kuwaweka ndani endapo watumishi wa ngazi za chini wanatuhumiwa kwa wizi au ubadhirifu wa mali ya umma lakini wanashindwa kuchukua hatua kwa wakubwa mfano katika suala la ufisadi au upotevu wa mali ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mlundikano wa wafungwa ni mkubwa katika Magereza. Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hili. Kuhusu ubambikizwaji wa kesi kwa wananchi wasio na hatia Serikali inasema nini? Ahsante.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ulinzi wake. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP* na viongozi wake kwa moyo walionao katika kulinda uhai na mali ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa bajeti mzuri ingawaje mambo ni mkubwa na mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nizungumzie masuala ya Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa raia na mali zao. Napongeza Wizara hasa *IGP* Said Mwema jinsi anayopambana na uhalifu nchini. Tatizo kubwa ambalo naishauri Seikali iwe makini sana katika kuteua Wakuu wa Polisi Wilaya (*OCD's*). Nafikiri wapo wanaoteuliwa kwa sababu ya kujuana wala sio uadilifu na utendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwengine MaAskari wenyе ngazi za chini wanakaa muda mrefu mno katika eneo moja la kituo cha kazi. Ikiwa wanakuwa wepesi kumlaghai kiongozi yejote wa juu anayehamia pale mfano Bukombe. Askari mwenye maisha ya chini sana lazima awe na nyumba mmoja, lakini kawaida ni nyumba zaidi ya

moja. Kinachotokea *OCD* atakayeletwa pale akakuta hali hiyo, cha kwanza ni kuwaagiza vijana wahakikishe anapata hela, ndipo rushwa, kesi za kubambikiza na uonevu unaogezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya kama Bukombe mtafute mtu ambaye moyo wake na nia yake ni kuwatumikia watu kama alivyokuwa Afande Mstaafu *OCD* – Gerald ambaye amekuwa kielelezo kizuri sana Wilayani kwa wananchi na viongozi, ingawaje alidharauliwa sana na Jeshi la Polisi. Mungu amfanye afanikiwe katika mambo yale yote hapo Ushirombo – Bukombe kama mwananchi wangu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na usalama mdogo wa wananchi na mali zao Bukombe, napenda kushauri Serikali ikiwezekana ifanye utaratibu maeneo hayo kuwepo Askari wa kutosha kwa ajili ya doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, doria isiwe ya kutumia gari, watembee watamaliza/kupunguza tatizo hili ambalo ni kero kwa wana Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, gari la Polisi, namshukuru Mungu kwani kila wakati nkipata nafasi ya kusema huwa naeleza kwa nini tunahitaji gari Wilayani Bukombe. Naomba mfahamu kuwa Bukombe ina km210,482 za Mraba, ina wakazi 525,746. Upungufu wa gari kutowatendea haki wana-Bukombe ambao wanaishi maeneo ambayo huenda wakimbizi wapo ndani ya misitu yetu. Naomba Serikali kwa kuwa mmeahidi mara nyingi, oneni aibu ndugu zangu ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ujenzi wa Makao Mkuu ya Polisi (W), kwa kuwa umuhimu wa kituo hiki wana-Bukombe tulianzisha ofisi zetu. Mheshimiwa *IGP* Mstaafu alitoa sehemu ya hela, hali iliyopo mahitaji ya nguvu za Serikali ili MaAskari wetu wapate sehemu nzuri ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Jeshi la Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Hivi viongozi wa juu mnashindwa nini kwenda kuona mahali Askari hawa wanapofanyia kazi? Inatia huruma tena inauma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nyumba za kuishi za watumishi. Naomba Serikali ianze kufikia namna ya kuwapatia/kuwajengea nyumba watumishi hawa kwani sasa hivi kila mmoja anaishi ama kwenye nyumba yake binafsi au popote atakapoona panafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Vituo vidogo vya Polisi. Kutokana na wingi wa watu zaidi ya 500,000 kuwa na vituo vidogo viwili (Masumbwe na Uyovu) ni hatari sana. Naomba Serikali ipitie upya ione namna ya kusogea huduma hii karibu na jamii. Najua upo mpango wa Polisi Jamii, huu ni mpango wa kinadharia kwani kwa vitendo halifanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, idadi ya Polisi. Naomba Serikali iongeze MaAskari Polisi, Wilayani Bukombe, sitegemei kupata Polisi wa kutosha nalo litafanana na kuomba Madaktari wa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawatakia kazi njema na Mungu awabariki, kumbukeni ahadi yenu ya kuja kutembelea Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Nampongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pungezi kwa Askari wetu wote. Nawapongeza Askari wote wa Polisi, Magereza pamoja na zimamoto kwa kazi nzuri na ya kuridhisha wanazozifanya katika mazingira magumu sana hususan katika nyanja za makazi duni, mishahara duni na vitendea kazi duni. Ninawahimiza wasikate tamaa. Matumaini yangu ni kwamba Serikali ina mipango mizuri ya kuboresha mazingira yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makazi ya Askari, hali ya makazi ya Askari wetu katika sehemu kubwa ya nchi yetu ni mbaya sana. Sijui kwa nini? Pamoja na umuhimu wa Askari katika kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Jeshi la Polisi limepata mkopo wa muda mrefu toka Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa nyumba za Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu mahitaji ya nyumba za Askari ni makubwa sana tena kwa taifa zima. Kwa hiyo, ujenzi wa nyumba hizi inabidi uende kwa awamu nchi nzima. Lakini sina hakika na formula iliyotumika kuelekeza sehemu ya mkopo huu katika ujenzi wa nyumba za Askari zaidi Dar es Salaam kuliko sehemu nyingine ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nyumba za Askari wa Tabora Mjini siyo tu ni chakavu sana ila ndogo ndogo sana kiasi cha kushindwa kukidhi mahitaji ya kibinadamu kwa heshima. Kwa nini Jeshi la Polisi lisingelitenga angalau sehemu ndogo ya mkopo huo wa *NSSF* ili kuanza kujenga angalau nyumba chache za kisasa kwa Askari wa Tabora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha siridhiki na gharama kubwa za ujenzi wa nyumba za Askari zinazoendelea sasa katika mazingira ambayo kama Jeshi letu la Polisi lingetumia teknolojia ya ujenzi rahisi kwa kutumia matofali ya kuchoma na yale ya kupanga na vile vile kutumia nguvu kazi ya wafungwa zingelipatikana nyumba nyingi zaidi za gharama nafuu lakini za kisasa na kwa hiyo kuwezaa kukidhi mahitaji makubwa ya nyumba za Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vitendea kazi. Uhaba wa vitendea kazi hususani magari na pikipiki ni mionganoni mwa matatizo sugu yanayo kabili MaJeshi yetu ya Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa vitendea kazi madhubuti na vya kuaminika halihitaji kusisitizwa. Serikali iwe na mkakati muhimu wa kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya uzeeni/pensheni. Wizara iharakishe marekebisho ya Sheria za MaJeshi yaliyo chini yake kwa madhumuni ya kuziboresha ili kuwawezesha Askari wanaostaafu kupata malipo mazuri kama wanavyopata wastaafu wengine katika sekta nyingine za Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *scheme of service*, sambamba na kuboresha malipo ya uzeeni, ni vema hata *scheme of services* za MaJeshi yetu nazo zikapitiwa kwa madhumuni ya kuziboresha kuendana na wakati.

MHE. FESLITER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri, Mheshimiwa Khamisi Kagasheki (Mb), Katibu Mkuu, Inspeksa General Said Mwema na watendaji wengine, kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kulinda nchi na raia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Serikali ya CCM kwa uamuza wa busara wa kujenga Chuo cha Upelelezi Mkoani Dodoma, kwa niaba ya wananchi wa Dodoma nawahakikishia ushirikiano wa karibu kufanikisha ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri awaeleze wananchi ukweli kuhusu wageni wengi sana walioko nchini na hasa Dar es Salaam je, wote wana vibali halali vinavyowaruhusu kuishi nchini? Je, wageni wanaofanya biashara mbalimbali hasa za madukani jijini Dar es Salaam tena wanafanya biashara ndogo ndogo sana kama vile kuuza maua, viatu aina ya raba na kadhalika wana vibali vya kuishi nchini na kujihusisha na biashara hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge lako Tukufu lilitenga shilingi billioni tatu kwa ajili ya vitambulisho vya uraia. Maelezo aliyyoyatoa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake hayatoshelezi kabisa. Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu hatua aliyofikia katika utengenezaji vitambulisho vya raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu wanaoishi katika nyumba za Polisi hawakatwi kodi kutokana na mishahara yao na wanalipiwa bili ya maji na umeme cha ajabu ni kuwa watumishi wa Idara ya Uhamiaji wanaoishi kwenye nyumba za idara wanakatwa kodi ya nyumba asilimia kumi kutoka katika mishahara yao nawananajilipia umeme na maji. Je, utaratibu huu wa wafanyakazi wa Wizara moja, wengine kulipishwa kodi na wengine kutolipa kodi, unatokanana na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hatua iiyochukuliwa na Wizara yake kwa kujenga nyumba za kuishi za Polisi Mkoani Dar es Salaam. Wizara ione umuhimu wa kujenga nyumba za Polisi katika Mikoa yote nchini kwani Polisi wengi wanaishi katika mazingira magumu sana. Nawapongeza Askari Polisi kwa kazi kubwa wanazozifanya. Polisi hupeleleza kesi kwa kutumia nauli zao, wanatumia mishahara yao kwa kupiga simu za upelelezi, muda wao wa mapumziko na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara haioni kuwa kuna haja sasa ya kuwapa posho/motisha kwa kuwapa nauli ya kufuatilia kesi, pesa za vocha na vitendea kazi vingine ili kufanya kazi zao kuwa rahisi? Je, Serikali haioni kuwa kutowapatia Askari vitendea kazi Askari wengi wanashawishika kuomba rushwa kwa watuhumiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Magereza, Serikali iangalie uwezekano wa kushirikiana na Mahakama kukata kesi kwa haraka na vile visingizio vya kuwa upelelezi haujakamilika utafutiwe ufumbuzi. Hii itasaidia kupunguza msongamano Magerezani na vile vile Sheria za Parole na Community Service Act zitumike vizuri ili lengo la kupunguza msongamano litimie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukimwi Magerezani, Waziri akijibu swali hapa Bungeni la Mheshimiwa Dr. Ally Taarab alisema kiwango cha maambukizo ni 7% hiki ni kiwango kikubwa sana, Serikali itueleze maambukizo hayo yanatokeaje au wanaingia Gerezani wakiwa na maambikizo tayari. Nashauri utafiti ufanyike ilikujuwa kama maambukizo hayaongezeki Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sheria zetu wala dini zetu haziruhusu ngono ya jinsia moja lakini zipo taarifa kuwa matendo hayo yapo katika Magereza na yawezekana maambukizo mapya hutokana na sababu hiyo, lazima tu-*face/tukubali reality* na itafutwe njia ya kupambana na hali hiyo ili maambukizo yasiongezeke. Ikiwezekana Serikali iruhusu wtembelewe na wake zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tabia ya kuwanyoa nywele zao kwa vifaa ambavyo vimetumiwa na zaidi ya mfungwa mmoja bado inaendelea hatua ichukuliwe ili kuacha kabisa tabia hiyo na Askari watakaoendelea na mtindo wa kuwanyolea vifaa ambavyo si salama wachukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukimwi, ni janga lazima tupambane kuzuia na hiyo asilimia saba (7%) ipungue. Serikali ije na njia na *commitment* kuwa *next time* wataleta ripoti ya maambukizo yatakayoonyesha kupungua kwa maambukizo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamiaji, kuna tatizo katika karatasi zetu/fomu zetu ambazo wageni hupewa kujaza wanapofika nchini kuna kipengele kinachosema sababu za kuingia nchini yako mengi likiwemo *Scale, Employment*.

Nashauri kipengele hicho kiondolewe uwepo utaratibu mwingine wa wageni wanaokuja kutafuta kazi nchini. Hii itapunguza wingi wa wageni hata wasio na sifa kutumia fomu hiyo kuonyesha nia yao na watawezajitetea walijaza hicho kipengele *airport* wakati wakijaza hiyo *Visa Form*. Nchi nyingine duniani hawaweki kipengele hicho ili kuzuia wageni wengi kujaza nafasi za ajira ya Watanzania na taratibu zingine rasmi hufuatwa.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja moja tu. Naomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina wa kifo cha Mheshimiwa Chacha Wangwe na ikiwezekana ripoti kamili itolewe ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED ALI SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ni muhimu sana kwa ulinzi wa wananchi na mali zao. Basi ni vyema sana Serikali ikawaangalia Askari wetu kwa jicho la huruma. Kwani tunajua kuwa Askari wetu wana kazi kubwa na ngumu, wanafanya kazi usiku na mchana bila kuchoka wanafanyakazi kwa uzalendo, wakiwa katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tunaiomba Serikali iwaangalie vizuri Askari wetu kwanza, kwa kuwapatia vitendea kazi kama vile, magari, mafuta ya magari na kadhalika. Vilevile naiomba Serikali iwape Askari wetu mishahara mizuri itayowawezesha kuishi bila usumbufu wowote wa kimaisha. Pia wapewe posho zote zinazostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ajali nyingi zinazotokea majini, watu wetu wanakufa kwa sababu:-

(a) Uzembe uanotokea baina ya Serikali na Wizara hii, kwani habari zinapofika Serikalini, Serikali inakua na kigugumizi kuzipeleka habari hizo kwa Jeshi letu.

(b) Wizara bado haijaona umuhimu wa kuwa na vitendea kazi vya kuokolea kama helkopta, maboya ya kuokolea, maboti yenye spidi kubwa na kadhalika yanayokwenda kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii kwa mwaka ujao wa fedha wa 2009/2010, kwa kiasi kikubwa kutoka hapa ilipo sasa (273,976,585,500) ili Askari wetu waweze kufanya kazi kwa utulivu kabisa bila rushwa wala vishawishi vinginevyo.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Inspekte Jenerali, Makamishna, Wakurugenzi

na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya, ingawa baadhi ya Askari hutia doa utendaji wa Wizara hii kwa kukosa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ni nzuri lakini nataka kufahamu wahalifu wenye ulemavu wanahudumiwaji Magerezani? Sina maana ya kuwatetea wahalifu hao kwa sababu kwanza wangejitahidi sana kukwepa kutenda uhalifu ili wasibughudhiwe, lakini kufahamu utaratibu ni vizuri ili niweze kutoa ushauri mzuri kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kupata ufanuzi wa suala hili, kwa vile wahusika wanalamikia taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu mdogo, naunga mkono hoja.

MHE. TATU NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari na kikosi cha TAZARA wana zaidi ya mwaka mmoja hawalipwi posho zao wanaposafiri kusindikiza *train* za mizigo au za abiria kati ya Dar es Salaam na Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya TAZARA hawalipi wala Jeshi Makao Makuu hawawalipi Askari hawa pamoja na mshahara mdogo, inabidi agawe pesa ya kula na kujikimu akiwa safarini na kuacha nyumbani kwa familia yake. Huu ni uonevu, Waziri eleze lini watalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuwaacha Askari katika kikosi kimoja kwa zaidi ya miaka kumi (10), wanakosa uadilifu. Askari anafanya kazi ya *patrol* kwa miaka zaidi ya kumi au *FFU* au *Traffic* au Reli ya Kati. Staili hii inavunja moyo Askari na wanafaya watakavyo taka, kutokana na mazoea ya kukaaq kwenye ofisi moja miaka nenda miaka rudi. Mkuu wa Jeshi, ninashauri afanye hadidu za rejea katika vikosi nilivyotaja, hasa Polisi Reli ya Kati na *FFU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, viongozi wakuu ndani ya Jeshi, waliokuwa Mikoani na kuletwa Makao Makuu, ingawa siyo wote, lakini Mkuu wa Jeshi awatazame sana, wengi wao hawakuwa na sifa nzuri. Wengine waliostaafu hivi karibuni walionekana kulijimbikizia mali nyingi, kwa kujenga nyumba nyingi, mahotel, ma-baa, ni kweli kipato halali? Waziri, viongozi wote wenye madaraka Mikoani na hapo Makao Makuu wafanye kazi kwa uadilifu ili hadhi ya Jeshi iendelee kuonekana na kuheshimiwa, kwani Askari wa chini wana walalamikia viongozi wao. Naomba aifanyie kazi hali hii ili Askari hao wachape kazi vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. USSI AMME PANDU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji na wataalamu wote wa Wizara hii kwa bajeti yao ambayo ni nzuri na yenye kutoa matumaini kwa Watanzania, lakini pia ni bajeti ambayo inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya C.C.M. ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hali ya usalama nzini. Pamoja na kasoro ndogo ndogo ambazo bado zimesalia, lakini ni lazima tuipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanya ya kuweka hali ya usalama nzini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hii ilikumbwa na wimbi zito la ujambazi na kusababisha watu wake kuishi bila kuwa na amani ya maisha yao na hata kwa mali zao, lakini baada ya kazi nzuri ya Wizara pamoja na ushirikiano mazuri ya *IGP* Serikali imeweza kupunguza wimbi la ujambazi nzini na wananchi sasa wamekuwa na amani. Lakini pia jambo zuri zaidi ni kuwa wananchi sasa wamekuwa na imani na Jeshi lao la Polisi. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, rushwa. Pamoja na sifa nzuri ya Jeshi hili la Polisi kuna baadhi ya wachache ambao wanalichafua Jeshi hili kwa kula rushwa.

Ushauri wangu ni kwamba sheria zitumike zaidi kuwabana wala rushwa ili kulisafisha Jeshi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. DR. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Nampongeza pia Katibu Mkuu na watendaji katika Idara zote za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuomba Wizara hii itusaidie mambo mawili:-

(i) Polisi Wilaya ya Same wapatiwe pipipiki ili waweze kufikia Kata za milimani kwa urahisi.

(ii) Kata za milimani zipatiwe ofisi na vitendea kazi ili Polisi wafanye kazi zao kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti ya 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, napenda nimpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea vizuri sana katika kipindi kifupi tangu akabidhiwe Wizara inayolalamikiwa sana na uduni wa utendaji kazi na rushwa iliyokithiri. Mimi binafsi, namtakia kheri Mheshimiwa Waziri na

viongozi wote katika Wizara hii muhimu kwa usalama wa raia. Ni imani yangu watajikita zaidi katika kuhakikisha kuwa wananchi wanarudisha imani kwa Polisi hapa nchini. Ninaamini kwa kukutana mara kwa mara na viongozi wao, nao wakiwa ni Watanzania Polisi hatimaye wataona umuhimu wa kusafisha jina la Polisi mbele ya raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo hapo juu, ninalo eneo moja tu la kuomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nikiomba anisaidie kunipatia kwa ajili ya wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu inahusu, uhusiano kati ya Jeshi la Polisi na Sungusungu. Sungusungu hususani katika eneo kubwa la kanda ya Ziwa na Shinyanga, “Usukumanji” wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana hasa katika kupunguza kasi ya wimbi la wizi na ujambazi! Kuna kipindi ilifikia katika maeneo yaliyokuwa na ulinzi imara wa sungusungu mtu angepoteza sindano au wembe hupelekewa nyumbani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la sungusungu wengi wao hawakuwa wameenda shule, haki zao hawazijui na hata mipaka ya kazi zao wakawa hawazijui! Kupitia mianya hii Polisi bila kuangalia matokeo mazuri ya kazi zao wakawa wanafutilia makosa yanayotendwa na Sungusungu katika shughuli zao! Sungusungu kupitia makosa yao wengi wakalundikwa jela, jambo ambalo linakatisha tamaa wananchi na hasa Jeshi la Sungusungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kile nilichokuwa nikikitegemea hakikutokea! Binafsi nilitarajia sana Jeshi la Polisi lingalitambua kwanza ubora wa wananchi wenye kuungana katika Sungusungu katika ulinzi wa raia na mali zao na wakajikita katika kuwelekeza Sungusungu kwa vipi wanaweza kuondokana na matatizo ya kukiuka taratibu na sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mheshimiwa Waziri kadri muda utakavyomruhusu aeleze japo kwa kifupi lini na kwa utaratibu gani husiano kati ya Jeshi la Polisi utaimarishwa. Naomba sana utaratibu huo urejeshwe mapema ili kurudisha haraka iwezekanavyo imani ya wananchi kwa Jeshi la Polisi na sungusungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Lawrence Masha kwa hotuba yao, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote. Ni hotuba nzuri iliyojibu kero za wananchi katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia za panya kwenye mipaka yetu. Naomba nianze na swala la wahamiaji haramu wanaoingia nchini mwetu. Tatizo hili ni kubwa na baya sana kwa kuwa mhamiaji haramu ni hatari na wengine wanakuja kufanya uhalifu na ni majambazi. Kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi wasio waaminifu ndio wamewafanya kuwa mradi wao kuwapitisha kwenye njia za panya (*panya route*) na baadaye

wakishaingia wanawaweka kwenye nyumba mbovu ndiko wanakolala na usiku hufanya mambo yao.

Vile vile hizi njia za panya zinaingiza na kutoa nje ya nchi bidhaa mbalimbali ambazo hazilipiwi ushuru. Je, sheria zilizopo ni kwamba hazitoshelezi au ni vipi? Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti maeneo haya ya mpakani pamoja na wale wanaobinika kuwaingiza wahamiaji hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inapoteza mapato mengi sana kutokana na bidhaa zinazopitishwa kwenye njia za panya mipakani. Kwa nini Serikali isianzishe vituo vidogo vidogo vyta Polisi, Uhamiaji na T.R.A. kwenye njia zote za panya zilizoko mipakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Askari wetu wanalala mipakani kulinda wahalifu hawa na mali za magendo na bado mali zinapita kila saa na wahamiaji huko huko wanapita. Ni vema Askari na TRA wawepo pale kwa ajili ya kukusanya mapato. Hili litaleta maana kuliko kusema (*panya route*) kila siku ambazo hazina faida. Tunataka *panya route* sasa viwe vituo kamili, Uhamiaji, Polisi na TRA na Serikali ipate mapato na wahamiaji haramu wadhibitiwe huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mirungi, tangu Serikali ilipopiga marufuku kutokuingiza miraa nchini. Serikali imefanikiwa au Serikali imepata faida gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili linalimwa Kenya, Uganda na Somalia, lakini walaji wako Tanzania. Askari wetu wanalalala mpakani kulinda miraa isipite mbona inapita tena kwa wingi sana. Je, huu sio mradi wa Askari wasio waaminifu? Ni ajabu sana kuwa biashara ya miraa sasa hivi inafanyika mpaka vijijini na kina mama wengi sana ndiyo biashara yao na hawalipi ushuru. Je, Serikali inapata faida gani? Nchi za Kenya, Uganda wanaendelea kulima kwa wingi na sisi tunazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iachie huru mirungi ipite wananchi waache kukimbizana na Askari mipakani. Hakuna jinsi ya kudhibiti miraa maana itaingizwa tu. Kwa nini wasiachiliwe huru ili watakapopita mpakani walipie ushuru na Serikali ipate mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwepo na utaratibu wa kuwazuia wageni kuingia na kwenda kufanya biashara machimboni. Hasa wageni wawekezaji wanaokuja kufanya biashara ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipige marufuku wageni kuhamia migodini mfano wageni wengine siyo waaminifu. Kwa mfano, wageni wanaotoka Senegal, Srilanka, Kenya, Uganda, Zambia wanaleta madini *fake* wanapofika eneo la machimbo wanawapatia wachimbaji wadogo wadogo ili wauze. Atakapokuja mnununu na fedha zake hununua bila kujua ni madini *fake*. Atakapokwenda, kuuza ndipo anapogundua kuwa siyo madini na hivyo utakuta amepoteza fedha nyingi kwa mamilioni. Wakati huo huo tunapoteza sifa ya nchi yetu na sifa ya madini yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali izingatie hilo. Ahsante sana, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa njia hii ya maandishi. Hivyo napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri/Naibu na Wakuu wote wa vyombo vyaa usalama na watendaji kuanzia Katibu Mkuu na watendaji wote.

Kazi kubwa wanayoifanya, imeonekana na matunda tunayaona ingawa ni kazi ngumu sana, labda tu niwatie moyo kwa kusema *Aruta Continuer*, mapambano bado kabisa, wafunge mkanda wasitazame nyuma wala maslahi, watangulize u-zalendo na mapenzi makubwa kwa Taifa lao. Kwani hata walioijenga Roma hawakuweza kufaidi chochote na hawakuwa wanalala walijitoa kwa maslahi ya vizazi vijavyo ambavyo ndio wanaitumia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mchango wangu leo ni mdogo tu ambaa ni maswali zaidi:-

(a) Hivi Wizara au Waziri anajisikia vipi kuona Askari wetu wanaishi maisha ambapo Askari na Mgambo hawana tofauti? Pengine hata Mgambo wana maisha mazuri zaidi kuliko Askari. Kwa nini Wizara isingie mikataba na mashirika ma *NSSF* ikajenga nyumba nzuri za kuishi Askari hawa?

Hivi Waziri, inakuwaje, Askari anayelinda jengo lenye thamani kubwa au banki yenye *billions of money*, au kumlinda kiongozi, halafu pa kuishi ni fedheha? Tafadhali sana naomba Wizara ichukue hatua madhubuti kujenga nyumba bora za watumishi hawa yaani Askari bila kupendelea mijini tu na Wilayani pia hata tarafani. Popote walipo isiwe Dar es Salaam tu.

(b) Je, inakuwaje takwimu za uhalifu zinaongezeka kuliko kupungua? Tueleweje kwamba kazi haifanyiki?

(c) Je, Waziri atakubaliana nami kwamba sababu kubwa ya ongezeko la uhalifu ni upungufu wa vitendea kazi? Huwezi ukategemea Askari aliye kwenye kituo cha Polisi kilichopo pale tarafa ya Ndago Iramba aletewe taarifa kuwa kuna uhalifu umetokea Uruguu au Mbelekesi, awahi wakati wa tukio kwa muda mwafaka kwani hana usafiri hata baiskeli hana, hivi atamkamata nani?

Je, wahalifu hao hawataendeleza uhalifu kwa kuamini kuwa Polisi hana meno ya kuuma? Tafadhali, naomba hatua zichukuliwe kupeleka vitendea kazi vituo vyaa Polisi hasa vyaa Tarafani, la hasha, nakiombea kituo cha Ndago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ajali za barabarani bado ni tatizo kubwa.

- (a) Je, ni kitu gani kinasababisha kuendelea kuwepo kwa ajali za barabarani?
- (b) Je, ni kwa nini mpaka sasa magari ya abiria (mabasi) bado milango ya *Emergency*? hayana
- (c) Je, kwa nini bado magari ya abiria (mabasi yaendayo Mikoani bado yanajaza sana na watu kusimama kwa kasha kupita vituo vyote (vizuizi) hadi kufika kuchukuliwa hatua na Askari wa barabarani? kubanana waendako bila
- (d) Je, Wizara haioni kuwa, kuongezwa kwa muda wa mabasi hadi saa 6.00 usiku, kunakaribisha ajali zaidi? kusafiri
- (e) Je, dereva wa gari la abiria anatakiwa kuendesha masaa mangapi?
- (f) Je, ni sababu zipi zinazopelekea wahamiaji haramu kuvuka mipaka na kuingia nchini?
- (g) Je, Wizara inatoa msimamo gani juu ya viongozi/wa Bunge kujiendesha wenyewe na kusababisha ajali kwani mambo mengi walijonayo hayawapi nafasi ya kuwa makini waendeshapo magari kwa safari ndefu na badala yake Wizara itoe tamko la viongozi hawa waendeshwe na madereva wenyewe sifa na walioajiriwa na Serikali? Ili kupunguza vifo vya viongozi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya ujumla, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara mbalimbali na Kitabu cha taarifa ya hali ya uhalifu nchini, January hadi December, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nauelekeza Polisi na Magereza. Polisi inalalamikiwa, mwaka 2007/2008 malalamiko ya jumla Kiwizara yalikuwa 1166, kati yake 1164, au 99.8% yalihusu Polisi juu ya:-

- Ubambikizaji wa kesi;
- Ucheleweshaji wa upeletezi; na
- Uporaji wa mali na fedha za watuhumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lalamiko lingine kubwa la wananchi ni watuhumiwa kuachiwa wanapokatwa na wananchi. Lakini kwa nini malalamiko haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi na haki za Askari Polisi.

- Masuala ya kiutumishi (hasa Askari rank za chini).
(Utumishi wa Polisi na utumishi wa umma)
 - Pongezi *IGP* Said Mwema kwa kuanzisha harakati za haki za Polisi.
- Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira. Kuajiriwa, kutambuliwa na kustaafu:-
- *Probation* ya miaka 12 ndiyo anaajiriwa = kibarua for 12 years.
 - *After 12 years* achague aingie pensheni au *gratuity* (mkupuo)
 - *Aki-opt Pensheni* - mpaka astaafu ndipo apate malipo - akifariki kabla halipwi: hawa ni wengi.
 - *Aki-opt Gratuity* - anaacha kazi wakati wowote na hulipwa
- Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu unawatia majaribuni Askari, mpaka Askari apate cheo cha *Assistant Inspector* ndiyo anaingizwa kwenye masharti ya utumishi wa umma.
- Nyongeza ya mishahara ikigota miaka sita (6) halipwi tena, kwa nini?
 - Kwenye pensheni watumishi Serikalini huchangia 5% na Serikali 5%, lakini Polisi huchangia zote 10% yeye peke yake, kwa nini?
 - *Fomular* ya pensheni ya Polisi iangaliwe upya. Utumishi wa miaka 25 analipwa pensheni ya Shs. Million 3 na NISHANI, afadhali apewe mabati badala ya nishani! Polisi hukaa hadi miaka 15 bila kupandishwa daraja, i nawakatisha tamaa.
- Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kuitumishi/uendeshaji:-
- Askari hawana Bima ya Afya, hupewa 200,000/= kwa mwaka (=17,000/=) kwa mwezi kwa kigezo kipi?;
 - Polisi wanalipwa *house rent allowance* Shs.1,500/= kwa mwezi!;
 - Madeni ya miaka mingi ya uhamisho na safari za kikazi hajalipwa;

- Askari akituhumiwa anaadhibiwa mara mbili, anafukuzwa kwanza, halafu Mahakamani. Hata akishinda kesi hawezi kurudi kazini. Hakuna chombo cha kutetea Askari. Ma-*OCD* wapewe mafungu Wilaya zao;

- Tatizo la nyumba za kuishi Askari, 80% huishi uraiani;
- Magu Barracks;
- Umeme nashukuru;
- Ukarabati umefanywa nusu;
- Vyoo viwili vinahitajika *urgent*; na
- Tunaomba gari la pili Wilaya ya Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza (Magu). Namuomba Mheshimiwa Waziri/Naibu Waziri aje Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la wananchi:-

- Wafungwa na mahabusu wa muda mrefu watengenezewa utaratibu wa kuonana faragha na zao ili kuepusha matatizo ya Ukimwi na
- Tatizo kubwa la usafiri. KIA moja mbovu mbovu. Magereza Magu ipate gari moja kati ya 64 yatakayonunuliwa 2008/09.
- Kuna *typewriter* moja tu ambayo haifanyi kazi vizuri.
- Nyumba za Askari, familia inaishi kwenye chumba kimoja na sebule moja. Serikali iwajengee nyumba.
- Choo cha Askari ni kibovu kinahitaji kufunikwa.
- Umaliziaji wa ukuta, ofisi na *store* ya sehemu ya akina mama (5,000,000/=)
- Maji upande wa gereza la akina mama (200,000/=)
- Rangi mabweni ya wanaume (200,000/=)
- Umeme Askari waliingiza kwa fedha yao; warudishiwe

- Wanaolisha mahabusu hawalipwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeletewa juzi ujumbe wa simu ufuatao:-

“Mheshimiwa Mbunge naomba unisaidie suala langu. Mimi ni Mwalimu Maela N. Maela niko Magu. Nilivamiwa na majambazi na kukatwa vidole vya mkono wangu wa kulia na hivyo kupata ulemavu. Lakini naambiwa sipaswi kulipwa fidia kwa kuwa nilikuwa nyumbani na si muda wa kazi. Nisaidie maana nazungushwa bila majibu”
Mheshimiwa Waziri, naomba unisaidie mwalimu huyu nimjibu vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja tena.

MHE. MAIDA H. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania pia kwa watendaji wa vyombo vya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la madai ya fedha za Askari Polisi Kisiwani Pemba. Mheshimiwa Waziri atakumbuka kuwa tokea Julai, 2005, japo madai mbalimbali ya Askari hao na mwaka huu wa 2008, Askari hao waliletewa vocha na wakatakiwa kuweka saini zao kama kawaida ya taratibu za malipo. La kushangaza baadaye walipatiwa taarifa kuwa vocha zimekosewa hazifa kufanyiwa malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo hii Askari hao bado hawajapatiwa fedha hiyo na vocha hizo zitakapofanyiwa ukaguzi zitathibitisha kuwa tayari wameshalipwa na wakati bado hawajalipwa. Je, Mheshimiwa Waziri analifahamu hilo na kama halifahamu, naiomba Wizara iweze kufuutilia haraka suala hilo ili Askari hao waweze kupatiwa malipo yao.

Kama tunavyojua kuwa Askari ni watu wenye kazi ngumu nchini katika kutafuta usalama wa nchi. Kuhusu suala la makazi bado ni kikwazo mazingira wanayoishi ni duni, mishahara vile vile hairidhishi kutokana na kazi zao wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Wizara kwa kuanza na ukarabati katika baadhi ya majengo na kwa kushirikiana na taasisi za fedha nchini ikiwemo NSSF kwa kujenga magorofa 30 yakiwemo yale ya Zanzibar. Lakini pamoja na Wizara kuanza na ukarabati huo na ule ujenzi wa magorofa hayo bado Wizara imekabiliwa na upungufu wa makazi ya Askari kulingana na Askari tulionao nchini. Naiomba Serikali katika maandalizi ya bajeti kila mwaka kuanza kuifkiria Wizara hii kwa kuiongezea fedha angalau kufikia nusu ya matatizo yanayoikabili. Mambo ni mengi muhimu ambayo yanasisimamia katika kuleta usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu sana kwa Wizara hii ambapo Askari tunawatumia katika ngazi mbalimbali ikiwemo, kulinda viongozi wetu wa nchi, usalama

wa raia na mali zao ni vyema bajeti ikawa ya kuridhisha. Askari walio wengi wamekuwa na malalamiko mbalimbali ambayo yamechukua muda mrefu kutatuliwa. Haya yanaweza kusababisha rushwa ndani ya Jeshi, ujambazi ndani ya Jeshi, wizi ndani ya Jeshi, mauaji ndani ya Jeshi na mwisho kutokuwa na imani na Serikali iliyoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ofisi, viti na meza navyo pia haviridhishi au hakuna kabisa, baadhi ya ofisi nyingi hazina umeme, hamna zana za kutosha au uduni wa zana hizo, simu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuona umuhimu wa Wizara hii kwa kuipangia bajeti inayostahiki kulingana na kazi wanazozifanya nchini. Mkoa wa Kaskazini Pemba yapo majengo mengi eneo la Polisi laini ambayo yamehamwa kutokana na hali ya upasukaji na kuwa hatari kwa makazi pia eneo la Konde ofisi hairidhishi kabisa zikiwemo nyumba katika eneo hilo. Naiomba Serikali kuliona tatizo hilo kubwa katika maeneo ya Matangatuani, Konde na Polisi laini katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ni aibu hata kumleta mgeni kukagua maeneo hayo. Kipindi cha Mheshimiwa Mwapachu alipokuwa Waziri wa Usalama wa Raia alifika kuziona katika maeneo yote niliyoyataja.

Kuhusu ajira katika Jeshi letu la Polisi, napenda kukumbushia kuwa mara nyingi tunapochukua vijana wa kuijunga na Jeshi hilo vigezo vinavyotumika ni kuanzia waliomaliza shule mwaka mmoja au miwili tu au umri wa miaka 25. Naiomba Wizara kuona kuwa bado nchini tunao vijana wengi amba wanao uwezo wa kumudu kazi hizo na wameshapita kiwango hicho. Naishauri Wizara kuweza kuchagua angalau baadhi ya vijana hao amba hawapo katika kiwango hicho kwa kuangalia uwezo walionao.

Kuhusu utaratibu wa wafungwa wanaopatiwa msamaha kila mwaka na Mheshimiwa Rais. Ni vigezo gani ambavyo vinatumika katika kutoa misamaha hiyo? Kwa sababu wapo wafungwa amba wametimiza miaka mingi sana lakini wanafikia hadi kumaliza miaka yao waliopangiwa bila kupata msamaha wowote. Lakini pia wapo wasiofikia hata mwaka mmoja wanapatiwa msamaha namuomba Mheshimiwa Waziri atupatie ufanuzi kuhusu jambo hilo, ni ubinaksi au ni rushwa vinavyotumika hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wakuu wote wa Idara mbalimbali katika Wizara kwa kutuletea hotuba nzuri ambayo inatia matumaini endapo itatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono kwa 100% na nitaomba kutoa ushauri kwa machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uchakafu kwenye Vituo vya Polisi. Pamoja na sifa nzuri ya usafi katika Jeshi la Polisi, kwa kweli uchafu katika vituo vya Polisi kikiwemo kile cha Moshi umekithiri pamoja na vioo ukutani lakini harufu inayokupokea

ukienda kutoa malalamiko *counter* inatisha huenda ni kwa vile mahabusu wako karibu sana, hapo sielewi. Hapa ninashauri hali hiyo irekebishwe kwani inatia aibu. Je, mahabusu hawahimizwi kufanya usafi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, miradi ya Magereza. Magereza imejizolea sifa kemkem kwa kutengeneza samani nzuri sana hata kufanikiwa kuwa wa kwanza kwenye nane nane mwaka huu. Ajabu ni kwamba Wizara yenewe ingetosha kabisa kutoa soko kubwa kwa bidhaa hizo lakini haifanyi hivyo. Hapa naomba kuuliza, hivi Magereza na Polisi hawana uhusiano? Ni kwa nini basi Polisi wasilipie *order* zao Magereza na kutengenezewa samani? Inasikitisha Polisi samani zao nyangi ni *imported* na hizidumu kwani matumizi yao ya mitulinga haihimili. Hapa ninaomba Mheshimiwa Waziri alitolee tamko swala la samani za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, upanuzi wa Chuo cha “CCP” Moshi. Ninatoa pongezi sana kwa chuo cha CCP. Pamoja na pongezi hizo naomba kuiuliza Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuboresha nyumba za Askari wafanyakazi wa pale ukizingatia kuwa chuo hicho sasa kimepanuka na kinafundisha hata Askari kutoka nchi za nje?

(ii) Ni lini uzio wa eneo lile utaimarishwa na kupafanya mahali pale parejee hadhi ya awali? Kuna *gate* zisizo na uzio, hii ni kichekesho kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natoa ushauri Jeshi la Polisi lilipe ankra zake za maji na umeme wakati muafaka kule Moshi – CCP, ni wasumbufu kwa MUWSA.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, naomba kumpongeza, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu Waziri kwa kuleta hoja hii mbele yetu, pia kwa uwasilishaji mzuri wa mpango wa bajeti yake kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nitoe mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

(a) Magari ya zimamoto. Utakumbuka kuwa Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya zimamoto kwa Halmashauri imbalimbali nchini. Lipo tatizo kati ya Halmashauri, hizi na Wizara ya Miundombinu ya kutaka magari haya yasajiliwe kama magari yaliyotumika wakati Halmashauri zinadai magari hayo ni mapya na yanakidhi hadhi na viwango, vilivyotolewa na Jeshi la zimamoto. Hii imesababisha utumiaji wa magari haya kuwa wa wasiwasi. Je, ni kwa nini, hali imejitokeza au kuna harufu ya ufisadi katika mradi huu wa magari ya zimamoto.

(b) Gari la Kamishna wa Zimamoto. Ili kuleta heshima katika Jeshi la zimamoto, nataka kujua ni lini Kamishna huyu atapewa usafiri wa uhakika.

(c) Jeshi la Magereza. Yapo malalamiko mengi kwa Jeshi hili yanayotolewa na Askari hawa, leo nitaongelea yafuatayo:-

(i) Kutopanda vyeo kwa wakati, Tume ya Utumishi wa Askari ni ya pamoja kati ya Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi. Kwa nini Askari upande wa Magereza wanachelewa kupanda vyeo ukiwalinganisha na wenzao wa Jeshi la Polisi, ingawa wote wamemaliza mafunzo wakati ule ule, naomba Jeshi hili lichunguze suala la vyeo.

(ii) Kuwakopa Askari – inatokea kuwa Askari anahamishiwa katika vituo zaidi ya viwili lakini haki zake za msingi hapati, hapati hela za uhamisho na kuelezwaa aendeleee kusubiri, si haki na si vyema kuwakopa Askari wanyonge. Hali hii irekebishwe haraka.

(iii) Suala la nyumba – baadhi ya nyumba za Askari wetu ni ndogo sana au ni vibanda tu na kwa familia zetu za kiafrika inabidi baadhi ya watoto walale sebuleni au uani hali hii haileti ustawi mzuri wa Askari wetu.

(d) *Ration Allowance.* Ninaomba sana posho za Askari ziongezeke kutokana na kupanda kwa gharama za maisha katika nchi yetu na zilipwe kwa wakati ili Askari asiwe na vishawishi.

(e) Makazi ya Askari tarajali. Askari wetu wanaotoka mafunzoni, wanakuwa chini ya uangalizi (*probation period*), ndio kipindi cha kuwajenga uzalendo wa kulinda raia na mali zao. Hawa vijana wanaishi maisha magumu, jengo wanaloofikia huwa linakuwa halina hadhi inayostahili. Nina imani kubwa sana na Serikali na Wizara hii jitihada kubwa za kuboresha nyumba za Askari wetu, pamoja na jitihada za ujenzi pale *Kilwa Road*, lakini ujenzi, wa jengo la Askari wanaoanza kazi ni vyema nalo likapewa kipaumbele.

(f) Nyumba za Askari Mbeya Mjini. Ninaipongeza Serikali na Jeshi la Polisi kwa kuanza ujenzi wa nyumba za Askari, ambazo kwa kiasi kikubwa zinalekea kwisha/kukamilika. Mradi huu endelevu lakini pia Jeshi liwe na azma ya kuomba viwanja katika miji inayopimwa na kupanykuwa, siyo yale ya enzi za mkoloni tu. Viwanja vya kujenga baadaye vipatikane. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja, kwa kuwa nina imani kubwa na utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya Askari kwa upande wa Tazara. Askari wetu wanafanya kazi nzuri ya kulinda uchumi wa nchi. Askari ndio wanaotumika kulinda miundombinu yetu ikiwepo Reli ya Tazara. Yapo malalamiko ya Askari wanao “escort” treni ya mizigo. Wanadai malipo yao ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali Askari hawa walilipwa asilimia 40% tu, bado wanadai asilimia 60% ambayo mpaka leo hawajalipwa. Hii ni haki yao ya msingi, kwani wameifanya kazi, ni vyema Serikali ikaangalia namna ya kulilipa deni hili la Askari.

Wakati wa kufunga mjadala nitapenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sababu za kutolipa fedha hizi, ni aibu kudaiwa (Serikali na watu wanyonge (Askari).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwani jitahada za kurekebisha baadhi ya mambo ni kubwa na inaonekana machoni pa watu.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongozi zangu za dhati kwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana ambayo wameanza kuifanya kwa ufanisi mkubwa tangu waingie katika Wizara hii. Mchango wangu wa leo utahusu Askari wa Jeshi la Polisi katika nyanja ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu iko katika kiwango cha juu kiusalama na kwa kuwa suala la michezo nchi yetu imekuwa ikijitahidi kufanya vizuri katika sekta hiyo. Je, kwa nini Wizara hii isifanye mabadiliko kwa Polisi wanaolinda katika Uwanja wa Taifa wakati wa mechi wawe wanawapa migongo wachezaji badala ya hali iliyopo hivi sasa ambayo Polisi wamekuwa wakiangalia mpira hali inayofanya hata wakati vurugu zinatokea wasiweze kujua chanzo na badala yake kukamata hata wasiohusika. Naishauri Polisi waelekeze macho yao kwa mashabiki badala ya kugeukia kuangalia mpira.

Lipo pia suala la kuwepo na baadhi ya Polisi wanawake wasio waaminifu ambapo hufanya mambo yanayoonekana kwa kweli kuwa kama wizi kwani wamekuwa wakipewa posho za usafiri na stahili zote pindi wanapotakiwa kuhamia sehemu fulani. Hata hivyo, baada ya kukaa kwa muda mfupi hufanywa mpango tena wa kurejea sehemu waliyotoka na kudai posho nyingine Gereza usafiri na stahiki za uhamisho. Wengi wao huwa wanatoa sababu za kufuata waume zao au familia. Hii ni kudhalilisha wanawake kwani pesa hizi ambazo wanalipwa mara mbili zingeweza kusaidia kufanya kazi nyingine za kuboresha maisha ya Polisi wengine. Je, Wizara iko tayari kufanya utafiti kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine la msamaha wa Rais kwa wafungwa suala hili, naomba liangaliwe upya kwa maana mara nyingi baada ya msamaha kumekuwepo na ongezeko kubwa la vitendo vya uhalifu. Naomba Wizara iwe inafanya utafiti wa wafungwa watakaosamehewa kabla ya uamuzi wa Rais kwani wengi wao hivi sasa huwa ni kero na wamekuwa baada ya msamaha hurudi tena katika Magereza kwa kutenda makosa mengine wakiwa uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu Wizara hii kupata tatizo la vijana wasomi wenye vyeo ambao wanaamua kuondoka katika Jeshi la Polisi kutokana na viwango vidogo vya mshahara. Naomba Serikali ituambie ina mikakati gani katika kuhakikisha kuwa vijana hawa wanakuwa na vyeo vya juu kutokana na elimu zao wanabaki. Naomba majibu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichangie hoja iliyotolewa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya kuchangia, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Kego Masha, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, Mkuu wa Jeshi la Polisi, (*IGP*) Saidi Mwema na watumishi wengine wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ilijoja maslahi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja hii umejaa zaidi maswali na mapendekezo kimuundo. Ukurusa wa nne na tano, unaonyesha kuwa kumekuwepo na ongezeko zaidi la matukio ya uhalifu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tabora, Iringa, Kilimanjaro, Ruvuma, Kagera, Shinyanga, Arusha na Pwani. Hotuba inasema ongezeko linachangiwa na kiwango kikubwa cha uhamiaji mijini ambalo haliendi sawa na ongezeko la Askari na kusababisha uwiano wa Askari kwa raia kuwa mkubwa zaidi uwiano huo umetajwa kuwa ni Askari mmoja kwa kila wananchi 1339, badala ya ule unaokubalika kimataifa. Maana yake Tanzania tunahitaji Askari Polisi wasiopungua laki moja ili kukidhi haja hii. Kwa hali hii, naomba Wizara inieleze ina mkakati gani wa kuhakikisha angalau nusu ya idadi inayohitajika inafikiwa? Ninaomba majibu wakati Waziri (anatoa hoja) atakapokuwa akihitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekiri kuwa mwaka wa jana wa fedha (2007/2008), ukurasa wa sita, ilitumia 91% ya bajeti iliyokuwa imetengewa. Je, Wizara haioni kwamba asilimia hizo tisa zilizobaki zinaweza zikaanza kutumika kuongeza ajira ndani ya Jeshi la Polisi? Je, asilimia hizi pia kwa nini zisitumike kuboresha marupurupu ya Askari Polisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kutofautiana na wenzetu wa nchi ya Marekani kisheria, bado yapo mazuri tunaweza kuyatumia kwetu. Hapa naongelea waendesha mashtaka.

(a) Imekuwa ni kawaida kwa Polisi kutumika katika kuendesha mashtaka ya Serikali/au kwa niaba ya Serikali. Hata hivyo Bunge lako Tukufu lilikwishapitisha sasa mashtaka haya yaendeshwe na Wanasheria wa Serikali, zoezi hili bado linaonekana halijakamilika. Je, Serikali haioni haya ya kuhakikisha zoezi hili au mabadiliko haya yanakamilika?

(b) Kwa nyongeza tu je, Serikali haioni ni vizuri au wakati mwafaka kuboresha uendeshaji wa mashtaka kwa kuwa na Idara ya Mawakili Watetezi wa Umma (*Public Defendants*)? Kuwepo kwa “*Public Defendants*” kutasaidia utendaji wa haki kwa kupatikana kwa utetezi wakiuweledi (*professional*) na kisheria kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kuajiri mawakili wa utetezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linalokera ni umri wa kustaa fu kwa wale “*Non-Commissioned Officers*”. Yapo matukio mengi ya ujambazi, mathalan, lile tukio la Ubungo, ambayo yameonekana kuhusisha Askari Polisi wa vyeo vya chini. Wengi wao

wameonekana kuwa na hali mbaya ya maisha, hasa baada ya kustaaifu. Ni maoni yangu kwamba, Wizara iachane na taratibu za majeshi ya nje ya Polisi, hususan kwenye umri wa kustaaifu. Askari wetu wanastaafu wakiwa vijana na hawajajiandaa kustaaifu. Matokeo yake wanachanganyikiwa hawajui hata pa kuanzia katika maisha ya kiraia na matokeo yake ni kujihusisha na ujambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la “*Dual Nationality*” ama uraia wa nchi mbili. Mimi binafsi naunga mkono suala hili, kwa sababu moja kuu. Kuwepo kwa uraia wa namna hio kwa nchi yetu, “*dual nationality*” inaweza kutuletea faida kubwa kiuchumi. Wako Watanzania waliokwisha ukana uraia wa Tanzania lakini wangependa sana na wanayo mitaji ya kuwekeza nchini.

Pia wapo raia wa-kigeni ambaao nao wana mitaji na wangependa kuwekeza nchini mwetu. Lakini makundi yote haya mawili yangependa kufanya hivyo kwa kufuata taratibu za uwekezaji zinazomlinda na kumpendelea Mtanzania. Mitaji hiyo tunaihitaji sana ili tuongeze pato la nchi yetu kupitia makusanyo ya kodi, ongezeko la ajira na ukuaji wa soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwa dhati kabisa kuunga mkono hoja.

MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kujibu maswali ya papo kwa papo kwa umahiri wa hali ya juu, hongera sana. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa utendaji wao wa kazi kwa muda huu mfupi waliokabidhiwa Wizara hii. Napenda kuwapongeza na kuwapa moyo waendelee na moto ule ule. Maneno machache kazi zaidi, kazi ya Wizara hii ni ya utendaji wa papo kwa papo. Inapotokea kuzungushwa zungushwa maana yake ni kuweka ufa wa rushwa, hasa kwa wale hawataki kutoa, hongereni sana. Naomba Wizara inapotoa usafiri hasa kwenye Majimbo yetu ya vijijini, basi tufikirieni zaidi. Wilaya ya Nzega ina Majimbo mawili (2) ya Bukene na Nzega. Wilaya ina kata thelathini na saba (37) na ukubwa huo tuna gari moja tu tena bovu ambalo liko Nzega Mjini. Bukene ina kata kumi na sita (16) kata zingine ziko maporini sana, Askari tunao wachache, tunaomba tuongezewe lakini haswa usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunatoka ujambazi wa kutumia silaha, Bukene hapo hapo Makao Makuu ya Jimbo, Askari wapo walipopata habari majambazi yakawa yamehamia kata ya Kahama ya Nhalanga, mchana yanajificha maporini, usiku yanafanya kazi zake. Matukio ya namna hii yako kwenye Jimbo zima, Askari hao wachache wanawenza, ila hawana usafiri. Gari litoke Nzega tena bovu ni leo lazima watakuta majambazi yamekimbia. Naomba tupewe angalau pikipiki sita yaani kila tarafa (nina tarafa mbili), zipate pikipiki tatu tatu yaani zije kabisa zimeandikwa ili zifike tarafa ya Mwakalundi, Pikipiki tatu na tarafa ya Bukene pikipiki tatu pia. Naamini pikipiki hizi zitatusaidia kuondoa ujambazi katika Jimbo langu. Natanguliza shukurani “*in advance*” kwa kupewa usafiri huo na kuongezewa Askari (ajira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sasa kuna ulinzi shirikishi na Askari Polisi na Sungusungu. Lakini cha kushangaza wakati mwingine pale Igusule mfano Sungusungu wanawakamata wahalifu/majambazi/wezi. Wakiwapeleka Polisi wanaachiwa kwa upelelezi, hapo hakuna mjadala ni sahihi.

Kinachosikitisha hawa watu wanawageuzia kibao wana bambikiziwa kesi Sungusungu, hasa Kata ya Igusule. Hii inawavunja moyo Sungusungu. Tunataka ulinzi shirikishi kweli, nasema haya yametokea kwa Askari Polisi toka Isaka, ambapo ndio karibu na Igusule, lakini Isaka ni Kahama. Wakati mwingine Askari wanatoka Kahama, naomba uchunguze hili na vitendo hivi vikomeshwe. Haki itendeke na tusiwavunje moyo Sungusungu hasa tunapoenda kwenye ulinzi shirikishi.

Naomba niwapongeze Kanisa la Siloam, pale Mbezi Makonde, Dar es Salaam likiongozwa na Mtume Munuo, kwa kazi nzuri waliofanya ya kukomesha na kuokoa roho yaani vijana waliokuwa majambazi, wavuta bangi, wakijichoma madawa ya kulevyta na wengine walikuwa wakiuza na kunywa gongo na kadhalika. Vijana arobaini (40) wameokoka na kesho 01/08/2008 wanaanza mafunzo ya Biblia. Nalipongeza sana Kanisa hili linaloabudu kwa kweli na roho. Namuombea Mtume Munuo na familia yake maisha marefu ili aweze kusaidiana na Serikali kurudisha maadili hasa kwa vijana wetu. Ni muujiza wa ajabu, vijana arobaini (40) wanatoa ushuhuda wenyewe jinsi walivyokuwa wanakaba na kadhalika, sehemu ya Ferry, Jangwani na kadhalika, sifa namrudishia Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii na Serikali kwa ujumla ifanye kazi na Kanisa hili, lishirikiane na Mtume Munuo, naamini vijana wataokoka, watu/wafanyakazi waokoke, hivyo tutakuwa tumepunguza au tumemaliza kabisa mafisadi, wala rushwa, waovu wote mbalimbali wote watabadilika kwao nasita kusema kwa Jina la Yesu, lakini ndio ukweli, kwa kifupi, tushirikiane na taasisi hii na nyingine za aina hii zinazofanya kazi ya kuwabadilisha vijana na wanawake skimu za maisha ili wakitoka hapo ni raia wema. Akiwezeshwa naamini Tanzania yetu itabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii na pia nampongeza sana *IGP*, Saidi Mwema na Makamanda wote wa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanazofanya za kupambana na uhalifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa maeneo ya Magomeni Mapipa – Jangwani na Kigogo Round About kwenda *Magomeni Traffic Light*. Tatizo la kutumia njia tatu ili kuondoa msongamano wa magari. *Kigogo Round About* haiko kwenye utaratibu wa njia tatu, naomba Askari wa *traffic* wasimamie suala hili na kuwakamata wanaokiuka taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna ajali na usumbufu mkubwa katika maeneo ya Magomeni – Jangwani wakati wa kutumia njia tatu. Naomba sana maeneo hayo yawe

na uangalizi wa kutosha wa Askari wa Usalama Barabarani ili kuondoa/kupunguza ajali wakati wa matumizi ya njia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujambazi wa kupora vitu kwa madereva hasa wanawake wanaposimama *Traffic Light* za *St. Peter – Osterybay*, kuna vibaka wengi eneo hilo hasa kuanzia saa tano usiku, ukisimama kwa ajili ya *traffic light* wanakuvamia wakiwa na mapanga, shoka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Jeshi la Polisi limshikishe adabu Askari wake wa Kituo cha Magomeni anayetoa siri za Polisi kwa wahalifu ili wasikamatwe au wakimbiye pale kunapokuwa na msako. Askari huyu ni hatari kwa usalama wa raia anayekwenda kutoa taarifa za uhalifu amekaa hapo miaka mingi na anawajua wahalifu wengi maeneo hayo ya Magomeni. Ukienda kutoa taarifa Polisi Magomeni kuhusu mhalifu na ye ye akiwepo ujue atamwambia mhusika muda huo huo kwa kumpigia simu. Hii ni hatari. Jina lake ninalo na ninamfahamu vizuri. Naunga mkono hoja.

MHE. HAMZA A. MWENEGOHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP* na watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ni kubwa sana. Wizara hii inajumuisha Polisi aina zote, yaani Polisi wa kawaida, *Traffic*, *FFU*, Uhamiaji, Zimamoto na Magereza. Dhana za kufanya kazi watu hawa ni ghali sana. Wafanyakazi hawa hufanya kazi za dharura kila wakati, wafanya kazi hawatoshi. Bajeti ambayo Wizara hii inatengewa ni ndogo sana. Wakati sasa umefika Wizara lazima ipangiwe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ni vema sana nikazungumzia masuala ya Jimbo la Morogoro Kusini. Jimbo hili ni kubwa sana. Kusini linapakana na Liwale, Lindi, Rufiji na Kisarawe. Kaskazini linapakana na Kilombero na Mikumi. Jimbo hili ni la maeneo ya milima mirefu ya Uluguru kwa upande wa kaskazini. Kwa upande wa Kusini ile sehemu ya *Seloms Game Reserve 1/3* ipo Jimboni. Jimbo lina wanyama wakali wengi kama simba, chui, tembo, mamba na wanyama wengi wakubwa na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo hili lipo umbali wa kilomita 194 toka Morogoro Mjini, Kituo cha Matombo cha Polisi kipo kilometa 75 toka Morogoro Mjini. Kituo cha pili cha Gomero kipo Kilomita 119 toka Matombo, vituo vyote hivi havina vyombo vyasafiri.

Kwa zaidi ya miaka mitano ninazunzumzia juu ya usafiri wa vyombo vyasafiri kazi. Polisi hawa wa Matombo na Kisaki Gomero wanatembea kwa miguu kwa mwendo mrefu sana na huku wakiwa wamebeba bunduki. Wahalifu wa kijambazi, magomvi makubwa, mapigano ya ugomvi kati ya wakulima na wafugaji. Naomba Wizara hii sasa inipe jibu la uhakika juu ya usafiri wa Polisi wa Matombo na Kisaki Gomero. Mimi sasa siombi gari, hata pikipiki zinatosha kusaidia Askari hawa. Naomba majibu ya uhakika. Naunga mkono hoja.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwa njia ya maandishi.

Kwanza napenda kuchangia matatizo makubwa mawili katika Gereza la Isupilo, tatizo la kwanza ni maji, tatizo hili ni kubwa na la muda mrefu sana. Ingawa matanki mawili tayari yapo lakini hayana maji ndani yake hivyo tunaiomba Wizara hii imalizie mradi huo.

Tatizo la pili ni umeme, tatizo hili lingeweza kutatuliwa kwa sababu umeme wa *grid* ya taifa uko kijiji cha Mtili, kijiji jirani tu na Gereza la Isupilo. Mimi nimefika mara nydingi Gerezani pale na Maafisa wa Gereza pamoja na wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo limenilazimisha kuandika mchango huu linamhusu Askari No. A.9622 SSGT HADHARAT MOLI. Yeye anafanya kazi katika Gereza la Isupilo, Askari huyu analalamika kuwa alichaguliwa kwenda katika mafunzo ambayo yeye yangemwezesha kupanda cheo na kuwa na nyota moja, lakini jambo linalomuumiza zaidi ni kuwa alipokwenda kwa R.P.O alimkatalia bila kutoa sababu zozote zile, ili haki itendeke, naona ni muhimu sana kijana huyo aende katika mafunzo yake kama alivyokuwa amechaguliwa hapo awali.

MHE. HAROUB S. MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia ila nina maombi machache yafuatayo:-

(1) Ofisi ya Mkoa Kusini Unguja. Jengo la ofisi hiyo ni chakavu sana ambalo linatia aibu kwa wapita nja kwani lipo barabarani kwa hiyo naomba likumbukwe.

(2) Magari mabovu ya Mkoa Kusini. Ofisi ya Kamanda wa Mkoa ina magari mawili ambayo yameharibika kwa muda mrefu na kutotengenezwa kwa ukosefu wa pesa. Hiyo ni hasara kubwa naomba fedha itolewe ili ziweze kufanya kazi.

(3) Nyumba za Askari Tunguu. Hali ya aibu na fedheha kwa makazi ya nyumba za Askari Tunguu namna yalivyo mabovu na hasa yalivyozungukwa na majengo mawili mazuri, Ofisi ya Bunge na Ofisi ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aje ajionee ili atoe maamuzi ya dharura na mimi niwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Polisi Nkasi liishe ili lifunguliwe. (Sitaunga hoja kama hakuna maelezo/ahadi ya kweli kweli)

Watumishi wa uhamiaji wasinyanyaswe wanapofanya kazi za upelelezi na kushika wahalifu wageni halafu viongozi wakubwa mfano, Waziri kuwabughudhi na kuwashika maofisa waliohusika. Watakuwa moyo na kuacha mambo yaende kiholela.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu huu kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wao wote. Pamoja na kazi yao nzuri wanayofanya Askari wetu wapo baadhi yao wanalitia dosari Jeshi la Polisi. Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu inaonesha kwamba mahabusu wengi katika Magereza nchini huwa wanabambikiziwa kesi. Hii sio tu aibu kwa Askari wetu bali pia ni maonevu wanayofanyiwa wananchi wetu. Hivyo basi, nashauri kwa Askari wetu kabla ya kumsingizia uwongo mwananchi ili apate nafasi ya kumuonea, ajiulize kwanzam je, kama ni yeche au mtu yeoyote wa karibu naye kwa mfano baba, mama, mjomba na kadhalika anafanyiwa hivyo angejisikiaje, angeona vizuri?

Mtu anapokuwa muovu hata apate kitu gani bado ataendelea kuwa muovu tu. Lakini kitendo cha kutowajali Askari wetu kwa kutowatimizia maslahi yao ya lazima na hivyo kupelekea maisha yao kuwa duni, yanapelekea baadhi ya Askari hao kuingia katika dimbwi la vitendo viovu kama rushwa na kadhalika. Takwimu zilizooneshwa katika kitabu cha “Taarifa ya Hali ya Uhalifu nchini Tanzania – Januari hadi Desemba, 2007” katika jedwali Na.3.3, kuhusu Mchanganuo wa watu walioathirika kwa ajali barabarani ukurasa wa 37 kule Zanzibar zinatisha sana. Watu 824 walikuwa kwa mwaka 2007 na watu 954 walijeruhiwa.

Zanzibar ina idadi ndogo ya watu hata kuliko Wilaya tu ya Tanzania Bara lakini inaonesha vifo vya watu 824 ambayo kwenye jedwali hili ni kubwa kuliko Mkoa wowote wa Tanzania Bara. Hii inaonesha kwamba pamoja na kuwa ajali haina kinga lakini hali nzima ya usalama barabarani bado haijaridhisha. Mheshimiwa Waziri alione hilo na ajitahidi kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tukubaliane tu kwamba maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Job Ndugai alipokuwa anasitisha shughuli hizi leo mchana alitoa mwelekeo kwamba, pamoja na hoja hii kuwa na wachangiaji wengi, lakini inatupasa tuwe na wachangiaji hawa wawili kwa jioni ya leo. Tukumbuke kwamba hoja hii ina karibu mafungu matano ya kuamuliwa hapa ndani leo. Kwa hiyo, tunahitaji muda wa kutosha kidogo.

Kwa hiyo, baada ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii iliyoanza tangu jana, sasa nitamwita mto hoja aweze kuchangia, lakini atatanguliwa kwanza na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutumia dakika 35 halafu nitamwita mta hoja mwenyewe, Mheshimiwa Waziri yeche atatumia muda wa takribani

dakika 40, hayo ndiyo makubaliano waliyoyafanya ndani ya Wizara na baadaye tutaingia kwenye hatua ya kupitia mafungu ya Wizara hiyo.

Sasa baada ya hayo naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika 35.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii nitoe shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimetolewa katika siku hizi mbili tangu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Lawrence Masha alipoitoa hoja ya Wizara yetu. Kubwa niseme tu kwamba wachangiaji wamekuwa wengi hasa ukiangalia michango ya maandishi maana kuna takribani michango 130 na ukiongeza ya wale waliochangia kwa kuzungumza nafikiri ni takribani 28, lakini hayo namwachia Mheshimiwa Waziri atakapokuja atazungumzia juu ya wachangiaji wa Wizara yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba hakika mchango huu wa Wabunge waliokuwa wengi kwa maandishi na wengi waliotaka kupata nafasi ya kuongea, kwa kweli umenipa faraja kubwa sana, kwa sababu imeonyesha kabisa Waheshimiwa Wabunge wanaithamini sana Wizara hii na wanaona mchango wake ulivyo mkubwa katika Taifa letu. Kwa kweli niseme kwamba uchambuzi uliofanywa hapa katika siku hizi mbili ulikuwa ni uchambuzi mkubwa kuhusu matatizo ya Wizara yetu.

Inanipa faraja sana kuona Waheshimiwa Wabunge wameweza kubaini mapungufu tuliyonayo lakini faraja zaidi kuona wengi wametoa mchango wao kuona ni jinsi gani tunawenza tukayatatua matatizo ndani na nje ya Wizara yetu. Hakika naomba niseme kwamba katika hizi siku mbili nimejiona ni kama mwanafunzi katika kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge na kusoma yale ambayo wametuandikia kimaandishi. Maana ilikuwa ni darasa tosha katika siku hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana shaka mimi naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge yote wanayoyasema hapa ni uwakilishi mkubwa wa wananchi ambao mnawawakilisha kama sisi tulivyo kwamba na sisi tuna Majimbo yetu, kwa hiyo, ningesema kwamba mnayoyasema kwa uhakika ni yale ambayo wananchi wenu wamekutumeni mje myaleta hapa katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ambayo yamezungumzwa jana na leo kwa uhakika sio matatizo ambayo yametokea kwa siku moja katika Wizara hii. Wale ambao wamefuatilia na wale ambao wamekuwa katika Bunge muda mrefu na wale ambao wamekuwa Serikalini muda mrefu haya ni matatizo kwa kweli ambayo yamejengeka katika kipindi cha muda mrefu, lakini napenda kusema kwamba ipo azma na ipo jitihada kubwa hasa katika uongozi uliopo sasa hivi kuona kwamba haya matatizo yanatatuliwa.

Lakini kwa wingi wa matatizo kama mlivyoyaona na kwa ufinyu wa hali ya fedha tuliyokuwa nayo itakuwa ni kusema uongo kwamba matatizo yote Waheshimiwa Wabunge waliyoyataja jana na leo yanaweza yakatatuliwa kwa wepesi au kwa haraka

sana. Lakini kubwa, naomba mtuamini na muamini hasa Mheshimiwa Waziri Masha kwamba azma na nia ipo ya kujaribu na kwenda kabisa utakavyoweza na tutakavyojaliwa katika kutatua matatizo tuliyokuwa nayo kwa sababu hatuzungumzii matatizo ya kitu kimoja, tunazungumzia matatizo yanayotukabili katika Taifa zima katika mipaka yote ya Taifa letu maana unapozungumzia Polisi unazungumza Taifa lote, unapozungumzia Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji ni unazungumza Taifa lote vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe kusema kwamba matatizo tuliyonayo ni mengi, lakini tutajitahidi kwa dhamira na nia nzuri kuona kwamba tunapata majibu katika masuala hayo na katika changamoto ambazo zinatukabili. Hapana shaka Bajeti tuliyonayo ndiyo Bajeti hiyo tulijoyaliwa kuwanayo. Maana yake Bajeti ya Serikali ni hiyo. Kwa hiyo, inabidi igawiwe katika Wizara zote zilizopo na inabidi iguse katika maeneo yote ya Taifa letu. Kwa hiyo, kiasi tulicho jaliwa ni hicho na kutokana na kiasi hicho, basi ninasema kwamba kwa kweli haitakuwa wepesi sana kusema tutawenza kuyatatua matatizo haya. Lakini naomba pia kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba kweli michango ni mingi na mtaniwia radhi kama sitajaliwa kutaja kila mchango wa kila Mbunge, lakini niseme kwamba tutajitahidi kadri tuwezavyo tuweze kuwajibika kimaandishi, wale wote ambao wamezileta hoja zao hapa Bunge jana na leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezileta na ambazo kwa kweli ni muhimu sana katika mtizamo wetu, sisi tumezigawa katika makundi. Kuna zile hoja ambazo zimezungumzia vitendea kazi katika maeneo yote yale, kuna hoja ambazo zinahusu maslahi ya watumishi kwa maana askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na kadhalika, kuna hoja zinazohusu makazi kwa maana nyumba wanazoishi askari, kuna zile zinazohusu rasilimali watu halafu upande kwa mfano wa Magereza wamekwenda zaidi kuhusu uzalishaji katika Magereza, usafirishaji na usafiri Magerezani na mambo mengine ambayo nimesema hapo awali kuhusu maslahi na vitendea kazi ambayo yanagusa katika Idara zote ambazo zinahusu Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitaanza na sio kwamba naanza kwa umuhimu wake, lakini nitaanza kwa jinsi ambavyo tuliyokuwa tunaandika na jinsi ambavyo tulijiandaa. Waheshimiwa Mariam Kasembe, Mohamed Aziz, Mwanawetu Zarafi, George Simbachawene, Fatma Alli na wengine wamezungumzia kuhusu masuala ya askari polisi, wajengewe nyumba za kuishi ili wasiendelee kuishi uraiani. Hilo hakika katika Bajeti yetu au katika hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri jana lilikuwemo na akaeleza ni vipi tunataka tushughulikie suala hilo. Ni kweli zipo hatari na kuna mambo ambayo sio barabara kwa askari kuishi uraiani na mengine mmeyataja Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, mimi nataka niseme kwamba hilo tumelizingatia na hatua za awali tayari zinafanyika na tunajitahidi katika njia moja ama nyingine kuona vipi tunaweza kwenda hatua kwa hatua tukaondokana na tatizo hilo ili maaskari waweze kutoka uraiani na waweze kuwa na makambi yao kama inavyokuwa desturi.

Mheshimiwa Stephen Galinoma ameomba kujengewa Kituo cha Polisi, huyu nimemtaja, lakini kuna wengi wameomba wajengewe vituo vya Polisi. Lakini niwarejeshe Waheshimiwa Wabunge kwamba jana katika hotuba yetu Mheshimiwa

Waziri ameелеza juu ya utaratibu ambao tulikuwa nao na kwa kweli kwa kuwa tatizo ni kubwa kiasi kwamba hatuwezi tukalifanya hili kwa mkupua na wala hatuwezi tukalifanya kwa wakati mmoja; litakwenda kwa awamu na tunaanza hivyo na zile Wilaya na ile Mikoa ambayo imejaliwa kwa mujibu wa taarifa ambayo tumeitoa, basi tutakwenda tukifanya hivyo taratibu ili kuona kwamba huko mbele tunakokwenda tunaweza tukamaliza. Maana yake kama nilivyosema haya ni matatizo, sio kwamba yameanza leo, ni matatizo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Fateh Saadi Mgeni na Mheshimiwa Rajab Mohamed Mussa walizungumzia kikosi cha wanamaji kiimashwe na nafikiri juu ya kikosi cha wanamaji kuimashwa, hili linaendana na suala ambalo kimaandishi tumepata kutoka kwa Mheshimiwa Mongella na nadhani hili atalizungumzia Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Diana Chilolo wamezungumzia juu ya ng'ombe 25 ambao wamesema kwenye michango yao wengine wa maandishi na wengine wa kuzungumza. Wamezungumzia kwamba ni lini Mheshimiwa Waziri atakwenda ili kumaliza tatizo hili?

Sasa kama tulivyosema katika jibu letu, maana swali hili liliwahi kuja katika Bunge na nilijibu mimi mwenyewe na swali la nyongeza alilijibu Mheshimiwa Waziri na alipojibu ni kweli tulikiri kwamba tatizo hili kweli limetokea kule Singida na Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba atakwenda Singida ili aweze kutazama hili suala linakwenda vipi.

Lakini napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Inspekte Jenerali wa Polisi hivi tunavyozungumza amekwishaunda Tume ya Maofisa toka Makao Makuu ya Polisi ambao wako Mkoani Singida kuchunguza suala hilo lote la hawa ng'ombe 25 na kuhusu suala la wale maafisa wawili ambao walifukuzwa kazi na nadhani wakati uchunguzi huo utakapomalizika taarifa hii italetwa rasmi kwa Wabunge husika kwa sababu hawa ni Wabunge wa Mkoani Singida na suala hili linawahu zaidi. Kwa hiyo, tutawapa taarifa hizo pindi tutakapopata ripoti hiyo kutoka kwa *IGP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir na Mheshimiwa Paul John Lwanji, wamezungumzia suala la kuhusu Serikali kuwalipa malipo ya uhamisho wanapohamishwa pamoja na familia zao. Lakini sio hao tu, wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kimaandishi na kusema kwamba malipo kwa maaskari wanakuwa hawalipwi wakati wanapohama kutoka kwenye stesheni moja kwenda stesheni na wanaambiwa kwamba walipe wenyewe pesa zao kutoka mifukoni mwao watakuja kurudishiwa baadaye au kupewa fidia na kadhalika. Sasa mimi naomba nijibu maswali hayo ya Waheshimiwa Wabunge kwamba nia ya Serikali ni kulipa posho ya askari kila anaposafiri kikazi au anapohamishwa kwenda kituo kingine cha kazi.

Lakini kutokana na upungufu wa kasma ya Serikali, hujitokeza kasoro za utekelezaji za hapa na pale. Hata hivyo, hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kuona tatizo hili kwa kweli linakuwa sio tatizo sugu au tatizo la kudumu. Niseme tu kwamba matatizo kama haya yanakuwepo, sio kwa sababu Serikali inataka mambo kama haya yatokee kwa

askari wake, nadhani Serikali isingependa kitu kama hiki kitokee. Sidhani kama Jeshi la Polisi linapenda jambo kama hili litokee; lakini ninaomba Waheshimiwa Wabunge mkubali na mzingatie kwamba ukitizama ufinyu wa Bajeti tuliyonayo na ukitizama mpangilio wa kazi za Wizara tulizonazo na ukatazama pesa ambazo tunazo za kusaidia mambo mbalimbali ya maendeleo hapa nchini, basi kidogo kwa kweli inakuwa ni taabu. Lakini ni jambo ambalo tunalizingatia na ni jambo ambalo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba linatokea sio kwa sababu ya nia mbaya, hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo linaendana sambamba na Waheshimiwa Wabunge waliouliza kuhusu kucheleweshwa kwa malipo ya kiinua mgongo kwa askari wanaostaafu na vilevile malipo mengine madogo madogo. Ni kweli tatizo la askari wanaostaafu kulipwa malipo ya kiinua mgongo siwezi nikalikana kwa sababu maaskari wenyewe wapo na nyie wawakilishi wa wananchi na askari ni sehemu ya wananchi hao, kwa hiyo, nina uhakika kwamba mnasema kitu ambacho mna uhakika nacho.

Nafikiri ingawa malalamiko yanakuwepo wakati mwagine zipo taratibu za ndani kwa ndani ambazo wakati mwagine zinakuwa hazifuatwi. Lakini zikishafuatwa, hakuna haki inayopotea na ndiyo maana unakuta katika pesa ambazo tumeweka katika Bajeti yetu lipo fungu kabisa ambalo linaonyesha kwamba yapo madeni ambayo Jeshi la Polisi linadaiwa ama Jeshi la Magereza linadaiwa na maaskari hao husika kwa matumizi kama haya ambayo yamefanyika. Tutakapopata Bajeti yetu ni kama kweli tunarudi kule kule kwa sababu kitu cha kwanza tutakachofanya katika mengineyo mengi ni kulipa baadhi ya haya madeni tuweze kuanza na mambo mengine. Kwa hiyo, unakuta kwamba kiasi ambacho tunakuwa tumepata kinaanza kutumika hata kabla hakijatumika katika shughuli nyingine ambazo tumepanga, lakini ni kwa sababu ya hali halisi hakuna njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Fatma Othaman Ali, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Dastan Mkapa, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa pia na wao wamezungumzia juu ya ujenzi wa vituo vya Polisi. Kama nilivyosema, awali wakati nilipokuwa najibu swali hili, nilisema kwamba ujenzi wa vituo vya polisi hujengwa kulingana na mahitaji ya vigezo mbalimbali, lakini kubwa zaidi ni kwamba hivi sasa Bajeti yetu ni finyu na kila Mbunge angependa awe na Kituo cha Polisi na hiyo ni haki yao kwa sababu suala la ulinzi ni suala muhimu. Ulinzi wa raia na mali zao ni haki ya kikatiba, lakini pia hiyo haki inaendana na uwezo ambao Serikali inakuwa nao. Kwa maana hiyo, ndiyo maana tunasema kwamba na hii azma mpya ya ulinzi shirikishi itabidi hata hivyo Wizara yetu sasa ya Mambo ya Ndani iwasiliane na TAMISEMI ili kupitia programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa kuwa na uwezekano wa kujenga vituo vya Polisi hasa katika Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Riziki Omar Juma wao wamezungumzia juu ya ajira za wanawake katika Jeshi la Polisi kwamba ni chache na kuna Wabunge wengine ambao wamezungumzia suala hilo. Ni kweli kwamba idadi ya wanawake wanaoajiriwa katika majeshi yetu hapa nchini likiwemo Jeshi la Polisi kwa kweli linatokana na historia. Lakini jinsi tunavyokwenda, unaona kabisa kwamba tunakwenda na tunapiga hatua na

hiyo hatua mnaweza mkaiona mbali na kule katika Jeshi la Polisi lakini hata ndani ya Bunge humu. Ukitizama Bunge lilivyokuwa miaka iliyopita na ukitizama jinsi tunavyokwenda sasa hivi unaona kabisa tunakwenda mbele na hilo suala zima lipo katika utaratibu mzima wa maboresho ya ajira ya askari na suala zima la maboresho namwachia Mheshimiwa Waziri atalizungumzia. Lakini kwa kweli kusema kwamba ajira kwa wanawake ni ndogo, haiwezi kuwa ndogo kwa sababu kuna makusudi ya kufanya iwe ndogo. Lakini mimi nafikiri pongezi inapostahiki mngeitoa kwa sababu jitihada zinafanyika kuona kwamba wanawake na wenyewe wanapata ajira katika Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Abduljabir Marombwa, Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Castor Ligalama wao wamezungumzia juu ya kuboresha maslahi ya askari pamoja na vitendea kazi yakiwemo majengo na vifaa mbalimbali. Sasa kama nilivyosema, narudia pale pale kwamba Serikali ina azma ya kufanya inaloweza kulifanya na nia ni nzuri kabisa. Lakini itayafanya yale ambyo inaweza kuyafanya kutokana na uvezeshwaji ilionao na kutokana na hili Bajeti yetu ilivyo na tunakuombeni Waheshimiwa Wabunge muipitishe na *inshallah* Mwenyezi Mungu atakupeni uwezo muipitishe jioni ya leo. (*Makofii*)

Kutokana na hiyo ndiyo nasema kwamba tutajitahidi kuona kwamba hayo yote ambayo mmeyasema tutayafanya lakini baya ni kuahidi kitu ambacho hatuwezi kukifanya kwa sababu uwezo wenyewe wa kufanya hayo tunakuwa hatuna. Lakini azma ya kufanya ipo, nia ya kabisa ipo kwa sababu askari ni askari wetu sote na sisi tuna azma ya kuwasikiliza na tuna azma ya kuona kwamba matatizo yao yanashughulikiwa na hili kusema kweli nataka niseme ingawaje Mheshimiwa Waziri atalisema ndani yetu sisi Wizara tumejaribu kutizama matatizo tuliyonayo kwa kweli ni mengi na tukisema tutegemei Bajeti tuliyonayo tutakwenda mpaka pale tutakapokwenda kwa mujibu wa Bajeti tuliyonayo. Sasa Mheshimiwa Waziri anajitahidi sana kuona kama anaweza akaenda nje ya Bajeti. Kuna kitu wanakiita *extra budgetary resources*. Atajaribu kuona kama anaweza akatafuta kwa njia zake mwenyewe na *contact* zake mwenyewe nje ya nchi au kwa watu walioko ndani ya nchi kuona kama tunaweza kwenda katika njia ambayo tunaweza tukayatizama mambo yote haya na nadhani katika programu yote ya maboresho ambayo Mheshimiwa Waziri mwenyewe ataizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu na rafiki yangu Lucas Selelii alileta hoja yake ya kusema kwamba Jeshi la Polisi liwachukulie sungusungu kwamba ni wadau wao muhimu katika kusaidia ulinzi wa raia na mali zao. Lakini hakuwa Mheshimiwa Selelii peke yake, wapo na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wameona kwamba katika yale maeneo ambapo Polisi labda wanakuwa hawezi kufanya kazi kwa sababu ya uchache wao, basi kwa kuwa wapo sungusungu ambao wamekuwa wanafanya kazi, basi rai ya Mheshimiwa Mbunge huyu na Wabunge wengine kwamba Polisi wawachukulie hawa kama ni wadau katika suala zima la ulinzi wa amani katika maeneo husika.

Hapo tunasema hivi, Jeshi la Polisi linatambua umuhimu wa kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao? Kuanzishwa kwa

utaratibu wa ulinzi shirikishi ni sehemu mojawapo ya Jeshi la Polisi kutekeleza mpango wake wa kuwashirikisha wadau wakiwemo sungusungu. Kwa jibu hili nataka nimfahamishe Mheshimiwa Selelii na Wabunge wengine ambao kwa kweli wamekuwa wanachukulia suala hili la sungusungu kwa uzito wake ni kwamba Jeshi la Polisi halina tatizo na suala hili. Ziko taratibu zake, lakini pia katika hii azma nzima na dhana nzima ya ulinzi shirikishi, basi nadhani hili suala litatizamwa katika mtizamo wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai ameuliza katika mchango wake wa maandishi kwamba, kwanini asichukue shilingi ya Mheshimiwa Waziri iwapo Kituo cha Polisi Kibaigwa hakitajengwa? Sasa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge niwaombeni na niseme kwamba azma yetu kama Serikali na azma ya Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kabisa angependa ajenge hivi vituo hata jana wacha kusema kesho, jana angelijenga.

Lakini kwa sababu nilizozisema na sababu nyinyi Waheshimiwa Wabunge mmetusaidia kuzisema na mmezisema kwa ubora zaidi kuliko hata sisi wengine tungeweza kuzisema ni kwamba azma ipo, lakini matatizo ni hayo ya uwezo. Nataka nimwambie Mheshimiwa Ndugai kwamba hapana usichukue shilingi nia yetu na azma yetu ni kuona kuwa haya yanafanyika. Lakini pia nimhakikishie kwamba Serikali inatambua kwamba Kibaigwa ni mji unaokuwa kibashara, hivyo polisi inacho kituo cha darala la (c) ambacho kina askari zaidi ya 14 wa Idara muhimu zinazotakiwa kuwepo, wapo pale Kibaigwa. Ili kuongeza huduma ya Polisi pale Kibaigwa kwa kushirikiana na Shirika la dini ya Kikatoliki Jeshi la Polisi, Mkuu wa Wilaya na Halmashauri wameanzisha mfuko wa kujenga kituo kikubwa zaidi ya kile kilichopo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na nadhani anafahamu hii kwamba kituo hicho kina usafiri wa gari lenye usafiri wa *PT 0960*. Katika michango mingine ambayo tumeipata kutoka kwa Wabunge mbalimbali Mheshimiwa Dr. Mlingwa, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Fatma Ali, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Prof. Idriss Mtulia, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Iddi Azan, Mheshimiwa Mwinyichome na wengine, wanazungumzia mpango wa ujenzi wa nyumba za askari Dar es Salaam tu.

Mpango huu upo na tumeanza hapo hapo Dar es Salaam lakini sio Dar es Salaam peke yake kwa sababu tunesema kwamba tutaanza na hili tumekuwa tunalijibu mara nyingi swali hili Bungeni, lakini pia tumekuwa tunalieleza kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaanza awamu kwa awamu na tutakwenda katika Mikoa taratibu tuwezavyo ili tufike hadi huko. Lengo la Wizara ni kuwarudisha kambini askari wote waishio uraiani na hii ndiyo nilioisema pale mwanzo. Hivyo mpango huu umeanza Dar es Salaam, utakwenda Zanzibar na kutokana na ufinyu wa Bajeti kama nilivyosema tutakwenda hatua kwa hatua mpaka tufikie lengo letu la kusema kwamba tunaweza tukawatoa uraiani. Kama nilivyosema hapo awali, hili si tatizo ambalo limeanza leo au jana ni tatizo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na hoja kutoka kwa baadhi ya Wabunge kuhusu Muswada wa kurekebisha Sheria mbalimbali za Jeshi la Polisi zilizopitwa na wakati na wanataka huo Muswada uletwe Bungeni ili hizi Sheria ziweze kubadilishwa haraka na mapema na yapo mambo mengi ambayo wameyatata Waheshimiwa Wabunge yanayohusiana na hiyo. Sasa mimi niseme mchakato na kweli nakumbuka maneno aliyoyasema Mheshimiwa Mwadini Jecha anasema mnachakata sana. Lakini nadhani mchakato wa programu ya maboresho ya Jeshi la Polisi unaoendelea hivi sasa Mheshimiwa Waziri atauzungumzia na nafikiri sio Wabunge wengi wanaufahamu kwa undani sana.

Lakini nadhani huko tunakokwenda mbele itakuwepo haja ili Wabunge kwa kweli waelewe kwa sababu ni kitu kikubwa na nasema kwamba ni kitu ambapo *IGP* tuliyi naye na ambaye mmempa sifa nyingi sana ni mtu ambaye ana mtizamo wa mbali. Unaona kabisa katika maboresho haya ambayo Mheshimiwa Waziri atazungumzia baadhi yake ni kwamba ipo haja kabisa ya kuona kwamba haya yote mnayozungumza ya Sheria zilizopita na wakati, masuala ambayo yamezungumzwa kwa uchungu sana na baadhi ya Wabunge kuhusu utaratibu wa pensheni ama *gratuity*, masuala mengine ambayo yamezungumzwa, basi hayo yatazungumzwa na majibu yake yatapatikana na nina uhakika Wabunge wataona kabisa jitihada zipo na tunakwenda vizuri na masuala yote ambayo yanahu su marupurupu ya Polisi, uboreshaji wa posho na mazingira wanayofanyia kazi hayo yote yatatizamwa na Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anazungumza.

Lakini niseme kwamba azma ni kuhakikisha kwamba tunaboresha kwa sababu hata sisi kama viongozi wa Wizara tunata Jeshi la Polisi ambalo ni imara barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ambayo naona nisiiache, ni vizuri niitaje, hoja ambayo aliileta Mheshimiwa Khamis Shoka, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Katika mambo mengi ambayo aliyazungumzia, Mheshimiwa Shoka, amezungumzia suala la Mariam Farid, yule mtoto aliyepotea, ama aliyekimbizwa na aliyekuwa Mwalimu wake Uganda. Nataka nimwambie kwamba asidhani kwamba Serikali haikufutilia. Serikali imefuatilia sana nyayo ambazo huyu Bwana Mganda ambaye anaitwa Kinume Innocent Creziah, wa Uganda, kuona alipitia wapi, maana tumejaribu Ofisi za *Interpol* za Kampala, Nairobi, Lusaka, Lilongwe, Maputo, Pretoria, Bujumbura, Kigali na Ofisi za Kanda zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwabie kwamba, tulipofikia sasa hivi, inasemekana, kwa taarifa ambazo Jeshi la Polisi wanazo, mtuhumiwa huyo na huyo binti walionekana katika mji wa Bizana, Mtaa wa Ndohozya, Kaskazini Magharibi mwa Afrika Kusini. Sasa hii ni taarifa ambayo Jeshi letu la Polisi linayo. Lakini, sasa basi, huwezi ukatoka hapa ukaenda kusema kwamba tunataka basi, tumekuja kumkamata, tunazo sheria zetu na ile nchi ina sheria zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea mpaka sasa hivi, Ofisi yetu hapa inaendelea kushirikiana na watu wa *Interpol*, wamefuatilia suala hili kupitia *Interpol* ya Afrika Kusini na niseme kwamba mpaka sasa hivi hawajatu jibu kwa sababu tunataka

ushirikiano wao. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba Jeshi la Polisi wamefanya kila jitihada, lakini ndio tumeweza kujua yupo hai na tumeweza kujua yuko wapi lakini sasa ndio tunaangalia taratibu kuona twende vipi ili kuweza kumpata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shoka alizungumzia juu ya taratibu na kanuni za kupandishwa vyeo vya Polisi na Magereza na kadhalika na malalamiko mengi yaliyopo lakini mimi naona hili nimwachie Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja atalizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na hoja mbalimbali ambazo zimezungumziwa kuhusu Magereza. Kuna masuala kuhusu msongamano wa wafungwa na mahabusu. Katika hili, wamezungumza Wabunge wengi, kimaandishi au kwa kuzungumza ambao ni Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Haji Sereweji, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Bakar Khamis Faki, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa wamezungumzia juu ya msongamano wa Magereza. Hatujakataa, kweli msongamano upo, lakini jitihada ambazo zinafanyika kupunguza msongamano tulionao, tumelisema na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake jana amesema kwamba tunajitahidi kuona ni njia gani tunaweza tukafanya kutoa elimu ya kutosha ili watu wasiende Magerezani, njia zinafanywa kupunguza wafungwa Magerezani kuititia njia za *parole*, kuititia huduma ya jamii pamoja na misamaha ya Rais. Lakini hizo ni njia au taratibu ambazo tunajaribu kuzifuata kuona kwamba tunapunguza msongamano. Lakini, tuisahau watu wanakuwa wengi katika Tanzania, uhalifu unakuwa mkubwa. Mambo haya tunajitahidi, hakuna nchi au Serikali inapenda kuwaweka wananchi wake Magerezani lakini inapobidi, basi inabidi tufanye hivyo lakini pia tunazingatia haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia ujenzi, upanuzi, ukarabati wa miundombinu ya Magereza na hili wamezungumzia Wabunge mbalimbali. Nataka kusema kwamba, jitihada zote zinafanyika lakini zitafanyika kuititia bajeti ambayo tunayo, lakini tunajitahidi hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri na usafirishaji wa Mahabusu kuwatoa Magerezani kwenda Mahakamani na kurejea. Haya yanafanyika na tunajitahidi. Kwa mfano, katika bajeti hii mkiipitisha, Magareza wanataka kununua magari 50 na labda yakipatikana hayo yatapunguza matatizo ambayo tunayo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyazungumzia sana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia juu ya maslahi ya watumishi wa Magereza na wa Jeshi la Polisi, yote hayo tumeyazingatia na nataka niseme kwamba tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unakweda na hoja zimekuwa nyingi. Suala la Zima Moto pia na yenye ni katika hayo hayo ambayo nimesema kwamba vitendea kazi, maslahi ya watumishi na makazi, tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni vigumu kwa muda tulionao kuweza kujibu hoja kwa hoja. Lakini mengi kwa kweli tumeyazingatia na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Lucy Owenya kuhusu lile suala lake, ni kweli kama alivyofuatilia, hili suala ni kwamba ilifika mahali Polisi walikuwa wamepoteza *track* kujua waende vipi lakini nataka nikwambie sasa wamefungua suala hilo upya na linashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, kwa Waziri Mkuu na kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri na natoa shukrani kwa Wabunge wote kwa *cooperation* yote mliyonipa. Ahsanteni sana na nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, maana ni hoja yangu mimi mwenyewe! (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuchangia hoja na sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri ili naye aweze kutumia dakika zake 40.

Niseme tu kwamba nimepokea vijinoti vingi, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiniuliza wingi wa neno Askari ni Maskari? Sasa, naona hilo limekuwa na utata, wengi wameniuliza. Sasa nalipeleka kwa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, halafu baadaye anaweza kutupa ufanuzi, wingi wa neno Askari kama ni Maskari au ni Askari! (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa namna ambavyo umeongoza mjadala huu na jinsi unavyoongoza shughuli za Bunge ukiwa hapo kwenye Kiti. Pia napenda kuwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii kwa siku ya leo na jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida yetu, kabla sijaanza kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue fursa hii kuwatambua wale wote waliochangia hoja hii ambayo iko mbele yetu siku ya leo. Waliochangia kwa kuzungumza ni Wabunge 29 na ambao wamechangia kwa maandishi ni Wabunge 129. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza kumtambua, Mheshimiwa Juma Kilimbah ambaye amechangia kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma ambaye alikuwa Msemaji Wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengine waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Ally Juma Haji, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Ramadhani

Maneno, Mheshimiwa Juma Nh'unga, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Faida Bakari, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba na Naibu wangu, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Balozi Dr. Gertrude Mongella, Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa *Capt.* John Komba, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Balozi Iddi Mshangama, Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhil, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

Wengine ni Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Prof. Feetham Banyakwa na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa.

Wengine ni Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry, Mheshimiwa Muhammad A. Chomboh, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Issa Kasim Issa, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Mwanakhamis Said, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Abdul Jabil Marombwa, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa

Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Faida Bakari.

Wengine ni Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji na Mheshimiwa Zabein Mhita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, kabla sijaanza kuchangia hoja ambazo ziko hapa mbele yetu siku ya leo, ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Nyamagana kwa kunivumilia katika kipindi chote ambacho niko mbali nao na pia niwashukuru sana Waheshimiwa Madiwani wangu na Wenyeviti wangu wa Kata, wa Chama, wa Wilaya na ngazi mbalimbali ambao wanansaidia kutunza Jimbo pale ambapo sipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninapenda kuwatambua wafuatao, Mstahiki Meya wa Jiji la Mwanza, Leonard Bihondo, Naibu Meya, John Ninja na Madiwani wengine, Bi. Kokotecha, Yahaya Nyaonge, Dismas Masunu, Mariam Maftaha, Mohamed Abdi Chakechake, Amos Onesmo, Dionis Mabura, Andrew Dalawa, Reuben Kasanga, Ezekiel Bahebe, Taus Maftaha, Kempanju, Sikitu Sanzioti na Eunice Bubinza. Bila hawa kwa kweli nisingeweza kufika mbali, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujitahidi kujibu hoja ambazo zilikuwa hapa mbele yetu siku ya leo. Amejitahidi kujibu hoja moja moja, mimi nitajaribu kuangalia hizi hoja kwa ujumla wake.

La kwanza ambalo na ninapenda kusema, ninapenda kurudia alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kati ya vitu ambavyo vimetufarji sisi, Naibu Waziri pamoja na mimi mwenyewe, ni namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamejitokeza kuonyesha upendo kwa Majeshi yetu ambayo yako chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibia kila Mbunge ambaye amechangia, amesononeka kutokana na hali halisi ambayo Askari wanaishi na ambayo wanafanya kazi. Ninapenda kuwafahamisha kwamba hapo Wizarani kwetu, mimi mwenyewe, Naibu Waziri na viongozi wote waandamizi wa Majeshi yetu, kila siku wanapofanya kazi wanafikiria hali za Askari wetu na namna ya kuboresha hali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanza kuongelea kuhusu hali ya Askari. Wachangiaji wengi walivyokuwa wanaongea, wamegusia makazi ya Askari na wameongelea kuhusu makazi ya Askari jinsi yalivyo katika hali mbaya, jinsi ambavyo Askari wetu hawatunzwi kama vile wanavyopaswa kutunzwa kuhusiana na suala zima la makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nieleze, ukweli ni kwamba, kabla sijawa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mimi mwenyewe nilikuwa sijui Askari wetu wanaishi vipi. Lakini, nawahakikishieni kwamba baada ya kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kutembela makazi yao, uchungu ambao mmeonyesha humu ndani, sidhani kama mnanizidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo mmeyaongelea Waheshimiwa Wabunge, nimetembelea maeneo mengi. Wote mmeongelea maeneo ambayo yako katika majimbo yenu, kuna maeneo mengi nimeyatemebelea. Nimetembelea eneo la Kigoto, Mwanza, nimetembelea Oysterbay Polisi, Dar es salaam lakini kitu ambacho ninapenda kuwaambia ni kwamba, tatizo la makazi ya Askari siyo katika Jeshi la Polisi peke yake, ni kwa Askari wote wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la *Immigration* pamoja na Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza nilivyokwenda kutembelea Gereza la Namajani kule Masasi, Mtwara, ukweli ni kwamba nilishindwa kutofautisha Bweni la Wafungwa na Makazi ya Askari. Hali ndivyo ilivyo, ni mbaya sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, nilivyorudi Wizarani, tulikaa na Viongozi Wandamizi wa Majeshi yote, tukaanza kuulizana ni kitu gani ambacho tunaweza kufanya ili kuboresha makazi ya Askari ili waishi katika hadhi ambayo wanapaswa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama mlivyokuwa mnasema, bajeti yetu ni ndogo, kaka yangu Mheshimiwa Mtemvu umesema kwamba katika bajeti ijayo tupewe paja, safari hii bahati mbaya paja hatukupewa. Lakini kwa kidogo kile ambacho tumepewa, tutajitahidi sana kutumia rasilimali watu na rasilimali tuliyonayo ndani ya Wizara yetu kwa ujumla ili kuhakikisha kwamba tunabadilisha hali ya makazi ya Askari katika Idara zetu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi hapa nilipokuwa nafungua semina ya Wakuu wa Magereza wa Mikoa hapa nchini, niliwaagiza kwamba kwa upande wa Magereza, wajitahidi kutumia *Prisons Corporation Co.* kujijengea makazi yao wenyewe na pale

ambapo tunatakiwa kujazia kutokana na vifungu tulivyonavyo kama ni suala la kutafuta mabati, kama ni suala la kutafuta misumari na kadhalika, Wizara itachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri, tumeunda Kikosi Maalum ndani ya Wizara yetu ambapo Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Polisi pamoja na Magereza, wamekubaliana kufanya kazi kwa pamoja kwa mantiki ya kwamba *Building Brigade* ya Jeshi la Polisi, *Building Brigade* ya Magereza na Idara zingine, zifanye kazi kwa pamoja kujenga nyumba za Askari, ndiyo kazi ambayo tumepanga kufanya kwa mwaka huu. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, suala la kutafuta Wakandarasi nje ya Wizara, kuanzia sasa ni mwiko ili tuweze kutunza fedha tuliyo nayo, ili kuweza kufanikisha yale ambayo tunahitaji kuyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si tu kuangalia suala la makazi, kwa sababu lazima nikubali, ni kweli bajeti yetu ni finyu, pia tumekaa na tumejaribu kutafakari ni vitu gani ambavyo tunaweza tukafanya ndani ya Wizara yetu, ndani ya uwezo wetu ili kuboresha maisha ya Askari nje ya bajeti. Ninapenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepeleka mapendekezo Wizara ya Fedha na yanafanyiwa kazi ili Askari pia ambao wako chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani nao wafaidike na *Duty Free* kama Askari wa JWTZ, hilo linafanyiwa kazi. Haya ni mambo ambayo yako ndani ya uwezo wetu ambayo tunaweza tukayafanya ili kuboresha maisha yao bila kuongezewa vifungu vya bajeti, hivyo kazi tunafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia suala la umri wa kustaafu kwa Askari. Labda nianze kwa kusema kwamba, nilivyoingia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nimekuta kwamba Jeshi la Polisi tayari lilikuwa na Programu ya Maboresho. Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi ilikuwa na missingi mikuu mitatu, Uweledi (*Professionalism*), Usasa (*Modenization*) na Ulinzi Shirikishi (*Community Policing*). Tumekaa, tumejaribu kuangalia, wenzetu katika Jeshi la Polisi wamekuwa na Programu moja nzuri sana, Majeshi yetu mengine wanaweza kujifunza kutokana na kazi ambayo imefanywa na Jeshi la Polisi. So na wao tumeishaweleza kwamba waige mfano, yaani Jeshi la Magereza, *Immigration* na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, waige mfano wa Jeshi la Polisi katika kuandaa Programu ya Maboresho. Kwa sababu tunafanya kazi kama Wizara moja, naamini yote haya yatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lengo la kufanya kazi kama Wizara moja, kati ya vitu ambavyo tumefanya hivi karibuni, Kamati yetu ya Maslahi kutokana na kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na *Immigration* wametolewa kwenye Tume ambayo iko chini ya Wizara ya Dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia, sasa hivi tumewaleta kwenye Tume ya Maslahi ya kwetu na ndio tuko katika mchakato wa kukamilisha suala hilo, Tume yetu imeshakaa na imeangalia suala la umri wa Askari wale wa ngazi ya chini kustaafu, suala ambalo limeongelewa na Wabunge wengi. Tumeandaa mapendekezo ambayo tuko kwenye mchakato wa kuyakamilisha kwamba wale Askari wote waliokuwa wanatakiwa kustaafu wakiwa na umri wa miaka 45, sasa watakuwa wanastaaafu wakiwa na miaka 50 na wale ambao walikuwa wanastaaafu wakiwa na umri wa miaka 50, tuko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba na wao watastaafu wakifikisha miaka 55. Yote hayo tunayafanya katika kutafuta namna ya kuweza

kuboresha maisha ya Askari wetu wote chini ya vitengo vyetu mbalimbali ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa suala la *promotion*, Kamati mwisho imekaa tarehe 24 mwezi wa Sita mwaka huu. Lakini ninapenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba ile dhana ya kwamba Askari hawapandishwi vyeo, tumejitahidi kuifanyia kazi na katika mwaka uliopita, lazima niwashukuru Mawaziri walionitangulia, Mheshimiwa Joseph James Mungai na Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, kwa sababu kazi hii kubwa ilikuwa imeanza katika kipindi cha kwao. Polisi wale wa *rank* za chini ambao mlikuwa mnasema wanaonewa, 5431, wamepata *promotion* ukilinganisha na Polisi wale wa vyeo vya juu 813. Ukienda kwenye ngazi ya Magereza, Askari wale wa ngazi ya chini 1843 wamepandishwa vyeo ukilinganisha na wale wa ngazi za juu 533. Naomba kuwahakikishieni kwamba tutaendelea kuwatunza Askari wetu, tunawajali sana Askari wetu na maslahi yao kwa kweli ndio kipaumbele chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swalî ambalo nimeulizwa kuhusu suala la elimu kwa Askari kwamba hatuwapatii nafasi za kwenda kusoma. Sasa naomba nijaribu kueleza na nitachukua mfano wa Jeshi la Polisi. Katika Jeshi la Polisi, kwa wastani kila mwaka tuna Askari sio chini ya 2,400 ambao wanasona nje ya Jeshi la Polisi. Tukichuka takwimu ambazo tulikuwa tunaongelea leo asubuhi, asubuhi nimewaeleza kwa wastani jinsi inavyotakiwa Kimataifa, tunatakiwa kuwa na Askari mmoja kwa wananchi 400, sisi tuna Askari mmoja kwa wananchi 1,300 na zaidi lakini pamoja na hali hiyo, kila mwaka tunaruhusu vijana wetu kwenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema ni hivi, tuko kwenye Programu ya Maboresho. Katika Programu yetu ya Maboresho kati ya vitu ambavyo tunaongelea ni Uweledi, hauwezi kuwa na Uweledi bila watu kwenda kusoma. Tunachosema kama unataka kwenda kusoma, unataka kwenda kusoma fani ambayo inatakiwa moja kwa moja ndani ya Jeshi katika kipindi kile na pale ambapo Jeshi lina uwezo wa kukuachia kwenda kusoma. Takwimu ambazo nimewaelezeni leo asubuhi ndivyo ilivyo na tunapenda sana kuruhusu vijana wetu waende kusoma lakini maombi ambayo yanakuja kuna watu wanaleta maombi ya kwenda kusoma *Forestry*, sasa Jeshi la Polisi na *Forestry* wapi na wapi? Si suala tu la kwenda kusoma kujiendeleza lakini tunahitaji watu ambao wanajiendeleza kutokana na mahitaji ya Jeshi la Polisi na Majeshi yetu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapenda kuwahakikishieni, ili kuweka mambo wazi, katika Programu ya Maboresho, Inspeksa Jenerali wa Polisi anaandaa *Human Resource Programme* maalum ili Askari wetu wote waelewe kwa undani ni maeneo gani ambayo wanataka kwenda kusoma katika kipindi gain na kwa namna gani ili wawzeze kujiendeleza. Kama tunakosa, tunakubali kwamba inawezekana kwamba ile *Human Resource Programme* ilikuwa haiko wazi kwa Askari. Tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuiweka wazi kwa Askari Polisi pamoja na Askari wengine katika Majeshi yetu mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu la mwisho kuhusu haki na stahili za Askari. Kuna waliokuwa wanasema kwamba mishahara hasa kwa wale *professionals* haiendani na mambo anayoyasoma, tumeona hayo katika michango ya maandishi. Katika Jeshi la Polisi sasa hivi inawezekana kwamba hutapata cheo kutokana na kiwango chako cha kisomo, lakini sasa hivi ndani ya Polisi kuna kitu tunaita *salary according to one self*, ina maana kama wewe ni Daktari hata kama cheo chako ni cha chini utalipwa sawa na Madaktari wenzako katika Wizara nyingine. Kwa kusema hivyo, ninawaombeni wasomi ambao wako huko nje ambao wanaogopa kuingia katika Majeshi yetu, waje, tutawalipa na sera yetu ni Sera ya Maboresho, tunawaombeni sana mje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii, kuongelea suala la mauaji ya ndugu zetu Maalbino, kuna baadhi ya Wabunge waliomba takwimu zilizo wazi, ni maalbino wangapi ambao wameuawa katika kipindi hiki, naomba nifanye hivyo na hizo takwimu niziweke wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwezi wa sita mwaka 2007 mpaka leo hii tunavyoongea, nasikitika kusema kwamba ni jumla ya ndugu zetu Maalbino 23 ambao wameuawa. Ndugu zetu hawa 23 ambao wameuawa wameuawa katika Mikoa ya Mwanza 14, Mkoa wa Mara 4, Arusha 1, Mbeya 1, Shinyanga 1, Ruvuma 1 na Mtwara 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jambo la aibu kubwa. Ni jambo ambalo Wizara yangu inalifanya kazi kila siku kukicha. Tumefanya semina mbalimbali katika Mikoa mbalimbali, tumekuwa tukishirikiana na taasisi za dini, tumeashirikiana na viongozi katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya kujaribu kuwaelimisha wananchi kwamba matukio haya hayana nafasi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi kwamba hatulifanyii kazi suala hili, tena baada ya hapa juzi juzi mara baada ya Watangazaji wa BBC kufanya upelelezi wao na kubaini kwamba kuna baadhi ya watu ambao wanajihusisha katika masuala haya, watu wameanza kuijuliza kwa nini BBC wameweza, kwa nini tumeshindwa? Ninapenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali hajashindwa, lakini namna tunavyofanya kazi sisi na namna wanavyofanya kazi Waandishi wa Habari ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwandishi wa Habari anafanya upelelezi anatangaza papo hapo, Polisi akifanya upelelezi anachunguza faili, inaandaliwa na matokeo yake mnayaona baada ya mtu kufungwa au kushtakiwa. Sisi hatuwezi kwenda kufanya upelelezi halafu kuja kutangaza kwamba jana tulikuwa sehemu fulani, tumeongea na watu fulani, tumefanya kitu fulani, hiyo haiwezekani. Ninapenda tu kuwafahamisha kwamba watuhumiwa ambao tumewakamata mpaka hivi sasa ni 34, uchunguzi bado unaendelea na Jeshi la Polisi litaendelea kufanya kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba tu kurudia kusema kwamba ni suala la aibu sana na imenisikitisha kwamba katika hizi siku mbili tatu nikipigiwa simu nikiona ni

simu ya nje unakuta aidha ni radio *France*, au radio *Deutch Welle* au *BBC* hawaulizii suala lingine lolote kuhusu Tanzania, wanaulizia tu suala la Tanzania na mauaji ya Maalbino, utafikiri ndiyo kitu pekee ambacho tunafanya hapa nchini. Nimeendelea kuwafahamisha kwamba siyo desturi yetu sisi Watanzania, ni watu wachache wenye akili chafu na Jeshi la Polisi, litafanya kila kinachowezekana kuwakamata haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuongelea suala la uraia na ninapenda kuongelea suala hili kwa sababu kuna utata ambao umejitokeza, watu wanaanza kuuliza, kwa nini tukiwa tunataka kutoa *passport* tunauliza maswali mengi? Kwa nini wenzetu, mtu yupo nje, yuko Uingereza tunaanza kuuliza umefikajefikaje huku, Ndugu zangu, uraia wa Tanzania unatawaliwa na Sheria ya mwaka 1995. Kabla ya hapo, kwa hapa Bara tulikuwa tuna Sheria Sura 512 ya mwaka 1961 na kwa Zanzibar tulikuwa tuna *Decree* No. 5 ya mwaka 1964 ambayo ilitanguliwa na Nationality *Decree* ya mwaka 1952.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zote hizi zilikuwa zimeweka viwango tofauti katika kutambua nani ni raia na nani si raia. Tukianza na *Nationality Decree* ya mwaka 1952 ya Zanzibar ilikuwa inasema mtu ye yote ambaye amezaliwa Zanzibar kabla au baada ni Mzanzibar, hiyo ikawa *repealed* mwaka 1964 na ikaweka masharti yake lakini tukaona kwamba uraia ulikuwa unafuata mkondo wa Baba sawa na Sheria yetu ya mwaka 1961 ambapo uraia ulikuwa unafuata pia mkondo wa Baba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995, ndiyo tulibadilisha sheria, tukasema kwamba uwe umezaliwa na Baba Mtanzania au Mama Mtanzania, ye yote yule, sawa, wewe unakuwa Mtanzania. Katika kipindi hiki chote, kulikuwa kuna watu ambao walikuwa wanapata *passport* kimakosa kwa sababu kulikuwa na suala la kufanya uhakiki, lakini pia tatizo kubwa ambalo limejitokeza sasa hivi hasa kwa wenzetu ambao wako huko Uingereza na nchi nyingine ambao wanatafuta *passport*, pia katika Sheria zetu za Uraia, tunasema huruhusiwi kuwa na Uraia wa nchi mbili hivyo ndivyo ilivyo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakuja ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza, anakuja ni mwaka 2007 anasema mimi nimeishi hapa Uingereza kwa miaka kumi, mimi ni Raia wa Tanzania, naomba *Passport*. Anakuja anakuletea ile *passport* ya zamani ile yenye gamba gumu anakuambia mimi ni Mtanzania, sasa tunamwuuliza hapa Uingereza unaishi vipi? Kwa sababu angekuwa ni mtu ambaye ni *resident* halali wa kule, ambaye amekaa na uraia wake wa Tanzania angekuja na lile gamba pale tulipobadilisha *passport* mara ya kwanza ili igongewe, arudi aendelee na uraia wake, kama hakuja na anaishi kule bila kukamatwa maana yake ni kwamba ana *status* ya kuishi kule, sasa atueleze kule anaishi kama nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunavyoolewa huyo anaishi kule kama Muingereza na kama ni hivyo, huyo hastahili kuwa Raia wa Tanzania na ndiyo maana tunauliza, siyo kwa sababu ye yote ile nyingine, hatuna nia ya kubagua mtu. Tunachosema, tuoneshe ushahidi kule ulikuwa unaishi vipi, ni hilo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima nikubali kwamba ndiyo kuna watu wengine tulikosea, tulikupa *passsport*, tulidhania labda ulikuwa unastahili, lakini na wanaotoa *passport* ni binadamu kuna kukosea, tukigundua tunasema. Lakini pia tuna utaratibu, unaweza ukaja ukamwomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba mimi nilikuwa nafikiria kwamba mimi ni raia wa Tanzania, nilikuwa sijui kwamba siyo raia, naomba unipatie uraia wa Tanzania, mbona tunatoa kila siku, sidhani kama kuna tatizo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naongelea suala la uraia, naomba nichukue fursa hii pia kuongelea suala la *Duo Nationality*. Katika majadiliano, imeonekana kwamba Wizara yangu imedanganya, imesemekana kwamba mwaka jana tulisema kwamba tumeipeleka Baraza la Mawaziri, mwaka huu mmesikia tena kwamba tunataka kuipeleka Baraza la Mawaziri. Kimsingi hatujadanganya, ndivyo ilivyokuwa, tulipeleka Baraza la Mawaziri ikarudishwa, ikafanyiwa kazi sasa hivi imepelekwa Zanzibar, tunaianya kazi na wenzetu, ikikamilika, tutapeleka tena Baraza la Mawaziri halafu tutaleta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna wengine hapa wamesema kwamba usilete kabisa. Leo nilikuwa na mwenzangu Naibu Waziri tukawa tunapiga hesabu, wale waliosema tunataka na wale waliosema hawataki ilikuwa kama nusu kwa nusu. Nafikiri mturuhusu tumalize kulifanyia kazi tulipeleke kwenye Baraza la Mawaziri, ikitoka huko tulete hapa muamue wenyewe kwama *Duo Nationality* iwepo au isiwepo. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti kabla sijamalizia, nimesikia kengele imelia, Wabunge walio wengi sana wamechangia wakiomba magari, naomba kuongelea kuhusu magari. Mmekwishaalezwa kwamba kasungura ni kadogo, katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2008/09 Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa upande wa Polisi, imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.426 kwa ajili ya ununuzi wa magari, tunanunua jumla ya magari 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ambazo zina uhakika wa kupata magari ya Polisi ni Mvemero, Kilindi na Misungwi. Kwa Upande wa Kikosi cha Usalama Barabarani, gari itapelekwa Mkoa wa Dodoma, Mwanza na Shinyanga. Magari yaliyobaki, tutakachofanya ni kufanya tathmini ya hali ya usalama wa eneo. Ninaomba mtuachie sisi chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara ya Polisi, tufanye tathmini hiyo. Tuna maeneo ambayo tunajua kabisa ni hatari, wanahitaji magari, tutawapelekea, hali halisi ndiyo hii. Ningependa sana kupeleka magari maeneo yote lakini jambo hilo halitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba kengele imelia, ninapenda kuongelea suala la mauaji ambayo yalitokea huko Moshi ya yule dereva ambaye aliunguzwa moto, tumeona kwenye magazeti na tumepata michango kuhusu mauaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba huyu dereva aliunguzwa, ni kweli kabisa kwamba tulifanya upelelezi mara ya kwanza kwa upande wa Jeshi la Polisi ikabidi tufanye upelelezi tena mara ya pili. Kwa bahati mbaya pale ambapo tulifanya upelelezi mara ya pili na tukaamua kuchukua hatua dhidi ya mtuhumiwa, mtuhumiwa huyo alitoroka nchini na sasa hivi tunashirikiana na wenzetu wa *Interpol* ili kuweza kumtafuta mtuhumiwa huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, nafikiri muda unataka kunitupa mkono, kabla kengele ya pili haijalia, ninapenda kuwasilisha kwako, marekebisho katika Kitabu cha Nne cha Makadirio ya Maendeleo, katika *Sub Vote* 2002, kifungu kidogo cha 6573, katika nafasi za fedha za ndani pale kwenye 0 inatakiwa isomeke milioni 100, jumla ya kifungu isomeke shilingi 11,153,313 kama nilivyosoma katika hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii, kuongelea suala la maziwa yetu, *Lake Victoria*, *lake Tanganyika* na kadhalika. Suala la ulinzi katika maziwa yetu, limeongelewa sana, ninapenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu imetenga shilingi bilioni moja, milioni arobaini na mbili, mia tano elfu kwa ajili ya ukarabati wa boti zetu ambazo ziko katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba pesa hizi hazitoshi na hapa tulipo sasa hivi tunatafuta namna ya kuweza kuongeza pesa nje ya bajeti kwa kutafuta wafadhili na kadhalika ili tupate boti zaidi katika maeneo yetu. Tunafahamu kabisa kwamba hii ilikuwa ni ahadi ya Waziri Mkuu mwaka jana na Wizara yangu ina kila nia ya kuhakikisha kwamba tunatimiza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kengele ilie nikiwa hapa, hoja zote ambazo hatujajibu mpaka hivi sasa, ninaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa ruhusa yenu, mturuhusu tujibu kwa maandishi. Kama niliyowaeleza, juzi ilikuwa ni *anniversary* yangu ya ndoa, sijapata nafasi ya kwenda kwenye hiyo *dinner*, leo mapema, ninaomba nafasi ya kwenda kwenye hiyo *dinner*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa mtoa hoja, kujibu takribani hoja kadhaa zilizoletwa na Waheshimiwa Wabunge na hoja yake kuungwa mkono, sasa tutaendelea na hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 14 - Fire and Rescue Force

Kif. 3001 - *Fire and Rescue Services* Sh. 3,118,343,300/=
Kif.3002-*Fireand Rescue Servises Training Instit* Sh.527,101,700/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Fungu 28 - Police Force

Kif. 1001 - *Administration and General* Sh.0
Kif.1002 - *Finance and Accounts* Sh. 0
Kif.1003 - *Policy and Planning* Sh.0
Kif. 1004 - *Public Safety and Security Monitoring*..... Sh.0
Kif. 1005 - *Information, Education and Communication*.... Sh.0
Kif. 1006 - *Procurement Management Unity*.... Sh.0
Kif. 2001 - *Police Operation*.... Sh.87,546,378,700/=
Kif. 2002 - *Police Marine*.... Sh.2,556,554,600/=
Kif. 2003 - *Railway Police Division*.... Sh.416,523,500/=
Kif.2004 - *Police Signals Branch*.... Sh.4586,959,300/=
Kif.2005 - *Police Zanzibar*.... Sh.9,967,116,500/=
Kif. 2006 - *Police Air Wing*.... Sh.1,704,892,200/=
Kif.2007 -*TAZARA Police*.... Sh.484,349,800/=
Kif.2008 - *Field Force Unit*.... Sh.438,764,200/=
Kif. 2009 - *Traffic Police*.... Sh.1,282,329,800/=
Kif.2010 - *Police Airport*.... Sh.450,229,400/=
Kif. 2011 - *Police Dog and Horses*.... Sh.918,839,300/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Kif. 2012 *DSM Special Zone*.... Sh.7,132,592,100/=

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hiki kinahusu Kanda Maalum ya Dar es Salaam na ukiangalia chini ya item 270100 hazikutolewa fedha. Isitoshe Kanda hii ina ofisi za Mikoa na Wilaya ambazo hazijajengwa, ninaomba Waziri atueleze ni mambo gani yanayofanyika kuhakikisha kwamba Kanda hii inapewa mahitaji yake ya miundombinu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Askari Polisi Dar es Salaam wanafanya kazi nzuri sana inabidi tuwasaidie ili waweze kufanya kazi yao vizuri zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tusaidie lakini Waheshimiwa Wabunge, unaposema masuala ya ujenzi na nini, yale yote yanaingia kwenye *development* bajeti. Mheshimiwa Waziri labda kama una majibu ya ziada kwa sababu hapa tunaangalia suala zima la uendeshaji, mishahara na kadhalika na siyo ujenzi na ukarabati. Lakini nimpe nafasi Mheshimiwa Waziri kama anataka kuongeza neno lolote.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema kwamba mishahara na kadhalika haionekani pale chini ya *Subvote* 2012 kwa sababu yote ipo kwenye *Programme 10, Administration* 1001.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keenja, yote ipo kwenye *Programme 10, Administration and General*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Kif. 3001 - *Police Collage Moshi*.....Sh.2,599,099,900/=

Kif. 3002 - *Police Collage*.....Sh.1,260,066,800/=

Kif.4001 - *Police Vehicles Maintanance Unit* Sh.485,043,600/=

Kif.5001 - *Police Medical Unit*.... Sh. 1,959,984,400/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Kif.6001- *Police Building Brigade*.....Sh.1,487,831,400/=

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nimezungumzia pamoja na mambo mengine, umuhimu wa kuboresha *building brigade*. Katika kifungu hiki, nataka nizungumzie kifungu 6001, *subvote* 310600, *plant equipment and machinery*, ni 0. Katika maelezo ya Waziri ametuambia kwamba kuanzia mwaka huu na kuendelea, shughuli zote za ujenzi zitafanywa na *Brigade* ya Jeshi letu lakini watawezaje hawa kufanya kazi zote hizi wakati bajeti kwenye *plant equipment and machinery* ni 0, naomba ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapo katika kifungu 310600, hatujaweka kitu chochote lakini hii ni kwa sababu moja, tayari katika *Brigade* ya *Police* wanazo baadhi ya *machine* ambazo wanahitaji kuwa nazo lakini kama nilivyoeleza sasa hivi Wizara yangu inajiangalia kama Wizara moja kwa ujumla. Pia tunayo *Building Brigade* ya *Prison* ambayo pia iko *very well equipped* na imefanya kazi nyingi hapa Tanzania ikiwemo katika kujenga nyumba za kisasa na kadhalika. So, *equipment* tayari wanazo na tutaendelea kuwaongezea kadri watakavyohitaji.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Kif. 7001 - *Criminal Investgation Division*Sh.10,868,423,200/=

Kif. 7002 - *Stock Theft Prevention Unit*.....Sh.457,250,300/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Fungu 29 - Magereza

Kif. 1001 - *Prisons Headquarters* Sh. 9,374,839,900/=
Kif. 2001- *Parole Department*..... Sh.367,797,100/=
Kif.2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation* Sh.55,328,543,500/=
Kif. 2003 - *Resettlement of Offenders*.... Sh.959,969,300/=
Kif. 3001 - *Prison Staff College* Sh.1,174,946,700/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Kif. 3002 - *Prisons Driving School*.... Sh.209,946,600/=
Kif. 3003 - *Prison Trade School* ... Sh.151,142,100/=
Kif. 3004 - *Prison College Kiwila*.... Sh.921,427,400/=
Kif. 4001 - *Prison Building Brigade*.... Sh.1,088,147,200/=
Kif. 4002 - *Prison Industries* Sh.180,310,600/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Kif. 4003 - *Prison Farms* Sh.676,971,900/=

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 4003, kifungu kidogo 270300, naona kimetengewa fedha kidogo. Lakini ninapenda kuulizia, huwa tunawaomba trekta kwa ajili ya Gereza langu la Butundu, tulishawapa shamba na hilo lakini sasa hivi halifanyiwi kazi. Sasa ninapenda kufahamu, je, utaratibu wa kutoa matrekta, mwaka jana tuliambiwa wanao utaratibu wa Magereza kukopa, je, kwa mwaka huu kuna utaratibu gani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabuzi, utaratibu wowote wa manunuvi ya vifaa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, haiingii kwenye *vote* hii, zote zinaonekana kwenye *development book*. Kwa hiyo, hapa ukiuliza ununuvi wa matrekta, kitengo hiki cha *prison farm*, Mheshimiwa Waziri, labda wewe unaingiza hapa, lakini kwa kweli hiyo yote inaingia kwenye *development*.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

(*Hapa kulikuwa na manung'uniko kutoka
kwa Waheshimiwa Wabunge*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kuendesha shughuli utafuatwa ule ulioandalishi na Kiti, kwa hiyo, tunaendelea.

Fungu 93 – Uhamiaji

Kif. 2001 - *Immigration Zanzibar* Sh.994,104,000/=
Kif. 2002 - *immigration Mainland* Sh.16,584,622,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote*)

Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ndani

Kif. 1001 - *Administration and General* Sh.1,506,141,500/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mmeona orodha ilivyo ndefu kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu tuliojiwekea na wa kawaida tulioanza nao, swali ni moja kwa kila Mbunge ili watu wote wapate nafasi ya kuuliza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kupata ufanuzi, sina tatizo na mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kwamba Gereza la Mpwapwa lina gari lakini gari hilo ni bovu miaka miwili sasa. Askari wanatembea kwa miguu kuwapeleka washtakiwa Mahakamani. Sasa nataka tu uthibitisho kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu gari lile utengenezaji wake ni gharama kubwa, je, atatupatia gari jipya?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumthibitishia Mheshimiwa George Lubeleje kwamba Gereza la Mpwapwa ni kati ya Gereza ambalo litapata gari jipya. (*Makofit*)

MHE. MASOUD ABDULLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu jana, nilitaka ufanuzi juu ya magari tisa ya zimamoto yaliyonunuliwa kutoka Uingereza, Ujerumanu na Dubai ambayo waliyasajili kama makuukuu au *used*, naomba ufanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo magari yaliundiwa Tume na ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na yalikuwa yamenunuliwa chini ya Wizara ya TAMISEMI siyo Wizara yangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud, utalileta kwa utaratibu utakaoona unafaa vinginevyo Mheshimiwa Waziri hawezi kuwa na majibu papo kwa papo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Waziri, Wizara ambayo ilihusika na jambo hili ni Wizara ya TAMISEMI na kwamba Waziri Mkuu aliunda timu kwa ajili ya kuchunguza na kuona kama kweli magari haya yaliyonunuliwa yalikuwa ni magari

makuukuu kama ilivyokuwa imekuwa *alleged*. Timu ile ilipofanya kazi ile na kuchunguza na kuangalia kwamba ni nini kilichotokea, ilithibitika kwamba magari yale yalikuwa ni magari mapya na wala hayakuwa magari makuukuu. Imeonekana kwamba katika *procurement* kwa maana ya manunuzi kuna makosa madogo madogo ambayo yalijitokeza na kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa sasa maelekezo mapya kwa ajili ya kuhakikisha haya marekebishesha yanafanyika.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kwa maandishi na kuzungumza, nilitaja juu ya ahadi ya Waziri ya kuweka umeme Kituo cha Polisi Iguguno ambapo nguzo iko mita mbili kutoka kwenye ukuta wa kituo hicho. Sasa nataka Waziri aniambie hiyo kazi itafanyika au ndiyo itakuwa ahadi hewa tena?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahadi hewa ama hiyo kazi itafanyika?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kazi itafanyika. (*Makofisi/Kicheko*)

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kwamba kuna Kituo cha *FFU* Matengatwani, Pemba katika Jimbo langu la Konde na cha Polisi Konde ambavyo vimejenga hata mimi sijazaliwa, leo nina miaka 61. Vituo hivi havijatengenezwa hata siku moja na mbaya zaidi hiki cha *FFU* hakina hata umeme, leo miaka 40 na zaidi, *FFU* wako pale kama kituo lakini wanalinda kwa Kandili! Je, lini tutapata umeme na lini tutapata matengenezo ya vituo hivyo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Tarab, nakumbuka hili suala nilikujibu. Lakini nadhani utakubaliana na mimi kwamba kwa kweli kile kituo cha Matengatwani, tulisema kitafungwa na ni kweli kimefungwa maana Askari hawapo na wale *FFU* wanatazama tu pale na tulisema kwamba tutakwenda kituo kilichokuwa jirani. Kwa hiyo, tukasema kwamba katika utengenezaji mkubwa ambao unakuja baadaye na huo utatokana na tutakavyokuwa tunapata fedha, basi tutazama hata hilo suala la umeme. Nafikiri tulizungumza na ningkuomba Mheshimiwa Dr. Tarab, unikubalie, ahsante.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, ni marafiki zangu wakubwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu kuhusu suala la Kituo cha Polisi Kibaigwa, hakutoa majibu ambayo kwa kweli yanaridhisha. Kibaigwa ni Mji Mdogo kisheria na panakua kwa haraka sana, kuna Soko la Kimataifa, pana biashara kubwa sana, usalama hakuna na *CRDB* na *NMB* wamekataa kujenga benki kwa sababu hakuna usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1998 wananchi wa Kibaigwa, walijenga Kituo cha Polisi, kikafunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati huo Mheshimiwa Fredrick Sumaye, Polisi wakasema kituo kile ni kidogo. Mwaka 2000 hadi 2004 nikahamasisha mimi mwenyewe wananchi wa Kibaigwa wakajenga Kituo kingine cha Polisi na ramani ililetwa na wao wenywewe Polisi kikubwa zaidi, kiko pale tangu mwaka

2004 mpaka leo hakuna kinachofanyika. Kinachofanyika ni kupeleka doria za kutoka kwa *RPC* kutoka kwa *RCO*, kwa ile gari ambayo ameitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, PT 960, kupitia usimamizi wa Inspekte Msomi. Nataka Mheshimiwa Waziri aniambie, hivi kweli wananchi wamejenga mara mbili lakini kituo pale hakuna na ndiyo mnasikia matokeo mara Pandambili mara nini, Kibaigwa pale panapaswa kuwa na kituo cha uhakika, kwa nini jambo hili hatekelezeki?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa niliyonayo ni kwamba pale Kibaigwa kituo kipo tatizo ni kwamba hakijafunguliwa. Nitakachomuahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tutajitahidi haraka iwezekanavyo kituo kifunguliwe ili kifanye kazi. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nawashukuru Polisi kwa katuondoa salama kule tulikokwenda kwenye maziko ingawaje hatukuzika. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKIDI: Poleni sana na karibu tena.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, nimesisitiza kwamba Jeshi la Polisi zaidi juu na tangu uongozi mpya umeingia, *IGP* mpya, linafanya kazi vizuri. Lakini nikasema kuna mambo ambayo lazima yaondolewe haraka, ubambikizaji wa kesi Bariadi ni mwangi na mara nyingine unahusishwa na siasa. Kama pametokea maafa unaambiwa ulipie petroli. Halafu kuna watu wengine wamekaa muda mrefu mno pale, mwishoni wananchi wakiona gari la Polisi linaondoka *police station* haliwezi likarudi bila chochote kwa maana ya mahabusu na vitu kama hivyo. Sasa nimemwambia Mheshimiwa Waziri, nataka tamko lake kabisa mnafanya nini ili kusaidia pale Bariadi kisiwe kitovu cha kuchafulia Jeshi la Polisi heshima ambayo tayari wamejjengea kutokana na uongozi huu mpya?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana baba yangu, Mheshimiwa John M. Cheyo kwa imani ambayo ameonyesha kwa Jeshi la Polisi hasa kwa ngazi ya juu. Nina imani kabisa kwamba Mheshimiwa Afande *IGP*, amemsikia, tutalifanyia kazi ili tatizo hilo ambalo liko katika Wilaya ya Bariadi, liondoke. (*Makofi*)

MHE. DR. LUKE J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kule Wilayani Mbozi katika Jimbo la Mbozi Magharibi hivi sasa kuna wimbi kubwa la ujambazi wa kutumia silaha katika kupora na kuteka nyara wasafiri. Jimbo hili lenye ukubwa wa kilomita za mraba 6,275 sawa na nusu ya eneo la Mkoa wa Kilimanjaro na sawa na mara tatu ya zaidi ya ukubwa wa Tanzania Visiwani, lina vituo vidogo viwili tu ambavyo vinatenganishwa na umbali wa kilomita karibu 200 hivi. Lakini hivi sasa kila siku tunashuhudia wimbi la utekaji nyara Wilayani Mbozi na hakuna gari na vituo hivyo viwili kwa eneo hilo ni sawa na hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Mheshimiwa Waziri anihakikishie ni lini watatupa gari Wilaya ya Mbozi kwa sababu hakuna gari na pia ni lini watajenga Vituo vidogo vya Polisi katika hizo Kata 11 za Jimbo la Mbozi Magharibi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumhakikishia kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, kama kweli hakuna gari katika Wilaya ya Mbozi, kati ya yale magari ambayo tunayo, tutapeleka. Tutakachofanya ni kwenda kuangalia na kuhakikisha kwamba magari kweli hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kujenga vituo vidogo vidogo vya Polisi, Jeshi la Polisi kwa sasa hivi kutokana na bajeti tuliyonayo, tunajikita katika kujenga Vituo vya Polisi katika ngazi ya Wilaya na tungeomba kwenye ngazi hizo za Vijiji na Kata wananchi wajitolee kutusaidia Jeshi la Polisi katika dhana ya Polisi Shirikishi ili kujenga vituo hivyo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, nilielezea matatizo wanayoyapata watumishi wa Jeshi la Polisi wakati wanaposafiri. Utaratibu unaotumiwa sasa hivi wakati wanaposafiri na familia zao wanatumia utaratibu wa *Warrant*, hawapewi fedha *cash* au wanaambiwa wajilipie nau li wanaporudi waje wadai ofisini, lakini zile fedha wakizidai zinachukua miaka mitatu mpaka miaka mitano hawajalipwa wakati mwingine fedha zile zinapotelea huko. Napenda kujua ni kwa nini Wizara isibadilishe utaratibu huo na kuweza kuwapatia fedha *cash* wanaposafiri? Ahsante.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza wakati nafunga mjadala huu, Jeshi la Polisi lipo katika kipindi cha maboresha. Tunaelewa kabisa kwamba matatizo hayo yalikuwepo na tunafanya kila kinachowezekana ili kuhakikisha kwamba hayatatokea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ninaweza kumhakikishia Mheshimiwa Magdalena Sakaya ni kwamba hakuna Polisi atakayesubiri kipindi cha miaka mitatu tena na tupo katika harakati za kulipa madeni yote ambayo yalikuwa yakidaiwa huko nyuma.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa kwenye mchango wa maandishi niliokuwa nimempeleke kuhusu wale Maaskari ambao hawakujitambulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nichukue nafasi hii pia kuwaomba wananchi wote wanapokuwa wanatuletea mawazo yao, ni vema wakaleta anuani zao na majina ili kama kuna majibu kwa maandishi tuweze kuwapeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba kwa wale ambao wana taaluma (*professionals*), ni kwamba

kuna mishahara ambayo itakuwepo kufuatana na zile taaluma. Kwa hiyo, siyo lazima huyo Askari awe amepanda cheo katika zile *rank*. Swali langu ni kwamba, je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kutoangalia pia uwezekano kupandisha *rank* ni kumnyima ile ari ya kujivunia Askari huyo anapokuwa Jeshini akifanya kazi kama Daktari na haoni ni vema akaangalia utaratibu wa kujaribu kujumuisha na suala la *rank* zao?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali. Kwanza, ninapenda kuweka wazi kwamba ni kweli kwamba watapata mishahara kutokana na fani zao na siyo kutokana na *rank* zao. Lakini suala la *rank* kama nilivyoeleza hapo awali, tupo katika kipindi cha maboresho lakini lazima izingatiwe kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi katika perimeter hata kama una Askari 10 wenye *PhD*, huwezi kuwa na *IGP* 10 ndani ya Jeshi la Polisi. Nafasi zinapatikana kutokana na nafasi ambazo zipo ndani ya Jeshi, lakini katika maboresho ambayo tunayafanya, hata nafasi na ngazi zitabadilika kwa kiasi fulani ili kuhakikisha kwamba wale ambao ni *professionals* nao wanaweza kupata nafasi na vyeo zaidi ndani ya Jeshi. Lakini tutazingatia fani zao kwa kuhakikisha kwamba wanapata mishahara sawa na wenzao katika Wizara nyingine mbalimbali.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu kwa maandishi pamoja na mambo mengine, nilizungumzia kuhusu suala la Jeshi la Polisi ambao wamekuwa wakilinda usalama wakati wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuulizam, hivi sasa mfumo uliopo ni kwamba Polisi wanapokuwa uwanjani hasa kwenye Uwanja wa Taifa wamekuwa wakiipa *audience* mgongo na wao wakitazama mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na pia vilevile uwepo wa vitendo vya uhalifu, je, Wizara hii haioni kwamba sasa umefika wakati kwa Polisi kufuata *system* za Kimataifa kwa wao kuupa mpira mgongo na wao kuangalia *audience* ili waweze kuangalia na kuwa na uhakika wa usalama zaidi hasa ikizingatiwa kwamba wapo katika Uwanja Mkubwa wa Kimataifa?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana dada yangu, Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa mchango wake. Ninapenda kusema kwamba mimi siyo mtaalam wa masuala ya ulinzi lakini ninaamini kabisa kwamba katika michezo ambayo mimi nimeangalia wapo wale wanaangalia upande wa mpira, wapo wengine ambao wanaangalia upande wa watazamaji. Nafikiri Afande *IGP* amesikia kama kweli wote wanaangalia mpira na hakuna anayeangalia watazamaji, naamini Afande *IGP*, atarekebisha. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa jana, nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo. Katika uchaguzi wa Kiteto, kulitokea vurugu na *IGP* aliunda Tume. Sasa naomba kujua ni nini kichojiri katika Tume ile?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumfahamisha dada yangu, Mheshimiwa Grace Kiwelu kwamba kweli Tume ilikuwa imeandaliwa na Tume ilikamilisha kazi yake. Tume imechukua *file* hizo na imezipeleka kwenye Ofisi ya *DPP* ambaye ataamua atafanya nini? Kwa hiyo, ninaomba tumruhusu *DDP* afanye kazi yake na pale atakapokuwa amekamilisha kama kutakuwa kuna mashtaka atayapeleka mbele na kama kutakuwa hakuna, tutafahamu.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa kuongea, nilimpungeza sana Mkuu wa Gereza la Magu, kwa kazi aliyofanya kwa kujitolea bila fedha za Serikali. Lakini pia nikaorodhesha katika mchango wangu wa maandishi matatizo na kero kubwa zilizopo katika Gereza lile la Magu na nikamwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri au Katibu, aje ajionee kwanza ile juhudhi ya Mkuu wa Gereza na pia matatizo makubwa yaliyopo pale. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari niongozane naye akaone hali halisi ya Gereza la Magu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, upo tayari kwenda?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwamba niko tayari kwenda lakini pia ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba pia Gereza la Magu litapata na gari. Nitaenda na hilo gari tutaliangalia kwa pamoja. (*Makofit/Kicheko*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilainisha mambo mengi yanayonikera Jimboni kwangu. Lakini kwa kuwa ninapaswa kuuliza swalii moja ni kwamba ninapenda kupata maelezo kuhusu Mwalimu huyu aliyekwenda kuchukuliwa shulenii na kupelekwa kwenye Kituo cha Polisi bila kosa na gari likapinduka akavunjika mguu ambapo mpaka leo anahangaika kupata fidia, nataka nihakikishiwe kama Serikali itamlipa fidia na, je, ni hatua gani iliyo chukuliwa kwa hao watu ambao walikwenda kumchukua? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Lwanji, ni swalii moja tu la fidia. Kwa sababu kila Mheshimiwa Mbunge anapaswa kuuliza swalii moja tu. Mheshimiwa Waziri fidia kwa huyo Mwalimu aliyekamatwa na akavunjika mguu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu kaka yangu Mheshimiwa John Lwanji kama ifuatavyo:-

Kwa bahati mbaya, hiyo taarifa nimeipata kwa mara ya kwanza siku ya leo. Nimewaomba watu wangu waende wakafuatilie. Mheshimiwa John Lwanji tuko karibu naye sana na hata alivyoeleza mwenyewe katika mchango wake wa maandishi kuna matatizo mengine amekuja kwangu ofisini na tumeyatatua. Ninamwomba avute subira, tuendelee kufuatilia aje ofisini kwangu wiki ijayo na ninaamini tutampatia jibu.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba kupata ufanuzi tu kwa swalii ndogo sana. Nilikuwa nimechangia kwa maandishi nikieleza juu ya wizi wa ng'ombe nane walioibowi pale Shelui wa Mzee

Shaban Mohamed. Wale ng'ombe waliibiwa na wakakamatwa katika kijiji cha Ndurumo. Baada ya kukamatwa, akatokea mtu mmoja pale akasema wale ng'ombe, yule mtu aliyekamatwa nao, anamwamini na anamjua hana tatizo, wale ng'ombe wakachukuliwa. Lakini baada ya siku mbili, alipokwenda mwenyewe Mzee Shaban na watoto wake wakagundua kwamba zile alama za wale ng'ombe ndiyo wale walioibiwa. Ikaonekana yule mtu alimdhaminii arejeshe ng'ombe wale kwa Mzee Shaban, wale ng'ombe wakarejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mtu aliyewarejesha, alirejesha ng'ombe 12, ng'ombe nane kwa Mzee Shaban na ng'ombe wawili ikiwa gharama za usumbufu na nauli na nini na ng'ombe wawili wakachukuliwa na Polisi Shelui. Hili suala nilikwishawahi kumweleza Naibu Waziri na baada ya siku mbili Polisi Shelui ikaenda ikamnyang'anya wale ng'ombe Mzee Shaban ikamrudishia yule mwizi. Nimemweleza Mheshimiwa Naibu Waziri na niliwahi kumwandikia Afande *IGP*. Sasa kutohana na hali halisi, yule mzee amekwishadhulumiwa wale ng'ombe mpaka sasa hivi na wale ng'ombe walioibiwa ndiyo wale wale kulingana na Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Ndurumo jinsi alivyowatambua. Sasa mimi nataka Mheshimiwa Waziri anieleze, hivi suala hili la wale ng'ombe wa yule mzee, imefikia wapi na atarejeshewa ng'ombe wake?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri suala hili limefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu ndugu yangu, Mheshimiwa Juma Killimbah kwamba anafahamu maana tuliwasiliana naye kuhusu suala hili na tumejaribu kulifuatilia kwa ukaribu zaidi na bado kuna taarifa ambazo nazisubiri. Nataka nimhakikishie kwamba kabla hatujatoka hapa Bungeni, nafikiri tutakuwa tumepata taarifa za kutosha kuhusu suala hili. Kwa sababu nimekuwa katika mawasiliano naye, nataka nimhakikishie kwamba tunasubiri hizo taarifa tukishazipata, nadhani tutafika mahali pazuri pa kuona tunakwenda vipi.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Sina nia ya kushika mshahara wala nini, naomba tu kupata ufanuzi. Kutohana na msongamano wa wafungwa Magerezani, je, wafungwa wenyewe ulemavu wanahudumiwa namna gani humo Magerezani?.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Margaret Mkanga kwamba inategemea na aina ya ulemavu ambao huyo mlemau anao. Jeshi langu la Magereza lipo makini sana na tunahakikisha kwamba tunawatunza kutohana na ulemavu walionao na tuhakikisha kwamba wanapata matunzo bora.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia sikuunga mkono hoja, suala la kuunga mkono hoja itategemea na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nataka nifahamu pamoja na mambo mengine suala la wizi ambao umekithiri Kinondoni, lakini lile suala la nyumba za Askari pale Magomeni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge tafadhali uliza swali moja.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali moja tu nauliza. Nyumba za Polisi pale Magomeni, kwa kweli zinatia aibu, ni mbovu, mbovu kupitia kiasi. Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini ujenzi utaanza ili Askari wetu waondokane na kero hiyo inayowakabili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nimejitahidi wakati nilipokuwa nikijibu hoja kwamba tunao ufinyu wa bajeti, hakuna kitu kibaya kama kuahidi kitu halafu usitimize. Azma tunayo na nia tunayo na tunavyopata fedha ndivyo tunavyokwenda kwa awamu. Nataka nimhakikishie tutafanya kazi hiyo, lakini kibaya ambacho hatuwezi kufanya ni kuahidi kwamba kitu fulani tutakifanya mwaka kesho au mwaka kesho kutwa halafu tusipokifanya akaja akatusuta humu ndani, lakini nataka nimwambie hivyo kwamba tutafanya, tafadhali.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi pamoja na michango mingine, nilielezea kero wanayoipata wavuvi wa Ziwa Tanganyika, wamekuwa wakivamiwa mara nyingi na majambazi na kuibiwa injini zao pamoja na hivyo, ulinzi siyo madhubuti na vile vile wamekuwa wakilazimika kuchangia mafuta ya petroli kwa ajili ya boti la polisi. Sasa nataka kujua sera hiyo itaisha lini, kwa sababu mwaka jana niliuliza, Naibu Waziri wa mwaka ule Mheshimiwa Mohamed Aboud, aliniambia kwamba hawatakiwi kulipia hayo mafuta, Serikali yenyewe itafanya. Sasa nataka kujua itakuwaje maana bado tatizo hili linaendelea na ni kero kubwa sana kwao?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimjibu dada yangu, Mheshimiwa Mhonga kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kwamba kuna tatizo hapo *Lake Tanganyika* na ni tatizo ambalo tunalitambua lakini si *Lake Tanganyika* peke yake na *Lake Victoria* ni katika maziwa yetu mengi.

Nilivyoeleza, tumetenga fedha mwaka huu bilioni moja na aronaini na mbili na milioni mia tano kwa ajili ya ukarabati wa boti ambazo tunazo na kadhalika. Mimi ninamwomba Mheshimiwa Mhonga kwamba avute subira kidogo. Wizara yetu inatafuta njia mbadala nje ya bajeti kujaribu kuangalia ni nini ambacho tunaweza kufanya ili kupata boti za kutosha ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanalindwa kwa usalama mkubwa sana. Lakini tutaendelea kufanya doria na wenzetu wa Jeshi la Taifa pamoja na wenzetu wa Wizara ya Uvuvi na tutajitahidi kuhakikisha kwamba kuna usalama katika Ziwa Tanganyika.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Ahsante Mwenyekiti. Kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kusema kwamba hapendi kutoa ahadi ambayo anajua hatakeleza.

Katika mchango wa maandishi, nilimkumbusha Waziri ahadi aliyotoa tarehe 13 mwezi wa nne mwaka jana, juu ya kukipatia gari kituo cha Mlimba. Ahadi hiyo mpaka leo haijatekelezwa. Sasa napenda awaeleze wana Mlimba Kituo hicho kitapata gari au la?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Lighallama kama ifuatavyo:-

Kituo kile anachokisema kina gari. Gari hiyo ni PT 974n kama sijakosea. Ukweli ni kwamba gari hiyo ni mbovu na siku mbili zilizopita tulikuwa tumetuma watu kwenda kuangalia hali ya ubovu wa gari hiyo. Lengo ni kwamba kama hiyo gari itatengenezeka, lakini tukibaini kwamba haiwezi kutengenezeka, kati ya magari yale 28 ambayo bado tunayo tunahakikisha kwamba tutamfikishia gari moja.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa jana, nilizungumzia mambo mengi sana lakini kwa kuwa nafasi ni moja nilikuwa naomba ufanuzi na nilitarajia Waziri kwa uzito wa jambo lile alivyosimama lazima angelizungumzia, kifo cha Hija na kifo cha Mine na yale magari yao yaliyochukuliwa na moja kuonekana Kamanda mkubwa kabisa wa Keshi akilitumia. Mimi na wananchi wa Dar es Salaam, tunapenda kusikia majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu kaka yangu, Mheshimiwa Mtemvu kama ifuatavyo:-

Naomba kwanza anisamehe kwamba katika majibu yangu ya awali nilikuwa sijalitolea jibu suala hili. Siyo kwa kudharau suala lenyewe, kwa kweli unavyosema ni suala moja muhimu sana, ni kwamba tu nilikuwa nimeishiwa muda.

Suala hili ni suala ambalo nalifahamu sana na nimeshatembelewa mara mbili, tatu na wahusika, baba yake Hija amenitembelea Ofisini na kaka yake marehemu Mine Chiomba, naye amenitembelea Ofisini na kuniuliza hili suala limefikia wapi. Suala hili kweli lilikuwa limefanyiwa uchunguzi na Tume ambayo ilikuwa imeteuliwa na Mheshimiwa Rais. Uchunguzi huo ulikuwa umenifikia na uchunguzi ndiyo hivi karibuni nimemaliza kuusoma na nimetoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi nini cha kufanya. Kitu ambacho naweza nikakuhakikisha ni kwamba wale wote ambao watabainika wamehusika na vifo vya ndugu Hija pamoja na ndugu Chiomba watachukuliwa hatua za ki-polisi. (*Makofi*)

Pia ninapenda kukufahamisha Mheshimiwa Mtemvu, kwamba ile gari ambayo ulikuwa umesema kwamba imechukuliwa na Afande mmoja ambaye yuko ndani ya Jeshi la Polisi, hiyo gari imekwishakamatwa. Tunayo pale Oysterbay Polisi, ipo na uchunguzi unafanyika na ninapenda kuongezea kwamba yale magari mawili mengine ambayo ulikuwa umeyaulizia yanaweza yakachukuliwa na familia ya ndugu Chiomba na familia ya ndugu Hija. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni Na. 104 ambayo inazungumzia kukamilika mjadala katika Kamati ya Matumizi na kwa hali halisi ambayo inayoendelea hapa ndani sasa hivi, kwa mujibu wa Mamlaka niliyonayo, sasa ninaomba nitengue utaratibu wa kuahirisha Bunge na tuongeze muda wa nusu saa zaidi ili tuweze kuendelea na kazi ambayo inaendelea mbele yetu kwa kuwa wachangiaji wako wengi.

Baada ya kutoa taarifa hiyo ya kikanuni, naomba niendelee, nimwite Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika mchango wangu wa maandishi na wa kuzungumza, nilizungumza mambo mengi lakini kwa sasa hivi napenda kuuliza swal...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kila mtu aendele moja kwa moja kwenye swal. Tunajua kila mtu ana mambo mengi aliyoyachangia, twende tu kwenye swal.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unazidi kula muda wangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba sana juu ya gari na nilishaahidiwa humu ndani ya jengo hili na hili ni jengo Tukufu, Mheshimiwa Waziri anapoahidi, ni vizuri suala hili likawa linatekelezwa. Sasa nimeomba sana gari kwa sababu ya mauaji yanayotokea na unakuta tatizo kubwa tunalolipata kwa upande wa Wilaya ya Geita ni kwa sababu Askari wetu hawana vifaa. Napenda angalau katika magari haya yaliyotolewa Mheshimiwa Waziri anipe matumaini na watu wangu wasikie, ahsante sana.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumhakikisha kaka yangu, Mheshimiwa Fautine Kabuzi Rwilomba kwamba tutakuja kufanya tathmini ya hali ya ulinzi na usalama katika eneo husika. Nilivyoeleza, tuna magari 28 ambayo tulikuwa hatujayapangia maeneo lakini tutayapangia maeneo kutokana na moja, ukubwa wa eneo ambalo linahitaji magari. Tutapanga kutokana na hali ya usalama katika eneo ili kuhakikisha kwamba watu wetu wako salama. Kwa hiyo, nimwomba kaka yangu, Mheshimiwa Kabuzi, turuhusu tufanye tathmini yetu ili tuhakikishe kwamba wananchi wa Tanzania kote wako salama. Lakini kama hali ni kama vile anavyosema na anaamini kabisa hali ni mbaya kuliko maeneo mengine hapa nchini basi kwa *standard* hiyo inaelekea basi anaweza akaja kupata lakini tusubiri tufanye hiyo tathmini.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Askari wanaokufa, hawatendewi haki na wale Askari ambao wako hai, kwa sababu kuna Askari mmoja ambaye anaitwa P/C Hassan M. Luya, Force No-E5552, alikufa mwaka 2000 mwezi wa tano, mirathi namba 481/2001. Mirathi yote ilikamilika, yule mama yake akapeleka mpaka Makao Makuu Dar es Salaam tangu mwaka 2001 lakini hakuweza kulipwa. Ikabidi mimi nikamsaidie, nikamwambia leta mirathi yako

yote nikupelekee, vielelezo vyake vyote nikavipeleka Makao Makuu Polisi Dar es Salaam. Nimefika pale nikaona wahusika, wakaniambia, vimefika, hakuna tatizo, wewe nenda tutamlipa huyu mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia tena mara ya pili, wakaniambia sasa hivi faili lake liko Hazina. Nikasema sawa twende wote Hazina. Tukaenda Hazina, wakaniambia jina lake liko kwenye kitabu namba moja. Tukatafuta namba moja, hakuna. Kitabu namba mbili, hakuna. Kitabu namba tatu, hakuna, 2006 ikaisha. Ikafika mwaka 2007, nikafuatilia vile vile, wakati mwingine nikawa nawapigia simu wakasema sasa hivi mirathi yake iko tayari, sasa tunaituma Kigoma Hazina Ndogo. Nikampa taarifa yule mama akafuatilia. Lakini akakuta lile jina lilokwenda kule siyo lake. Nikafuatilia tena Makao Makuu Polisi Dar es Salaam, nikamkuta mhusika yupo nikamwambia sasa hivi twende mpaka Hazina, tukaenda mpaka Hazina kutafute lile jina. Nikalikuta limeandikwa tangu tarehe 22 mwezi wa saba 2002, ina maana pale Hazina ndipo lilipofikishwa tarehe hiyo, lakini mpaka leo yule mtu hajapata mirathi yake. Anasumbuka na mimi nimetembea mpaka miguu imeniingia shingoni. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema sasa iliyobakia nitaliulizia kwenye bajeti. Je, huyu mama atapata mirathi yake au ndiyo wahusika wenyewe walishakula mirathi hiyo? Maana tangu mwaka 2002 mpaka leo ni miaka minane, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sijapata, suala hili kama limeshafika Hazina, ni suala la Wizara ya Fedha.

*(Hapa kulikuwa na minong'ono kutoka
kwa Waheshimiwa Wabunge)*

MWENYEKITI: Naomba Waheshimiwa Wabunge, ngoja Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kwanza, ngojeni Mwenyekiti naendelea. (*Makofi*)

Ni suala la Wizara ya Fedha, sasa tutakachokifanya, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha wote watupatie maelezo katika suala hili.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpe pole mama yangu, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba kwa taabu ambayo amepata katika kufuatilia mirathi ambayo ametueleza na kwa moyo aliojitlea kufuatilia mirathi hii. Mimi ninaomba nishirikiane naye, aje Ofisini kwangu, wote tutembee kwa mguu mpaka huko Hazina ili tufuatilie mirathi hiyo mpaka ipatikane. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waziri wa Fedha!

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia taarifa hiyo kwa mara ya kwanza na kama kweli faili liko Hazina, nitamwomba wakati wote nikiwa Dar es salaam, aje ofisini tutasaidiana. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anaeleza kuhusu wale ng'ombe 25 wa wizi, alieleza kwamba atakuja kule Singida na mimi sina tatizo, namwamini kwamba atakuja Singida ili kumpa yule Mzee Mahola, Msukuma wa watu wale ng'ombe wake 25, sina tatizo na hilo. Tatizo langu ni pale, kwa wale watumishi, Askari wawili Julius na Tungaraza ambao wamefukuzwa kinyume na taratibu kwa sababu wao wamekabidhi ng'ombe kwa *OCCID* na ng'ombe wamepotelea kwa *OCCID*. Sasa wanafukuzwa vipi hawa na wao kazi yao wametekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa amesema katika maeleo yake kwamba *IGP* ameunda Tume leo. Mimi sikubaliani kwa sababu suala hili limekaa Makao Makuu ya Wizara miaka miwili toka mwaka 2006. *IGP* huyu huyu na mheshimu sana Mheshimiwa *IGP* Mwema, namheshimu Waziri na Naibu Waziri, miaka miwili imekaa pale Wizarani hawajaunda Tume, leo watakuja kuunda hiyo Tume ifanye kazi gani? Mimi sikubaliani na hilo, ziko *option* mbili.

Moja Tume ya Serikali, mimi naweza nikakubaliana nayo ya Serikali siyo ya Wizara, kwa maana Mwanasheria Mkuu, sijui nani na nani, pengine naweza nikakubaliana nayo. Vinginevyo Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Spika, naomba uruhusu sisi Wabunge wa Mkoa wa Singida siyo Missanga, sisi Wabunge wa Mkoa wa Singida, tuombe Bunge lako Tukufu liteue Tume ya Bunge kwenda kuchunguza tatizo la ng'ombe 25 nani katafuna, kwa nini hawa Askari hawarudishwi kazini wakati wao hawana kazi na nashauri kesho tukutane na *IGP* juu ya mazungumzo zaidi. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mzee wangu, Mheshimiwa Missanga kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba suala hili limekuwa limekaa katika Jeshi la Polisi kwa muda mrefu. Ninamwomba Mheshimiwa Missanga, afikirie yafuatayo:-

Suala hili limeletwa kwetu, kwa Naibu Waziri na kwangu Waziri ambaye tumekaa katika Wizara hiyo katika kipindi cha miezi mitatu. Mimi hapa ni Mwanasheria, Naibu wangu ni Mwanasheria, hiyo Tume ambayo imeundwa ni ya *CID* ambayo siyo kwamba imeundwa leo ni kwamba imefika huko leo inafanya hiyo kazi. Taarifa hiyo itabidi ifike kwangu ambapo pamoja na kuwa Waziri ni Mwanasheria na Naibu wangu pia ni Mwanasheria, ninakuomba imani ambayo umeonyesha kwetu mpaka hivi uendelee kuonyesha na kama nilivyoahidi, baada ya Bunge hili nitakuja mimi mwenyewe. Nimeshaahidi kukutana na Wabunge wote wa Singida ili tuliongelee suala hili. Mimi ninaomba Mheshimiwa uvute subira, najua imechukua muda mrefu lakini nia yangu na lengo langu ni kuhakikisha kwamba suala hili linatatuliwa.

MWENYEKITI: Lakini ni busara kesho mkafanya hili la kukutana na Wabunge wa Mkoa wa Singida. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba radhi kwamba kwa kesho inaweza ikawa ngumu, kesho asubuhi naenda

kumuona Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Lakini ninakubali kwamba wiki ijayo tuko tayari kukutana na Wabunge wote wa Singida kama nilivyowahi kuahidi.

MWENYEKITI: Sawa Mheshimiwa Waziri.

MHE. ISSA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nampongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na IGP kwa jitihada zao kwamba yule mgonjwa amepelekwa India. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kuzuia mshahara wa Waziri lakini nataka ufanuzi tu kuhusu habari ya Askari wa Uhamiaji. Kwa nini wanakatwa asilimia 10 ya mshahara wao katika pango la nyumba ambayo ni chumba kimoja na ukumbi tu wakati wenza Polisi hawakatwi mkato kama hayo? Nataka maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu, maelezo ya huo mkato. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Huo mkato ni kweli upo, siyo kwamba tunakataa lakini kwa mujibu wa taratibu zilizopo sasa hivi, ni katika mambo ya kurepea nyumba zenyewe. Ingawaje kweli nyumba zenyewe ni dhalili, zimechoka, za zamani lakini bado watu wanakaa katika majengo hayo. Kwa hiyo, ni ile pesa ambayo inachukuliwa katika azma ya kusema kwamba wanafanya repea za majengo hayo lakini siyo kwamba inatolewa ndiyo kodi ya kulipia pango, hapana!

MWENYEKITI: Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, labda tu muangalie huo utaratibu, kwa nini kuwe na tofauti kwa kiasi hicho? Nadhani Wizara mnatakiwa kulifanyia kazi suala hilo. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana shaka tutaliangalia.

MWENYEKITI: Maana yake...

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilichangia kwa maandishi, kwanza ukurasa wa 30 kipengele namba 56...

MWENYEKITI: Ukurasa wa 30 wa nini?

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Halmalshauri za Miji, Manispaa pamoja na Jiji katika ununuzi wa magari ya kuzima moto. Wao ndiyo washauri wakubwa na Wizara ya Miundombinu ilikuwa haiwezi kukubali ili *TRA* itoe namba mpaka wao wametoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa nazungumza au kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumzia gari la zimamoto la Kibaha kuwa ushauri uliotolewa na

huyo Kamishna Mkuu kuhusu gari lile si sahihi. Siku ya pili gari lile likapelekwa Kibaha. Siku ya tatu likafanyiwa *demonstration*, matokeo wananchi wote wakaambiya msisikilize uongo unaotolewa na watu wengine. Siku ya tano, nyumba ya Bibi Rukia Mbonde ikaungua moto. Diwani akapiga simu kuomba msaada wa gari lile la kuzima moto, akaambiya gari lile limerudi gereji. Wakati wote gari hili lilikuwa halipewi namba, Kamishna Mkuu hataki kuthibitisha lile gari kama ni zima na alikuwa analijua ni bovu na mimi nimeambia Serikali kwa kutumia vyombo vya Serikali ile gari si zima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba ndugu yangu Waziri, kwa nia nzuri tu, atuambie, aliwashauri namna gani Halmashauri ama siyo nitatumia kipengele namba 117 cha Kanuni ya Bunge kuhakikisha Kamati Teule inaundwa na nikikuambia mimi ni Mwenyekiti wa *African Parliamentary Network against corruption*, sitaki kusababisha *chaos*, ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu mama yangu, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kuhusu hilo gari kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kwamba Wizara yangu inatoa ushauri. Ushauri tunaoutoa pale, ni kuhusu *standard* ambayo inatakiwa kufuatwa wakienda kununua gari. Hatuendi sisi kuchagua gari, wala siyo sisi tunaonunua gari, naamini ni Halmashauri yako ndiyo ilienda kununua hiyo gari. Sasa sisi *standard* tumetoa kama wao hawakufuata, nakushauri Mheshimiwa Gama wewe ambaye pia ni Diwani kwenye Halmashauri yako, uangalie pale kwenye Halmashauri kwa nini *standard* ambayo ilikuwa imetolewa na Wizara yangu haikufuatwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama umaona haya mambo hayajakaa sawasawa, ziko taratibu nyingine za kufuatilia.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Wakati nachangia kwa kuongea juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilimwuliza juu ya gari iliyopo Kituo cha Chalinze ambayo inafanya kazi ya doria maeneo ya mbali na wakati huo huo mafuta wanayopata ni lita 600 kwa mwezi ambazo zinaishia mwanzoni mwa mwezi tu husika na wakati huo ile gari inafanya kazi ya kupeleka mahabusu Bagamoyo badala ya Ubena ambapo ni karibu. Sasa nilitaka ufanuzi aniambie kuna uwezekano gani wa kuongeza mgao wa mafuta ili kazi ya doria iweze kufanyika ambapo ukizingatia hapa juzi tu mpiga kura wangu mmoja ameuawa na majambazi pale Chalinze?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu kaka yangu Mheshimiwa Maneno kwamba hilo suala la mgao wa mafuta siyo tu katika eneo lake lakini katika maeneo mengine ambayo watu walikuwa wamechangia, nitawasiliana na Mheshimiwa *IGP* ili kuhakikisha kwamba mgao wa mafuta unakuwa mgao ambao unastahili katika maeneo yote.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nimezungumza mambo mengi lakini kubwa ambalo nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie ni pale Watanzania tunapopewa nafasi ya kuwa na silaha za kujihami na taratibu zake zinaanzia Wilayani, Mkoani lakini sehemu ya mwisho kabisa iko katika Jeshi la Polisi. Sasa nilipokuwa natoa maelezo katika mchango wangu nimesema hivi sasa kuna matukio tisa ya hatari katika kumpatia mtu silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la rushwa lakini Mheshimiwa Mwenyekiti hapa ndiyo penye rushwa ya hatari. Mimi najaza fomu ya kupatiwa silaha na nikifika hatua hii ya mwisho katika Kitengo hiki, mie naitwa Hafidh Ali lakini sipewi silaha. Silaha hii anapewa Mohamed Rajab kwa njia iliyokuwa si halali kwa kutoa shilingi milioni mbili, matukio kama haya hivi sasa yako tisa. Mheshimiwa Waziri anaweza kunisaidia ni hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika wa matokeo haya tisa na Askari wake wamechukuliwa hatua gani mpaka hivi sasa na anatuambia nini katika Bunge hili ili tujihami katika nchi yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri utajibu la kwanza maana hapa yamepigwa kama maswali kama matatu ya mfululizo. Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tupeane nafasi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa ambayo ameitoa Mheshimiwa Hafidh Ali, ndiyo taarifa nimeipata kwa mara ya kwanza kwa siku ya leo. Ninamwomba Mheshimiwa Hafidh Ali kwamba katika kipindi cha Bunge hili mimi na yeze tukae tena haraka iwezekanavyo, tuongelee hiyo taarifa ili niweze kufanya uchunguzi wa kina ndani ya Wizara yangu ili kuhakikisha kwamba matukio haya hayatokei tena. (*Makofi*)

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia, nimeeleza hali ya ujambazi uliokithiri Wilaya ya Geita. Namheshimu sana Mheshimiwa Waziri, lakini nimesikitishwa na kauli yake wakati akimjibu Mheshimiwa Fautine Rwiomba kuhusu ombi la kupewa gari pale Wilaya ya Geita kwa sababu ya hali halisi iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na Naibu wake *IGP*, Katibu Mkuu siyo ma-TX, ni Watanzania. Wanafahamu hali ya nchi ilivyo sasa hivi, kila sehemu, wanajua Wilaya zipi zenye matatizo na ndiyo maana asubuhi ametupa kitabu hiki, taarifa ya hali ya uhalifu nchini, hiki ni kitabu cha Wizara na Polisi hapa. Sasa leo hawajui mpaka wakakae kwanza waangalie na kila siku ma-*RPC* wanatoa taarifa ya uhalifu katika Mikoa yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Geita, nimeeleza yapo mambo mengi sana yanabishwa lakini mojawapo ni zile operesheni zilizofanywa na Mikoa ya Kagera na Kigoma na Kamanda Tosi. Kwa hiyo, yale majambazi wanakimbia pale jirani Geita, yaani unawafukuza ndege kwenye shamba hili, ndege wanaenda kwenye shamba ambalo halina mlinzi. Kuna gari moja tu ya *OCD* kila siku inatembea kilomita 500 na zaidi. Wilaya ni kubwa sasa, namwomba Waziri, je, atakubali kwamba yeze si mgeni hapa

Tanzania na kwamba sasa Geita inastahili kupata gari la Polisi kufuatana na hali ya ujambazi? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu kaka yangu, Mheshimiwa Musalika kama ifuatavyo:-

Moja, si tu mgeni katika Wilaya ya Geita, mimi mwenyewe natoka katika Mkoa wa Mwanza, matatizo ya Geita nayafahamu vizuri sana. Lakini pia kama nilivyoeleza, kuna Mikoa mingine na Wilaya nyingine hapa nchini ambazo pia zina matatizo. Sijakataa kwamba watapata gari, nilichosema ni kwamba tunakaa na kuangalia wapi tupeleke magari kwa sababu kuna maeneo mengine yanaweza yakahitaji gari moja itabidi tupeleke magari mawili. Kuna maeneo mengine ambapo tunaweza tukabadilisha magari na kupeleka magari kutoka maeneo mengine, ndiyo maana kuna suala la tathmini. Tokea mwaka jana mpaka mwaka huu, tunahakikisha kwamba Wilaya zote zitakuwa na gari ambayo inafanya kazi na tunahakikisha pia kwamba Wilaya zile ambapo kuna tatizo la usalama, tutawaongezea magari. Lakini kikubwa ni kuangalia ukubwa wa eneo na ukubwa wa Geita sio kwamba haujulikani, unafahamika. Tutaangalia hali ya ujambazi na usalama. Tatizo la Geita linafahamika. Sasa ningewomba tu Mheshimiwa Musalika sidhani kama tutakuwa tunatofautiana sana lakini nakuomba tu usubiri kidogo, pale tutakopomala hii kazi, magari yatasambazwa.

MWENYEKITU: Ahsante.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea juu ya hali inayojengeka sasa hivi ya kuwakopa Askari hasa Aaskari wa vyeo vya chini, fedha za uhamisho, posho zao wanazostahili na fedha za kupandishwa vyeo hasa kwa Jeshi letu la Polisi na Magereza. Nikatoa mfano wa Askari wanaosindikiza treni ya mizigo katika reli ya *TAZARA* ambayo kwa muda mrefu wamekuwa wakidai, lakini hawalipwi inavyostahili. Ninaomba kujua ni lini Serikali italeta utaratibu endelevu wa kutowakopa Askari kwa sababu na wenyewe ni Watanzania wanaostahili kuishi ndani ya nchi yao.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali la Mheshimiwa Mpesa, ni kweli anayoyasema na ni kitu ambacho hata sisi ndani ya Wizara tunakichukulia kwa uzito sana na imekuwa vizuri kwamba unayasema maneno haya uongozi wa Jeshi la Polisi uko hapa. Lakini kama nilivyosema wakati nilipokuwa najibu hoja zenu, Mheshimiwa Mbunge Mpesa ni kwamba tumeomba bajeti ili tuweze kulipa madeni hayo ikiwemo malimbikizo ya Askari na tukishafanya hivyo katika zoezi lote hili la kuboresha na kutafuta njia nyingine, nafikiri tutaweza tukafikia mahali kwamba hili suala la kuwa tunategemea Askari wanatoa pesa mfukoni mwao halifu wanakuja kulipwa baadaye, nafikiri tutakuwa tumevuka hapo. Kwa kweli tunakiri kwamba si kitu cha kawaida lakini kwa sababu ya mazingira yalivyokuwa lakini tunataka tutoke huko twende mbele, ahsante.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa nilipokuwa nachangia, niliondoa shilingi moja katika Wizara hii na baada ya hapo

Mheshimiwa waziri na Naibu Waziri tuliongea nao vizuri na wakaahidi kwamba lile jengo lililokaa miaka 25 bila kuisha na bila kufunguliwa, sasa litakwisha kwa bajeti hii na kwamba fungu hilo lipo.

Sasa ili kuzingatia Kanuni ya 103(2) na kile cha (7) ambacho kinamtaka Mbunge aliyetoa shilingi kwamba anaweza kuirudisha kwa kutumia kifungu hicho kidogo cha saba, naomba nirudishe shilingi hiyo kwa sababu tayari wamekwishanikubalia. Je, unaweza ukadiruhusu sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, athibitishe tu kwamba ni kweli lazima mwaka huu ofisi ile itakwisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, haya maongezi yalikuwaje? Ni kweli?
(*Kicheko*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nyami ni kweli. Mheshimiwa Salim.
(*Makofi/Kicheko*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ukurasa wa 21, ameeleza kuwa ndani ya Jeshi la Magereza, lipo Shirika la Magereza ambalo mionganoni mwa kazi zake ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hapo zamani Jeshi la Magereza lilikuwa linasifikasi sana kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na lilifikia wakati wa kujitosheleza kwa mahitaji ya ndani. Lakini tumefikia mahali sasa hivi Jeshi linaomba bajeti ya Serikali kwa kulisha wafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kwamba kutokana na hii *food crisis* iliyopo duniani, sasa hivi bei ya chakula imepanda na chakula kimekuwa ni haba, je, Wizara imejipanga vipi kushirikiana na juhudhi za Serikali ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula nchini? Ahsante.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim, kama ifuatavyo:-

Nafikiri tukiangalia bajeti ya Wizara yetu na tukiangalia kwamba huwa hatupati pesa za kutosha, watu wanashangaa inakuwaje wafungwa wanakula mwaka hadi mwaka. Pamoja na kwamba huwa tunawakopa wazabuni, ukweli ni kwamba Jeshi la Magereza kupitia mashamba yake chini ya *Prison's Cooperation Soul*, kwa kiwango kikubwa sana inalisha wafungwa kwenye Magereza yetu. Lakini pamoja na hayo, kati ya mipango tulionayo katika mwaka huu wa fedha, ni kuhakikisha kwamba mashamba yetu makubwa ambayo yapo katika maeneo ambayo yanaweza yakafanyiwa *irrigation*, tutayaboresha ili kuweza kuongeza uzalishaji katika mashamba yetu ya Magereza.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilizungumza kwa uchungu sana kuhusiana na hali ya ujambazi Wilayani Karagwe, jambo ambalo sio

la kusubiri ni la dharura, kwa sababu sasa hivi majambazi wamefikia mpaka kuwashambulia abiria kwa mabomu ya mkono. Niliomba nisaidiwe magari manne katika hali ya dharura, sasa wakati Mheshimiwa Waziri anazungumza hapa, kusema kweli ametoa ahadi ya jumla lakini hali ya Karagwe ni ya kusikitisha sana na wananchi wa wilaya ya karagwe, wangetamani angalau wasikie ahadi ya Mheshimiwa Waziri ili leo waweze kupata usingizi. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri tafadhali kati ya yale magari manne niliyoomba, leo nisikie kauli ya Serikali, ni mangapi nitapewa? Nakushukuru sana.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu kaka yangu Mheshimiwa Blandes, kama ifuatavyo;-

Kama nilivyoeleza nikiwa nawaeleza Wabunge wengine hapa katika Kamati, tutaangalia hali ya usalama, tutaangalia ukubwa wa eneo na ukubwa wa eneo lake tunaufahamu na hali ya pale tunajua ni juzijuzi tu nimepoteza Askari kule katika basi ambalo lilitkwa. Uwezo wa kumpelekea magari manne kwa kweli sina lakini angalau gari moja litapatikana katika kipindi hiki cha bajeti. (*Makofii*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia kuhusu Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni. Nikiwa nimerejea swalı langu lililojibwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mohamed Aboud, alipokuwa Naibu Waziri, kwenye Wizara hiyo kwamba kituo hicho kina hali mbaya sana, hakina hadhi ya Wilaya, kimechakaa, kinavuja sana na hata masika yakiingia kesho pale ni matatizo makubwa. Nilipojibwa hapa, niliambiwa kwamba lengo la Serikali ni kujenga kituo kipyä na ilishapeleka shilingi 10,000,000/= kwa ajili ya kutafuta eneo na kufanya uthamini na shughuli nyingine zote za kupata eneo na hayo mambo yalishakamilika. Sasa nauliza, kituo hicho mbona kwenye bajeti hatujaona hata senti tano ya kuanza ujenzi wa kituo hicho? Ina maana sasa hilo eneo ni sinema tu na wakati niliambiwa hapa kwamba wakati tunataka kujenga, tutatoa hela ya kukarabati, hakuna hela ya ukarabati wala hela ya kujenga. Nataka niambiwe Manyoni, Wilaya ambayo ina ujambazi wa kuteka magari na shida zote, mbona kituo mashakani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kumjibu Mheshimiwa Chilolo kwamba ni kweli ahadi ya Serikali ilifanywa kama anavyosema. Lakini nafikiri kama nilivyomueleza na nilivyowaeleza wengine ni kwamba upo ufinyu wa bajeti hapa na kutokana na ufinyu wa bajeti ndio maana kwa kweli inakuwa taabu sana. Ninakuomba Mheshimiwa Mbunge, hili jambo tulizungumze, najua una machungu sana na ninajua kweli tatizo lipo lakini ninakuomba hili jambo tulizungumze ili tuweze kufahamishana vizuri na tuone tutakwenda vipi. Kwa sababu nachelea kusema kwamba kila kitakachosemwa hapa ambacho hakikutimizwa, tunaweza tukajikuta tunaweka ahadi nyingi kuliko uwezo ambao tunaweza kuwa nao. Kwa hiyo, ninakuomba tu kwamba, ni kweli ahadi ilifanyika, hatukatai, lakini baada ya hizi shughuli mimi ningeomba tukae tutizame ni nini tunaweza tukafanya. Lakini nakuahidi kwa kuwa ahadi imekuwepo basi hapana shaka tutatimiza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda niliobakiwa nao hauwezi kutosha tena kundelea na shughuli hii ya kuhoji swal moja baada ya lingine. Kwa hiyo, kwa mujibu wa taratibu na kanuni zetu, sasa nitaomba Katibu atuingize kwenye *guillotine* ili tuweze kuitisha mafungu yote kwa utaratibu ambao tunaufahamu.

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh.606,813,300/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh.487,771,800/=
Kif. 1004 – <i>Community Service Secretariat</i>	Sh.576,656,700/=
Kif. 1005 – <i>Information, Education and Communication</i>	Sh.123,911,300/=
Kif. 1006 – <i>Management of Information Systems</i> ...	Sh.111,218,900/=
Kif. 1007 – <i>Internal Audit</i>	Sh.125,900,000/=
Kif. 1008 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh.142,921,100/=
Kif. 1009 – <i>Complaints Division</i>	Sh.327,106,900/=
Kif. 3001 – <i>Fire and Rescue Services</i>	Sh.0/=
Kif. 3002 – <i>Fire and Resare Services Training Inst</i>	Sh.0/=
Kif. 4002 – <i>Refugees Unit</i>	Sh.903,701,100/=

*(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 14 - Fire and Rescue Force

Kif. 3001 – <i>Fire and Rescue Services</i>	Sh.2,000,000,000/=
Kif. 3002 – <i>Fire and Rescue Services Training Institution</i>	Sh.1,000,000,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 28 - Ministry of Home Affairs - Police Force

Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh.0/=
Kif. 2001 – <i>Police Main Force</i>	Sh.9,763,955,000/=
Kif. 2002 – <i>Police Marine</i>	Sh.0/=
Kif. 5001 – <i>Police Medical Unit</i>	Sh.200,000,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 29 - Ministry of Home Affairs - Prisons Services

Kif. 1001 – *Prisons Headquaters* Sh.800,000,000/=
Kif. 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation*..... Sh.2,381,000,000/=
Kif. 4001 – *Prison Building Brigade* Sh.1,800,000,000/=
Kif. 4002 – *Prison Industries* Sh.400,000,000/=
Kif. 4003 – *Prison Farms* Sh.500,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 51 - Ministry of Home Affairs

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh.665,000,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh.5,790,853,500/=
Kif. 4001 – *Refugees Unit* Sh.100,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 93 - immigration Department

Kif. 2002 – *Immigration Mainland*..... Sh.11,053,313,000/=

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)
(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2008/2009 na kupitishwa bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, bado sijawahoji, nashangaa Serikali mmeanza kupiga makofi, sijawahoji bado. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka
2008/2009 yalipitishwa na Bunge)**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yake nzima ambayo wanahusika na *vote* ambayo tumeipitisha leo na tuwatakie tu kila la heri. Mawaziri hawa kwa kweli wameanza kazi kwa nguvu ya kutosha na leo mmeonesha umahiri, maswali leo yamekuwa mengi haijapata kutokea. Lakini niombe tu Waheshimiwa Wabunge, nisema kwamba kwa mujibu wa taratibu zetu ilibidi tufikie hapo ambapo tumefikia. Kwa hiyo, nawapongeza sana na ninawatachia kila la heri katika kusimamia shughuli za kiutendaji na utekelezaji wa bajeti hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya dakika hizi tano nilizobakiwa nazo hazijaisha, labda nichukue nafasi hii nitoe matangazo mawili. Tangazo la kwanza, nimeombwa na Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Chakula Kilimo na Ushirika, niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, wote kwamba mnaalikwa kushiriki kwenye Maonesho ya Nane Nane Kitaifa ambayo yatafanyika hapa Dodoma. Maonesho hayo yatafunguliwa tarehe 01/08/2008, lakini Waheshimiwa Wabunge, tumealikwa rasmi kutembelea maonesho hayo kuanzia tarehe 2,3 na kuendelea kwa utaratibu ufuatao.

Tarehe 2/8/2008, Kamati ya Kilimo na Ardhi, Kamati ya Kilimo na Mazingira, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini. Tarehe 3/8/2008, Kamati ya Fedha na Uchumi, Hesabu za Serikali na Hesabu za Serikali za Mitaa. Tarehe 4/8/2008, Kamati ya Viwanda na Biashara, Mashirika ya Umma, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Tarehe 5/8/2008, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Haki Maadili na Madaraka ya Bunge na Kamati ya Sheria Ndogo na tarehe 6/8/2008, Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Huduma za Jamii na Maendeleo ya Jamii. Ofisi ya Bunge, itaandaa utaratibu na tutaona ni namna gani tunaweza kufanikisha mwaliko huo muhimu sana, Waheshimiwa Wabunge, tukawakilishe wakulima wetu.

Tangazo lingine tu labda niseme kwamba Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, amenipa majibu ya swali nililomuuliza. Amesema neno Askari halina wingi, hivyo neno maaskari sio sahihi. Kwa mfano, umoja tunasema kwamba Askari ameletwa, wakiwa wengi tunasema Askari wameletwa. Kwa hiyo, wale waliokuwa wanakosea katika kutamka neno hilo, neno Askari halina wingi kwa maana ya Maaskari, hayo ndio majibu niliyopata. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii, kuwashukuru na kuwapongeza kwa kumaliza kazi ya Wizara hii muhimu sana. Niwape pole wenzetu waliokwenda kutuwakilisha kwenye msiba lakini tumshukuru Mungu wamerudi salama na baada ya shughuli hii ya leo muda umetuishia kabisa na shughuli zetu zimetuishia, basi naomba sasa nahirishe shughuli hizi za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi ndani ya Ukumbi wa Bunge huu.

(Saa 2.15 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,

tarehe 1 Agosti, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)